19 MEI, 2025

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 19 Mei, 2025

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 339

Ukarabati Kituo cha Afya Mwika

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati na kuongeza majengo ya Maabara katika Kituo cha Afya cha Mwika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mwika kilijengwa Mwaka 1905. Kituo hicho ni miongoni mwa vituo vya afya Kongwe 203

ambavyo Ofisi ya Rais TAMISEMI ilivifanyia tathmini kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha ukarabati wa hospitali 50 kongwe nchini na baadaye itafanya ukarabati wa vituo vya afya na zahanati kongwe kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya cha Mwika. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nilipouliza swali kama hili kuhusu ukarabati wa Kituo hiki cha Mwika, Serikali iliniambia kwamba kiko kwenye mradi unaotekelezwa kwa ufadhili wa *World Bank* na kituo hiki kilikuwa namba 64 kwenye ile orodha. Ninaomba Waziri anihakikishie kama mradi huu umeanza kutekelezwa kimesha-*move* kwenda namba ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna kituo cha afya cha mkakati ambacho tulipendekeza kule Vunjo kijengwe pale Kilwa Vunjo Kusini kwenye eneo la Koresa (ni kati ya vile vituo ambavyo vimeombewa shilingi milioni 250). Ninaomba Waziri atoe kauli kwamba; je, fedha hizo zimeshakwenda? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei kwamba Kituo cha afya cha Mwika ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo vimewekwa kwenye mpango wa ukarabati kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia *(World Bank)* na tayari tumeshakiainisha kwa ajili ya kupelekewa fedha za ukarabati. Hata hivyo, tumeanza na ukarabati wa hospitali za halmashauri, tunakwenda kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati ambazo hazina vituo vya afya lakini baadaye tutakwenda kukarabati vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kimei kwamba Kituo cha Afya cha Mwika kipo kwenye orodha ya *World Bank* na fedha zitapelekwa kwa ajili ya ukarabati na kimewekwa kwenye *round* ya pili kwenye Mfuko huo wa Dunia. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie yeye na wananchi wa Jimbo la Vunjo kwamba Kituo hiki Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hasan inatambua kwamba ni kikongwe na ni chakavu. Pia, nimhakikishie tu kwamba fedha zitakwenda kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kilwa Vunjo. Mheshimiwa Kimei aliwasilisha Kata ya kimkakati na tayari Mheshimiwa Rais ameanza kutoa fedha katika majimbo 120 ya mwanzo. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wameanza kupokea fedha hizo katika kata za kimkakati na zoezi la kupeleka fedha hizo linaendelea. Kwa hiyo, nimakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Kata hiyo pia ya Kilwa-Vunjo, fedha zitakwenda wakati wowote ili kituo hicho kiweze kujengwa.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka pesa katika Kituo cha Afya Kata ya Udekwa kwa sababu wananchi wanatembea umbali mrefu sana kufuata matibabu mpaka Ilula zaidi ya kilometa 50? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, moja ya vigezo vya kupeleka vituo vya afya katika kata za kimkakati ni umbali mkubwa wa kituo cha afya au kata ambayo inahitaji kituo hicho kutoka Kituo cha afya kilicho jirani zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Ritta Kabati kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kata ya Udekwa na tutakwenda kufanya tathmini ikiwa kinakidhi vigezo vya idadi ya wananchi na umbali wa kilometa 50,

basi tutaona namna ya kuweka kwenye mpango mkakati kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa kutoa shilingi milioni 250 tayari sisi tumeshazipokea kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Busolwa. Swali; ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyuma ama jengo la mama na mtoto kwenye Kituo cha Afya Nyijundu pamoja na Kafita? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Amar kwamba jimbo lake tayari wameshapokea shilingi milioni 250 ambazo zilikuwa ni ahadi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa majimbo yote 214. Hii ni habari njema kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa majimbo haya ambao wameanza kupata hizo fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie kwanza Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa jambo hili limekuwa likifuatiliwa mara kwa mara kwamba Serikali imeanza kupeleka fedha hizo tuwe na Subira, lakini tuendelee kuwasiliana na wakurugenzi wa halmashauri kuona kama fedha zimeingia kwa ajili ya kuanza utekelezaji mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ikiwa vituo hivyo vinakidhi vigezo vya kata za kimkakati, Serikali kwa awamu itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo hivyo. Kwa hivyo ninaomba awasilishe kata hizo na sisi tutazifanyia kazi kuona kama zinakidhi vigezo ili kazi za ujenzi zianze kutekelezwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 340

Kukamilika kwa Kituo cha Afya Mwasayi - Maswa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Mwasayi ambacho kimepelekewa vifaatiba lakini hakina majengo ya kutosha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mwasayi kilianza kutoa huduma katika ngazi ya zahanati mwaka 1962 na kupandishwa hadhi mwaka 1977 na kuanza kutoa huduma ngazi ya kituo cha afya. Aidha, majengo ya kituo hiki ni machache na chakavu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi na jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Mwasayi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga na kupeleka fedha kwenye halmashauri zote nchini kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu iliyosalia ili vituo vya afya viweze kutoa huduma stahiki.

SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali na kuishukuru kwa kupeleka fedha hizo shilingi milioni 250 na asubuhi hii nimehakikisha kupitia Mkurugenzi wangu kwamba fedha hiyo imekwishafika. Kwa vile, wananchi wa Kata ya Zanzui

na Kata ya Kadoto pia wameshaanza ujenzi wa vituo viwili vya afya kwenye hizo kata; je, Serikali iko tayari kuunga mkono juhudi za wananchi hao? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita siku zote imekuwa tayari kuwaunga mkono wananchi katika ujenzi wa vituo vya huduma ya afya, kama ambavyo tayari imeshapeleka shilingi milioni 250 kwenye Kituo cha Afya cha Mwasayi. Nimhakikishie, katika Kata hizo za Zanzui na hiyo nyingine ambayo ameitaja tutahakikisha pia tunaanza kutenga fedha kwenye bajeti zetu kwa ajili ya kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vituo hivyo vya afya kwa awamu. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Makorongo kilianza kutumika miaka 10 iliyopita kikiwa hakina majengo ya *OPD* na maabara. Ninataka kujua ni lini Serikali itatoa fedha ili kukamilisha ujenzi huo? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba vipo vituo vya afya ambavyo vimeanza kutoa huduma, lakini vina upungufu wa majengo muhimu kwa ajili ya huduma hizo kikiwepo kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Chemba amekitaja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba, tayari Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulishaainisha vituo vya afya vyenye majengo pungufu na vituo vya afya chakavu na kongwe 203 na tayari tumeanza kuandaa bajeti kwa awamu kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo vya afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge, majengo hayo ya maabara, wodi ya wanawake, wanaume na majengo mengine yatakwenda kujengwa kwenye kituo hicho cha afya. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake.

Na. 341

Hitaji la Shule ya Sekondari Kata ya Kanindo – Ulyankulu

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga sekondari nyingine katika Kata ya Kanindo kwa kuwa Shule ya Sekondari Kanindo ina wanafunzi wengi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Kanindo ina wanafunzi 648 wa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne wakijumuisha wavulana 255 na wasichana 393.

Mheshimiwa Spika, shule hiyo ina vyumba vya madarasa 19 ambavyo vinatosheleza mahitaji kwa wanafunzi waliopo. Aidha, shule ina hosteli inayohudumia wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali kikiwemo Kijiji cha Mbeta. Vilevile, baadhi ya wanafunzi wamehamishiwa shule mpya ya Ikonongo kwa lengo la kuwapunguzia mwendo mrefu wa kutembea.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Majibu ya Serikali yanadhihirisha kwamba hitaji la kujengewa sekondari mpya katika Kata ya Kanindo liko palepale kutokana na sababu kwamba tayari kwenye majibu ya Serikali yanasema kuna wanafunzi wamehamishwa kutoka Shule ya Sekondari Kanindo na kupelekwa Shule ya Sekondari Ikonongo ambayo ipo kata nyingine ya Milambo, lakini bado wanafunzi wanaosoma hapo wanatembea umbali mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kutoka Kijiji cha Mbeta mpaka ilipo shule ya Sekondari Kanindo ni kilometa 15, lakini kuna vijiji vingine tena vinne ambavyo ni kilometa kuanzia 16 mpaka 20 kufikia shule. Swali la kwanza; je, Serikali sasa haioni kuna haja ya kuwaunga mkono hao wananchi ambao tayari wameshatenga ekari 20 kwa ajili ya ujenzi wa sekondari hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Rehema umeshaanza swali la pili au bado ni la kwanza?

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, la kwanza.

SPIKA: Mheshimiwa, la kwanza umeshatoa maelezo mwanzo na swali umeshauliza, sasa nenda kwenye swali la pili.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa shule hiyo ina hosteli ambayo ilijengwa na shirika la *UN,* bweni lenyewe ni moja ambalo lina uwezo wa kuwa-*accommodate* wanafunzi 48 tu. Je, Serikali iko tayari sasa wakati tukiendelea kusubiri ujenzi wa shule mpya kutujengea hosteli zingine ili wanafunzi wanaotoka mbali waweze kusoma katika mazingira ambayo mi karibu na nyumbani kwao? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Rehema Migilla kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha inaendelea

kuboresha sekta hii muhimu ya elimu msingi. Katika kipindi cha miaka minne katika Jimbo la Ulyankulu imejenga shule za sekondari nne na mipango ya kuendeleza miundombinu kwa kujenga shule nyingine bado ipo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Rehema Migilla kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha inaleta fedha katika Jimbo hili la Ulyankulu kwa ajili ya kuendelea kujenga shule ambazo zitaweza kuwatosheleza wananchi wako ili vijana waweze kupata sehemu ya kuendelea kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake kuhusu ujenzi wa hosteli. Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo itaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba kwa kushirikiana pia na wananchi (wazazi wa wanafunzi) kujenga hosteli ili ziweze kuwasaidia wanafunzi wetu na hasa wale ambao wanasafiri umbali mrefu, kwa maana Serikali msingi mzima wa kujenga shule hizi za kata ni kuhakikisha kwamba zinapunguza msongamano kwenye maeneo ambayo wanafunzi ni wengi, lakini pia inapunguza umbali mrefu wa wanafunzi kutembea kufika katika shule.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada hizi mbili ili kuhakikisha kwamba inaendelea kujenga hizi shule ambazo zitaweza kuwawezesha wanafunzi katika Jimbo lako la Ulyankulu waweze kupata sehemu nzuri ya kujifunzia.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwenye Wilaya ya Kilindi, Kata ya Msanja ndiyo kata yenye idadi kubwa ya wananchi, lakini ina shule ya sekondari moja. Je, nini mpango wa Serikali wa kujenga shule mpya? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, katika

kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, shule 2,441 zimejengwa za sekondari. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Omari Kigua kwamba hata katika Kata hii ya Msanja ambapo kuna uhitaji wa shule mpya hii ya sekondari ya kata, nimhakikishie Serikali kupitia mpango wake wa kutenga fedha kila mwaka wa bajeti itafika ili kuhakikisha shule hiyo imejengwa ili kupunguza msongamano, lakini pia kupunguza umbali mrefu ambao wanafunzi wetu wanatembea kufika shuleni. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Serikali itajenga shule ya sekondari katika Kata ya Makangarawe ndani ya Jimbo la Temeke? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na jitihada kubwa sana za kuendelea kuimarisha miundombinu katika Sekta ya Elimu na hasa kuhakikisha pia, inaongeza ujenzi wa shule za sekondari. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dorothy Kilave kwamba, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halamashauri na kupitia fedha kutoka Serikali Kuu itafika katika eneo alilolitaja la Makangarawe, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, shule hii inajengwa, ili iweze kuwanufaisha wanafunzi wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, kuna wanafunzi wa sekondari zaidi ya 100 kutoka katika Visiwa vya Buguma, Sozia na Nafuba. Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi wa visiwa hivi kukamilisha ujenzi wa shule ya sekondari katika Kisiwa cha Nafuba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuboresha Sekta ya Elimu Msingi kwa kuhakikisha, miongoni mwa mambo mengine, inajenga miundombinu ya shule. Katika eneo la visiwa ambalo Mheshimiwa Mbunge Charles Kajege amelitaja, ninaomba nimhakikishie kwamba, tutaendelea kuhakikisha fedha zinafika. Kila mwaka wa bajeti tutatenga fedha na zinafika, kwa ajili ya kuhakikisha shule katika maeneo hayo zinajengwa ili watoto wa wananchi katika visiwa hivi na wenyewe waweze kupata shule, kwa ajili ya kupata elimu. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari Shambalai, Mlongwema na Ubiri hazina uzio. Je, ni lini Serikali itajenga uzio katika shule hizo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga uzio katika shule zetu, kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa wanafunzi na usalama wa mali za shule. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Shabani Shekilindi kwamba, kupitia mapato ya ndani ya halmashauri tutajenga uzio katika shule alizozitaja, kwa ajili ya kuhakikisha usalama huo wa wanafunzi unapatikana na pia wa mali za shule.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 342

Kurejesha Mto Kondoa Kwenye Njia ya Asili

MHE. ALLY J. MAKOA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kazi ya kurejesha Mto Kondoa katika njia yake ya asili?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* imefanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kubaini chanzo cha kuhama kwa Mto Kondoa. Miongoni mwa sababu zilizobainika ni pamoja na uwepo wa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu, kama vile ufugaji, kilimo, ujenzi na uchimbaji wa madini ndani ya meta 60 zinazosababisha kuongezeka kwa upana wa kingo za mto na kupungua kwa kina kutokana na kujaa kwa udongo ndani ya wa mto. Hali hii imesababisha wakati wa mvua maji kuacha njia yake ya asili na kuelekea kwenye maeneo mengine na kuleta uharibifu wa mashamba na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari hizo, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma, kuhamasisha jamii kuacha kufanya shughuli zisizo endelevu ndani ya meta 60 za mto husika, ili kupunguza tatizo la kuhama kwa mto huo mara kwa mara. Aidha, ninaomba kutoa rai kwa wananchi kuendelea kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, wanapofanya shughuli za kibinadamu ili kukabiliana na uharibifu wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ally Juma Makoa, swali la nyongeza.

MHE. ALLY J. MAKOA: Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, tayari athari zimetokea, sasa ni nini mpango wa Serikali sasa kuhakikisha mto huo unarejeshwa kwenye mkondo wake wa asili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, *NEMC* walifika kule, ninataka kujua sasa, walikuja na suluhisho gani kurejesha ule mto katika mkondo wake wa asili, ili kuepusha madhara ya uharibifu ambayo yanaendelea kutokea kwenye mali za wananchi pamoja na miundombinu ya Serikali? Ninashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Makoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo mpango ambao, kama Serikali, tumeshaanza kuuandaa, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunaokoa huu Mto Kondoa. Moja ni kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais *(NEMC)* kwa kushirikiana na halmashauri, tayari kupitia bajeti ambayo tumeisoma tutahakikisha tunatenga fedha kwa lengo na madhumuni ya kuweza kufanya baadhi ya mambo katika mto huu, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu. Kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba, tunaufufua mto huu kwa kutoa mchanga na vitu vingine, ili mto huu urudi kwenye asili yake.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi wa Jimbo hilo la Kondoa waendelee kuwa na subira. Fedha hizi zitakapokuwa tayari basi tutahakikisha kwamba, tunazipeleka, kwa ajili ya kuokoa hiyo hali.

Mheshimiwa Spika, lipo suluhisho ambalo tumeshalifikia; la kwanza ni kutafuta fedha, kama hatujapata fedha hatuwezi kufanya hili jambo. Kwa hiyo, tutakapopata fedha tutahakikisha kwamba, tunakwenda kutoa elimu na tutahakikisha kwamba,

tunakwenda kufanya baadhi ya mambo ikiwemo kurejesha mto huu katika hali kwa sababu, changamoto kubwa ya mto huu ni pamoja na kutuama kwa mchanga na kupanuka kwa mto siku hadi siku. Ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mabadiliko ya tabia-nchi ni janga la Kitaifa ambalo linaathiri sehemu tofauti, ikiwemo Zanzibar na huku Tanzania Bara. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Serikali ya Zanzibar zitapeleka fedha lini, ili kusaidia kuondoa matatizo hayo ya tabianchi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, zipo juhudi nyingi sana ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, tumekuwa tunashirikiana kwenye hatua mbalimbali za kutafuta fedha, kwa ajili ya kukabiliana na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Fedha hizo, baadhi zimeshapatikana na ndiyo maana kuna miradi mingi tumeianzisha kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo imeanzishwa Zanzibar, Unguja na Pemba, ikiwemo mikubwa ya kukabiliana na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, hasa miradi ya kurejesha ardhi, ambayo imekata tamaa, miradi ya mifugo, miradi ya maji, miradi ya ujenzi wa kuta na miradi mingine mbalimbali. Ninamwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kushirikiana kutafuta fedha na hata tunapokwenda kwenye vikao vikubwa vya Kimataifa, vya kwenda kutafuta fedha za mabadiliko ya tabianchi huwa tunawashirikisha wenzetu wa Zanzibar kwa lengo na madhumuni ya tunapopata tuhakikishe na kule tunapeleka, kwa ajili ya kutengeneza miradi hiyo. Ninakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Assenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itafukua Mto Lumemo na kuboresha tuta la Mto Lumemo, upande wa Kata ya Lumemo, ili kupunguza athari za mafuriko kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga Abubakari wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika shilingi bilioni 81 ambazo Waheshimiwa Wabunge wametuidhinishia katika bajeti ambayo tumeisoma mwezi uliopita, tarehe 25, Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, miongoni mwa kazi ambazo tunakwenda kuzifanya ni kuhakikisha kwamba, kwanza tunakwenda kusafisha mito ambayo imekuwa ni changamoto, hasa kipindi hiki cha mvua na kile kipindi kingine ambacho mito huwa inajaa mchanga na mambo mengine. Kikubwa zaidi ni, fedha zile tunakwenda kuzitumia, kwa ajili ya kujenga kuta mbalimbali, ikiwemo maeneo ya huko Kilombero, Nungwi, Mtwara, Lindi na maeneo mengine yenye changamoto ambazo hizi kuta zinahitajika zijengwe. Tunakwenda kufanya hiyo kazi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto iliyopo Mto Kondoa inafanana na ile iliyopo Mto Ruvuma. Sasahivi Mto Ruvuma unahama njia yake ya asili na hivyo kuleta madhara katika Vijiji vya Maembe Chini, Kitaya na Kilambo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na tatizo hilo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Ni kwamba, kama nilivyoeleza katika majibu yaliyopita, changamoto kubwa ni tunatafuta fedha; fedha zitakapopatikana tunakwenda kutatua changamoto ya mito yote Tanzania, ama mito yote ambayo imeleta changamoto, hasa kile kipindi cha mvua kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, changomoto hizi za mito hii, ukiachia mbali mvua kubwa ambayo inanyesha, bado kuna baadhi ya wananchi wanasababisha. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane hili; kwamba, tuendelee kuwaambia wananchi wetu wasifanye shughuli za kibinadamu katika vyanzo hivi vya maji. Aidha, wazingatie Sheria yetu, ile ya Mazingira, sheria ya mita 60. Wafanye, lakini mbali kidogo kwa lengo na madhumuni ya mito hii ibakie kuwa salama, kwa ajili ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Ninakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, ninafurahia sana majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. La kwangu ni, sisi Sikonge 100% ni wana mazingira na tuna mambo mengi ya kujadiliana ana kwa ana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Tangu Wizara hii ianzishwe hajawahi kutembelea Sikonge. Je, lini atatembelea Sikonge, ili tukae kwa pamoja tumwoneshe, kwa maneno mengine tujadili kwa pamoja?

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mbunge, wewe si ndiyo uko kwa niaba ya Wanasikonge? Si ukae tu na Mheshimiwa Naibu Waziri? Au kuna changamoto maalum inayohusu mito ili ndiyo nijue sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu, ama? *(Makofi)*

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, mito yetu mingi *perennial* inakauka. Sasa kuna mambo mengi ya kujadili na yeye kuyaona ili tuweze kupata *solution*. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, pokea ombi hilo la Mheshimiwa Kakunda.

Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, swali lake litaulizwa, kwa niaba yake na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally.

Na. 343

Viwanja vya Michezo Sekondari ya Ziba, Manonga

MHE. AZIZA S. ALLY K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Viwanja vya Michezo Sekondari ya Ziba, Manonga?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Prof. Kabudi, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inayo nia ya dhati ya kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo katika shule zote nchini kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Michezo kwa sasa huzalisha ajira kwa vijana, hulitangaza Taifa Kimataifa pamoja na kuliletea heshima. Hivyo, ninakiri uwekezaji katika viwanja vya michezo shuleni ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara haina bajeti ya kuwezesha ujenzi wa viwanja katika Shule ya Sekondari Ziba,

iliyopo Manonga. Wizara ipo tayari kutuma wataalam katika shule hiyo, kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa miundombinu ya viwanja. Aidha, Wizara inaushauri Uongozi wa Shule ya Sekondari Ziba kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Tabora ambao ni wadau wakubwa wa Wizara katika Sekta ya Michezo, ili kufanikisha ukarabati wa viwanja vya michezo shuleni, ikiwemo Shule ya Sekondari ya Ziba. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, swali la nyongeza.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali inatambua Shule ya Ziba ni shule mojawapo ya wasichana ambao wanacheza mpira wa miguu na ndiyo inayotoa vipaji mbalimbali katika shule Kitaifa na kuwakilisha uchezaji wa mpira wa miguu Kimataifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kujali viwanja katika shule mbalimbali nchini; viwanja pamoja na michezo kwa kuwa, michezo ni biashara kubwa sana katika nchi yetu, ili iweze kutoa vipaji mbalimbali vya vijana watakaoenda kucheza Kimataifa? Ninashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali inaipongeza sana Shule ya Sekondari ya Ziba, ambayo imefanya vizuri sana katika kulea vipaji vya watoto wa kike, wasichana, katika michezo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mchezo wa mpira. Kwa kuzingatia hilo Wizara itatuma wataalam kwenda katika Shule hiyo ya Ziba ili kuona ni jinsi gani watashirikiana, lakini pia, pamoja na Mbunge wa Manonga, ili kuendeleza vipaji hivyo ambavyo ni muhimu kwa Taifa letu na kuona uwezekano wa tutakapokuwa na *academy* ya michezo, ambayo inajengwa Malya katika Mkoa wa Mwanza, ishirikiane vipi na Shule ya Sekondari ya Ziba na shule nyingine ambazo zina wasichana wenye vipaji kama hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa viwanja vya michezo katika shule. Wizara na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inachambua kuona umuhimu wa kuwa na mpango maalum wa kuweza kuboresha viwanja vya michezo katika shule zote za msingi na sekondari. Hivyo, halmashauri zetu za wilaya, za manispaa na majiji zinatakiwa, katika bajeti zao, ziweke umuhimu katika ujenzi wa viwanja katika shule za msingi na shule za sekondari.

SPIKA: Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Songwe ni mkoa mpya, ambao hauna uwanja wa michezo, kama vile ulivyo Uwanja wa Sokoine Mbeya. Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa michezo katika mkoa huo na Makao Makuu ya Mkoa pale Vwawa? Ahsante.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Waziri, wakati Mheshimiwa Mulugo anauliza ametutaja hapo, Sokoine; lakini Uwanja wa Sokoine una hali mbaya sana. Kwa hiyo, uyajibu yote mawili. *(Makofi)*

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ninatambua hali ya Uwanja wa Sokoine na mahitaji ya viwanja katika sehemu mbalimbali za Tanzania; Serikali imewekeza fedha nyingi katika miundombinu ya michezo. Kama mnavyofahamu tunajenga uwanja mpya wa mpira wenye uwezo wa kuchukua watu 32,000 kule Arusha, tunajenga mwingine hapa Dodoma wenye uwezo huohuo. Tayari katika bajeti ambayo imekwishapitishwa tunaanza uchambuzi yakinifu wa kujenga viwanja vingine katika sehemu mbalimbali za Tanzania vipatavyo 26. Ninaamini kabisa katika hilo, Songwe inaweza kuwa mojawapo ya mikoa, kama itakidhi viwango vitakavyokuwa vimewekwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwanja wa Sokoine, nao umo katika mpango wa kuangaliwa tutakapokuwa tumeanzisha Wakala wa Miundombinu ya Michezo, ili kuhakikisha sasa viwanja vyote Tanzania vinasimamiwa na Wakala huyo badala ya Wizara.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Wakala anaanzishwa lini, ili ndiyo tujue na sisi tutatazamwa miaka miwili, mitatu, minne inayokuja?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, tuombeane heri. *Inshallah* baada ya Oktoba. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hapo sasa inabidi ujibu tu swali letu la Wanambeya kwa kweli. Naona kuna Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa majibu mazuri kwa niaba ya Serikali, lakini ninapenda kuongeza kwamba, katika Maandalizi ya *AFCON,* 2027 Serikali imetenga viwanja vitano, ili vifanyiwe ukarabati. Viwanja hivyo ni Jamhuri, Morogoro; Mkwakwani, Tanga; Sokoine, Mbeya; CCM Kirumba, Mwanza; pamoja na Majimaji, Songea. Hivyo, Kiwanja cha Sokoine cha Mbeya kitaingia kwenye programu ya ukarabati wa viwanja, kwa ajili ya Mazoezi ya *AFCON,* 2027. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Rungwe tuna kiwanja kikubwa ambacho kinazungukwa na shule za sekondari mbili na chuo, kinaitwa Kiwanja cha Dkt. Tulia Ackson. Ni lini Serikali italeta fedha kukarabati kiwanja hicho? *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ninapenda kueleza kwamba, Wizara ina mkakati mkubwa sana wa kuboresha viwanja vyote nchini. Kutegemeana na upatikanaji wa rasilimali fedha tutahakikisha viwanja hivyo vinatengenezwa au vinakarabatiwa, ikiwa ni pamoja na kiwanja hicho kinachobeba jina la Mheshimiwa Dkt.

Tulia Ackson Mwansasu. Uwezekano upo wa kuangalia kama kinakidhi viwango vya kuwa Kambi ya Kitaifa ya Mashindano ya UMITASHUMITA na UMISETA, kikikidhi viwango hivyo, basi ukarabati wa kiwanja hicho utafanywa haraka sana, ili kuenzi jina la huyo ambaye kiwanja hicho amepewa. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbulu ni chimbuko la wanamichezo nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa pamoja na Sekta Binafsi kwa kuwa, Uwanja wa *Nyerere Stadium* katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu unamilikiwa na taasisi binafsi? Ninakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Issaay kwa kufuatilia sana maendeleo ya michezo, hasa katika Mkoa wa Manyara, ambao unafahamika kuwa na sifa ya kutoa wanariadha wengi. Kwa kutambua hilo, Baraza la Michezo la Taifa limenunua ardhi kubwa Babati, ili kujenga kituo cha kufanya mazoezi, kwa ajili ya wanariadha; ambacho kitatumika, kwa ajili ya Mkoa wa Manyara na wanariadha wote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la hicho kiwanja, kama nilivyosema, tunakuja na mkakati wa kuboresha viwanja vyote ikiwa ni pamoja sasa na kuwa na menejimenti kamili ya usimamizi wa viwanja. Kwa sababu tunaendelea katika hilo, ninaamini kabisa Manyara na Kiwanja hicho cha Mbulu, itapewa kipaumbele. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Na. 344

Kufufua Kiwanda cha Kahawa *Ngara Arab Globe*

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y. MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha *Ngara Arab Globe* cha kuchakata Kahawa ghafi, ili kuongeza thamani ya Zao la Kahawa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha kuchakata kahawa cha *Ngara Arab Globe International Limited* ni kiwanda cha wawekezaji (Sekta Binafsi) kinachomilikiwa na Watanzania na Wanyarwanda. Hata hivyo, kiwanda hiki kwa sasa hakifanyi kazi kutokana na changamoto ya Wawekezaji kushindwa kuhimili ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, Serikali imechukua hatua ya kukutana na wawekezaji wa kiwanda na kuwashauri kutafuta wabia wenye nia na uwezo wa kuwekeza katika Sekta ya Kahawa.

SPIKA: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Kahawa ya Tanzania imekuwa ikiuzwa nje, ikiwa bado ni ghafi bado haijawa *processed*, sasa ninataka kuuliza; je, Serikali ina mpango gani wakuwavutia au kuwakaribisha wawekezaji waje kuwekeza kwenye viwanda ili kahawa ya Tanzania iweze kupanda bei?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuwafanya wawekezaji wawe karibu sana na nchi yetu, kwa maana ya kufanya maboresho mbalimbali. Ndiyo maana katika kiwanda hiki tumekaa na wawekezaji waliowekeza ambao kimsingi uwezo wao ni mdogo na kuwashawishi waweze kuingia ubia na watu wenye uwezo ili kuhakikisha kwamba kahawa yetu inapata ufanisi wa kutosha katika maboresho ya hatua za awali kabla ya kuingia kwenye soko.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, sasa aulize swali lake.

Na. 345

Ujenzi wa Uzio wa Umeme Reli ya *SGR*

MHE. MAULID SALEH ALI aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga uzio wa umeme kwenye Reli ya *SGR* kutoka Ngerengere hadi Dodoma?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli *(TRC)* ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa ujenzi wa uzio katika

mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa *(SGR)* kwa kipande cha Morogoro hadi Dodoma. Hivi sasa, ujenzi wa uzio huo umefikia 95.12%. *TRC* inaendelea kumsimamia mkandarasi ili kuhakikisha kazi hiyo inakamilika kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, swali la nyongeza.

MHE. MAULID SALEH ALI: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; nitauliza swali moja. Kutokana kwa kuhamasika kwa wananchi kutumia usafiri wa treni ya *SGR*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza *route* zake kutoka Dodoma – Dar es Salaam?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, kwa swali lake la nyongeza. Ninakubaliana naye kwamba tangu usafiri wa treni ya *SGR* ulipoanzishwa mwamko umekuwa ni mkubwa sana kwa Watanzania, wamefurahia huduma hii na mahitaji yameongezeka zaidi. Kutokana na hali hiyo tayari hivi ninavyozungumza timu ya wataalam imeshaanza kufanya kazi ili kuchambua na kutazama mahitaji halisi ili hatimaye sasa tuweze kufikiria tuanzishe *route* pengine ziwe lini. Kwa sababu ukiangalia *weekend* mahitaji yanakuwa makubwa zaidi kuliko katikati ya wiki; kwa hiyo wataalam wanafanya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Maulid na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao kimsingi wamekuwa wakifuatilia jambo hili, timu hiyo itakapokamilika tayari Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Mbarawa ameelekeza kwamba kazi hiyo ianze mara moja, *route* hizo ziongezwe. Jambo jema na zuri ni kwamba tayari Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, alikwishatupatia fedha na vitendea kazi vipo vya kutosha; kwa hiyo tunaamini kwamba kazi hiyo inakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Jijini Dar es Salaam, kupitia Lindi na Mtwara hadi Mbamba Bay? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, samahani, kutoka Dar es Salaam?

SPIKA: Kutoka Dar es Salaam, kupitia Mtwara mpaka Mbamba Bay.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Ndulane kwa swali lake zuri. Kwa sasa Serikali haijaanza upembuzi yakinifu wala usanifu wa kina kuhusiana na reli kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi. Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa reli ya kusini, yaani kutoka Mtwara *Port* kwenda mpaka Mbamba Bay kupitia matawi ya Liganga na Mchuchuma tayari tumeshakamilisha *study*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali ipo kwenye hatua ya utafutaji wa fedha ili kuweza kuunganisha kipande hicho kiweze kujengwa kwa njia ya *SGR;* na kutokana na umuhimu mkubwa wa makaa ya mawe ambayo tuna zaidi ya makaa ya mawe zaidi ya *metric tons* milioni 428, tuna chuma cha kutosha, lakini pia ni kutekeleza maoni ya waasisi wa nchi zetu hizi za Malawi, Tanzania pamoja na Msumbiji katika kuhakikisha kwamba tunaziunganisha kupitia Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi.

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ile ahadi yake ya kutengeneza reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam kwenda Kilimanjaro? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali lake Mheshimiwa Shally Raymond. Ni kweli kabisa

kwamba Serikali inao mpango wa kujenga reli ya kisasa *SGR* inayounganisha Tanga kwenda mpaka Arusha kuunganisha mpaka Musoma na hii ni kutokana na uwepo wa madini ya kutosha ya *nickel* kule Dutwa, madini ya magadisoda kule Engaruka pamoja na kule Minjingu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kueleza pia vizuri. Reli hii ya kisasa ni gharama kubwa sana kuijenga, kwa hiyo unapoamua kufanya maamuzi ya kujenga lazima uwe na uhakika na mzigo uliopo. Kipande hiki tayari tumeshajiridhisha mzigo upo wa kutosha. Kwa sasa tumeshakamilisha *study* tupo kwenye hatua za utafutaji wa fedha ili tukikamilisha tuweze kuanza kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajenga kilometa 2,300 kwa sasa hivi. Tuna kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, tuna kutoka Tabora mpaka Kigoma na tumeanza kutoka Uvinza mpaka Burundi. Hivyo sio rahisi tukafanya mambo yote kwa wakati mmoja, hizi kilometa 2,300 hakuna nchi Barani Afrika imewahi hata kufikiria na hivyo inaifanya nchi yetu na kumfanya Dkt. Samia, kuwa ndiye Rais, kinara wa reli ya kisasa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, reli hii ya kisasa anayoijenga Dkt. Samia, inamfanya kuwa ndiye Rais, kinara wa ujenzi wa reli ya kisasa Barani Afrika na kumfanya kuwa wa tano duniani. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuvumilie amalize kazi hii ambayo ameshaianza ili baadaye tuweze kuanza na sehemu hizo zingine ambazo kimsingi wamekuwa wakizihitaji.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 346

Kuimarisha Mawasiliano ya Simu Kaskazini Unguja

MHE. TAMIMA HAJI ABASS aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali kuimarisha mawasiliano ya simu kwenye vijiji vyenye changamoto ya huduma hiyo Mkoa wa Kaskazini Unguja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilitekeleza mradi wa kimkakati wa kufikisha mawasiliano katika Shehia 38 zilizokua na changamoto ya mawasiliano, ambapo jumla ya minara 42 ilijengwa kwa kushirikiana na mtoa huduma *Honora (YAS)*. Kati ya minara hiyo Mkoa wa Kaskazini Unguja ulinufaika kwa kujengewa minara 12. Mradi huu ulikamilika kikamilifu na kwasasa wananchi wananufaika na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge, ameuliza swali kuhusu jitihada za Serikali katika kutatua changamoto ya mawasiliano ya simu katika vijiji vya Mkoa wa Kaskazini Unguja, inaashiria kuwa bado kuna changamoto. Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini kwenye mkoa husika ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano. Endapo ikibainika kuwepo kwa tatizo la mawasiliano katika mkoa huo, utaingizwa katika zabuni ya miradi itakayotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

MHE. TAMIMA HAJI ABASS: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Kama alivyosema kama bado kuna changamoto, ni kweli. Je, yupo tayari tuambatane kwenda Kijiji cha Tazari kwenda kuona hali halisi na kutufanyia namna ya uharaka wa mawasiliano hayo? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Tamima. Kuhusiana na suala la utayari, kama tulivyoongea mara nyingi kuhusiana na hili eneo la Tazari Jimbo la Nungwi, tayari nimeagiza wataalam saa saba watamtafuta, wataongea kwa kina ili kupanga namna njema ya kwenda kufanya ziara. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza niruhusu nimpongeze Naibu Waziri kwa kutekeleza ahadi yake hapa Bungeni ya kuja Mtambwe, Kijiji cha Kidundo, na alikuja akakutana na wananchi. Je, ni lini utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri pale ama kujengewa minara, mradi wananchi wapate mawasiliano ya simu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, nipokee pongezi; ule mradi tayari upo kwenye mpango mzuri, kadri fedha tunavyozipata na yenyewe ipo kwenye mgawo, wanakuja kutekeleza. Nilijionea ile kadhia, kwa hiyo wananchi wale wanaletewa mawasiliano ya uhakika. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Hai bado kuna vijiji mbalimbali havina mtandao na wananchi wanapata tabu. Kwa mfano, Kata ya Kia, Mtakuja na Sanya Station. Pia Kata ya Masama Magharibi, Masama Kati,

Masama Mashariki na Machame Kaskazini Kijiji cha Uduru Mwana maeneo haya mtandao hakuna. Serikali ina mpango gani...

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha, hilo bado ni swali la nyongeza, vijiji vyote hivi? Haya uliza swali lako.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha vijiji hivi vinapata mawasiliano ya hakika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote tunayafikia na wananchi wa maeneo hayo yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, tunawapa mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu, kadri tunavyopata fedha, hasa mwaka ujao wa fedha, tutahakikisha wataalam wanakuja wanafanya tathmini ya ukubwa wa changamoto; na nimhakikishie kuwa tutajenga minara na kuleta mawasiliano ya uhakika. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bunda Mjini, Kata ya Mcharo, Mtaa wa Kiharagweta mawasiliano ya simu yapo chini sana. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba inaboresha mawasiliano katika maeneo hayo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maboto. Hapa kati ya mji kama mawasiliano yapo hafifu tutatuma wataalam wetu kuja kupima, kufanya tathmini ya changamoto. Hapa ninaona ni suala tu la uboreshaji na ku-

upgrade. Kama ni *2G* tuweke angalau *3G*, *4G* ili mawasiliano yaweze kupatikana. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na mpango wa kupeleka mawasiliano katika Kata ya Kihanga na imefanikiwa kupeleka katika Kijiji cha Igangidung'u lakini bado Kijiji cha Makombe. Je, ni lini sasa Serikali itatupelekea mawasiliano huko Makombe? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Kijiji cha Makombe nacho tutakiweka katika mpango kazi wa mwaka ujao wa fedha, kadri fedha zitakavyopatikana. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, Mbunge wa Kwimba, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

Na. 347

Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Magu - Hungumalwa

MHE. PAULINE P. GEKUL K.n.y. MHE. SHANIF M. JAMAL aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Barabara ya Magu – Ngudu – Hungumarwa kilometa 10 ambapo Mkataba ulishasainiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Isandula - Magu kwenda Bukwimba - Ngudu hadi Hungumalwa yenye urefu wa kilometa 50 sehemu ya Isandula - Bukwimba *Station* kilometa 10 ulishaanza na utekelezaji wake umefikia asilimia tano. Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya malipo ya awali ili mkandarasi aweze kuendelea na kazi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kazi inayoendelea Kwimba; lakini nina maswali mawili ya nyongeza yanayotoka Babati. Swali la kwanza; Mradi wa *Bypass* wa Babati ulipositishwa wakasema wananchi wale waliyoathirika Serikali itafikiria kuwalipa fidia na wananchi wameandika barua *TANROADS*. Je, ni lini wananchi wale waliyoathirika na Mradi wa *Bypass* Babati Serikali itawalipa fidia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya Babati – Kiteto – Simanjiro imechukua zaidi ya miaka 10 Serikali imekuwa ikijenga taratibu. Wananchi wa Manyara wamekuwa wakiathirika, wanapita Arusha na Kondoa. Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Singe – Kiteto – Simanjiro utakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, nitaomba Mheshimiwa Mbunge kama atapata nafasi niweze kulifanyia kazi kwa usahihi zaidi kuhusu fidia na hasa baada ya kuona *Bypass* ambayo ilikuwa imeainishwa. Kwa sasa tumesitisha ili niweze kujua kwenye fidia tumefikia hatua gani kuhusu madai ya wananchi wa Babati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili linalohusu Barabara ya Babati kwenda Kiteto; tunajenga kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuijenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami kwa sababu usanifu umeshakamilika. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, mvua zinazoendelea kunyesha kwenye maeneo ya Kaskazini, hasa Mkoa wa Tanga, zimeathiri sana miundombinu ya barabara na kukatisha mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo. Je, Serikali ina kauli ipi juu ya hali hii? Ninakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli, mvua nyingi zinanyesha Mikoa ya Kaskazini, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Morogoro, Lindi pamoja na Rukwa; kuna mvua nyingi sana. Miundombinu kwa kweli imeathirika sana na hasa kwenye barabara ambazo ni za changarawe.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi tumeshaomba fedha kwa ajili ya fedha ya dharura ili kurejesha mawasiliano kabla ya kuanza kufanya matengenezo ya kawaida ambayo fedha tumeshatenga, lakini tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mawasiliano yaliyokatika yanarejeshwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mogitu – Haydom usanifu wa kina na upembuzi yakinifu umekamilika kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Je, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 barabara ile itafanyiwa kazi gani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara tumekamilisha. Mheshimiwa Mbunge kama ataangalia kitabu tumeiweka kwenye mpango kwa mwaka ujao. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 348

Ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi Tarafa ya Ilagala – Uvinza

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Malagarasi katika Tarafa ya Ilagala – Uvinza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Malagarasi ya Chini lenye urefu wa mita 200 katika Barabara ya Simbo – Ilagala hadi Kalya yenye urefu wa kilometa 234 imekamilika. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru kwa majibu yake ya kujirudiarudia, hii ni mara ya nne nikiwa ninauliza swali hili. Swali la kwanza, ninaomba kujua utekelezaji huu utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; daraja hili lina manufaa ya kiuchumi na kijamii katika Mkoa wa Kigoma. Je, hawaoni kuwa kuna haja ya kufanya haraka?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Kigoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, atakubaliana nami hapa hapakuwa na Daraja, tulikuwa tunavusha kwa vivuko, tumeshasanifu tumeshakamilisha. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge daraja hili litagharimu shilingi bilioni 24 na bahati nzuri ni kati ya madaraja ambayo yanaenda kutekelezwa kwa fedha ya *World Bank* na tunavyoongea sasa hivi *World Bank* wamesharidhia hizo hela zipatikane ili tuweze kujenga na kuacha na kivuko cha kwenda Kalya ambacho tunajua changamoto zilizokuwepo. Mheshimiwa Dkt. Samia, ametafuta fedha na tunakwenda kuanzisha hilo daraja muda si mrefu. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tija ya Bandari ya Ndumbi inategemea sana kukamilika kwa Barabara itakayojengwa kwa kiwango cha lami kutoka Rwanda hadi Ndumbi, barabara hiyo imeshasainiwa. Ni lini fedha itatolewa ili mkandarasi aanze kazi mara moja? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua umuhimu wa hiyo barabara na tayari tumeshapata mkandarasi tumeshasaini, tunachosubiri ni kumlipa huyo mkandarasi ili kazi ianze. Kwa kweli ameshaleta maombi ya malipo ya awali na Serikali tunatafuta fedha tumlipe ili kazi hiyo ianze ya kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami kutoka Rwanda hadi Ndumbi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, Barabara ya Chapwa - Chiwezi - Chindi - Msangano ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipotutembelea mwaka 2020. Ninataka kufahamu barabara hii imefikia hatua gani hasa katika ujenzi wa daraja katika mto uliopo pale Chindi? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Tutawasiliana na wenzetu wa *TARURA* kwa sababu hii barabara bado inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA* tujue wapi Serikali imefikia katika kuitekeleza hii ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 349

Ujenzi wa Barabara ya Morogoro hadi *Njombe Border*

MHE. GODWIN E. KUNAMBI aliuliza:-

Je, lini Mkandarasi atapatikana na kuanza ujenzi wa Barabara ya Morogoro hadi Njombe *Border* kutoka Ifakara hadi Chita?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke hadi Kibena yenye urefu wa kilometa 346.43 kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ambapo kwa sehemu ya Kwanza ya Ifakara – Mbingu (kilometa 62.5) ujenzi unaendelea na Mkandarasi wa sehemu ya Pili ya Mbingu – Chita (kilometa 37.5) ameanza maandalizi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya Kibena – Kidegembye (kilometa 42) taratibu za ununuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zipo katika hatua za mwisho. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea kwa sehemu ya Kihansi – Mlimba hadi Madeke yenye urefu wa kilometa 95.26. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru wewe binafsi, ulipata fursa ya kupita kwenye barabara hii wakati umetembelea jimboni kwangu, Mungu akubariki sana baada tu ya wewe kutembelea jimboni kwangu Serikali ililipa *part payment* ya mkandarasi wa kwanza. Ninaomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kipande hiki cha kutoka Ifakara hapa Mbingu kilometa 62.5, habari ya kwamba mkandarasi kazi inaendelea, sasa yapata miaka miwili mkandarasi yupo *site* tangu alipwe shilingi 5,000,000,000, bado nne tu anasema akilipwa aanze kazi. Ninaomba majibu ya uhakika ya Serikali, ni lini Serikali itamalizia hizo shilingi 4,000,000,000 ili mkandarasi huyu afanye kazi hiyo? Kwa sababu yupo *site* miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kipande cha kutoka Mbingu - Chita kilometa 37.5. Je, naye huyu mkandarasi atalipwa lini? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siku zote majibu ya Serikali ni ya uhakika na hata haya nitakayotoa ama niliyoyatoa ni ya uhakika. Kipande cha Ifakara – Mbingu kama alivyosema tumeshamlipa sehemu ya malipo mkandarasi ambaye yupo *site* na atakubaliana nami

kwamba kwa sasa kwa kweli eneo hilo mvua inanyesha nyingi na ni vigumu sana kwa mkandarasi kufanya kazi kubwa hasa zile tunazoita za *earth work*.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hali itakapotengamaa mkandarasi yupo *site* na ataendelea kufanya kazi. Kwa sasa nadhani atakubaliana nami anaendelea kuziba mashimo au kurudishia mawasiliano yanapokuwa yamekatika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipande cha pili, Mbingu - Chita kama alivyosema tayari mkandarasi tumeshampata na tumhakikishie kwamba tayari Wizara ya Fedha inafanya taratibu za kumlipa malipo ya awali ili naye aanze hiyo kazi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na niishukuru Serikali kwa kuridhia kutangaza Barabara ya Utegi - Shirati kwenda Kilongwe kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Pamoja na hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Barabara ya Kuruya – Kumoge- Kinesi ni lini upembuzi yakinifu ya barabara hii utakamilika kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimhakikishie Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya kwamba barabara aliyoitaja kwa mujibu wa taratibu za usanifu hakuna kitakachokwamisha kwa sababu haitegemei mvua ama hali ya hewa. Kwa mujibu wa mkataba ulivyo, tutahakikisha kwamba usanifu unakamilika kwa muda kama tulivyopanga kwenye mkataba. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ruanda – Iyula – Idiwili - Nyimbili hadi Vwawa ni lini wakandarasi wanawake watapatikana ili kuanza ujenzi? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa swali hili zuri na nilieleze Bunge kwamba katika hii awamu moja ya mambo ambayo tumeyafanya kwa barabara aliyouliza, ni Mheshimiwa Rais kuelekeza kwamba wakandarasi wanawake waweze kupewa kazi na hii barabara imegawanywa, ina kilomita 20 wale wakandarasi wote wanawake ambao watafanya wamepewa kilometa tano tano ambayo ndiyo hiyo barabara anayoongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyoongelea sasa hivi tupo kwenye hatua za manunuzi ili wakandarasi hao waanze kazi hiyo ya kujenga hiyo barabara ya kilometa 20. Kilometa moja imeshajengwa, lakini hizo kilometa 20 muda si mrefu zinaanza kujengwa na tuna hakika zitaanza kujengwa kabla ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 kwisha. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, Barabara ya Makete - Mbeya mvua inanyesha miezi nane katika mwaka mkandarasi hajalipwa hadi sasa hivi. Ni ipi kauli ya Serikali malipo kwa mkandarasi huyu, ili afanye kazi kwa uhakika na kwa wakati? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli ni eneo ambalo lina mvua muda wote ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zote ambazo wakandarasi wapo *site,* kama Wizara tumeshawasilisha maombi kwa maana ya mahitaji ya fedha ikiwemo hiyo barabara yake na tuna uhakika lazima tumlipe mapema ili hali ya hewa inavyokaa vizuri wakandarasi hao waanze kufanya kazi. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Gambo, nimekuona lakini umesimama baadaye, swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Barabara ya Arusha – Kibaya - Kongwa ambayo Arusha inategemea kujengewa kilometa 70. Je, ni lini mkandarasi atakwenda *site* maana mkataba ulishasainiwa tayari?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara hii ilikuwa ndio moja ya zile barabara ndefu za *EPC+F* na Serikali iliamua ianze kujenga kutokea Arusha ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba zile barabara ambazo zitatumika *AFCON* ziwe ni sehemu ya hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshasaini mkataba na mkandarasi na wakandarasi hao wapo wanapitia kwa sababu ilikuwa ni barabara ndefu kuzifupisha na kuziweka katika zile kilometa 70 ambazo zitajengwa na muda si mrefu tunategemea kwamba tutawalipa malipo ya awali ili waweze kuanza kazi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 350

Ushirikishwaji Wazee katika Shughuli za Uzalishaji Mali

MHE. BONNAH L. KAMOLI aliuliza:-

Je, namna gani Serikali inatekeleza takwa la Sera la ushirikishwaji wa Wazee katika shughuli za uzalishaji mali?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Wazee imetambua umuhimu wa wazee kushiriki katika shughuli za kiuchumi ili kuinua kipato chao. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeanzisha vikundi 395 vya uzalishaji mali vya wazee ambapo jumla ya wazee 10,926 (Me 5,333 na Ke 5,593) walinufaika na miradi mbalimbali ikiwemo ya kuwezeshwa kujihusisha na shughuli ndogo ndogo za kilimo cha mboga mboga, kuwa na vitalu vya miche ya matunda, ufugaji wa nyuki, mbuzi, ng'ombe na kuku.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa wito kwa wazee kutumia mazingira yao kufanya shughuli ndogondogo ambazo zinasaidia kuimarisha afya ya mwili na akili. Aidha, ninasisitiza jamii kuendelea kuunga mkono juhudi na shughuli zinazofanywa na wazee katika jamii zetu ili kuimarisha ustawi wao. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, swali la nyongeza.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa Serikali kwa kutoa majibu mazuri, lakini ninataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili. Swali la kwanza; programu ambazo zinafanyika zinaonekana kwamba zinafanyika kwa wazee waliopo Kijijini. Je, Serikali ina mpango gani na wazee ambao wanaishi mjini hasa Wazee wa Jimbo la Segerea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama tunavyojua kwenye programu nyingine ambazo zinaendelea kwa vijana pamoja na wanawake ambao wanapata 10%. Je, kwa nini, Serikali isianzishe programu ya kuwasaidia wazee ambao kama wanaopata vijana, wanawake na walemavu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inajali sana wazee na inatoa fursa kwa wazee wote haina ubaguzi. Niwaombe tu wazee wakiwemo na Wazee wa Segerea kutumia fursa hizi kuhakikisha wanaendelea kupata maisha yao na uwezeshaji wa kiuchumi katika familia zao na kupata faraja katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wazee na kupata fursa mbalimbali. Vilevile, sasa hivi kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii na kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunayo mikopo midogo midogo ambayo inawawezesha wananchi pamoja na wazee imechanganya watu wote kutumia fursa hizi waonane na Maafisa Maendeleo katika halmashauri zao ili kupata vitambulisho na kuchukua mikopo hiyo katika Benki za *NMB* ambayo tulishafunga nayo mikataba. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaweka mpango wezeshi kwa wazee katika Mkoa wa Mtwara ili kuwafanya wafanye shughuli ndogo ndogo za uzalishaji mali? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wazee na nimwombe Mheshimiwa Mbunge afike katika Ofisi ya Halmashauri Kuu ya Mtwara waonane na Maafisa Maendeleo ili wazee hao wapate elimu na waweze kujiwezesha kiuchumi na kupata fursa na maisha ya kujiendeleza ili waone umuhimu wa Serikali yao ya Awamu ya Sita. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa zile fedha za uwezeshaji kwa ajili ya akinamama pamoja na vijana na watu wenye ulemavu zinatoka kwenye Halmashauri zetu. Ni kwa nini, sasa Serikali isianze kutenga fedha kutoka kwenye Bajeti Kuu ya Serikali kwa ajili ya kuongeza nguvu ili yale makundi yaweze kupata fedha za kutosha katika biashara zao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Serikali inaendelea kutoa fursa mbalimbali kwa ajili ya kuwapa mikopo midogo midogo wafanyabiashara ndogo ndogo wakiwemo wazee.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema waende katika Halmashauri wakutane na Maafisa Maendeleo kuwapa elimu ili waweze kupata vitambulisho hivyo ili waweze kujiendesha na mifuko hiyo midogo midogo na biashara zao ziweze kukuwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kusikiliza maswali kutoka kwenu, lakini pia kupokea majibu kutoka upande wa Serikali. Kuna Mbunge amesimama pale nilikuwa ninasubiri aketi. Haya.

Tutaanza na wageni kwanza waliopo hapa Bungeni asubuhi hii, kisha yatakuja kwenu matangazo mengine.

Kwanza, ni wageni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii; wapo Dkt. Hassan Abbasi, ambaye ni Katibu Mkuu; Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia

Maliasili; na Ndugu Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Utalii. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Jenerali Mstaafu George Waitara, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA);* Meja Jenerali Mstaafu Hamis Semfuko, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*; Dkt. Oswald Masebo, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Makumbusho ya Taifa; Ndugu Dkt. David Manyanza, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori *(TAWIRI);* na Profesa Verdiana Masanja, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia Prof. Yunus Mgaya, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori *(MWEKA)*; Ndugu Iman Kajula, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Taifa cha Utalii; Dkt. Angela Mwakatobe, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora; Prof. Jafari Kidegesho, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania; Prof. Yonika Ngaga, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi; na Ndugu Said Kamugisha, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo vilevile CPA Christina Mongi, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Misitu Tanzania; Profesa Dos Santos Silayo, Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS);* Ndugu Mussa Kuji, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA);* Dkt. Elirehema Doriye, Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *((NCAA);* na Ndugu Mlage Kabange, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori *(TAWA)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Eblate Mjingo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Wanyapori Tanzania; Ndugu Ephraim Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania; Dkt. Noel Lwoga, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania; Dkt. Revocatus Mushumbusi, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu

Tanzania; na Dkt. Alex Lobora, Mkurugenzi wa Wanyamapori. Karibuni. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Irene Kikoti, Mbunge wa Bunge la Vijana la Afrika Mashariki, nilisita kidogo kumWita Mheshimiwa kwa sababu sijui kama na wao wanaitwa Waheshimiwa, karibu sana Bungeni lakini hapa ameandikwa Mheshimiwa kwa hiyo nisije nikahukumiwa, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Bunge la Vijana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ni Ndugu Mkuwe Issale, Mke wa Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu wa Wizara, sijui amekaa upande gani? Sawa, huyu wengine wanamfahamu kwa jina la *Mamy Baby*. Yupo pia mtoto wa Dkt. Hassan Abbas ambaye anaitwa Sabrina Abbas. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ni Madiwani wa Viti Maalum na Wenyeviti wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Wilaya ya Wanging'ombe na Ludewa Mkoa wa Njombe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia anao wageni wengine ambao ni viongozi wa kampuni ya *Pan African Tourism Board* wakiongezwa na Rais wa Bodi Ndugu Mariam Lesian. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao sasa wageni wengine ambao ni wageni wenu. Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, huyu ni mpigakura wake kutoka Songea Mkoani Ruvuma, Ndugu Magdalena Kitwana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejmenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni wapiga kura wake na wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambaye ni Ndugu Hakizimana Jean Dieu ambaye ni rafiki yake kutoka Kigali Nchini Rwanda. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ambaye ni Braison Tambu, mpiga kura wake kutoka Musoma Mkoani Mara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Riziki Said Lulinda ambaye ni Ndugu Bernard Mwanawile kutoka Taasisi ya Mazingira *(The Media and Climate Change Conservation Organization)* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Augustine Holle Vuma ambao ni viongozi wa kampuni ya *Alfredos Tours Limited,* wauzaji wa suti kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 41 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni Kwaya ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Ihimbo, kutoka Kata ya Ihimbo, Wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa, wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Ihimbo Mheshimiwa Hezron Nganyagwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni pia waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Kwanza ni wanafunzi 50 na Wahadhiri wawili wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* kutoka Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 72 na Walimu 20 wa Shule ya Msingi Padri Dinno kutoka Manyoni, Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 46 na Walimu wanne wa shule ya awali na msingi Austine kutoka Mpwapwa Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi wa Shule Ndugu Siana Lema. Karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi 45 wa Serikali ya wanafunzi wa Taasisi ya Uhasibu Arusha Kampasi ya Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba siku ya kesho Jumanne tarehe 20 Mei, 2025 kutakuwa na kikao cha Spika na Wabunge wote, Wabunge wote tunasisitizwa kuhudhuria kikao hicho ambacho kitafanyika kuanzia saa kumi. Kwa hiyo, ikiwa wapo Wabunge ambao hawapo Dodoma basi tafadhali mnaokaa nao jirani kwenye viti, tafadhali wajulisheni kesho wawe Dodoma saa kumi kutakuwa na kikao cha Wabunge wote.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, basi tunaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu wa Bunge, nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayo taarifa fupi kwa ajili ya Bunge kwa ajili ya jambo ambalo tulikuwa tumemwomba akalifanyie kazi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Ismani.

TAARIFA YA SERIKALI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, kufuatia Tangazo la Gazeti la Serikali la tarehe 28 Aprili, 2025 lenye *GN. No. 146* la Mwaka 2025, Serikali iliwasilisha Bungeni Taarifa ya Matoleo la Matangazo, yaani Hati pamoja na *GN. No. 146* siku ya tarehe 11 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha hapa Bungeni, wewe ulielekeza Serikali kukutana na Waheshimiwa Wabunge

wawili, Mbunge wa Kiteto na Mbunge wa Chemba ili wajiridhishe kama *GN* hiyo inatatua changamoto walizowahi kuwasilisha Bungeni kuhusiana na Pori la Akiba la Mkungunero hususani kuhusu mipaka mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano nao na baada ya kushauriana ndani ya Serikali, Serikali sikivu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeona ni busara kuondoa *GN* au hilo Tangazo la Serikali Namba 146 kwenye orodha ya Hati husika ili kuipa Serikali muda zaidi kuona namna bora za kutatua changamoto zilizojitokeza zinazohusu mipaka mipya baina ya Pori la Akiba la Mkungunero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa hii napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeondoa tangazo hilo rasmi. *(Makofi)*

(Tangazo la Serikali la Tarehe 28 Aprili, 2025 lenye GN. No. 146 la Mwaka 2025 liliondolewa Rasmi na Serikali)

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni taarifa fupi ya Mheshimiwa Waziri, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyopitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai, afya njema, usalama na amani katika Taifa letu na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza jukumu letu la msingi la kuipokea na kuijadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwelekeo wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kwa mara nyingine kusimamia Sekta ya Maliasili na Utalii. Ninaendelea kumwombea afya njema, hekima na nguvu zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa zaidi. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu, uwajibikaji, weledi na uzalendo mkubwa ili kuhakikisha kuwa sekta hii inazidi kuwa nguzo imara ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, ninaomba nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, wenye dira, hekima na maono ya maendeleo ya nchi yetu. Uongozi wake umeifanya nchi yetu kuendelea kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahenga wanasema: "Chanda Chema Huvikwa Pete" ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu ujao Oktoba, 2025. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia kila la kheri katika safari hii muhimu ya kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za dhati kabisa katika kuimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Aidha, ninampongeza kwa kupitishwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali. Uongozi wao madhubuti kabisa na maelekezo wanayoyatoa mara kwa mara yamewezesha kufanikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za Taifa na kuchochea ukuaji wa utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, ninaomba nikupongeze wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani,

kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu na kwa weledi, busara na hekima. Aidha, nikupongeze kwa kazi nzuri na ya mfano unayoendelea kuifanya katika Umoja wa Mabunge Duniani ambayo si tu unaitangaza Tanzania bali pia inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha majadiliano ya kidemokrasia na mshikamano wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kukusaidia kwa umahiri mkubwa katika kuendesha Shughuli za Bunge. Pia niwapongeze Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa umakini wao mkubwa katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii, nikizingatia kuwa umoja ni nguvu, niwapongeze Mawaziri wenzangu na Manaibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia kazi mbalimbali na kuwaletea Watanzania maendeleo kwa kasi kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi imara kabisa wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha sambamba na maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na hususan Wabunge wa Mkoa wa Njombe ninapotokea na Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na malikale pamoja na uendelezaji wa utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhamira ya dhati kabisa na nikizingatia kauli ya kwamba "Kidole Kimoja Hakivunji Chawa", ninawashukuru viongozi wenzangu na Watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kujituma kwao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Naibu Waziri kwa msaada mkubwa anaonipa na ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, ninapenda kumshukuru Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu; Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu (Maliasili); na Ndugu Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu (Utalii) kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, ambao leo umewatambulisha hapa, Wakuu wa Taasisi wote wa Wizara ambao wapo hapa, Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – *TANAPA*, *NCAA, TAWA, TFS, TAWIRI, AWM, PWTI*, Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga, *TAFORI, FTI, FWITC, BTI, FITI, TaFF, TTB, NCT, NMT* pamoja na Watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kimsingi, ushirikiano wao, weledi na kujituma kumefanikisha kwa kiasi kikubwa malengo tuliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninaishukuru familia yangu hususan watoto, Vantwa, Praisegod, Happy, Sullu, Princess, Sani, Matilda na wengine wote kwa namna wanavyonitia moyo, kuniombea ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Ninamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kuwalinda. Vilevile ninawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe 'Wanyalukolo' kwa ushirikiano na kutambua dhamana ya Taifa niliyokabidhiwa, ninawaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nanyi katika juhudi za kuleta maendeleo katika Mkoa wetu kwa maslahi mapana ya Taifa na leo baadhi yao waliotoka Njombe wapo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimpongeze kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kupelekea kwa mara nyingine tena kuchaguliwa kwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) Kanda ya Afrika Profesa Mohamed Janabi, hongera sana Watanzania na hongera Profesa Janabi na hongera sana sana viongozi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, Ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mheshimiwa Cleopa David Msuya. Tutaendelea kumkumbuka kwa umahiri wake mkubwa katika usimamizi na uwajibikaji katika kuleta maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kutoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani, Ukanda wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali inayoendelea nchini kutokana na matokeo ya uhifadhi na mwingiliano wa binadamu na wanyamapori, kwa unyenyekevu mkubwa ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki na wananchi waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wananchi ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati thabiti na madhubuti ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao. Kwa pamoja tunaweza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutambua mchango wa dhati wa Askari na Maafisa wa Jeshi la Uhifadhi ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri na weledi katika kulinda na kuhifadhi Maliasili za Taifa letu wakiwemo wanyamapori, nyuki na mali kale.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu huu fedha, baadhi ya askari hawa shupavu walipoteza maisha yao na wengine walipata majeraha wakiwa kazini wakitimiza wajibu wao kwa Taifa. Mashujaa wetu *CR III* Arafat Saidi Miyimba kutoka *TANAPA;* Askari wa Vijiji *(VGS)* Bwana Issa Manyinja wa *WMA* ya Magingo Wilaya ya Liwale; Bwana Masanja Michael wa *WMA* ya Uyumbu Wilaya ya Urambo; Bwana Felician Mgomela; Bwana Shakimu Mohamed na Bwana Boliva Betram Mapunda kutoka *TFS* kwa kweli walipoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, askari wengine 46 kutoka Taasisi za Uhifadhi za *TANAPA*, *NCAA, TAWA* na *TFS* walijeruhiwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Matukio haya yalitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na majangili waliovamia maeneo ya hifadhi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema wazazi wao, ndugu zao na tunazidi kutoa pole kwa majeruhi na Mungu azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, lakini tunazidi kutoa pole kwa waliopata majeraha. Mungu awajaalie waweze kupona haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, wakati ninawasilisha ninaomba nianze na mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri kabisa na shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwongoza Watalii Namba Moja nchini, Serikali imeendelea kutekeleza masuala

mbalimbali katika sekta za uhifadhi na utalii. Hakika tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika miaka hii minne na mwaka mmoja huu wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuainisha kwa muhtasari mafanikio ya kihistoria yasiyopungua 10 yaliyopatikana kutokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza; kuongezeka kwa idadi ya watalii. Mwaka huu historia imeandikwa; idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa 132.1% kutoka watalii 922,000 mwaka 2021 hadi watalii milioni 2.1 mwaka 2024. Aidha, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa 307% kutoka watalii 788,000 mwaka 2021 hadi kufikia watalii milioni 3.2 mwaka 2024. Hatua hii imewezesha idadi ya watalii kufika milioni 5.3. Ndiyo maana tulikuja na ile *plate number* T503 USD. Hapa tunasema tumefikia watalii milioni 5.3.

Mheshimiwa Spika, hii ni sawa na 107.2% ya lengo la watalii 5,000,000 kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya CCM ya Mwaka 2020; tuliambiwa fikisheni watalii 5,000,000. Hapa tunatangaza rasmi tumefikisha watalii 5,300,000. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rasmi sasa nieleze Bunge lako Tukufu kuwa kwa lengo la idadi ya watalii lililowekwa na Ilani, tumetekeleza ikiwa ni mwaka mmoja kabla ya muda kufika. Hongera kwetu sote Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa rekodi hizo pia, Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani *(UN Tourism),* limeitaja Tanzania kuwa nchi inayoongoza Afrika kwa mwaka 2024 kwa kuwa na ongezeko kubwa la watalii ikilinganishwa na kabla ya janga la UVIKO-19 ambapo utalii Tanzania ulikua kwa 48%, Ethiopia 40%, Morocco 35%, Kenya 11% na Tunisia 9%. Haya ni matokeo yaliyochagizwa na maono ya Mheshimiwa Rais na kujitoa kwake Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na hasa katika ile filamu ya *The Royal Tour* na ile ya *Amazing Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunapata *booking* za watalii mwaka 2026, 2027 na 2028. Tumeshaanza kupokea *booking*. Tunakushukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii (hili ni eneo lingine la pili). Siyo tu kuongezeka kwa watalii, lakini pia katika kipindi hiki, mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 sawa na ongezeko la 200% kwa watalii wa kimataifa. Hatua hii imeifanya Tanzania kwa mujibu wa *UN Tourism*, kushika nafasi ya tisa duniani na ya tatu Barani Afrika kwa ongezeko la mapato ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya UVIKO-19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali. Ninayo furaha na heshima pia kuonesha kwamba maduhuli ya Serikali nayo yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 397.42 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi shilingi bilioni 901 mwaka wa fedha 2023/2024. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kuanzia Julai 2024, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya shilingi bilioni 912.9 sawa na 94% ya lengo la makusanyo, kiwango ambacho ni kikubwa kuliko wakati wote kuwahi kupatikana katika historia ya sekta hii. Hii ni kutokana na uongozi bora wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kutokana na amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la nne; Tanzania imeendelea kutambulika na kung'ara kimataifa. Hapa tunasema, tumeweza kushinda tuzo mbalimbali za utalii katika Nyanja za kimataifa ikiwemo zile mashuhuri zaidi duniani katika Sekta ya Utalii ziitwazo *World Travel Awards* ambapo, katika mwaka mmoja uliopita Tanzania imeibuka kinara kama ifuatavyo; hapa ninaomba ku-*share* eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshinda Tuzo ya Dunia ya kuwa eneo linaloongoza duniani kwa utalii wa safari *(World's Leading Safari Destination, 2024)*. Pia, tumeshinda tuzo ya kuwa na eneo linalovutia zaidi kiutalii *(Africa's Leading Tourism Destination, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tumeshinda Tuzo ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuendelea kuwa hifadhi bora duniani kwa kipindi cha miaka sita mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2024. Tumeshinda Tuzo ya Mlima Kilimanjaro kuwa kivutio bora cha utalii Barani Afrika *(Africa's Leading Tourism Destination, 2024);* na tumeshinda Tuzo ya Tanzania kuendelea kuwa kinara. Hivyo niseme Tanzania kushinda kuwa mwenyeji wa Tuzo za Utalii Duniani Kanda ya Afrika na Bahari ya Hindi zitakazofanyika Dar es Salaam, Tanzania tarehe 28 Juni, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa niseme kwamba, sisi tumechaguliwa kuwa mwenyeji wa tuzo hizo, yaani badala ya kwenda kupokea tuzo katika nchi nyingine safari hii wao wanakuja kwetu Tanzania. Kwa hiyo, Tanzania tutakuwa mwenyeji wa tuzo za utalii duniani Kanda ya Afrika na Bahari ya Hindi zitakazofanyika Dar es Salaam, tarehe 28 Juni, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori. Kwa kweli haya ni mafanikio mengine na hapa kwa mujibu wa namba ni fanikio namba tano. Kupitia mikakati madhubuti ya kudhibiti ujangili, tumeendelea kuimarisha doria na matumizi ya teknolojia na tumeshuhudia ongezeko la idadi ya wanyamapori na hali ya usalama katika maeneo ya hifadhi kuliko wakati wowote duniani katika historia yetu.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni kwa mujibu wa tafiti za mashirika ya kimataifa kama *IUCN* na Taasisi yetu ya Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)*. Nchi yetu Tanzania imeendelea kuongoza Afrika na duniani kwa kuwa na idadi ya simba wapatao 17,000; lakini pia ikiongoza Afrika kwa nyati wapatao 225,000 na chui 24,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya sita; Serikali imeendelea kushuhudia kuimarika kwa biashara ya mazao ya misitu na nyuki nchini. Katika kipindi cha miaka mitano kumekuwa na ongezeko la kiwango cha uzalishaji wa malighafi mbao katika mashamba ya Serikali yanayolima miti kibiashara kutoka mita za ujazo milioni 1.1 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia mita za ujazo milioni 1.2 mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, kesho tutakuwa na siku ya nyuki duniani. Kwa heshima na taadhima, ninawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote katika Viwanja vya *Chinangali Park*. Karibuni sana Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge katika siku ya nyuki duniani hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya miti vimeongezeka kutoka viwanda vya kati na vikubwa. Awali tulikuwa na viwanda 636 mwaka 2020, lakini sasa tuna viwanda 1,671 mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi imeongezeka kufikia shilingi bilioni 458.47 mwaka 2024/2025 sawa na 333.8% ikilinganishwa na shilingi bilioni 105 mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa asali, hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani milioni 1.3 zilikuwa zinahitajika kwenye masoko ya nje, lakini sisi tumeweza kufanikisha kuzalisha tani za asali zenye thamani ya shilingi bilioni 15.85 ambazo zimeuzwa nje ya nchi sawa na 206.9% ikilinganishwa na kiasi cha tani 430.61 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.16 zilizouzwa nje ya nchi kwa kipindi kama hicho mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa maendeleo haya, Shirika la Wafugaji Nyuki Duniani limeiteua Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wafugaji Nyuki Duniani *(APIMONDIA)* mwaka 2027. Mkutano huu utahudhuriwa na watu zaidi ya 4,000 kutoka sehemu mbalimbali za dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya saba; kufuatia juhudi za Serikali na wadau, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro limerejeshewa hadhi yake ya kuwa eneo maalum la jiolojia ya Ngorongoro Lengai *(UNESCO Global Geopark)*. Mwaka 2022, eneo hili lilikua kwenye orodha ya hifadhi za jiolojia zilizopoteza hadhi. Hata hivyo, mwezi Desemba, 2024 lilirejeshewa hadhi yake. Hadhi hii itaongeza thamani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, idadi ya watalii na watafiti watakaotembelea Tanzania kwa shughuli

mbalimbali pamoja na kuongeza idadi ya vivutio vya utalii hususan utalii wa miamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya nane ni namna ambavyo katika kipindi hiki Wizara imefanikiwa kuanza kutekeleza hatua madhubuti na za kimkakati za kusaidia Sekta Binafsi iweze kukua katika sekta ya utalii, kupunguza na kuondoa tozo na kero zilizokuwa zinakwaza wadau kama ifuatavyo; hapa ninaomba nitoe ushuhuda kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mabadiliko ya viwango vya Ada ya Leseni ya Biashara za Utalii *(TTBL)* kwa ajili ya wawekezaji wazawa wa huduma za malazi zilizopangwa katika daraja za ubora na zile ambazo hazijapangwa daraja kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mathalan, tumepunguza Daraja la Nyota Tano ambalo awali walikuwa wanalipa Dola 2,500. Hivi sasa daraja la Nyota Tano tumepunguza kutoka Dola 2,500 hadi Dola 1500; Daraja la Nyota Nne kutoka *USD* 2,000 hadi *USD* 1,000 kwa malipo ya hizi hoteli; Daraja la Nyota Tatu tumepunguza kutoka Dola 1,500 hadi Dola 500; Daraja la Nyota Mbili kutoka *USD* 1,200 hadi Dola 300; Daraja la Nyota Moja kutoka *USD* 1,000 hadi Dola 200. Gharama hizi sasa zinalipwa kwa shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefuta malipo ya waongoza watalii *(park fees),* waliyokuwa wakitozwa kila walipokuwa wakiingia hifadhini kuingiza wageni. Sasa kila mwongoza watalii mwenye leseni hai na halali kwa kweli hatatozwa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanza pia kutekeleza punguzo la ada ya wakala wa kupandisha mlima kutoka Dola za Marekani 2,000 hadi shilingi za Tanzania milioni tatu kwa wale ambao wanapandisha milima wageni wetu. Pia, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la gharama ya leseni za waongoza watalii *(TTBL)* kutoka Dola za Marekani 50 hadi shilingi 35,000 tu kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali kwa ujumla itaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na Sekta Binafsi katika kuongeza ufanisi wa sekta za uhifadhi na utalii kupitia vikao vya kisekta chini ya *Tanzania National Business Council* na mikutano ya mara kwa mara ya wadau ambayo tunaiita *Ministerial Public Private Dialogue*.

Mheshimiwa Spika, eneo la tisa; katika kutambua na kuhamasisha wadau kuendeleza uhifadhi na utalii, Wizara imekuja na ubunifu wa kuzindua tuzo maalum zijulikanazo kama *The Serengeti Awards* zenye lengo la kutambua mchango wa wadau katika kuendeleza uhifadhi na kutangaza utalii.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa tuzo hii ulifanyika Desemba, 2024, Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 500 ambapo miongoni mwa watu mashuhuri waliopata tuzo ni Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amepata Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono *(Visionary Leadership Award)*; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii na familia ya mgunduzi mashuhuri duniani wa zamadamu Louis na Mary Leakey. Tuzo hizi zitaendelea kuimarishwa na kutolewa kila mwaka ili kuendelea kuhamasisha na kutambua michango mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema pia fanikio lingine ambalo sasa litakuwa ni kati ya yale mafanikio 10. Sisi tunajivunia na niseme kwamba ni kuanza kuonekana kwa matokeo ya kile ambacho Bunge lako Tukufu pia limekuwa likitusisitizia kutekeleza mikakati ya kutangaza utalii kwa njia ya tovuti na kuyafikia masoko mapya zaidi ya yale yaliyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hili, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo Balozi zetu za India, China pamoja na Kamati ya Rais ya Kutangaza Utalii, ilifanikiwa kufanya mikakati mahususi mbalimbali ikiwemo hii ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mkakati kuhusu China; kama mnavyojua mbali na *Royal Tour*, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walishiriki filamu nyingine tena iitwayo *Amazing Tanzania* na mcheza filamu mashuhuri wa China anayeitwa Jin Dong. Filamu hii baada ya kuzinduliwa Mei, 2024 kule Beijing, ilizinduliwa tena hapa nchini Jijini Dar es Salaam, Tanzania Novemba mwaka 2024 na inaendelea kutazamwa.

Mheshimiwa Spika, tayari filamu hiyo imesababisha watalii kutoka China kuongezeka kutoka 45,400 kwa mwaka 2023, sasa tumefikia soko kutoka China na watalii 71,140 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la 56%. Aidha, filamu hii ilichagizwa na waandaaji wa kipindi maarufu nchini China kinachohusisha mastaa cha *Divas Hit the Road* kuja nchini na kuonesha zaidi utalii wetu ambapo baada ya kipindi kuoneshwa kupitia Televisheni ya Hunan na mitandao ya kijamii, kilitazamwa na watu takriban bilioni 1.2 ndani ya China na nchi za jirani. Juhudi kama hizo pia zimechochewa na ongezeko la idadi ya watalii kutoka Soko la Kimkakati la India kufikia 63,391 mwaka 2024 kutoka 54,558 mwaka 2023 sawa na ongezeko la 16.2%.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya kwa uchache, yanadhihirisha uthubutu na weledi wa Serikali ya Awamu ya Sita na yanaonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika kulinda, kuendeleza na kutumia kwa tija rasilimali zetu za Taifa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na umahiri mkubwa, huku akizingatia falsafa yake ya *4R;* maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya kwa kuzingatia utawala bora na kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii. Huyu ni chanda chema tunastahili kumvika pete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nielekee kwenye utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Wizara ya

Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takribani 307,000, sawa na 32.5% ya eneo lote la nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba takribani 29, Mapori Tengefu 23, Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori *(WMAs)* 40, ambapo kati ya hizo 26 zimeidhinishwa na 14 ziko kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, Maeneo matatu ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya Asili 464, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 25, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 142 na Makumbusho za Taifa Saba.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na malikale yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi Kitaifa na Kimataifa. Niseme tu kwamba, Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia 21.5% katika pato ghafi la Taifa, ambapo 17.2% ni utalii na asilimia 4.3 ni misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, aidha, sekta hii inachangia 30.9% ya mapato ya fedha za kigeni ambapo 25% yanatokana na utalii, asilimia 5.9 ni misitu na nyuki na kuajiri watu takribani milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Vilevile, sehemu kubwa ya Watanzania katika maeneo ya vijijini hutegemea rasilimali hizo, kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Moja, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 968.8. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7555.4 zinakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA* na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali, kupitia *TRA* na shilingi bilioni 213 zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mifuko na baadhi ya Taasisi zake kupitia Mfumo wa *MNRT Portal*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 912.9, sawa na 94.2%, ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, shilingi 730 zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA*. Aidha, shilingi bilioni 182 zimekusanywa na Wizara kutokana na Idara, Mifuko na Taasisi zake kupitia Mfumo wa *MNRT Portal*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 708, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 532.4 ni, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 176.3 ni, kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 540.28, sawa na 76.2%. Fedha hizi zinajumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni 436.38, na Fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi bilioni 103.89. Katika fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, shilingi bilioni 247.63 ni fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi 188.74 ni Mishahara.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukiri kwamba, mwingiliano wa wanadamu na wanyamapori kwa baadhi ya wananchi kuingia hifadhini kufanya shughuli za kilimo na ufugaji na hata makazi na kuvamiwa kwa shoroba za kupita wanyamapori kumeendelea kuwa changamoto na kuleta migongano yenye madhara kwa wananchi na hifadhi zetu. Kama tulivyoahidi mwaka jana 2024, Serikali imeongeza juhudi za kukabiliana na changamoto hii kwa kutekeleza mipango madhubuti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ujenzi wa vizimba vya kudhibiti mamba na viboko. Wizara, kupitia *TAWA*, *TANAPA* na *TAWIRI,* imekamilisha ujenzi wa vizimba 12 vya kudhibiti mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya za Bunda, Korogwe, Ludewa, Uvinza, Tandahimba, Nanyumbu na Mkinga. Vilevile, ujenzi wa vizimba sita unaendelea katika Wilaya za Buchosa, Sengerema, Bunda, Newala na Kibiti. Vizimba hivyo vitasaidia kuimarisha usalama wa wananchi wanaotumia maji ya mito na maziwa katika maeneo hayo na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imekamilisha ujenzi wa mabwawa 10 katika Hifadhi za Taifa Nyerere mawili, Tarangire matatu, Mikumi moja, Serengeti mawili, Pori la Akiba Rungwa moja na *Makuyuni Wildlife Park* moja, pamoja na kisima kimoja katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Aidha, ujenzi wa mabwawa mengine saba unaendelea katika Mapori ya Akiba Selous – Liwale, Rungwa, Muhesi, Kizigo na Msanjesi. Miundombinu hii itasaidia kupunguza matukio ya Wanyamapori wakali na waharibifu, hasa kipindi cha kiangazi, ambapo baadhi ya wanyamapori hutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutumia teknolojia za kisasa kufuatilia mienendo ya wanyamapori, ikiwemo tembo, kwa kuwafunga Mikanda Maalum ya Mawasiliano *(GPS - Satellite Collars),* ili kupata taarifa za moja kwa moja zinazoonesha mienendo yao na kuwadhibiti kabla hawajasababisha madhara kwa binadamu. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara, kwa kushirikiana na wadau, imenunua Mikanda Maalumu ya Mawasiliano *(GPS - Satellite Collars)* 54.

Mheshimiwa Spika, Mikanda hii imefungwa kwa tembo viongozi wa makundi 45 katika Mifumo Ikolojia ya Serengeti miwili, Burigi-Chato-Ibanda-Rumanyika sita, Mkomazi-Handeni saba, Moyowosi-Kigosi kumi na moja, Ruaha-Rungwa minne, Tarangire-Manyara mitano na Nyerere-Selous-Mikumi kumi. Aidha, simba watatu na mbwa mwitu sita wamefungwa mikanda ya mawasiliano katika Mfumo Ikolojia Selous-Nyerere-Mikumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara vilevile imenunua ndege nyuki *(drones)* 17 na mabomu baridi 12,072, kwa ajili ya kuwadhibiti tembo katika maeneo yenye changamoto. Aidha, taratibu za manunuzi za ndege nyuki *(drones)* 18 na mabomu baridi 4,512 zinaendelea. Matumizi ya teknolojia hizo yamewezesha kupata taarifa kwa haraka na kurejesha makundi ya tembo kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia *TANAPA* na Ngorongoro, imekamilisha ujenzi wa vituo vinne vya Askari wa Uhifadhi wa Wanyamapori katika Wilaya za Korogwe, Same, Namtumbo na

Ruangwa. Aidha, ujenzi wa vituo sita katika Wilaya za Bunda, Serengeti, Bariadi, Kalambo, Kilwa na Mbarali unaendelea. Sambamba na ujenzi wa vituo hivyo, Wizara kupitia *TAWA* imeendelea kuweka Vituo vya Muda vya Askari kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu, kwa ajili ya kudhibiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeweka vituo mbalimbali, ili kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika wilaya 40, zikiwemo Manyoni, Itigi, Morogoro Vijijini, Chalinze, Meatu, Bariadi, Itilima, Buchosa, Tunduru, Liwale, Kaliua, Nachingwea, Handeni, Simanjiro na Babati. Hatua hii ya vituo itasaidia katika kudhibiti Wanyamapori wakali na waharibifu kwa haraka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, tunaendelea kutoa elimu, vifaa na mafunzo kwa wananchi. Wizara imetoa mafunzo maalumu kwa Wakufunzi 170 kutoka Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Itigi, Wanging'ombe, Mbarali na Iringa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi 635,228 katika vijiji 945 vinavyopakana na maeneo ya hifadhi. Sambamba na hilo, Wizara imetoa semina kwa Maafisa Wanyamapori 122 wa Wilaya, Makatibu 50 wa Kamati za Kudumu za Bunge na wadau wengine wa uhifadhi. Vilevile, Wizara imenunua pikipiki 49, kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uhifadhi kwa Maafisa Wanyamapori wa Wilaya 22, *WMA* saba na pikipiki 20, kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye kanda 10 za kiikolojia za kupambana na ujangili. Juhudi hizi zimesaidia kujenga uelewa na kuimarisha ulinzi na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara, kupitia Taasisi zake za uhifadhi, ilifanikiwa kudhibiti matukio 4,012 ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, katika jitihada za kuokoa maisha ya wananchi na mali zao wakati wa kudhibiti matukio tajwa, wanyamapori wakali na waharibifu 296 walivunwa wakiwemo mamba 63, viboko 63, tembo 34, nyati 15, fisi 71, simba 10 na chui mmoja, ili kuokoa maisha ya wanadamu.

Mheshimiwa Spika, simba 10 vilevile walihamishwa kutoka eneo la Kijiji cha Mdori na kupelekwa katika Mapori ya Akiba, Rungwa sita na Pande. Nyani 90 waliondolewa maeneo mbalimbali, ikiwemo Geita Mjini na kupelekwa Msitu wa Hifadhi Kigosi na chui watatu waliondolewa Kijiji cha Nyichoka na kuhamishiwa Hifadhi ya Taifa Serengeti na Bustani ya Wanyamapori Ruhila.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, Wizara imelipa viwango vipya vilivyoongezwa maradufu kwa wananchi wanaoathiriwa na wanyama wakali, ambapo hadi Aprili, 2025 kiasi cha fedha, shilingi bilioni 4.6 ikiwa ni kifuta jasho na machozi kwa wananchi 16,939 walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu kwa matukio yaliyotokea katika kipindi cha mwaka 2021 hadi kufikia Aprili, 2025 katika halmashauri za wilaya 78, kimelipwa. Aidha, Wizara inaendelea na malipo ya kifuta jasho na machozi kiasi cha shillingi bilioni 1.8 kwa wananchi 5,542 wa halmashauri za wilaya 18.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali, ili kuhakikisha uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu unadhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Nitoe rai kwa wadau wote kuiunga mkono Serikali katika jitihada hizi. Katika mwaka ujao 2026 Serikali itaimarisha eneo hili kwa kuanza kutumia Mfumo wa Kidigitali uitwao *PAIS,* kurahisisha haya malipo.

Mheshimiwa Spika, tuangalie sasa kuendelea kuongoa shoroba zilizovamiwa. Wizara imeendelea na utaratibu wa kuongoa maeneo ya kimkakati ya uhifadhi, ikiwemo Eneo la Ghuba ya Speke na Bonde la Mto Kilombero, ili kuwezesha ustahimilivu wa mifumo ikolojia Serengeti – Mara na Nyerere – Selous – Niassa.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2025 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 61.86, kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha uhifadhi katika Maeneo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Kilombero na Hifadhi ya Taifa Mahale. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 53.23 zimelipwa kwa kaya 3,493 na kuhamisha

makaburi 618 katika Kata ya Nyatwali iliyopo eneo la Ghuba ya Speke, Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara; shilingi bilioni 1.68 zimelipwa kwa kaya 205 zilizofanyiwa uthamini katika Kijiji cha Kalilani kilichopo Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma na shilingi bilioni 6.78 zimelipwa kwa kaya 998 na kuhamisha makaburi 107 ya Kijiji cha Ngombo kilichopo katika Pori la Akiba, Kilombero.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022–2026. Mpango huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kusimamia Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori *(WMAs)* wa Mwaka 2023 - 2033 kwa lengo la kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za wanyamapori. Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu unadhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ya kutangaza na kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwemo kutangaza utalii kupitia, Mashirika ya Ndege ya Kitaifa na Kimataifa, hususani *Air Tanzania Company Limited, Turkish Airlines, Emirates* na *Qatar Airways* kwa kuweka matangazo mbalimbali, pia, kutumia Ligi za Michezo zenye wafuatiliaji wengi ikiwemo *CHAN*, *AFCON* na Ligi za Mpira zilizopo nchini na nje ya nchi. Wizara itaendelea na utangazaji wa Filamu ya *Amazing Tanzania* kwenye vyombo mbalimbali vya habari vya Nchini China. Halikadhalika, Wizara itakamilisha uandaaji wa maudhui ya kutangaza vivutio vya utalii katika Soko la India kupitia watu maarufu wa nchini humo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 16 yenye ukubwa wa hekta 221,825 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi 32. Aidha, Wizara itafanya jumla ya doria takribani 16,688 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wizara itaimarisha mipaka ya misitu 170 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 554, kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,394, kuweka vigingi, mabango na kununua ndege nyuki *(drones)*. Sambamba na hilo, Wizara itawezesha uanzishwaji wa hifadhi za nyuki tatu, hifadhi za misitu zenye ukubwa wa hekta 10,000 na kuandaa mipango mitano ya usimamizi wa hifadhi za misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya shilingi bilioni 48.31 zimetengwa, kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, ikiwemo ununuzi wa helikopta mbili, kupitia Taasisi za Uhifadhi za *TANAPA* na Ngorongoro, uchimbaji wa mabwawa takribani 12 katika Mapori ya Akiba saba na Hifadhi za Taifa mbili, uchimbaji wa visima vya maji 18 katika Hifadhi za Taifa sita. Aidha, Wizara itajenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 53, ambapo kilometa 38 ni kutoka Tabora hadi Mto Mara katika Hifadhi ya Serengeti na kilometa 15 kutoka Lango la Loduare kuelekea Oldiani katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kujenga vituo 19 vya askari kwenye maeneo yenye changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya za Tunduru, Kiteto, Ikungi, Nkasi, Itilima, Manyoni, Kilosa, Rufiji, Babati, Morogoro, Karatu, Monduli na Hifadhi za Taifa za Ibanda Kyerwa, Mto Ugala, Rumanyika Karagwe na ujenzi wa vizimba 50 katika maeneo yenye changamoto ya mamba na viboko katika halmashauri mbalimbali za wilaya. Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika kukabiliana na Wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege nyuki 12 na mikanda maalum ya mawasiliano 50, kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori hao.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatangaza maeneo sita ya malikale kuwa Urithi wa Taifa, kukusanya taarifa za kiuhifadhi za maeneo 25 ya malikale, kwa ajili ya kuhuisha orodha ya Urithi wa Taifa, kufanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo nane yaliyopo kwenye Orodha ya Urithi wa Taifa katika Mikoa ya Mara, Geita, Kagera na Shinyanga. Kufanya ukaguzi wa hali ya uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 10 ya malikale, makumbusho saba, kusajili makumbusho binafsi, pamoja na ukarabati wa maeneo mbalimbali na kuratibu utatuzi wa migogoro ya mipaka katika maeneo matano ya malikale.

Mheshimiwa Spika, sasa tuzungumzie maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imekadiria kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni 1.18 kutoka kwenye Idara na Taasisi zake. Ninaomba nirudie, Wizara yetu inakadiria kukusanya maduhuli, mapato ya shilingi trilioni 1.18 kutoka kwenye Idara na Taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 359.98. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 254.23 zitagharamia matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 105.74 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha mishahara bilioni 130.70 na matumizi mengineyo bilioni 123.52. fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha bilioni 32.47 fedha za ndani na shilingi bilioni 73.27 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 254.23 zinajumuisha shilingi bilioni 32.52 kwa ajili ya Wizara na shilingi bilioni 221 kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, shilingi bilioni 10.18 ni mishahara na shilingi bilioni 22.33 ni matumizi mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha shilingi bilioni 120.51 za mishahara na shilingi bilioni 101.18 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha; ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 359,982,271,000.00 kwa matumizi ya Fungu 69 kwa mwaka wa

fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 254,232,349,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 105,749,922,000.00 ni za miradi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi bilioni 130,709,054,000.00 za mishahara na shilingi bilioni 123,523,295,000.00 za matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni 32,476,051,000.00 fedha za ndani na shilingi 73,273,871,000.00 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii tena kukushukuru wewe mwenyewe kwa dhati na Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; ninapenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushirikiana katika uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji wa utalii. Aidha, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Vilevile nawashukuru sana wadau wote ambao wamekuwa wakishirikiana nasi. Kutokana na muda sitaweza kuwataja wote, lakini tunawashukuru sana. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii *www.maliasili.go.tz*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI H. CHANA (MB), WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/20267 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyopitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali

kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai, afya njema, usalama na amani katika Taifa letu na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza jukumu letu la msingi la kuipokea na kuijadili taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

3. Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kwa mara nyingine kusimamia Sekta ya Maliasili na Utalii. Naendelea kumuombea afya njema, hekima na nguvu zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa zaidi. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu, uwajibikaji, weledi na uzalendo mkubwa ili kuhakikisha kuwa sekta hii inazidi kuwa nguzo imara ya uchumi wa nchi yetu, huku tukihifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

4. kwa namna ya kipekee, ninaomba nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, wenye dira, hekima na maono ya maendeleo ya Taifa letu. Uongozi wake umeifanya nchi yetu kuendelea kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, nimpongeze kwa namna alivyoiongoza vyema Serikali ya Awamu ya Sita katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Sisi sote ni mashahidi wa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Maliasili na Utalii.

5. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahenga wanasema: "**Chanda Chema Huvikwa Pete**" ninapenda kumpongeza kwa

dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia kila la heri katika safari hii muhimu ya kulitumikia Taifa letu kwa uzalendo na dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo kwa Watanzania.

6. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Taifa letu. Kwa hakika, miongozo na maelekezo yake yamekuwa chachu katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya maendeleo na kuhakikisha maliasili zetu zinahifadhiwa na sekta ya utalii inaendelezwa kwa manufaa ya Taifa.

7. naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za dhati katika kuimarisha uchumi na maendeleo ya Wananchi wa Zanzibar. Aidha, nampongeza kwa kupitishwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

8. Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali. Uongozi wao madhubuti na maelekezo wanayotoa mara kwa mara yamewezesha kufanikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za Taifa na kuchochea ukuaji wa utalii nchini.

9. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, naomba nikupongeze wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Uongozi wako thabiti unaendelea kulifanya Bunge letu kuwa chombo imara cha kutunga Sheria, kuisimamia Serikali na kuwakilisha wananchi kwa ufanisi. Aidha, nikupongeze kwa kazi nzuri na ya mfano unayoendelea kuifanya katika Umoja wa Mabunge Duniani ambayo si tu inaitangaza Tanzania bali pia inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha majadiliano ya kidemokrasia na mshikamano wa Kimataifa.

10. Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kukusaidia kwa umahiri mkubwa kuendesha shughuli za Bunge. Pia niwapongeze Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa umakini wao mkubwa katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge.

11. Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua fursa hii, nikizingatia kuwa "**Umoja Ni Nguvu**" kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Manaibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia kuwaletea Watanzania maendeleo kwa kasi kubwa zaidi. Aidha, ninawashukuru kwa namna wanavyoshirikiana na Sekta ya Maliasili na Utalii katika utekelezaji wa majukumu yake. Tunathamini sana mchango wao, kwa pamoja tutaendelea kujenga Taifa lenye nguvu na ustawi wa wananchi.

12. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) Mwenyekiti; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka huu wa Fedha

sambamba na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka ujao wa Fedha. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa ili kuhakikisha kuwa sekta hii inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sambamba na hilo, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati hizo kwa ufanisi katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

13. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na malikale pamoja na uendelezaji wa utalii nchini. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi ya kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

14. Mheshimiwa Spika, kwa dhamira ya dhati kabisa na nikizingatia kauli ya kwamba "**Kidole Kimoja Hakivunji Chawa**", niwashukuru Viongozi wenzangu na Watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kujituma kwao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Uongozi wao thabiti umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii muhimu. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula (Mb.), Naibu Waziri kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu; Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu (Maliasili); na Bwana Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu (Utalii) kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

15. Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA,

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu – FWITC, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT na Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT pamoja na Watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Ushirikiano wao, weledi na kujituma kumefanikisha kwa kiasi kikubwa malengo tuliyojiwekea. Kwa pamoja mmeonesha kuwa kazi ya timu ndiyo msingi wa mafanikio ya kweli.

16. Mheshimiwa Spika, tunaaswa kuwa "**Mwenda Omo na Tezi Marejeo Ngamani** basi kipekee kabisa, naishukuru familia yangu kwa namna wanavyonitia moyo na kuniombea ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kuwalinda. Vilevile, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa ushirikiano na kutambua dhamana ya kitaifa niliyokabidhiwa. Nawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nanyi katika juhudi za kuleta maendeleo katika Mkoa wetu kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

17. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa ninaomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mheshimiwa Cleopa David Msuya. Tutaendelea kumkumbuka kwa umahiri wake mkubwa katika usimamizi na uwajibikaji katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Kwa hakika, ametuachia hazina isiyomithilika katika uongozi wa weledi, ukimya na uzalendo kwa nchi yake.

18. Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kutoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Ukanda wa Afrika. Kwa namna ya pekee, naungana na Watanzania wote kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wetu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

19. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia pia hali inayoendelea nchini kutokana na matokeo ya uhifadhi na muingiliano wa binadamu na wanyamapori, kwa unyenyekevu mkubwa, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wananchi ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kutekeleza mikakati thabiti na madhubuti ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao. **Kwa pamoja tunaweza.**

20. Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kutambua mchango wa dhati wa Askari na Maafisa wa Jeshi la Uhifadhi ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri na weledi katika kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu zikiwemo wanyamapori, misitu, nyuki na malikale. Katika mwaka huu wa fedha, baadhi ya askari hawa shupavu, walipoteza maisha wakiwa kazini wakitimiza wajibu wao kwa Taifa na wengine walipata majeraha. Mashujaa wetu CR III Arafat Saidi Miyimba kutoka TANAPA; Askari wa Vijiji (VGS) Bwana Issa Manyinja wa WMA ya Magingo Wilaya ya Liwale; Bwana Masanja Michael wa WMA ya Uyumbu Wilaya ya Urambo; Bwana Felician Isdory Mgomela; Bwana Shakimu Mohamed na Bwana Boliva Betram Mapunda kutoka TFS walipoteza maisha. Aidha, askari wengine 46 kutoka taasisi za uhifadhi za TANAPA, NCAA, TAWA na TFS

walijeruhiwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Matukio haya yalitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na majangili waliovamia maeneo ya hifadhi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina.

21. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

22. Mheshimiwa Spika, maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) ya tarehe 30 Agosti, 2023 kupitia Tangazo la Serikali Namba 619A yanaainisha majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo mbalimbali inayolenga uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki, malikale na maendeleo ya utalii;

(ii) Kusimamia ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu kwa kufanya doria ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu;

(iii) Kujenga uwezo wa Sekta ya Maliasili na Utalii ili iweze kusimamia rasilimali za maliasili na malikale, kuendeleza utalii, kufanya tafiti na kutoa mafunzo kupitia vyuo vilivyo chini ya Wizara;

(iv) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili, utalii na malikale;

(v) Kushirikisha wadau mbalimbali katika utunzaji na uhifadhi wa maliasili na malikale kwa kutoa elimu na huduma za ugani; na

(vi) Kukuza na kuendeleza mazao ya utalii, kuimarisha utangazaji na kuboresha huduma za utalii kwa lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa.

3.0 MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

23. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri na shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muongoza Watalii Namba Moja nchini, Serikali imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali katika sekta za uhifadhi na utalii na hakika tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika miaka hii minne na mwaka mmoja huu wa utekelezaji wa Bajeti. Nitumie fursa hii kuainisha kwa muhtasari **MAFANIKIO 10 YA KIHISTORIA** yaliyopatikana kutokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa idadi ya watalii

Idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa **asilimia 132.1** kutoka watalii **922,692** Mwaka 2021 hadi watalii **2,141,895** Mwaka 2024. Aidha, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa **asilimia 307.9** kutoka watalii **788,933** Mwaka 2021 hadi kufikia watalii **3,218,352** mwaka 2024. Hatua hii imewezesha idadi ya watalii kufikia **5,360,247** sawa na **asilimia 107.2** ya lengo la watalii **5,000,000** kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2020.

Kwa rekodi hizo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UN Tourism), limeitaja Tanzania kuwa nchi ilizoongoza Afrika kwa mwaka 2024 kwa kuwa na ongezeko kubwa la watalii ikilinganishwa na kabla ya janga la UVIKO-19 ambapo utalii Tanzania ulikua kwa asimilia

48, Ethiopia (40%), Morocco (35%), Kenya (11%) na Tunisia (9%). Haya ni matokeo yaliyochagizwa na maono na kujitoa kwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika filamu za **Tanzania: The Royal Tour** na ile ya **Amazing Tanzania**.



Best Performing Destinations in Africa 2024 - International Tourist Arrivals % Change Over 2019 (UN Tourism - April, 2025)

(ii) Kuongezeka kwa Mapato Yatokanayo na Shughuli za Utalii

Mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani **bilioni 1.3** Mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani **bilioni 3.9** Mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 200** kwa watalii wa kimataifa. Aidha, mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka Shilingi **bilioni 46.3** Mwaka 2021 hadi Shilingi **bilioni 209.8** Mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 353.1**. Hatua hii imeifanya Tanzania kuwa nafasi ya tisa (9) duniani na kushika nafasi ya tatu (3) Barani Afrika kwa ongezeko la mapato ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya UVIKO-19.

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

Maduhuli ya Serikali yaliongezeka kutoka Shilingi **397,428,671,968.00** Mwaka 2020/2021 hadi Shilingi **901,088,264,662.24** Mwaka 2023/2024. Vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kuanzia Julai 2024, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 912,900,341,299.80** sawa na **asilimia 94.2** ya lengo la makusanyo.

(iv) Tanzania Imeendelea Kutambulika na Kung'ara Kimataifa

Tanzania imeendelea kung'ara kwa kushinda Tuzo mbalimbali za utalii katika nyanja za Kimataifa. Hatua hiyo imedhihirishwa kwa mafanikio ya kishindo kwa kupata Tuzo maarufu Duniani za World Travel Awards – WTA zinazotolewa na taasisi ya World Luxury Media Group Limited ya nchini Uingereza katika msingi wa kutambua na kutangaza ubora wa vivutio na huduma za utalii, ambapo Tanzania imeshinda Tuzo saba (7) za Kimataifa ambazo ni: Eneo linalovutia zaidi kiutalii (Africa's Leading Destination, 2024); Eneo linaloongoza kwa utalii wa safari (World's Leading Safari Destination, 2024); Hifadhi ya Taifa Serengeti kuendelea kuwa bora Duniani kwa miaka sita (6) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2024; Mlima Kilimanjaro kuwa kivutio bora cha utalii barani Afrika (African Leading Tourism Attraction, 2024); Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kutambuliwa kama eneo la pili bora zaidi duniani kwa safari na utalii na gazeti la The Times of India (World's SecondBest Destination by Times of India, 2024); Utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa iliyotolewa na Shirika la Utafiti wa Ubora (European Society for Quality Research – ESQR), ambapo TANAPA imeshinda kwa mara ya tano mfululizo kuanzia mwaka 2020 hadi 2024; na Bodi ya Utalii kushinda Tuzo ya Bodi Bora Afrika. Tuzo hizi zimeendelea kuwa chachu ya kujitangaza na kutambulika katika majukwaa ya kimataifa na kuchagiza ongezeko la idadi ya watalii wanaotembelea nchini. Kwa upande mwingine, Tanzania imepewa hadhi ya kuwa mwenyeji wa Tuzo za World Travel Awards kwa Kanda ya Afrika zitakazotolewa mwezi Juni, 2025.

Kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula (Mb) wakifurahia tuzo ambayo Tanzania ilishinda kama eneo linaloongoza kwa utalii wa safari Duniani. Kulia ni baadhi ya tuzo zilizopokelewa kwa mwaka 2024.

(v) Kuimarika kwa Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Wanyamapori

Kupitia mikakati madhubuti ya kudhibiti ujangili, kuimarisha doria na matumizi ya teknolojia tumeshuhudia ongezeko la idadi ya wanyamapori na hali ya usalama katika maeneo ya hifadhi kuliko wakati wowote katika historia yetu. Kwa mujibu wa tafiti za mashirika ya kimataifa kama IUCN na Taasisi yetu ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), nchi yetu Tanzania imeendelea kuongoza Afrika na duniani kwa kuwa na simba wapatao 17,000; lakini pia ikiongoza Afrika kwa nyati 225,000 na chui 24,000. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya faru weusi imeongezeka kutoka faru 163 Mwaka 2021 hadi 263 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 61. Sambamba na hilo, takwimu zinaonesha matukio ya ujangili wa tembo yamepungua kwa takriban asilimia 90.

(vi) Kuimarika kwa Biashara ya Mazao ya Misitu na Nyuki

Serikali imeendelea kushuhudia kuimarika kwa biashara ya mazao ya misitu na nyuki nchini. Kuimarika kwa biashara hii kunatokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika kipindi cha miaka mitano (5), kumekuwa na ongezeko la kiwango cha uzalishaji wa malighafi mbao katika mashamba ya Serikali yanayolimwa miti kibiashara kutoka mita za

ujazo 1,108,791 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia mita za ujazo 1,264,535 mwaka wa fedha 2024/2025. Vilevile, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu vimeongezeka kutoka viwanda vya kati na vikubwa 636 mwaka 2020 hadi kufikia 1,671 mwaka 2025 na viwanda vidogo vidogo kama useremala zaidi ya 7,000. Sambamba na hilo, thamani ya mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi imeongezeka kufikia Shilingi 458,474,543,027.45 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 333.8 ikilinganishwa na Shilingi 105,689,957,500.00 mwaka 2020/2021.

Kwa upande mwingine, Wizara imewezesha ujenzi wa viwanda vya kati na vikubwa vya kuchakata na kuongeza thamani mazao ya nyuki na kufanya idadi ya viwanda hivyo kuongezeka kutoka kiwanda kimoja (1) mwaka 2020 hadi kufikia viwanda nane (8) mwaka 2025. Viwanda hivi vimejengwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Iringa, Katavi na Geita. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani 1,321.35 za asali zenye thamani ya shilingi 15,856,164,000.00 zimeuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 206.9 ikilinganishwa na kiasi cha tani 430.61 zenye thamani ya Shilingi 5,167,332,000.00 zilizouzwa nje ya nchi kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa maendeleo haya, Shirika la Wafugaji Nyuki Duniani limeiteua Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wafugaji nyuki duniani (APIMONDIA) mwaka 2027, utakaohudhuriwa na watu zaidi ya 4,000 kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

(vii) Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro Kurejeshewa Hadhi ya Hifadhi ya Jiolojia ya Ngorongoro Lengai (UNESCO Global Geopark)

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro limerejeshewa hadhi ya hifadhi ya jiolojia ya Ngorongoro Lengai (UNESCO Global Geopark). Mwaka 2022, eneo hili lilikua kwenye orodha ya hifadhi za jiolojia zilizopoteza hadhi, hata hivyo mwezi Desemba 2024 lilirejeshewa hadhi yake kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ikiwemo kuimarisha shughuli za uhifadhi katika maeneo ya urithi wa jiolojia, kutangaza pamoja na kufuata masharti na miongozo ya UNESCO katika kulinda hadhi ya eneo hilo. Hadhi hii itaongeza thamani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, idadi ya watalii na watafiti watakaotembelea

Tanzania kwa shughuli mbalimbali pamoja na kuongeza idadi ya vivutio vya utalii hususan utalii wa miamba.

(viii) Mafanikio ya 4R za Rais Samia Katika Kukuza Biashara ya Utalii kwa Kuiwezesha Sekta Binafsi

Katika kipindi hiki, Wizara imefanikiwa kuanza kutekeleza hatua madhubuti na za kimkakati za kusaidia sekta binafsi iweze kukua katika sekta ya utalii kwa kupunguza na kuondoa tozo na kero zilizokuwa zinawakwaza wadau kama ifuatavyo: -

a) Kufanya mabadiliko ya viwango vya Ada ya Leseni ya Biashara za Utalii (TTBL) kwa ajili ya wawekezaji wazawa wa huduma za malazi zilizopangwa katika daraja za ubora na zile ambazo hazijapangwa katika daraja kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji. Mathalan, Wizara imepunguza: Daraja la Nyota 5 kutoka USD 2,500 hadi USD1500; Daraja la Nyota 4 kutoka USD 2,000 hadi USD 1000; Daraja la Nyota 3 kutoka USD 1,500 hadi USD 500; Daraja la Nyota 2 kutoka USD 1,200 hadi USD 300; Daraja la Nyota 1 kutoka USD 1,000 hadi USD 200. Gharama hizi sasa zinalipwa kwa shilingi ya Tanzania;

b) Kufuta malipo ya waongoza watalii (park fees) walizokuwa wakitozwa kila walipokuwa wakiingia hifadhini kuingiza wageni. Sasa kila muongoza watalii mwenye leseni hai na halali hatatozwa chochote; na

c) Kuanza kutekeleza punguzo la ada ya Wakala wa kupandisha mlima kutoka Dola za Marekani 2000 hadi shilingi za Tanzania milioni tatu (3,000,000). Aidha, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la gharama ya leseni ya waongoza watalii (TTBL) kutoka Dola za Marekani 50 hadi Shilingi 35,000 tu kwa mwaka.

Wizara na Serikali kwa ujumla itaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi katika kuongeza ufanisi wa sekta za uhifadhi na utalii kupitia vikao vya kisekta chini ya TNBC pamoja na mikutano ya mara kwa mara na wadau.

(ix) Kuandaa Tuzo za Kwanza za Uhifadhi na Utalii

Katika kutambua na kuhamasisha wadau kuendeleza uhifadhi na utalii, Wizara imezindua tuzo maalum zilizojulikana kama The Serengeti Awards zenye lengo la kutambua mchango wa wadau katika kuendeleza uhifadhi na kutangaza utalii. Uzinduzi wa tuzo hii ulifanyika Disemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 500 ambapo miongoni mwa watu mashuhuri waliopata Tuzo ni: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan (Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono yaani **Visionary Leadership Award**); Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii na familia ya mgunduzi mashuhuri duniani wa zamadamu Louis na Mary Leakey. Tuzo hizi zitaendelea kuimarishwa na kutolewa kila mwaka ili kuendelea kuhamasisha na kutambua michango mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Maliasili na Utalii.

(x) Mafanikio ya Mikakati Mahsusi ya Kutangaza Utalii

Katika kutekeleza mikakati ya kutangaza utalii kwa njia tofauti na kuyafikia masoko mapya zaidi ya yale yaliyozoeleka, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo Balozi zetu za India na China pamoja na Kamati ya Rais ya Kuitangaza Tanzania, ilifanya mikakati mahsusi miwili. Kuhusu China: Kama mnavyojua mbali na Royal Tour, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, walishiriki filamu nyingine tena na mcheza filamu mashuhuri wa China Bw. Jin Dong iitwayo Amazing Tanzania. Filamu hii baada ya kuzinduliwa Mei, 2024 kule Beijing ilizinduliwa tena hapa nchini jijini Dar es Salaam Novemba mwaka 2024 na inaendelea kutazamwa. Tayari filamu hiyo imesababisha watalii kutoka China kuongezeka kutoka 45,463 kwa mwaka 2023 hadi kufikia 71,140 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56.5. Aidha, filamu hii ilichagiza waandaaji wa kipindi maarufu nchini China kinachohusisha mastaa cha Divas Hit the Road kuja nchini na kuonesha zaidi utalii wetu ambapo baada ya kipindi kuoneshwa kupitia Televisheni ya Hunan na mitandao ya kijamii, kilitazamwa na watu takriban bilioni 1.2 ndani ya China na nchi za jirani. Juhudi kama hizo pia zimechochea ongezeko la idadi ya watalii kutoka soko la

kimkakati la India kufikia 63,391 mwaka 2024 kutoka 54,558 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16.2.

24. Mheshimiwa Spika, mafanikio haya, kwa uchache, yanadhihirisha uthubutu na weledi wa Serikali ya Awamu ya Sita na yanaonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika kulinda, kuendeleza na kutumia kwa tija rasilimali zetu za Taifa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na umahiri mkubwa huku akizingatia falsafa yake ya maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya kwa kuzingatia utawala bora na kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii. Huyu ni "**Chanda Chema Tunastahili Kumvika Pete**."

4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

25. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la Nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 40 ambapo kati ya hizo 26 zimeidhinishwa na 14 ziko kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, maeneo 3 ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya Asili 464, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 25, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 142 na Makumbusho za Taifa 7.

26. Mheshimiwa Spika, maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na malikale yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa. Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia asilimia 21.5 katika Pato ghafi la Taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii na asilimia 4.3 ni misitu na nyuki. Aidha, Sekta hii inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni

ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii; na asilimia 5.9 misitu na nyuki; na kuajiri watu takriban milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Vilevile, sehemu kubwa ya Watanzania katika maeneo ya vijijini hutegemea rasilimali hizo kwa ajili ya kujikimu.

27. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/2025, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

28. Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kuwasilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

4.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

30. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 968,842,018,480.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 755,422,955,480.00** zinakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia TRA; na **Shilingi 213,419,063,000.00** zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale - NFA na Taasisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI,

Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT na Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT kupitia mfumo wa MNRT Portal.

31. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 912,900,341,299.80** sawa na **asilimia 94.2** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 730,734,560,183.53** zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **Shilingi 182,165,781,116.27** zimekusanywa na Wizara kutokana na Idara, Mifuko na Taasisi zake kupitia mfumo wa MNRT Portal.

4.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

32. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 708,891,841,026.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 532,499,328,026.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 176,392,513,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

33. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 540,281,908,764.35** sawa na asilimia **76.2.** Fedha hizi zinajumuisha Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 436,384,697,790.06** na Fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 103,897,210,974.29.** Katika fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, **Shilingi 247,635,129,105.04** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 188,749,568,685.02** ni Mishahara.

4.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

4.3.1 Sekta ya Wanyamapori

34. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Wanyamapori ina dhamana ya kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya utafiti wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Sekta hii inasimamia Hifadhi za Taifa 21, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo 3 ya ardhioevu na bustani 5 za wanyamapori zinazomilikiwa na Serikali. Vilevile,

sekta hii inaratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo 40 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, mashamba 5 ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 41 za wanyamapori, maeneo 30 ya uzalishaji wa wanyamapori (captive wildlife breeding facilities) pamoja na ranchi 5 za sekta binafsi.

35. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya sekta ya wanyamapori hufanywa na Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Aidha, utekelezaji wa majukumu hayo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya Mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura ya 283; Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura ya 284; Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Sura ya 209; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura ya 260.

4.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

36. Mheshimiwa Spika, Wizara imetunga Kanuni za Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi katika maeneo ya Hifadhi za wanyamapori (Mapori ya Akiba na Tengefu) zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 781 la mwaka 2024; Kanuni za Biashara za Nyara zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 884 la mwaka 2024, na Kanuni za Utalii wa Picha zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 875 la mwaka 2024. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 780 la mwaka 2024 na Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) za mwaka 2018. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa Mipango ya Jumla ya Usimamizi wa Rasilimali za Wanyamapori (General Management Plan) ya Jumuiya za ISAWIMA (Kaliua), Ifinga (Madaba), Uyumbu (Urambo), na UKUTU (Morogoro). Katika hatua nyingine, Wizara imeandaa Mwongozo wa upatikanaji wa mazao ya

wanyamapori na mimea inayosimamiwa na Mkataba wa CITES ili kuimarisha utekelezaji wa mkataba huo. Kanuni hizi zinalenga kuimarisha uhifadhi shirikishi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

37. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Utatuzi wa Migongano kati ya Binadamu na Wanyamapori. Katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara kupitia TAWA, TANAPA na TAWIRI imekamilisha ujenzi wa vizimba 12 vya kudhibiti mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya za Bunda (3), Korogwe (1), Ludewa (2), Uvinza (2), Tandahimba (2), Nanyumbu (1) na Mkinga (1). Vilevile, ujenzi wa vizimba sita (6) unaendelea katika Wilaya za Buchosa (2), Sengerema (1), Bunda (1), Newala (1) na Kibiti (1). Vizimba hivyo vitasaidia kuimarisha usalama wa wananchi wanaotumia maji ya mito na maziwa katika maeneo hayo.

Kizimba cha kuzuia mamba na viboko kilichojengwa katika Kijiji cha Kwaisewa, Wilaya ya Korogwe.

38. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imekamilisha ujenzi wa mabwawa 10 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (2), Tarangire (3), Mikumi (1) na Serengeti (2); Pori la Akiba Rungwa (1); na Makuyuni Wildlife Park (1) pamoja na kisima kimoja katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Aidha, ujenzi wa mabwawa mengine saba (7) unaendelea katika Mapori ya Akiba Selous – Liwale (1), Rungwa (1), Muhesi (2), Kizigo (2) na Msanjesi (1). Miundombinu hii itasaidia kupunguza matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu hasa kipindi cha kiangazi

ambapo baadhi ya wanyamapori hutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na chakula.

Bwawa la maji katika Pori la Akiba Rungwa.

39. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutumia teknolojia za kisasa kufuatilia mienendo ya wanyamapori, ikiwemo tembo kwa kuwafunga Mikanda Maalum ya Mawasiliano (GPS - Satellite Collars) ili kupata taarifa za moja kwa moja zinazoonyesha mienendo yao na kuwadhibiti kabla hawajasababisha madhara kwa binadamu. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau imenunua Mikanda Maalum ya Mawasiliano (GPS - Satellite Collars) 54. Mikanda hii imefungwa kwa tembo viongozi wa makundi 45 katika Mifumo Ikolojia ya Serengeti (2), Burigi-Chato-IbandaRumanyika (6), Mkomazi-Handeni (7), Moyowosi-Kigosi (11), Ruaha-Rungwa (4), Tarangire-Manyara (5) na Nyerere-SelousMikumi (10). Aidha, simba watatu (3) na mbwa mwitu sita (6) wamefungwa mikanda ya mawasiliano katika Mfumo Ikolojia Selous-Nyerere-Mikumi. Vilevile, Wizara imenunua ndege nyuki (drones) 17 na mabomu baridi 12,072 kwa ajili ya kuwadhibiti tembo katika maeneo yenye changamoto. Aidha, taratibu za manunuzi za ndege nyuki (drones) 18 na mabomu baridi 4,512 zinaendelea. Matumizi ya teknolojia hizo yamewezesha kupata taarifa kwa haraka na kurejesha makundi ya tembo kwenye hifadhi.

Kushoto ni Askari wa Uhifadhi akijiandaa kurusha Ndege nyuki (drone) inayotumika katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika makazi ya watu na kulia ni ndege nyuki ikiwa imerushwa.

40. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara kupitia TANAPA na NCAA imekamilisha ujenzi wa vituo vinne (4) vya askari wa uhifadhi wa wanyamapori katika Wilaya za Korogwe, Same, Namtumbo na Ruangwa. Aidha, ujenzi wa vituo sita (6) katika wilaya za Bunda, Serengeti, Bariadi, Kalambo, Kilwa na Mbarali unaendelea. Sambamba na ujenzi wa vituo hivyo, Wizara kupitia TAWA imeendelea kuweka vituo vya muda vya askari kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika Wilaya 40 zikiwemo Manyoni, Itigi, Morogoro Vijijini, Chalinze, Meatu, Bariadi, Itilima, Buchosa, Tunduru, Liwale, Kaliua, Nachingwea, Handeni, Simanjiro na Babati. Hatua hii itasaidia katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa haraka katika maeneo mbalimbali nchini.

Kushoto ni Kituo cha Askari katika Kijiji cha Machang'anja, Wilaya ya Ruangwa na kulia ni Kituo cha Askari katika Kijiji cha Mheza, Wilayani Same.

41. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Wizara imeajiri askari 542 na kuwapanga kwenye vituo mbalimbali kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ikiwemo kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa uhifadhi, inaendelea kuimarisha uwezo wa jamii katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutoa mafunzo mbalimbali ikiwemo matumizi ya mabomu baridi kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 214 kutoka Halmashauri za Wilaya 40 zikiwemo Babati, Bunda, Ikungi, Karatu, Korogwe, Ludewa, Makambako, Makete, Mbarali, Mkinga, Monduli, Itilima, Manyoni, Chalinze, Lindi, Mvomero, Mwanga, Nachingwea, Njombe, Same, Serengeti na Wanging'ombe. Mafunzo haya yameongeza ufanisi na uwezo wa jamii katika kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu, hivyo kupunguza madhara kwa binadamu na mali zao. Vilevile, Wizara kupitia TAWA imeendelea kuwashirikisha VGS 184 na vikundi vya ulinzi shirikishi 230 katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini.

42. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo maalum kwa wakufunzi 170 kutoka Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Itigi, Wanging'ombe, Mbarali na Iringa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi 635,228 katika vijiji 945 vinavyopakana na maeneo ya hifadhi. Sambamba na hilo, Wizara imetoa semina kwa Maafisa Wanyamapori 122 wa Wilaya, Makatibu 50 wa Kamati za Kudumu za Bunge na wadau wengine wa uhifadhi. Vilevile, Wizara imenunua pikipiki 49 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uhifadhi

kwa Maafisa Wanyamapori wa Wilaya (22), WMA (7) na pikipiki 20 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye kanda 10 za kiikolojia za kupambana na ujangili. Juhudi hizi zimesaidia kujenga uelewa na kuimarisha ulinzi na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya wananchi.

43. Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara kupitia Taasisi zake za uhifadhi, ilifanikiwa kudhibiti matukio 4,012 ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, katika jitihada za kuokoa maisha ya wananchi na mali zao wakati wa kudhibiti matukio tajwa, wanyamapori wakali na waharibifu 296 walivunwa wakiwemo mamba 63, viboko 63, tembo 34, nyati 15, fisi 71, simba 10 na chui mmoja (1). Vilevile, simba 10 walihamishwa kutoka eneo la Kijiji cha Mdori na kupelekwa katika Mapori ya Akiba Rungwa (6) na Pande (4); nyani 90 waliondolewa Geita mjini na kupelekwa Msitu wa Hifadhi Kigosi; na Chui watatu (3) waliondolewa kijiji cha Nyichoka na kuhamishiwa Hifadhi ya Taifa Serengeti (1) na Bustani ya Wanyamapori Ruhila (2). Katika hatua nyingine, Wizara imelipa kiasi cha Shilingi 4,604,909,750 ikiwa ni kifuta jasho na machozi kwa wananchi 16,939 walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu kwa matukio yaliyotokea katika kipindi cha mwaka 2021 hadi kufikia Aprili, 2025 katika Halmashauri za Wilaya 78. Aidha, Wizara inaendelea na malipo ya kifuta jasho na machozi kiasi cha Shillingi 1,082,049,500 kwa wananchi 5,542 wa Halmashauri za Wilaya 18. Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu unadhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Nitoe rai kwa wadau wote kuiunga mkono Serikali katika jitihada hizi.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na uratibu wa kuongoa maeneo ya kimkakati ya uhifadhi ikiwemo eneo la Ghuba ya Speke na Bonde la Mto Kilombero ili kuwezesha ustahimilivu wa mifumo ikolojia ya Serengeti-Mara na NyerereSelous-Niassa. Hadi Aprili, 2025, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 61,863,151,045.85 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha uhifadhi katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Kilombero na Hifadhi ya Taifa Mahale. Kati ya kiasi

hicho, Shilingi 53,234,754,978.85 zimelipwa kwa kaya 3,493 na kuhamisha makaburi 618 katika Kata ya Nyatwali iliyopo eneo la Ghuba ya Speke Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara; Shilingi 1,681,882,027.00 zimelipwa kwa kaya 205 zilizofanyiwa uthamini katika kijiji cha Kalilani kilichopo Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma na Shilingi 6,783,714,589.20 zimelipwa kwa kaya 998 na kuhamisha makaburi 107 ya Kijiji cha Ngombo kilichopo katika Pori la Akiba Kilombero. Kiasi cha Shilingi 137,929,949.02 kwa ajili ya kuhamisha makaburi 26 na kaya 52 za kijiji cha Ngombo wahusika hawakujitokeza hata hivyo Serikali imeendelea kutoa matangazo ya kuhamasisha wananchi hao wajitokeze.

45. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022–2026. Mpango huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Rais–TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Maji; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi imefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kukamilisha Mwongozo wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori Nchini ambao unaainisha hatua mbalimbali za kuzingatiwa wakati wa kuongoa shoroba hizo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la STEP imekamilisha kazi ya kuongoa ushoroba wa UdzungwaNyerere ambao umetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 226 la tarehe 04 Aprili, 2025. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa viongozi na wananchi katika Manispaa ya Singida na Wilaya za Mkalama na Monduli ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya kusimika mabango 20 katika shoroba zilizopo katika maeneo hayo ili kutoa tahadhari kwa wananchi kuhusu uwepo wa shoroba za wanyamapori kwa lengo la kupunguza migongano na kuimarisha ustawi wa jamii katika maeneo hayo.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kusimamia Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori – WMAs wa Mwaka 2023 - 2033 kwa lengo la kuimarisha usimamizi

shirikishi wa rasilimali za wanyamapori. Hadi Aprili 2025, tathmini ya maeneo mapya yaliyopendekezwa kwa ajili ya kuanzisha Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori imekamilika katika maeneo manne (4) ikijumuisha Mawima (Uvinza), Ifinga (Madaba), Minyughe (Ikungi), na Ndonda (Nachingwea na Nanyumbu). Sambamba na hilo, Wizara imewajengea uwezo viongozi 312 wa WMA 12 zilizopo katika Ukanda wa Magharibi na Kusini kuhusu usimamizi na uendelezaji wa jumuiya hizo ili kuimarisha uhifadhi na maendeleo ya wananchi. Aidha, Wizara imefanya tathmini na ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Jumuiya 12 za Mbarang'andu, Kimbanda, Kisungule (Namtumbo); NALIKA, Chingoli (Tunduru); Magingo (Liwale); MUNGATA na Juhiwangumwa (Rufiji); Uyumbu (Urambo); Ipole (Sikonge); Mpimbwe (Mpimbwe); na ISAWIMA (Kaliua) za Ukanda wa Kusini na Magharibi kwa lengo la kubaini changamoto zinazozikabili na namna ya kuzitatua.

47. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ujangili nchini, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa mwaka 2023-2033 kwa kuratibu doria maalum zinazoongozwa na taarifa fiche kupitia Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili kwenye mifumo Ikolojia mbalimbali nchini na maeneo ya mpakani kati ya Tanzania, Kenya na Zambia. Doria maalum hizi zimewezesha kukamata jumla ya watuhumiwa 66, vipande 68 vya meno ya tembo, magamba 546 ya kakakuona, kobe 132, kenge 13 na aina mbalimbali ya mijusi 213 iliyokuwa ikisafirishwa kwenda nje ya nchi, bunduki mbili (2) na risasi 18 zilizokuwa zikitumika kwenye matukio ya ujangili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Uhifadhi imefanikiwa kuingiza mada zinazohusiana na masuala ya biashara haramu ya nyara kwenye mitaala inayotumika kufundishia vyuo vya Jeshi la Polisi nchini. Utaratibu huu umeimarisha uwezo wa Askari na Maafisa wa Jeshi la Polisi katika utambuzi wa nyara na mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wahalifu katika usafirishaji haramu wa nyara na mbinu za kukabiliana na vitendo hivyo.

48. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa, Wizara iliandaa Mkutano wa 14 wa Baraza la Usimamizi wa Mkataba wa Lusaka uliofanyika tarehe 06 hadi 08 Mei, 2025 Jijini Arusha. Mkutano huu ulihudhuriwa na washiriki 51

kutoka nchi 5 za Tanzania, Kenya, Zambia, Congo na Sudani Kusini pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNEP, UNODC na AWF. Mkutano huo umewezesha nchi wanachama kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu wa wanyamapori na misitu unaovuka mipaka. Aidha, Mkutano huu umechagua safu mpya ya uongozi kwa kipindi cha miaka miwili (2) ijayo ikiwajumuisha, Rais ambaye ni Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi H. Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Rosalie Matondo, Waziri wa Uchumi na Misitu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Picha ya kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akikabidhiwa Hati ya Mkataba wa Lusaka na Waziri wa Utalii na Wanyamapori wa Jamhuri ya Kenya na Rais wa Baraza la 13 la Uongozi, Mhe. Rebecca Miano ikiwa ni ishara ya kukabidhi kijiti cha Urais wa Baraza kwa Mhe. Balozi Chana na

Picha ya kulia ni Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akimkabidhi kinyago cha faru Mhe. Miano ikiwa ni ishara ya kupokea kijiti cha nafasi ya Urais wa Baraza la Usimamizi la Mkataba wa Lusaka katika Mkutano wa 14 wa Baraza hilo.

4.3.1.2 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania -TWPF

49. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Doria maalum za kuzuia ujangili zinazotekelezwa na Kikosi Kazi

Taifa Dhidi Ujangili, kuidadi wanyamapori nchi nzima; vyuo vya mafunzo kutekeleza majukumu yake; utatuzi wa migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishaji hadhi maeneo ya hifadhi; uanzishaji na uendelezaji wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwa jamii (WMAs); utoaji elimu ya uhifadhi kwa wananchi; uratibu wa uhifadhi wa faru nchini; uongoaji wa shoroba za wanyamapori; utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia katika Sekta ya Wanyamapori; kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi.

4.3.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

50. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kuboresha uhifadhi, kuimarisha mahusiano na jamii na kuendeleza miundombinu ya utalii. Hadi kufikia Aprili 2025, Shirika limefanya doria 36,411 ambapo watuhumiwa 3,450 wa makosa mbalimbali ya ujangili walikamatwa. Aidha, silaha 43 (shortgun 10 na gobore 33) na mitego ya nyaya 13,276 iliyokuwa ikitumika kuwatega wanyamapori zilikamatwa na kuteguliwa. Sambamba na hilo, Shirika limeendelea kutumia teknolojia za kisasa kuboresha usimamizi na ulinzi wa wanyamapori, ikiwemo matumizi ya visukuma-mawimbi, doria kwa kutumia ndege, na uwekaji wa alama za masikio kwa faru. Hatua hizi zimechangia kuimarika kwa usalama wa hifadhi na kupunguza matukio ya ujangili.

Baadhi ya mitego ya nyaya na silaha zilizokamatwa katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

51. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mahusiano kati ya Hifadhi za Taifa na wananchi waishio pembezoni hususan kupitia Mpango wa Ujirani Mwema, Shirika limechangia utekelezaji wa jumla ya miradi 47 katika katika Sekta za Afya (4), Elimu (21), Maji (10), Ulinzi (8) na Uchumi (4) katika Wilaya za Bunda, Tarime, Kaliua, Kyerwa, Karatu, Arumeru, Serengeti, Bariadi, Kalambo, Mbarali, Kilwa, Ruangwa, Tunduru, Kigoma, Hai, Chato, Mwanga, Mpanda, Urambo, Biharamulo, Makete, Rufiji, Uvinza, Korogwe, Kondoa, Simanjiro, Babati, Liwale, Moshi, Rombo na Longido. Miradi hii pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi imewezesha kuboresha mahusiano na jamii; na kudhibiti matukio mbalimbali ya uhalifu sambamba na jamii kupata taarifa zinazohusu uhifadhi. Sambamba na hilo, Shirika limekamilisha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 18 (10 vya Wilaya ya Tanganyika na 8 vya Wilaya ya Uvinza) na kutoa mafunzo ya COCOBA kwa vikundi 36 vyenye wanachama 659 katika Wilaya za Bariadi, Tarime na Bunda kupitia Hifadhi ya Taifa Serengeti. Kuendeleza vikundi vya kukuza uchumi katika Wilaya za Busega, Meatu na Itilima. Aidha, Shirika limekarabati barabara za mchepuko zenye urefu wa kilomita 73.52 (Wilaya ya Serengeti kilometa 27.82 zenye makalavati 5 na Wilaya ya Ngorongoro kilometa 46.7).

52. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kudhibiti mimea vamizi katika maeneo ya hifadhi ili kukabiliana na athari zinazosababishwa na mimea hiyo ndani ya hifadhi. Hadi kufikia Aprili 2025, mimea vamizi imeondolewa katika eneo lenye ukubwa wa hekta 2,400.23 kwenye Hifadhi za Taifa Arusha, Burigi-Chato, Gombe, Ibanda-Kyerwa, Katavi, Kitulo, Ziwa Manyara, Mikumi, Mkomazi, Nyerere, Ruaha, Kisiwa cha Rubondo, milima ya Mahale na Rumanyika-Karagwe. Vilevile, Mpango wa usimamizi wa moto katika Hifadhi ya Taifa Nyerere umeandaliwa. Hatua hii imesaidia kuhakikisha makazi na malisho ya wanyamapori yanaendelea kuwa ya asili kwa ajili ya kuimarisha mifumo ikolojia.

53. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Shirika limeendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara zenye urefu wa kilomita 2,403.4 katika Hifadhi za Taifa Arusha (97), Katavi (247), Kilimanjaro (73),

Kitulo (26), Ziwa Manyara (85.4), Mikumi (87.5), Mkomazi (116.5), Ruaha (371), Kisiwa cha Rubondo (23), Saadani (118), Serengeti (682), Tarangire (113), BurigiChato (84), Ibanda-Kyerwa (43), Rumanyika-Karagwe (19) na Nyerere (218). Aidha, ujenzi wa daraja la Matete katika Hifadhi ya Taifa Tarangire umefikia asilimia 68 ya utekelezaji. Shirika pia limekamilisha ukarabati mkubwa wa viwanja vya ndege vitatu (3) vya Lobo, Kusini na Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Shirika limeendelea kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwa viwanja sita (6) vya ndege katika hifadhi za Taifa za Saadan (1), Mkomazi (1), Ruaha (1), Serengeti (2) na Katavi (1) ili kuimarisha usalama wa usafiri wa anga na kuvutia watalii zaidi kutembelea hifadhi hizo.

Ukarabati wa viwanja vya ndege vya Lobo, Kusini na Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

54. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea na ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya nyota tatu katika eneo la Rubambagwe wilayani Chato chini ya Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Aidha, Shirika limeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mabanda matatu (3) ya wageni (cottages) katika eneo la Horombo Hut yenye uwezo wa kubeba vitanda 90 na ujenzi wa vyoo vya wageni katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, banda 1 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, vibanda vitano (5) vya kupumzikia wageni (visitor's sheds) katika Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na kuweka samani katika hosteli ya Hifadhi ya Taifa Saadani. Vilevile, Shirika limejenga malango saba (7) ya kuingilia wageni katika hifadhi za Taifa Serengeti (2), Tarangire (1), Nyerere (2), Ibanda-Kyerwa (1) na Mkomazi (1). Miundombinu hii imelenga kuboresha huduma za utalii na

ukusanyaji wa mapato. Kwa upande mwingine, Shirika limejenga kituo cha taarifa katika eneo la Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Lango la kuingilia wageni (Machochwe Gate) katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

55. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi na kupanua wigo wa shughuli za utalii, Shirika limeendelea kuibua na kuendeleza mazao mapya ya utalii, ikiwemo ujenzi wa uwanja wa mpira wa gofu katika Hifadhi ya Taifa Serengeti ambao umefikia asilimia 60 ya utekelezaji wake ikiwa ni ujenzi wa jumla ya mashimo 18, visima (2), mabwawa (2), miundombinu ya maji na umeme. Aidha, ujenzi wa daraja la juu lenye urefu wa kilometa moja katika Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa umekamilika kwa asilimia 67. Vilevile, Shirika limeanzisha utalii wa kuogelea kwenye chemchem ya maji moto katika Hifadhi ya Taifa Ruaha; utalii wa kuruka kwa ndege ndogo katika hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Arusha na Ziwa Manyara na utalii wa kulala nje kuangalia nyota katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanzisha utalii wa faru katika Hifadhi za Taifa za Burigi-Chato na Mikumi unaendelea.

56. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kurusha matangazo ya moja kwa moja, kushiriki matukio ya utalii na kutumia mitandao ya kijamii ili kuvutia watalii kutembelea hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika

lilishiriki katika matukio 11 ya utalii ndani ya Nchi yakiwemo Land rover festival, Zanzibar Tourism and Investment Show, Wiki ya Mwanakatavi, Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa Tanzania (TIFAD), Sabasaba, NaneNane, KILI FAIR, Kizimkazi Festival, Karibu Kusini na Majimaji Festival Vilevile, Shirika limeshiriki katika maonesho manne (4) ya kimataifa ambayo ni World Travel Market (WTM) Uingereza, Qatar International Exhibition for Travel & Tourism (MART), International Gita Mahotsav 2024 in India na Swahili International Tourism Festival (SITE) Tanzania.

57. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutambulika kimataifa na kushinda tuzo tatu (3) za kimataifa na tuzo moja (1) nchini za kutambua umahiri na ubora katika kutoa huduma, uhifadhi na utalii pamoja na uandaaji wa taarifa za fedha. Tuzo hizo ni ile ya utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa iliyotolewa na Shirika la Utafiti wa Ubora (European Society for Quality Research – ESQR), ambapo Shirika limeshinda kwa mara ya tano mfululizo kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Aidha, Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kushikilia nafasi ya kwanza duniani kama Hifadhi Bora Barani Afrika (Africa's Leading National Park) kwa miaka sita mfululizo kuanzia 2019 hadi 2024, huku Mlima Kilimanjaro ukishinda tuzo ya Kivutio Bora cha Utalii Barani Afrika kwa mwaka 2024. Vilevile, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imetambuliwa kama eneo la pili bora zaidi duniani kwa safari na utalii na gazeti la The Times of India (World's Second-Best Destination by Times of India, 2024). Tuzo hizi zinatarajiwa kuwahamasisha wadau kuendelea kutoa huduma bora katika sekta ya utalii.

58. Mheshimiwa Spika, kufuatia juhudi hizo zilizofanywa na Shirika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya watalii 1,285,876 walitembelea hifadhi za Taifa na kuwezesha makusanyo ya **Shilingi 433,612,732,617.63** sawa na asilimia 100.64 ya lengo la makusanyo ya **Shilingi 430,864,198,480.00** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

59. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wake, Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba za watumishi 30 katika Hifadhi za Taifa za Mkomazi (8), Nyerere (12),

Ruaha (5), Burigi-Chato (3), Rumanyika-Karagwe (1) na Milima ya Mahale (1). Sambamba na hilo mifumo mipya ya nishati ya jua imewekwa katika vituo 12 vya askari Hifadhi ya Taifa Serengeti na utafiti wa maji (hydrological survey) katika vituo 2 vya askari umefanyika pamoja na kukarabati visima vinne (4) vya mafuta katika Hifadhi ya Taifa Nyerere. Aidha, Shirika limeajiri watumishi 550 wa kada mbalimbali na kufikia asilimia 76.5 ya uhitaji wa watumishi katika Shirika. Vilevile, Shirika limewezesha watumishi 115 kufanya mafunzo ya muda mrefu na watumishi 227 mafunzo ya muda mfupi. Kwa upande mwingine, Shirika limenunua malori 5 kwa ajili ya hifadhi za Taifa za Serengeti 2 na Nyerere 3, mitambo 5 ya kutengeneza barabara Hifadhi ya Taifa Serengeti (grader 2, compactor 1, excavator 1 na back hoe loader 1), na injini za boti tatu (3) katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

4.3.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

60. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa wanyamapori ili kudhibiti ujangili, uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na biashara haramu ya nyara kwa kufanya doria 12,586. Kupitia doria hizo, jumla ya mifugo 48,126 na watuhumiwa 2,513 wamekamatwa. Aidha, kupitia doria hizo bunduki 62, risasi 795 zimekamatwa na mitego 2,061 ya nyaya za kutegea wanyamapori imeteguliwa. Vilevile, katika kuongeza nguvu kazi Mamlaka imeajiri askari 221 wa ajira ya kudumu na askari 280 wa ajira ya muda mfupi.

61. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na shughuli za utalii, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya askari katika Pori Tengefu Lunda Nkwambi (1) na Mapori ya Akiba Wami-Mbiki (1) na Lwafi (1). Aidha, Mamlaka imekarabati vituo vinne (4) vya askari katika Pori la Akiba Maswa, kukamilisha ujenzi wa uzio katika bustani ya Wanyamapori Ruhila na ujenzi wa eneo la kupumzika wageni (Tourism Lounge) katika Pori la Akiba Mpanga-Kipengere upo katika hatua za mwisho kukamilika. Vilevile, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 120.5 katika Pori la Akiba Pande (km 10.5), Rungwa (km 80) na

Makuyuni (km 30). Pia, ujenzi wa barabara unaendelea katika Mapori ya Akiba Wami-Mbiki na Mpanga-Kipengere.

62. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kutatua migogoro ya mipaka katika maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za mipaka ambapo hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya vigingi 691 vimesimikwa katika Pori la Akiba Kilombero. Aidha, uhakiki wa mipaka ya Mapori ya Akiba Selous na Swagaswaga umekamilika na taratibu za utangazaji kwenye Gazeti la Serikali zinaendelea. Katika hatua nyingine, Mamlaka imekamilisha uandaaji wa Mipango ya Jumla ya Usimamizi (GMP) kwa Mapori ya Akiba Rukwa, Lukwika-Lumesule, Liparamba na Msanjesi.

63. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kutangaza uwindaji wa kitalii, utalii wa picha pamoja na fursa za uwekezaji kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Mamlaka imeshiriki katika maonesho matatu (3) ya Kitaifa ambayo ni; Maonesho ya Biashara ya 48 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane na Kizimkazi Festival (Zanzibar). Aidha, Mamlaka imeshiriki onesho moja (1) la Kikanda la East Africa Trade Fair (Mwanza) na maonesho saba (7) ya Kimataifa ambayo ni Energy Summit (Dar es Salaam), Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2024), Dallas Safari Club International - USA, WTM Africa (Cape Town), International Road show, Conservation and Trade in elephant Specimen (Botswana) na Tourism Investment Forum Africa (Cape Town). Kufuatia juhudi hizo, idadi ya watalii waliotembelea maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka kwa ajili ya shughuli za utalii imeongezeka na kufikia watalii wa picha 209,522 ikilinganishwa na watalii 155,037 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 35.14 na idadi ya wawindaji imeongezeka kufikia 530 ikilinganishwa na wawindaji 484 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 9.5.

64. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imesaini mikataba mitatu (3) ya uwekezaji katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni (1), Pori la Akiba Kijereshi (1) na Mkataba wa Uwekezaji Mahiri kwenye Maeneo ya Wanyamapori (Special Wildlife Investment Concession Areas - SWICA) kwa kitalu cha uwindaji katika Pori la

Akiba Selous (1) ambapo Kupitia uwekezaji huo, Serikali inatarajia kupata Shilingi bilioni 3.33 kwa mwaka. Kwa ujumla, kupitia uwekezaji na shughuli za utalii Mamlaka imeendelea kukusanya mapato ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya Shilingi 65,935,682,043.68 sawa na asilimia 69.73 ya lengo la makusanyo ya Shilingi 94,558,757,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

65. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha mahusiano kati ya hifadhi na jamii na kuhakikisha wananchi wananufaika na uhifadhi, Serikali imeendelea kurejesha stahili kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 14, Halmashauri za Wilaya 29 na Vijiji 100 ambapo jumla ya Shilingi 17,101,288,431.08 zimetolewa. Aidha, TAWA imechangia jumla ya shilingi 162,036,860.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa na jamii. Miongoni mwa miradi hiyo ni kuchimba kisima katika Wilaya ya Rufiji; ununuzi wa madawati 295, meza mbili (2) na viti viwili (2) kwa ajili ya shule nane (8) za Wilaya za Bariadi (3) na Itilima (5); ununuzi wa viti 16 na meza tano (5) kwa zahanati ya Visakazi iliyopo Wilaya ya Chalinze; ununuzi wa madawati 300 kwa shule sita (6) za Sekondari katika Wilaya ya Longido; ununuzi wa mifuko 325 ya saruji kwa ajili ya kuchangia miradi ya ujenzi katika Wilaya ya Makete (40), Wanging'ombe (40), Mbarali (45), Sumbawanga (75), Chemba (100) na Nanyumbu (25); na kuchangia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Zahanati za Kyanyari Wilaya ya Butiama na Ruvu Mbuyuni Wilaya ya Same. Mamlaka pia, imeendelea kuratibu shughuli za Uvuvi na Ufugaji Nyuki katika Mapori ya Akiba ya Ugalla, Uwanda, Moyowosi, Rukwa na Kilombero ambapo jumla ya wavuvi 20,914 na wafugaji nyuki 131 kutoka vijiji 98 katika Wilaya 12 walipewa vibali.

66. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi mbili (2) katika Pori la Akiba Muhesi na Kanda ya Ziwa (Bunda); ukarabati wa nyumba 12 katika Pori la Akiba Selous na kukamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuuzia nyara katika mikoa ya Arusha na Mwanza. Aidha, Mamlaka imenunua magari saba (7) ya doria, mitambo miwili (2) na gari aina ya boza la maji moja (1) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara. Vilevile, ujenzi wa ofisi tatu (3) kwa ajili ya Kanda ya Magharibi (1) na Mapori ya Akiba

Wami-Mbiki (1) na Kilombero (1) unaendelea. Vilevile, Mamlaka imewezesha watumishi 44 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 454 mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ikiwemo udereva, urubani, ufuatiliaji na tathmini, usalama wa kimtandao (Cyber Security), ukakamavu, na upelelezi wa makosa dhidi ya wanyamapori. Aidha, Mamlaka ilishiriki katika mashindano ya SHIMUTA yaliyofanyika katika mkoa wa Tanga na kufanikiwa kupata medali ya fedha katika mchezo wa kuvuta kamba na medali moja ya shaba katika mchezo wa riadha.

Mitambo ya ujenzi wa barabara na jengo la ofisi ya Pori la Akiba Muhesi.

4.3.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)

67. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea na ulinzi wa maliasili na malikale zilizopo ndani ya Hifadhi kwa kufanya doria 4,592. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 331, mifugo 11,332, meno ya tembo 11, vipande vya meno ya tembo 27 na bunduki 1 pamoja na kutegua mitego 153 ya nyaya za kutegea wanyamapori. Aidha, Mamlaka imejenga vituo viwili (2) vya askari katika Bonde la Kreta ya Ngorongoro kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na ufuatiliaji wa wanyamapori. Katika hatua nyingine, Mamlaka imesafisha mpaka wa kilomita 85, kuweka vigingi 22 na kukarabati vigingi saba (7) kwa ajili ya alama ya mpaka wa eneo la Hifadhi hatua hii itawezesha kupunguza migogoro ya mipaka kati ya eneo la hifadhi na wananchi na matukio ya moto holela. Kwa upande mwingine, Mamlaka imetoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kukabiliana na

changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, mimea vamizi na mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya mikutano 112 katika wilaya za Karatu (41), Meatu (15) Monduli (12) na Ngorongoro (44) ambapo jumla ya wananchi 4,402 walifikiwa.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuendeleza uhifadhi wa faru nchini, Mamlaka imeongeza jumla ya faru weupe 17 kutoka Afrika Kusini. Faru hawa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuimarisha mfumo ikolojia katika hifadhi na ushirikiano baina ya Serikali ya Afrika Kusini na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la uhifadhi wa wanyamapori. Aidha, katika kuhakikisha faru hawa wanahifadhiwa kikamilifu, Mamlaka imejenga boma moja (1) kwa ajili ya ufuatiliaji na uangalizi wa karibu miendendo yao. Vilevile, Askari wawili (2) wamepatiwa mafunzo mahsusi kwa ajili ya uangalizi wa faru hawa. Halikadhalika, Mamlaka imeendelea kuboresha ulinzi wa faru kwa kuwawekea alama maalum za utambuzi na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao.

Kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) na Kiongozi wa Kimila kutoka Afrika Kusini, iNkosi Zwelinzima Gumede wakisaini Hati ya Makabidhiano ya faru weupe kutoka Afrika Kusini katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kulia ni baadhi ya faru hao.

69. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha nyanda za malisho ya wanyamapori, Mamlaka imeendelea na juhudi za kudhibiti mimea vamizi (Invasive Plant Species) kwa kufyeka na kung'oa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 460 pamoja na kuchoma moto eneo lenye ukubwa wa hekta 3,098 kwa

utaratibu wa moto mpango (prescribed burning) ndani ya Bonde la Kreta na eneo la Ndutu.

70. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Utalii, Mamlaka imeendelea kuimarisha miundombinu ya utalii kwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Enduleni -Ndutu yenye urefu wa kilomita 34.5 kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Mamlaka imekarabati mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 369 unaojumuisha barabara kuu ya Loduare hadi Golini (km 88), barabara za bonde la Kreta (km 110), View point hadi Nayobi (km 78), Golini hadi Ndutu (km 23), na mtandao wa Ndutu (km 70) na kukarabati kiwanja kidogo cha ndege cha Ndutu. Vilevile, Mamlaka imekamilisha zoezi la kuweka vibao 150 vya maelezo na maelekezo katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Hifadhi na ujenzi wa view point tatu (3) katika eneo la Seneto, Empakai na Gilai. Sambamba na hilo, Mamlaka imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya umeme, vyoo na mifumo ya maji katika maeneo yanayotumiwa na watalii katika maeneo ya Loduare, Ngoitoktok, Olduvai, Seneto ya Juu, Seneto ya Chini, Lerai picnic site, Nyati Public campsite na View point.

Muonekano wa barabara kuu ya Loduare hadi Golini iliyoboreshwa katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

71. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza thamani ya vivutio vya malikale, Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai katika eneo la Kamny Wilaya ya Karatu ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95. Sambamba na hilo, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa majengo maalum mawili (2) ya kuhifadhi nyayo za zamadamu,

choo kimoja (1) na vibanda viwili (2) kwa ajili ya kupumzikia wageni katika eneo la nyayo za Laetoli. Vilevile, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya maji katika kituo cha utalii cha Kimondo kilichopo Mbozi-Songwe na kuendelea na ujenzi wa lango la kuingilia kwenye mapango ya Amboni-Tanga.

Mradi wa ujenzi wa makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai katika eneo
la Kamny, Wilaya ya Karatu.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), akiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea eneo la Mapango ya Amboni, Tanga.

72. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kutangaza vivutio vya utalii kwa kufanya kampeni tatu (3) kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani ambazo ni Merry and Wild - Ngorongoro awaits, Diko la Amboni na Mwanamke Talii, Twenzetu Ngorongoro. Aidha, Mamlaka imeshiriki katika maonesho 12 ndani ya nchi na maonesho sita (6) nje ya nchi. Juhudi hizi zimechangia kuleta matokeo chanya hususan katika kuongeza idadi ya watalii waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya watalii 925,163 walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na idadi ya watalii katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Idadi hii ya watalii imewezesha Mamlaka kukusanya jumla ya Shilingi 231,186,145,522.22 sawa na asilimia 100.52 ya lengo la Shilingi 230,000,000,000.00 zilizopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

73. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea na jukumu la kuendeleza jamii ya wenyeji waishio ndani ya Hifadhi kwa kutoa ufadhili wa ada, fedha ya kujikimu na nauli kwa wanafunzi 1,683 katika ngazi mbalimbali za elimu ikiwemo; Chuo Kikuu (52), vyuo vya kati (245) na sekondari (1,386). Aidha, hadi kufikia Aprili, 2025 Mamlaka imegawa kilo 1,200 za sukari na kilo 13,075 za unga wa mahindi kwa ajili ya huduma ya uji katika shule 27 zilizopo ndani ya eneo la Hifadhi. Vilevile, Mamlaka imewezesha utoaji wa huduma za afya bure kwa wakazi katika Zahanati ya Ngorongoro.

74. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha watumishi wanatekeleza majukumu yao kwa weledi, Mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya kitaaluma. Hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya watumishi 612 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nyanja za uongozi, itifaki, maadili, kanuni za jumla za Jeshi la Uhifadhi, matumizi ya silaha ndogo na urubani wa ndege nyuki. Aidha, Mamlaka imewezesha watumishi 45 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 21 mafunzo ya awali ya Jeshi la Uhifadhi ili kuweza kutekeleza majukumu yao na kuboresha utendaji kazi. Vilevile, Mamlaka imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Kamyn, Wilayani Karatu ambao ujenzi umefikia asilimia 87.

Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro katika eneo la Kamyn, Wilayani Karatu

4.3.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

75. Mheshimiwa Spika, TAWIRI ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori nchini kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau namna bora ya uhifadhi endelevu na maendeleo ya utalii. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, TAWIRI imetekeleza zoezi la kuidadi wanyamapori nchi nzima. Hadi kufikia sasa, zoezi limekamilika katika mifumo ikolojia sita (6) yenye maeneo makubwa zaidi kati ya 11, ikiwemo Katavi–Rukwa, Ruaha–Rungwa, Nyerere–Selous– Mikumi, Ziwa Natron–Kilimanjaro Magharibi, Mkomazi–Handeni na Tarangire–Manyara yenye ukubwa wa kilometa za mraba 241,537 sawa na asilimia 73.3 ya eneo lote linalotakiwa kufanyiwa sensa ambalo ukubwa wake ni kilometa za mraba 329,537. Aidha, mifumo ikolojia iliyosalia inategemewa kukamilika kabla ya mwaka wa fedha kumalizika. Matokeo ya awali yanaonesha kuendelea kuimarika kwa aina na idadi ya wanyamapori ikiwa ni kiashiria cha kuimarika kwa uhifadhi, jambo ambalo litaendeleza utalii.

Zoezi la kuidadi wanyamapori kwa njia ya anga kwa kutumia ndege ndogo na teknolojia ya kamera za kisasa na namna mpya ya upigaji picha kutoka angani ijulikanayo kama "Oblique Camera Count".

76. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kubuni teknolojia ili kuboresha namna ya kuhesabu wanyamapori kwa njia ya anga. Ubunifu huu umejikita katika teknolojia ijulikanayo kama Oblique Camera Count, ambayo inatumia kamera za kisasa zaidi na namna mpya ya upigaji picha za wanyamapori kutoka angani wakati wa zoezi la sensa na matumizi ya akili mnemba katika kutambua spishi na idadi ya wanyamapori waliopigwa picha. Teknolojia hii inatumika kwa mara ya kwanza nchini kwenye zoezi la sensa za wanyamapori zinazoendelea, sambamba na ile ya awali ili kuweza kupata ulinganifu wa ubora wa matokeo. Matokeo ya awali yanaonesha matumizi ya teknolojia hii yameongeza ufanisi katika zoezi la sensa, kupunguza gharama na muda wa kupata matokeo.

77. Mheshimiwa Spika, Taasisi pia imetekeleza miradi 13 ya utafiti, iliyojikita katika kutatua changamoto za uhifadhi zikiwemo: migongano kati ya binadamu na wanyamapori (4), matumizi ya teknolojia katika uhifadhi (1), afya ya mifumo ikolojia (2), nyuki na

mazao yake (1), mahusiano ya viumbe na ikolojia zao (3), uhifadhi wa bioanuai (1) na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia (1). Aidha, Taasisi imeratibu na kusimamia miradi ya utafiti 100 yenye jumla ya watafiti 326 wa ndani na nje ya nchi waliosajiliwa. Matokeo ya tafiti hizi yanalenga kutatua changamoto za uhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori na kuendeleza utalii.

78. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha afya za wanyamapori, Taasisi imeendelea kufanya tafiti na ufuatiliaji wa magonjwa ya wanyamapori yanayoweza kuathiri uhifadhi na utalii. Kwa kipindi hiki, tafiti na ufuatiliaji zimefanyika katika mifumo ikolojia ya Kaskazini Magharibi na Kusini mwa Tanzania ambapo jumla ya sampuli 1,050 zilikusanywa kwa ajili ya uchunguzi. Matokeo yameonesha kutokuwepo kwa vimelea vya milipuko ya magojwa ya wanyamapori ambayo yangeweza kuleta athari kwenye uhifadhi na maendeleo ya utalii.

79. Mheshimiwa Spika, Taasisi pia imefanya utafiti wa nyuki wa kujua namna matumizi tofauti ya ardhi yanavyoathiri utendaji kazi na uzalishaji wa makundi ya nyuki. Utafiti huu unafanyika katika manzuki tatu (3) zilizopo katika maeneo ya West Kilimanjaro ambapo kuna mashamba ya miti (plantation forests), Magugu kwenye mashamba ya mazao (agricultural areas), na kituo cha Tabora kwenye misitu ya asili (natural forests). Matokeo ya awali yameonesha kwamba tabia na shughuli za makundi ya nyuki zinatofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na matumizi tofauti ya ardhi. Aidha, kwa upande wa uzalishaji (utunzaji wa chavua na asali), maeneo ya mashamba ya miti (plantation forests) yameonesha kuwa na sifa bora zaidi ikifuatiwa na maeneo yaliyozungukwa na ardhi ya kilimo (agricultural areas) na mwisho ni maeneo ya misitu asilia.

80. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji kazi na uwezo wa taasisi kutoa huduma, watumishi 11 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 35 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi 23 wameajiriwa ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi. Kwa upande mwingine, Taasisi imekamilisha ujenzi mfumo wa TEHAMA na

kuanza kutumia kwa lengo la kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori na tayari umeunganishwa na mfumo wa Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) unaowezesha usajili na upatikanaji wa vibali vya utafiti kidijitali.

4.3.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA – CAWM

81. Mheshimiwa Spika, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo kuanzia Cheti cha Msingi, Cheti cha Ufundi, Stashahada ya kawaida, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Vilevile, Chuo kina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,216 sawa na asilimia 122 ya lengo la wanafunzi 1,000 ambapo wanafunzi 457 ni wanawake na 759 ni wanaume. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 257 (watanzania 227 na wa nje 30). Washiriki kutoka nje ya Tanzania walitoka katika nchi za Ethiopia tisa (9), Kenya nane (8), Rwanda tatu (3), Saudi Arabia sita (6) na Uganda wanne (4). Mafunzo yaliyotolewa ni uongozaji wa watalii wa kupanda mlima (Mountain Guide Course), waongozaji wa wageni (Safari guides), waangalizi wa mazingira na ufuatiliaji wa kidijitali wa matukio ya ujangili. Katika hatua nyingine, Chuo kimeandaa mitaala 9 ya kozi za muda mrefu na mitaala 13 ya kozi za muda mfupi katika Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa taka.

82. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Chuo kimekamilisha ujenzi wa jengo la mafunzo la ghorofa mbili lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na ofisi za wahadhiri pamoja na kuweka samani, kufunga kompyuta 25 na projector 10 katika jengo hilo. Aidha, ujenzi wa darasa, jiko, vyoo na mabafu unaendelea katika eneo la mafunzo kwa vitendo lililoko Kijiji cha Arash, Tarafa ya Loliondo. Vilevile, ukarabati wa nyumba nne (4) za watumishi, vyumba vitano (5) vya madarasa, hosteli mbili (2) za wanafunzi umefanyika na kuweka taa za barabarani ili kuimarisha usalama. Sambamba na hilo, Chuo kimenunua mini bus (Coaster) (1), magari mawili (2) maalum aina ya KAMAZ pamoja na mahema 50, magodoro 70 na GPS 20 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

83. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Wanyamapori na Utalii, Chuo kinafanya tafiti katika nyanja za Bioanuwai, Uhifadhi wa mazingira na jamii ya mimea, Uhifadhi wa wanyamapori, Magonjwa ya wanyamapori na binadamu, Usimamizi wa utalii na Migogoro baina ya wanyamapori na binadamu katika maeneo mbalimbali nchini. Miongoni mwa Tafiti hizo zimewezesha ugunduzi wa viuatilifu hai (biopesticides) vya kupambana na wadudu waenezao magonjwa kwa wanyama na wadudu waharibifu wa mazao na kutatua baadhi ya changamoto za uhifadhi wa wanyamapori na utalii nchini.

84. Mheshimiwa Spika, kutokana na tafiti hizo, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Dkt. Never Mwambela alitunukiwa tuzo mbili za kutambua ubora wa matokeo ya tafiti na ubunifu katika kutatua changamoto za uhifadhi wa mazingira ambazo ni Tuzo ya kiuatilifu hai bora kinachochangia kuhifadhi mazingira (Agro-ecological Food Futures Prize) iliyotolewa na Taasisi ya Biovision ya nchini Switzerland; na Tuzo ya Mtafiti bora Barani Afrika juu ya ubunifu bioanuai zinazochochea uhifadhi wa mazingira (European Coimbra Award for Young African Researchers) iliyotolewa na Umoja wa Ulaya.

85. Mheshimiwa Spika, Chuo kimetekeleza Mradi wa ukusanyaji wa taarifa za uwindaji haramu katika Mapori ya Akiba ya Mkungunero, Maswa, Kijereshi na Swagaswaga. Kupitia mradi huo, viongozi wa hifadhi hizo na askari 40 wamejengewa uwezo wa kukusanya takwimu za uwindaji, wanyamapori wakali na waharibifu na kuandaa taarifa za kitaalamu kwa kutumia njia za kidijitali.

86. Mheshimiwa Spika, Chuo kimefanya Kongamano la Kimataifa la Biolojia ya Uhifadhi Kanda ya Afrika (African Congress on Conservation Biology – ACCB) ambalo ni kongamano la nne (4) kufanyika tangu kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo na ni mara ya kwanza kufanyika nchini. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki 201 kutoka nchi 24 duniani kwa lengo la kubadilishana taarifa za utafiti na kuwatambua wahifadhi na jamii zilizo mstari wa mbele katika masuala ya uhifadhi. Katika Kongamano hilo

jumla ya dhahania 210 za kisayansi zinazohusu Uhifadhi ziliwasilishwa. Kongamano hilo limewezesha Chuo kujitangaza kimataifa na washiriki kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya uhifadhi.

87. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kuwajengea watumishi uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa kuwawezesha watumishi 18 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 80 mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali. Aidha, watumishi 123 wamepatiwa mafunzo kuhusu maadili na mapambano dhidi ya rushwa.

4.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi – PWTI

88. Mheshimiwa Spika, Taasisi ina jukumu la kutoa mafunzo kwa kozi za uaskari wa Wanyamapori na uongozaji watalii, kutoa ushauri elekezi na kutoa mafunzo ya kozi za muda mfupi. Kufikia mwezi Aprili, 2025 Taasisi imedahili wanachuo 696 sawa na asilimia 87 ya lengo la wanachuo 800 waliotarajiwa kudahiliwa kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 158 wa kozi fupi ya Uaskari wa Misitu na hifadhi za fukwe na Uaskari Wanyamapori VGS (36) kutoka mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Simiyu, Pwani, Tanga na Arusha. Katika hatua nyingine, Mitaala miwili (2) ambayo ni Stashahada ya Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na Usalama imeandaliwa.

89. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya mafunzo, Taasisi imekarabati nyumba tano (5) za watumishi na uzio wa ukuta wenye urefu wa mita 240 kuzunguka eneo la Taasisi na ujenzi wa bweni litakalochukua wanafunzi wa kiume 240 unaendelea. Aidha, watumishi watatu (3) wamewezeshwa kuendelea na masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu na mtumishi mmoja (1) katika masomo ya Astashahada ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Himasheria. Sambamba na hilo, Taasisi imeshiriki katika maonesho ya ndani ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Wanyamapori Duniani pamoja na Siku ya Misitu Duniani kwa lengo la kutangaza kazi zake kwa wadau.

4.3.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga – CBCTC

90. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kimeanzishwa kwa lengo la kuijengea jamii uwezo kwa njia ya mafunzo ili iweze kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili kwa maendeleo endelevu. Hadi kufikia Aprili, 2025 kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 329, kati yao wanafunzi 158 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii na 171 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS). Aidha, Kituo kimeshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya 48 (Sabasaba), Maadhimisho ya Siku ya Wakulima (Nanenane), Siku ya Wanyamapori Duniani, na Siku ya Misitu Duniani na Kumbukizi ya Vita vya Majimaji kwa lengo la kujitangaza na kutoa elimu ya uhifadhi wa wanyamapori.

91. Mheshimiwa Spika katika kuboresha mazingira ya kufundishia na miundombinu, kituo kimeendelea na ujenzi wa darasa moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 150 kwa fedha za ndani. Sambamba na hilo, kituo kupitia ufadhili wa Serikali ya Ujerumani katika mradi wa "SECAD" kimekamilisha uchimbaji wa kisima, kujenga bweni moja (1) la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 ambalo limefikia asilimia 85, darasa moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 lililofikia asilimia 90 pamoja na mnara wa kuwekea tanki la maji uliofikia asilimia 87. Aidha, kituo kimewezesha mtumishi mmoja (1) kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi wawili (2) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili na Stashahada.

4.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

92. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta hizi unasimamiwa na Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 na

Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 270. Vilevile, jukumu la uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) Tabora, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) na Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC) Mafinga, Iringa. Pia, Serikali za Mitaa (Vijiji na Halmashauri) zina jukumu la kuhifadhi na kusimamia rasilimali hizo katika maeneo yao.

4.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

93. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa rasilimali za misitu na nyuki zinahifadhiwa na kusimamiwa ipasavyo, Wizara imeandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Matumizi ya Msumeno wa Moto, Tangazo la Serikali Namba 62/2025; na Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia kwenda Nje ya nchi, Tangazo la Serikali Namba 807/2024. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki, Tangazo la Serikali Namba 760/2023; Kanuni za Jumla za Mazao ya Misitu, Tangazo la Serikali Namba 59/2022 pamoja na kufanya marekebisho ya Kanuni ya Uzalishaji, Usafirishaji na Uuzaji wa Mkaa Mbadala, Tangazo la Serikali Namba 1085/2024. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kitaalam kuhusu Miti ya Mbao inayofaa kwenye Ujenzi na Kutengeneza Samani. Kwa upande mwingine, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) wa mwaka 2007. Matokeo ya tathmini yamebaini kuwa hali ya uhifadhi wa misitu iliyo katika utaratibu wa usimamizi shirikishi imeendelea kuimarika. Wizara inatoa wito kwa jamii kuendelea kushirikiana na Wizara kulinda na kuhifadhi misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

94. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kuelimishwa na kuhamasika kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Upandaji Miti Kitaifa. Maadhimisho haya ni utekelezaji wa maelekezo ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo lilielekeza kuwa kila tarehe 21 Machi ya kila mwaka iwe ni siku ya

maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na kuwataka nchi wanachama kuadhimisha siku hiyo. Kwa upande wa Tanzania, maadhimisho haya yalifanyika Mkoani Njombe na kuongozwa na Kaulimbiu "Ongeza thamani ya mazao ya Misitu kwa uendelevu wa rasilimali kwa kizazi hiki na kijacho''. Aidha, kupitia maadhimisho hayo wananchi walishiriki katika Kampeni ya Upandaji Miti iliyozinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kushiriki midahalo ya kujadili fursa zilizopo kwenye sekta ya misitu; zoezi la upandaji miti katika Wilaya zote za Mkoa wa Njombe na maonesho ya bidhaa za mazao ya misitu na huduma za utalii. Sambamba na tukio hili, Wizara inaratibu maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park hapa Jijini Dodoma kuanzia tarehe 17 hadi 20 Mei, 2025. Hivyo, natumia nafasi hii kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea maonesho haya kwa lengo la kujifunza na kupata huduma na bidhaa mbalimbali zinazotokana na ufugaji nyuki.

95. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kushiriki kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora. Mpango huu unalenga kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali kutoka tani 33,861 za sasa hadi kufikia tani 75,000 ifikapo Juni, 2035 na kuongeza mauzo ya mazao ya nyuki katika masoko ya kikanda na kimataifa. Aidha, Mpango unatarajiwa kuongeza ajira mpya 43,055 kupitia shughuli zilizopo katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki. Mpango utatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa na kusaini Hati ya Makubaliano ya usimamizi wa mradi wa ufugaji nyuki kati ya Wizara, WAGA WMA na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Kwa lengo la kuongeza wigo wa biashara ya asali, kwa niaba ya Serikali Wizara imesaini Itifaki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China inayoruhusu uuzaji wa Asali ya Tanzania nchini China. Utiaji saini wa Itifaki hii umefungua milango kwa wafanyabiashara wa Tanzania kuuza asali inayozalishwa nchini katika soko la nchini China. Sambamba na hili, Wizara imeratibu uzinduzi wa Alama ya

Asali ya Tanzania (Honey Trademark) yenye usajili TZ/T/2023/3136 uliofanyika Oktoba, 2024. Alama hii ni utambulisho wa asali ya Tanzania katika soko la kitaifa, kikanda na kimataifa. Kutokana na jitihada hizi za Serikali, napenda kutoa wito wafanyabiashara wa Tanzania kuendelea kuchangamikia fursa hizi ili kuweza kuongeza kipato kwa Taifa letu kupitia biashara ya mazao ya nyuki.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana (Mb) akizindua nembo ya asali ya Tanzania itakayotumika kuitambulisha bidhaa hiyo katika Soko la Dunia.

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki, kwa kuratibu vikao viwili (2) vya wadau wa misitu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), vikao saba (7) vya Kamati ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA) na vikao viwili (2) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC). Aidha, Wizara imezindua Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC) na kufanya Kikao kimoja (1) cha Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa. Wizara pia imefanya vikao vinne (4) baina ya Sekta binafsi na Serikali (Private Public Dialogue) kwa lengo la kutatua vikwazo vya kibiashara katika sekta ya misitu na kikao cha kujadili fursa za uendeshaji wa Biashara ya Mazao ya Misitu na Kilimo Misitu (Agroforestry). Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya Viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu katika mikoa ya Iringa na Njombe pamoja na viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki katika mikoa ya Tabora na Kigoma. Tathmini imebaini kuwa bado kwa sehemu kubwa viwanda vilivyopo vinafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na ufinyu wa malighafi. Wizara

inaendelea kuhimiza watu binafsi na Makampuni kuwekeza katika mashamba ya miti pamoja na mashamba makubwa ya kuzalisha asali. Sambamba na hilo, Wizara imetoa mafunzo kwa kampuni 48 za wafanyabiashara wa mazao ya misitu wa halmashauri za Mafinga, Mufindi na Njombe kuhusu utekelezaji wa kanuni na taratibu za uzalishaji na usafirishaji wa venia pamoja na mazao ya misitu yaliyohandisiwa. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa Wafugaji Nyuki Jumuiya WAGA WMA iliyopo Wilayani Mufindi, na Jumuiya ya Wafugaji Nyuki Muhesi na Mwakintaru za halmashauri ya Itigi. Katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (COP-29) kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Jijini Baku, Azerbaijan kwa lengo la kupata fursa za wawekezaji kwa ajili ya uhifadhi na shughuli za utalii unaozingatia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

4.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

97. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa lengo la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Aidha, Wakala unatekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo: Kuanzisha na kusimamia Misitu ya hifadhi, Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu, mashamba ya miti na manzuki ya Serikali kuu; Kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla (General Land) pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki.

98. Mheshimiwa Spika, Katika kuzuia uharibifu wa rasilimali za misitu na nyuki nchini, Wakala umefanya jumla ya doria 405 za kiintelijensia na doria 17,510 za kawaida katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Kupitia doria hizo, jumla ya watuhumiwa 3,459 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Aidha, doria hizo zimewezesha kukamatwa na kutaifishwa kwa magunia ya mkaa 36,625 yaliyovunwa bila kufuata utaratibu, mbao 40,621 zenye mita za ujazo 2,671, kuni zenye mita za ujazo 285 na magogo 1,267 yenye mita za ujazo 226.6. Pia mifugo 27,011, pikipiki 2,727, magari 297 na boti tatu (3) zilikamatwa na taratibu mbalimbali za kisheria zinaendelea. Katika hatua

nyingine, Wakala umeandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 62 yenye ukubwa wa hekta 775,917. Vilevile, Wakala umesafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 2,023.2, kusimamia minara 10 ya kuangalizia matukio na vituo saba (7) vya kufuatilia na kudhibiti matukio ya moto. Pia, Wakala umetoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na kudhibiti moto kwa vikosi 35 vyenye jumla ya watu 405 vya kudhibiti moto na wananchi 15,632 kutoka vijiji 269 vinavyopakana na hifadhi za misitu katika maeneo mbalimbali nchini.

99. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa bioanuai za kipekee na mimea iliyo hatarini kutoweka, Wakala umepandisha hadhi misitu ya hifadhi miwili (2) hifadhi za Rau (mkoani Kilimanjaro) na Nou (mkoani Manyara) yenye ukubwa hekta 30,396.7 kuwa hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia. Aidha, upandishaji hadhi huu unapelekea utendaji endelevu wa misitu kwa faida za kimazingira, shughuli za utalii na uwekezaji ambapo utaongeza idadi ya watalii na kuimarisha uhifadhi wa misitu hiyo. Katika hatua nyingine, Wakala umetangaza kisheria misitu 43 kuwa Hifadhi za Misitu.

100. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza kasi ya uhifadhi na upandaji miti kuifanya nchi kuwa ya Kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu Nchini, Wakala umeanzisha vyanzo sita (6) vya kuzalisha mbegu bora za miti vyenye ukubwa wa hekta 60 ambavyo vimechangia uzalishaji wa zaidi ya tani 20.2 za mbegu bora za miti toka vyanzo mbalimbali vya mbegu. Aidha, Wakala umezalisha miche ya miti milioni 33.2 jamii (species) mbalimbali ambayo imeendelea kupandwa katika mashamba 24 ya Serikali na kugawa kwa watu binafsi, taasisi na mashirika ya umma na binafsi. Vilevile, Wakala umepanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8,270.2; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 1,794; kupalilia eneo lenye hekta 23,276; kupogolea hekta 10,769; kupunguzia miti kwenye hekta 2,108 katika mashamba yanayosimamiwa na Wakala. Pia, Wakala umepanda miche ya mikoko 15,650 kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 60 katika mwambao wa bahari ya Hindi kwenye Wilaya za Lindi, Kilwa, Temeke, Mafia na Tanga.

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson akizindua Kampeni ya upandaji miti mkoani Mbeya.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula, akipokea maelezo kuhusu moja ya kiliba cha miti kutoka kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Silayo, Bw. Juma Mwita Mseti, katika Shamba hilo lililopo mkoani Geita.

101. Mheshimiwa Spika, Wakala umeimarisha shughuli za ufugaji nyuki kwa kusimamia manzuki 222 na mashamba matatu (3) ya Nyuki ya Kipembawe (Chunya), Mwambao (Handeni na Kilindi) na shamba la Kati (katika wilaya za Manyoni, Chemba na

Kondoa) ambapo tani 22.5 za asali na tani 0.9 za nta zenye thamani ya Shilingi 282,713,700 zimezalishwa. Vilevile, maafisa ufugaji nyuki na maafisa misitu 35 wa halmashauri na vikundi 53 vya ufugaji nyuki vyenye jumla ya wafugaji nyuki 1,825 wamepewa mafunzo kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya ufugaji nyuki; kuhamasisha ufugaji nyuki kibiashara; na uchakataji na ufungashaji bora wa mazao ya nyuki. Aidha, Wakala umekusanya sampuli 132 za asali katika Wilaya 30 na kupelekwa kwenye maabara ya kimataifa nje ya nchi kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa mazao ya nyuki yanayozalishwa nchini. Matokeo ya ubora wa sampuli hizo yatawezesha asali ya Tanzania kuendelea kuruhusiwa kuuzwa katika masoko ya kikanda na kimataifa.

102. Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mengi nchini, kumekuwepo na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Kufuatia changamoto hii, Wakala umeendelea kutatua migogoro baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi kwa kuboresha huduma za ugani katika vijiji vinavyopakana na hifadhi za misitu na kuimarisha mipaka katika misitu ya hifadhi. Aidha, Wakala umeimarisha mipaka ya misitu 116 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 425; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,568; kuweka vigingi 672, mabango 157; na kuchimba mitaro 41 inayoonesha uelekeo wa mipaka ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala umetoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa misitu kwa wananchi 6,074 kutoka vijiji 75 vinavyopakana na misitu ya hifadhi.

103. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza utalii wa misitu na malikale, Wakala umeboresha miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu yenye vivutio vya utalii ikolojia kwa kujenga njia mpya za kutembea watalii zenye urefu wa kilomita 43.6, kukarabati kilomita 339.12 za njia za watalii na kilomita 122 za barabara katika hifadhi za misitu (10) na vituo viwili (2) vya Malikale. Aidha, Wakala umejenga daraja la kitalii, kukarabati mabanda mawili (2) ya kupumzikia watalii; kambi 21 za watalii na minara miwili (2) ya kutazama vivutio. Sambamba na hilo, Wakala umeendelea kutangaza vivutio vya utalii Ikolojia na Malikale

katika hifadhi za misitu kwa kuzalisha na kurusha video fupi za picha mjongeo 287, jumbe fupi 372, vipindi 71 vya redio na 85 vya televisheni pamoja na kusambaza machapisho takriban 10,837 yenye jumbe za kuhamasisha utalii. Vilevile, Wakala umeandaa matangazo 21 yanayoonyesha vivutio vya utalii ikolojia yaliyorushwa katika mechi za ligi kuu ya NBC katika Uwanja wa Azam Complex.

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) akiambatana na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii walipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa daraja la watembea kwa miguu (Board Walk) katika Hifadhi ya Misitu ya Mikoko Sahare, Tanga.

104. Mheshimiwa Spika, Wakala umeshiriki matamasha tisa (9) ya ndani na nje ya nchi na umeandaa matamasha 10 kama sehemu ya kutangaza utalii wa misitu yakiwemo Meru Forest Festival, Bata Msituni Festival, Tukacharu Rau Forest, Morogoro Car Rally, Mount Rungwe Hiking Challenge na Mount Hanang Bush Challenge. Juhudi hizi zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya utalii ikolojia kufikia 275,723 Aprili 2025 ikilinganishwa na watalii 211,764 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 30. Aidha, mapato yanayotokana na shughuli za utalii ikolojia yameongezeka na kufikia Shilingi 2,169,832,146 Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na Shilingi 1,689,095,459 zilizokusanywa kipindi kama hicho Mwaka 2024.

105. Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umetoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 13,755 katika vijiji 94 vinavyopakana na hifadhi za misitu. Aidha, Wakala umegawa miche ya miti 10,769,510 yenye thamani ya Shilingi 3,908,244,024 na mizinga ya nyuki 1,059 yenye thamani ya Shilingi 158,850,000. Vilevile, Wakala umewezesha ujenzi wa jengo la utawala la Shule ya Sekondari Wino Mkoani Ruvuma; kuwezesha ununuzi wa samani (madawati 330, meza 2 na viti 10) na vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Shilingi 665,361,027 kwa shule za msingi 13 na Sekondari 14 katika maeneo mbalimbali nchini.

106. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, Wakala umewezesha mafunzo ya utayari kwa watumishi 89 na mafunzo ya uongozi kwa watumishi 481; mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 95 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 443 katika nyanja mbalimbali. Mafunzo haya yatawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi. Aidha, katika kuongeza nguvukazi ya Wakala, usaili wa watumishi 205 umefanyika ambapo taratibu za ajira zinaendelea kupitia Sekretarieti ya Ajira.

107. Mheshimiwa Spika, Wakala umepata ufadhili wa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Uhifadhi wa Misitu ya Mikoko kutoka Shirika la Maendeleo ya Serikali ya Ufaransa (AFD) wenye thamani ya Shilingi bilioni 122 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2025/2026 – 2030/2031). Mradi huu unalenga kujenga uwezo wa TFS kusimamia mashamba ya miti kwa jumla na kuongeza kasi ya upandaji miti ambapo jumla ya hekta 22,500 zitapandwa katika Mashamba ya Miti Silayo Mkoani Geita, Mtibwa, Morogoro na Wino lililopo Mkoani Ruvuma. Vilevile, mradi utawezesha usimamizi wa hifadhi za mikoko katika wilaya za Rufiji, Kilwa na Kibiti na kuongeza fursa za kiuchumi kwa kuwezesha miradi mbalimbali ya kiuchumi kwa wananchi wanaoishi karibu na misitu hiyo ili kupunguza utegemezi kwenye misitu.

4.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

108. Mheshimiwa Spika, Taasisi ina jukumu la kufanya na kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki, kutoa ushauri wa kitaalam na kusambaza matokeo ya utafiti katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki kwa wadau. Katika kuhakikisha kuwa jamii inapata matokeo ya tafiti mbalimbali za misitu na nyuki, TAFORI iliandaa Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi lililoongozwa na mada isemayo "Kurejesha Mandhari ya Misitu kwa Maendeleo Endelevu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Restoring Forest Landscapes for Sustainable Development and Climate Change Mitigation)". Kongamano hili lilifanyika mwezi Disemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki 996 kutoka Tanzania na Mataifa mbalimbali ikiwemo Kenya, Afrika Kusini, Uswisi, Japan, Estonia, Ufini na Ujerumani. Aidha, kupitia kongamano hili mada 72 ziliwasilishwa zilizojikita katika maeneo ya ufadhili na ubunifu wa teknolojia kwenye Sekta ya Misitu na Nyuki; urejeshwaji wa maeneo yaliyoharibiwa na uhifadhi wa bioanuai; ubunifu na matumizi ya teknolojia katika viwanda vya misitu na nyuki; athari za mabadiliko ya tabianchi katika mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na nyuki; ushirikishwaji wa jinsia katika Sekta ya Misitu na Nyuki; na matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Kutokana na kongamanao hilo, maazimio 18 yalitolewa yenye lengo la kuboresha uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki.

109. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, TAFORI imefanya jumla ya tafiti 19 zikiwemo tafiti tano (5) za kimkakati zilizojikita katika mimea vamizi, nyuki na mazao yake, ubunifu na teknolojia ya viwanda vya misitu, uongezaji thamani wa mazao ya misitu na nyuki, mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya nishati mbadala na magonjwa ya miti. Matokeo ya tafiti hizi yanalenga kutatua changamoto za uhifadhi na kuendeleza sekta ya misitu na nyuki.

110. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kufanya tathmini ya rasilimali za misitu kwa lengo la kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu vilivyopo nchini. Matokeo ya tathmini yamebaini uwepo wa jumla ya viwanda vya misitu 614 katika mikoa ya

Arusha (136), Kilimanjaro (311), Tanga (130), Morogoro (12), Dar es Salaam (11) na Pwani (14). Vilevile, imebaini kuwa hekta 18,836.04 za mashamba ya miti zipo mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Mashariki. Mahitaji ya malighafi kwa viwanda vya misitu vilivyopo katika kanda hizo ni mita za ujazo 1,136,000.00 kwa mwaka na kiasi kinachopatikana kwa mwaka ni mita za ujazo 312,430.00 sawa na asilimia 27.3 ya mahitaji. Matokeo haya yanaonesha kuwa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo kutokana na ufinyu wa malighafi. Hali hii inachochea na kuhamasisha fursa za uwekezaji zaidi katika kuanzisha mashamba mapya ya miti nchini.

111. Mheshimiwa Spika, TAFORI pia imefanya tathmini ya kiwango cha asali kinachozalishwa kwa mizinga ya aina mbalimbali nchini. Tathmini hii inaendelea kufanyika katika manzuki 21 za majaribio ya kisayansi zilizoanzishwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Chamwino, Manyoni, Sikonge, Kasulu, Mlele, Bukombe, Butiama, Itilima, Morogoro, Kibiti, Handeni, Pangani, Mtama (Rondo), Tunduru, Mufindi, Njombe, Chunya, Siha, Same na Simanjiro. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa kiasi cha wastani wa kilo 19.10 za asali huzalishwa kwenye mzinga wa nyuki wa kisasa ikilinganishwa na kilo 10 zinazozalishwa kutoka katika mzinga wa kienyeji. Matokeo ya tathmini hii yanachochea jamii kutumia mizinga ya kisasa ili kuongeza kiwango na ubora wa mazao ya nyuki. Katika hatua nyingine, TAFORI imefanya utafiti wa kuangalia sifa za asali inayozalishwa katika uoto mbalimbali nchini ambapo matokeo ya utafiti huo yamebaini uwepo wa asali zenye sifa tofauti za ubora zikiwemo ladha, rangi na viambata muhimu. Hatua hii imewezesha kutengenezwa kwa Alama ya Asali ya Tanzania (Honey Trademark) itakayotumiwa na wafanyabiashara kama alama ya kuitambulisha asali ya Tanzania katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

112. Mheshimiwa Spika, TAFORI kwa kushirikiana na Taasisi ya Tiba Asilia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili inafanya utafiti juu ya matumizi na hali ya uhifadhi wa mimea dawa iliyopo mashambani kwa uboreshaji wa maisha na uhifadhi wa misitu katika Milima ya Tao la Mashariki. Utafiti huu umefanyika katika Wilaya za Kilolo mkoani Iringa na Kilombero mkoani

Morogoro. Utafiti umeonesha kuwa asilimia 71 ya mimea dawa inapatikana kwenye mashamba ya watu binafsi. Miongoni mwa mimea dawa hiyo ni; Mhungulungu, Mnyonyo, Bangalala, Kiguti, Kimakasa, Kilimandembwe, Kinunu, Lihungutua, Limulimuli, Lipasa, Mhanza, Mwambandusi na Mverevere. Hali hii inaonesha kuongezeka kwa uhifadhi wa mimea dawa katika maeneo ya Milima ya Tao la Mashariki. Aidha, mimea dawa 122 imetambuliwa kwenye maeneo hayo ambayo yanahitaji kuhifadhiwa kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

113. Mheshimiwa Spika, TAFORI imefanya utafiti wa kuchunguza afya ya udongo katika maeneo yaliyopandwa miti ya misindano na mikaratusi kwa mzunguko wa pili (second rotation) kwa lengo la kutambua virutubisho vitakavyowezesha upatikanaji wa mazao bora ya miti yakiwemo mbao, nguzo, vinia na tetefya. Utafiti huu umefanyika katika Shamba la Miti la Sao Hill ambapo matokeo yameonesha kuwepo kwa upungufu wa madini aina ya Phosphorus na Nitrogen na ongezeko la madini aina ya Potassium na kaboni iliyokusanyika kutokana na kuoza kwa majani ya miti hasa kwenye tabaka la juu la udongo. Upungufu wa madini ya Phosphorus na Nitrogen umeonesha kutoathiri ukuaji wa miti kwa kuzalisha mita za ujazo zipatazo 71 kwa hekta ikilinganishwa na mita za ujazo zipatazo 68 kwa hekta kwenye maeneo yaliopandwa miti kwa mzunguko wa kwanza. Utofauti wa mita za ujazo umetokana na uwepo wa mboji itokanayo na majani ya miti yaliyooza. Aidha, ubora wa mbao kutoka kwenye mizunguko yote miwili haukutofautiana. Kutokana na matokeo haya, inashauriwa kusifanyike uchomaji wa majani na mabaki mengine ya miti wakati wa uandaaji wa mashamba ili kuendelea kulinda rutuba ya udongo.

114. Mheshimiwa Spika, TAFORI inatekeleza mradi wa utafiti ujulikanao kama Mimea ya Asili kwa Mazingira na Watu (Native Plants for Environment and People - NATIVE PEP) wenye lengo la kudhibiti mimea vamizi kwenye maeneo ya wafugaji hususan katika mikoa ya Arusha (Longido) na Kilimanjaro (Siha). Aidha, mradi unatarajiwa kuwezesha urudishaji wa uoto wa asili katika maeneo yaliyovamiwa na mimea vamizi ambapo katika awamu ya kwanza majaribio ya mbinu mbalimbali za kurudisha uoto wa

asili yameanzishwa katika vijiji vya Tingatinga Wilaya ya Longido na Mawasiliano Wilaya ya Siha. Ufuatiliaji wa majaribio unaendelea ili kubaini mbinu sahihi zitakazotumika kurejesha uoto wa asili katika maeneo hayo. Utafiti huu unasaidia kuimarisha ulinzi dhidi ya mimea vamizi kwenye hifadhi za misitu na wanayamapori hapa nchini. Kwa upande mwingine, TAFORI inashirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na wataalam kutoka nchini Cuba kufanya tathmini ya aina, mtawanyiko, athari na mbinu za udhibiti wa mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Matokeo ya awali yamebaini uwepo wa aina mbalimbali za mimea vamizi kama vile; Gutenbergia cordifolia, Bidens schimperi, Parthenium hysterophorus, Verbena officinalis, Chromolaena odorata, Opuntia vulgaris, Datura stramonium, Parthenium hysterophorus, Eichhornia crassipes (Water Hyacinth), na Salvinia species. Kufuatia matokeo hayo, TAFORI inaendelea kushirikiana na watafiti wa ndani na nje ya nchi kubuni mbinu zitakazowezesha kudhibiti uvamizi na kuenea kwa mimea vamizi katika maeneo ya hifadhi na vijiji.

115. Mheshimiwa Spika, TAFORI imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kukarabati jengo la Kituo cha Utafiti cha Malya mkoani Mwanza na kuanza ujenzi wa ofisi za Kituo cha Utafiti Tabora. Vilevile, taasisi imewezesha watumishi 29 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi pamoja na kupandisha vyeo watumishi 28.

4.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora – (BTI)

116. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora (BTI) kina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada (Technician Certificate) na Stashahada (Ordinary Diploma) ya Ufugaji Nyuki, mafunzo ya muda mfupi, Ushauri juu ya masuala ya Ufugaji Nyuki na Utafiti. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 287 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimefanya tafiti mbili (2) zinazohusu tathmini ya matumizi ya mizinga ya kisasa katika shughuli za ufugaji nyuki; na masuala yanayoathiri matumizi ya mizinga ya kisasa kwa wafugaji nyuki katika Wilaya ya Sikonge.

Matokeo ya tafiti hizi yameonyesha kuwa bado kwa kiasi kikubwa wafugaji nyuki wanaendelea kutumia mizinga ya kienyeji ambayo huzalisha kiwango kidogo cha asali.

117. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Chuo kilitoa ushauri wa kitaalamu juu ya masuala mbalimbali ya mnyororo wa thamani wa Ufugaji Nyuki kwa vikundi 30 vya wafugaji nyuki na wadau 1,726 kutoka wilaya za Meatu, Maswa, Magu, Sikonge, Mlele, Tanganyika, Kasulu, Kibondo, Buhigwe, Manyoni, pamoja na Zanzibar. Katika hatua nyingine, Chuo kimekamilisha ukarabati wa nyumba mbili (2) za watumishi na kinaendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara na bweni la wasichana. Aidha, Chuo kimewezesha mtumishi mmoja (1) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 16 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Sambamba na hilo, Chuo kimeshiriki katika matukio na maonesho mbalimbali kama Sabasaba, Nanenane, Siku ya Misitu Duniani na maonesho asali kwa lengo la kutangaza majukumu yake kwa wadau ili kuongeza idadi ya wadau watakaohitaji kuhudumiwa na chuo katika masuala yanayohusu sekta ndogo ya nyuki.

4.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

118. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Viwanda vya Misitu kina jukumu la kutoa mafunzo na ujuzi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa ngazi ya Astashahada na stashahada. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo kimedahili wanafunzi 388 wanawake ni asilimia 52 na wanaume ni asilimia 48. Ongezeko la udahili wa wanawake umetokana na hamasa ya Serikali pamoja na fursa nyingi zilizopo katika sekta ya misitu.

119. Mheshimiwa Spika; Chuo pia kimetoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalamu kwa jamii ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, wananchi 250 wamepata mafunzo katika maeneo ya upangaji madaraja na matumizi bora ya mbao, udhibiti wa moto misituni, biashara ya mazao ya misitu na kaboni, ufundi seremala na uchakataji magogo kwa kutumia teknolojia za kisasa. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa

bweni la wanafunzi wa kike litakalochukua wanafunzi 200, ununuzi wa mitambo ya kukaushia na kutibu mbao pamoja vifaa vya maabara ya kupimia ubora wa mazao ya misitu. Katika hatua nyingine, Chuo kimewezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na tatu (13) mafunzo ya muda mfupi kwaajili ya kuboresha utendaji kazi.

4.3.2.6 Chuo Cha Misitu, Olmotonyi - FTI 1869680

120. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Misitu, Olmotonyi kina jukumu la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu wa misitu, mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalamu wa misitu na uhifadhi wa mazingira. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimedahili na kutoa mafunzo ya astashahada na stashahada ya misitu kwa wanafunzi 884. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya kuzuia na kudhibiti moto kwa maafisa misitu 50 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Vilevile, Chuo kimesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Chuo Kikuu cha HAMK cha nchini Finland, Chuo cha Misitu ya Luua cha nchini Estonia na Chuo cha Misitu Zambia cha nchini Zambia kwa ajili ya kujengeana uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi sanifu na ufundi stadi wa misitu na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufanisi wa kazi, Chuo kimewezesha watumishi watano (5) kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 10 kupata mafunzo ya muda mfupi. Katika kuongeza chachu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, Chuo kiliotesha miche ya miti 110,000 ambapo miche hiyo imepandwa katika Shamba la Miti la Chuo.

4.3.2.7 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

122. Mheshimiwa Spika, Mfuko una jukumu la kuwezesha na kugharamia shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko umetoa ruzuku ya Shilingi 1,835,603,754.16 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi 143 inayoendelea na Shilingi 1,183,393,500.00 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji miradi mipya 96 ikiwemo miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kurahisisha utoaji

wa mafunzo katika Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu (FITI) na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI). Aidha, Mfuko umewezesha uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni, uanzishwaji wa mashamba ya miti, na uboreshaji uhifadhi wa misitu kupitia ufugaji nyuki na miradi ya utengenezaji na matumizi ya nishati mbadala. Miradi hiyo inatekelezwa katika Wilaya 97 za mikoa 26 ya Tanzania Bara. Vilevile, Mfuko umetoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kuandaa maandiko ya kuomba ruzuku kwa ajili ya miradi ya uhifadhi kwa wadau 1,864 ikihusisha vikundi (164) vyenye jumla ya washiriki 1,464, shule na watu binafsi (102), Asasi zisizo za kiserikali (73), Taasisi za Serikali (27) na Maafisa Misitu (64) wa TFS na Halmashauri. Kufuatia mafunzo hayo, maombi ya ruzuku zaidi ya 600 yamewasilishwa.

Jengo la mihadhara linaloendelea kujengwa katika huo cha BTI.

123. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Mfuko umeendelea kutoa ufadhili wa masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu nje ya nchi katika fani zenye wataalam wachache au ambazo hazina wataalam nchini ambazo ni magonjwa ya miti (Forest pathology) na uboreshaji wa vizazi vya miti (Tree breeding). Mafunzo yametolewa kwa watumishi 3 kutoka TFS, TAFORI na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Aidha, Mfuko umewezesha TAFORI kukamilisha tafiti 5 za kimkakati ikiwemo utafiti wa kuongeza mchango wa Sekta ya Misitu na Nyuki katika Pato la Taifa. Vilevile, Mfuko ulitoa tuzo kwa wanafunzi 27 waliofanya vizuri katika mafunzo ya nadharia na vitendo katika ngazi ya Astashahada (16), Stashahada (8) na Shahada (3) ya misitu.

124. Mheshimiwa Spika, Mfuko uliwezesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC); Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Mwongozo wa Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa (EWP); na Kikundi kazi cha Misitu kilichopo chini ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC). Aidha, Mfuko uliwezesha na kushiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (COP-29) kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Jijini Baku, Azerbaijan. Vilevile, Mfuko uliwezesha Kongamano la Tatu la Kisayansi la TAFORI kuhusu mchango wa utafiti katika kurejesha mandhari ya misitu na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

125. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Mfuko unaongeza vyanzo vyake vya mapato ili kuwezesha na kugharamia ipasavyo shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki, Mfuko umeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kutafuta fedha (Fundraising Strategy). Sambamba na hilo, Mfuko umeboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua magari mawili (2); kugharamia mafunzo ya watumisihi wa Mfuko, kuandaa miongozo ya utekelezaji wa Muundo na Mgawanyo wa majukumu ya Mfuko na kununua kiwanja na kuandaa mchoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko Jijini Dodoma.

4.3.3 Sekta ya Utalii

126. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii ndani na nje ya Nchi. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999, Sheria ya Utalii, Sura ya 65 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364. Kulingana na Muundo, jukumu hilo linatekelezwa kupitia Idara ya Utalii inayosimamia maendeleo ya utalii, udhibiti wa ubora na huduma; Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iliyokasimiwa dhamana ya kutangaza na kuhamasisha utalii ndani na nje ya nchi; na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) wenye jukumu la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani ya utalii na ukarimu.

4.3.3.1 Idara ya Utalii

127. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendeleza na kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imebaini vivutio vipya 337 vya utalii. Vivutio vilivyobainishwa vinajumuisha vivutio vya asili, visivyo vya asili, utamaduni, kihistoria na kidini. Kupitia zoezi hilo, vivutio 193 vimekidhi vigezo vya kuendelezwa na kutangazwa. Vivutio hivyo vipo katika mikoa ya Mtwara (19), Lindi (22), Mbeya (28), Songwe (16), Katavi (8), Kigoma (16), Iringa (23), Njombe (26), Ruvuma (32) na Rukwa (14). Miongoni mwa vivutio vilivyobainishwa ni pamoja na Boma la Mjerumani Newala Lindi, Tamasha la Utamaduni la MAKUYA (Manispaa ya Mtwara) na Mkomaindo (Masasi) Tukio la Kuhama kwa Nyangumi linalojulikana kama Humback whales migration (Msimbati), Maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi na eneo la fukwe za ziwa Tanganyika. Zoezi hilo limelenga pia kupunguza utegemezi kwenye zao la wanyamapori pamoja na kuongeza siku za watalii kukaa nchini sambamba na kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Hatua inayofuata ni kuvisajili vivutio hivyo vya utalii kama ambavyo Sheria ya Utalii Sura ya 65 inavyoelekeza ili viweze kuendelezwa na kutangazwa.

128. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ya utalii na kuvutia wawekezaji wa huduma mbalimbali za utalii, Wizara imefanya maboresho ya Kanuni ya Ada na Tozo ya mwaka 2015 ambapo hivi sasa Ada zote za Leseni za Biashara za Utalii - TTBL zinalipwa kwa Shilingi za Kitanzania badala ya Dola ya Marekani. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara ilianza kutekeleza mageuzi katika mifumo ya tozo mbalimbali ili kuipa unafuu sekta binafsi. Mathalani, tumepunguza tozo ya Daraja la Nyota 5 kutoka USD 2,500 hadi USD 1500; Daraja la Nyota 4 kutoka USD 2,000 hadi USD 1000; Daraja la Nyota 3 kutoka USD 1,500 hadi USD 500; Daraja la Nyota 2 kutoka USD 1,200 hadi USD 300; Daraja la Nyota 1 kutoka USD 1,000 hadi USD 200. Gharama hizi sasa zinalipwa kwa shilingi ya Tanzania. Vilevile, Wizara imefuta malipo ya waongoza watalii (park fees) walizokuwa wakitozwa kila walipokuwa wakiingia hifadhini kuingiza wageni. Sasa kila muongoza watalii mwenye leseni hai na halali hatatozwa chochote. Pia, Wizara imeanza kutekeleza

punguzo la ada ya Wakala wa kupandisha mlima kutoka Dola za Marekani 2,000 hadi Shilingi za Tanzania milioni tatu (3,000,000). Sambamba na hilo, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la gharama ya leseni ya waongoza watalii (TTBL) kutoka Dola za Marekani 50 hadi Shilingi 35,000 tu kwa mwaka. Wizara na Serikali kwa ujumla itaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi katika kuongeza ufanisi wa sekta za uhifadhi na utalii kupitia vikao vya kisekta chini ya TNBC lakini na mikutano ya mara kwa mara na wadau.

129. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutekeleza mifumo ya kidijitali ambapo umeanza utaratibu wa wadau kujisajili na kupata leseni za biashara ya utalii kwa njia ya mtandao wa MNRT Portal ambayo imepunguza muda na gharama za upatikanaji wa leseni hizo. Kutokana na maboresho hayo, idadi ya wakala wa biashara za utalii nchini imeongezeka kutoka 3,019 kwa mwaka 2023 hadi kufikia 4,316 Aprili, 2025 na idadi ya Waongoza Watalii imeongezeka kutoka 5,076 mwaka 2023 hadi kufikia 8,914 Aprili, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 54.9. Sambamba na maboresho hayo, Kanuni ya Mabalozi wa Hiari wa Utalii ya mwaka 2025 imetungwa kwa lengo la kutoa miongozo ya uteuzi wa Mabalozi wa Hiari wa kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

130. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi ya uhakiki na utambuzi wa huduma za malazi, Wizara ilifanya zoezi uhakiki na utambuzi wa huduma za malazi katika mikoa yote 26 hadi kufikia Aprili, 2025. Aidha, jumla ya huduma za malazi 2,038 mpya zilifanyiwa uhakiki na utambuzi zikiwa na Mtawanyiko wa Dar es Salaam (47), Arusha (90), Mbeya (47), Mwanza (106), Mara (125), Manyara (52), Kilimanjaro (53), Tanga (87), Morogoro (62), Pwani (37), Dodoma (293) Iringa (179), Singida (108) Kagera (165), Geita (148), Kigoma (115), Njombe (30), Songwe (44), Rukwa (26), Katavi (37), Tabora (20), Shinyanga (14), Simiyu (4), Lindi (42), Mtwara (55) na Ruvuma (52). Sambamba na hilo, kati ya huduma za malazi hizo mpya zilizo hakikiwa, huduma za malazi 362 zimekidhi vigezo vya kuwa na sifa ya kupangwa katika viwango vya ubora wa nyota.

131. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imeendelea na ukaguzi wa Wakala wa biashara za utalii na waongoza watalii katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Njombe, Mbeya na Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kuwa wadau hao wanazingatia na kufuata taratibu zilizopo za biashara ya utalii. Aidha, kupitia ukaguzi huo, wakala 229 na waongoza wageni 101 walisajiliwa na kulipia Leseni ya Biashara ya Utalii (TTBL) na leseni ya Waongoza Watalii, ambapo jumla ya Shilingi 719,259,600.00 zilikusanywa. Awamu ya pili ya kazi hii inatarajiwa kuendelea kufanyika katika mikoa 14 iliyobaki na katika malango ya hifadhi nchini.

132. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano na matukio ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo: Mkutano wa 122 wa Baraza Tendaji la Shirika la Utalii Duniani (UN-Tourism Executive Council) uliofanyika nchini Colombia; Mkutano wa 67 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Utalii Afrika (UN Tourism CAF) uliofanyika sambamba na Mkutano wa pili wa Brand Africa nchini Zambia. Wizara pia imeshiriki katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Ushirikiano wa Kidiplomasia Kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China Jijini Dar es Salaam ambapo ulifanyika uzinduzi wa Filamu ya Amazing Tanzania iliyooneshwa kwa zaidi ya watu 1,000. Lengo la filamu hiyo ni kuvutia watalii wengi zaidi kutoka soko la China ambalo ni moja ya masoko ya utalii ya kimkakati. Aidha, kupitia filamu hiyo, idadi ya watalii kutoka China imeongezeka kutoka wageni 45,463 kwa mwaka 2023 hadi kufikia wageni 71,140 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56.5. Vilevile, Kampuni ya Changsha Utopia ya nchini China ilirekodi kipindi maarufu cha uhalisia cha Divas Hit the Road katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo kilioneshwa katika Televisheni ya Hunan na kutazamwa na watu takriban bilioni 1.2 ndani ya China na nchi za jirani. Halikadhalika, Kampuni hiyo imefanikiwa kuleta watu wawili mashuhuri wa nchini China mwezi Aprili, 2025 ili kurekodi kipindi cha uhalisia kinachojulikana kama Swapping Lives katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi za Taifa za Tarangire na Ziwa Manyara.

133. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kukuza zao la utalii kupitia majukwaa, mikutano na matukio nchini. Juhudi hizo zimefanikisha Tanzania kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa pamoja na majukwaa mbalimbali kama vile: Jukwaa la Pili la Kikanda la Utalii wa Vyakula la Shirika la Utalii Duniani (Second UN Tourism Regional Forum on Gastronomy Tourism for Africa) uliofanyika tarehe 23 hadi 25, Aprili 2025 Jijini Arusha. Jukwaa hilo lilihudhuriwa na Mke wa Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, Dkt. Auxillia C. Mnangagwa, Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Maafisa Waandamizi wa Serikali kutoka nchi mbalimbali za Ukanda wa Afrika wanaohusika na utalii; wawakilishi wa balozi za nchi mbalimbali za ukanda wa Afrika na baadhi ya taasisi za Kimataifa; wataalamu wa utalii na mapishi kutoka Sekta Binafsi ya utalii nchini na nje ya nchi. Mgeni Rasmi wa Jukwaa hilo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani Bw. Zurab Pololikashvili.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), akikabidhiwa cheti na Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani, Bw. Zurab Pololikashvili, cha ufadhili wa masomo kwa njia ya mtandao katika fani ya mapishi wakati wa hafla ya ufunguzi wa Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Chakula la Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) kwa Kanda ya Afrika, jijini Arusha.

134. Mheshimiwa Spika, katika kutambua na kuhamasisha wadau kuendeleza utalii, Wizara imeandaa na kuzindua tuzo za Uhifadhi na Utalii zijulikanazo kama The Serengeti Awards zenye lengo la kutambua mchango wa wadau katika kuendeleza uhifadhi na kutangaza utalii. Uzinduzi wa tuzo hii ulifanyika Desemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 500 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitunukiwa Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono (Visionary Leadership) ikiwa ni sehemu ya kutambua mchago wake kwenye mafanikio ya Sekta ya Maliasili na Utalii. Vilevile, Wizara ilitoa Tuzo 10 za Heshima na Shukrani kwa wadau mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kutambua michango yao katika Uhifadhi wa Maliasili, Malikale pamoja na uendelezaji utalii. Tuzo hizi zitaendelea kutolewa kila mwaka ili kuendelea kuhamasisha na kutambua michango mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Maliasili na Utalii.

4.3.3.2 Tozo ya Maendeleo ya Utalii – TDL

135. Mheshimiwa Spika, Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy-TDL) ina jukumu la kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uendelezaji utalii nchini ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazao ya utalii, kudhibiti ubora wa huduma za biashara za utalii, kutangaza utalii ndani na nje ya nchi, kuimarisha miundombinu ya utalii, kujenga uwezo na kufanya tafiti katika sekta ya Utalii. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, TDL imewezesha kuanza kwa ujenzi wa baadhi ya miundombinu ya utalii, kubaini vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji, kuwezesha uhakiki (inventory) wa huduma za malazi na ukaguzi wa wakala wa biashara ya utalii ili kuboresha huduma za kitalii na ukarimu.

136. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendeleza kampeni ya kutangaza utalii, TDL imewezesha uzinduzi wa filamu ya Amazing Tanzania pamoja na kufanikisha sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China. Aidha, TDL imewezesha uandaaji na ushiriki wa Tanzania katika maonesho, matamasha na matukio ya utalii ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Jukwaa la Pili la Utalii wa Chakula (Second UN Tourism Gastronomy) na uzinduzi wa tukio la Tuzo za Utalii. Katika

hatua nyingine, TDL imewezesha uratibu na kushiriki katika misafara ya utangazaji utalii (tourism roadshow) katika nchi mbalimbali; na kuandaa ziara za mafunzo (Fam Trip) kwa diaspora, mawakala wa usafiri wa kimataifa, watu mashuhuri, waandishi pamoja na vyombo vya Habari ili kuongeza uelewa kuhusu vivutio vya utalii. Aidha, imewezesha kufanyika mazungumzo ya awali na vilabu vikubwa vya mpira wa miguu duniani na vyombo vya habari vya kimataifa kama sehemu ya jitihada za kukuza utalii kupitia ushirikiano wa kimkakati katika kutangaza vivutio vyetu duniani. Wizara itaendelea kuhakikisha usimamizi thabiti na wenye kuleta tija wa fedha hizi.

4.3.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

137. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania ina jukumu la kutumia mbinu mbalimbali za utangazaji utalii ili kuifanya Tanzania iwe kituo kikuu kimojawapo mashuhuri cha utalii duniani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi imeendelea kuratibu ushiriki wa nchi katika kuhamasisha na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali Duniani. Katika kipindi husika, Bodi imetangaza utalii kupitia maonesho saba (7) ya Kimataifa katika nchi ambazo ni masoko ya utalii ya msingi na kimkakati. Maonesho hayo ni pamoja na: WTM – London (Uingereza), ITB – Berlin (Ujerumani), OTM (India), FITUR (Hispania), Gita Mahotsav (India), Qatar Travel Market (Qatar) na Magical Kenya Tourism Expo (Kenya). Kupitia maonesho hayo takriban makampuni 150 ya nchini yalifanya mazungumzo na wafanyabiashara na watalii wa nchi hizo. Ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo umeendelea kuwa chachu ya ongezeko la watalii kutoka Nchi husika. Mathalan, idadi ya watalii kutoka Ujerumani imeongezeka kutoka watalii 23,615 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 102,798 mwaka 2024 sawa na asilimia 335.3.

138. Mheshimiwa Spika, Bodi imeendelea kushirikiana na Ofisi za Balozi za Tanzania katika kutangaza utalii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kuratibu ziara za mafunzo kwa wakala wa utalii, waandishi wa habari na watu mashuhuri; kuwapatia nyenzo za utangazaji utalii; kuratibu maonesho na misafara ya utangazaji utalii; kuratibu makala za utangazaji utalii pamoja na kuratibu

"branding" za Ofisi za Balozi zilizopo nje ya nchi. Bodi kwa kushirikiana na Ofisi ya Ubalozi za Tanzania katika masoko ya kimkakati imeandaa na kushiriki katika misafara miwili ya utangazaji utalii (Roadshows) ya nchini India (New Delhi, Chennai, na Bengalore); na Nchi za Ulaya Magharibi ambazo ni Ujerumani (Cologne), Uingereza (London na Manchester), Ubelgiji (Antwerp) na Uholanzi (Amsterdam) ambapo jumla ya wakala wa biashara za utalii 51 kutoka nchini Tanzania walikutana na makampuni 790 na kufanya biashara zinazohusiana na utalii. Jitihada hizo zimechochea ongezeko la idadi ya watalii kutoka soko la kimkakati la India kufikia 63,391 mwaka 2024 kutoka 54,558 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Ofisi zingine za Balozi za Tanzania kwenye masoko ya kimkakati ambayo Bodi imeshirikiana nayo ni Brazil na Canada kwa kuratibu ziara ya mafunzo kwa wakala wa utalii 19. Wakala hao wanatarajiwa kuitangaza Tanzania katika Nchi zao na hivyo kuchochea ongezeko la watalii ikizingatiwa kuwa Brazil na Canada ni miongoni mwa Nchi zenye uchumi mkubwa Duniani. Vilevile, Ofisi za Balozi za Tanzania nchini Nigeria, Ujerumani, Sweden, Zimbabwe, Msumbiji, Rwanda na Zambia walipatiwa nyenzo za utangazaji utalii kama vile QR codes zenye taarifa za vivutio vya utalii, video na vipeperushi. Ushirikiano wa Bodi na Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi umechochea ongezeko la watalii kutoka Nchi husika. Mathalan, idadi ya watalii kutoka Uingereza imeongezeka kutoka watalii 27,667 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 88,345 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 219.3.

139. Mheshimiwa Spika, Bodi imeandaa makala mbili (2) za kivutio cha Kisiwa cha Mafia ambapo moja (1) imeendelea kurushwa katika kituo cha televisheni Tanzania Safari Channel na nyingine inatumika katika matukio ya kimataifa kwa lengo la kukitangaza Kisiwa hicho kama kivutio cha ikolojia. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya Moments Entertainment kutoka Afrika Kusini imeratibu maandalizi ya makala moja (1) inayolenga kuonesha mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Vilevile, Bodi imeshiriki katika uzinduzi wa Filamu ya "Tantalizing Tanzania" Jijini Mumbai, India iliomhusisha Bi. Shakti Mohan, Mcheza Muziki maarufu nchini humo mwenye ushawishi mkubwa anaefuatiliwa na wafuasi zaidi ya milioni 17.5 katika

mitandao ya kijamii. Kwa upande mwingine, Bodi imeendelea kutangaza utalii kupitia mitandao ya kijamii kwa kutengeneza maudhui na kuyatangaza kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo Instagram, Linkedin, X, TikTok, Facebook na Youtube.

140. Mheshimiwa Spika, kupitia ushiriki wa Bodi katika msafara wa utangazaji utalii nchini India, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya Jio Creative Lab imeratibu utayarishaji wa makala ya kutangaza utalii katika soko la India na Bara la Asia. Makala hiyo imehusisha watu mashuhuri wane (4) katika tasnia ya filamu wanaoitwa Kunwar Amar Jeet Singh, Anushka Sen, Siddharth Nigam na Sumedh Vasudev Mudgalkar ambao wana wafuasi zaidi ya milioni 50 kwenye mitandao ya kijamii kutembelea Hifadhi za Serengeti na Kilimanjaro; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Kisiwa cha Mafia. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya Jio Creative Lab, inakamilisha uhariri wa maudhui ya makala hizo, sambamba na kufanya makubaliano na vyombo vya habari vya India vitakavyorusha makala husika katika lugha mbalimbali za nchi hiyo ikiwemo Hindi, Bengali, Tamil, Gujarati na Telegu. Kupitia ushirikiano kati ya nchi hizi mbili, idadi ya watalii kutoka India imeendelea kuongezeka kutoka watalii 12,393 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 63,391 mwaka 2024 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 411.5.

Mwenendo wa idadi ya watalii kutoka nchini India waliotembelea Tanzania kati ya mwaka 2020 na 2024.

141. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutangaza utalii, Bodi iliratibu onesho la Nane la "Swahili International Tourism Expo (S!TE 2024)" kuanzia tarehe 11 hadi 13 Oktoba, 2024 Jijini Dar es Salaam. Kupitia Onesho hilo, waoneshaji 92 na wanunuzi 124 kutoka nchi 24 katika mabara ya Amerika, Ulaya, Asia na Afrika walishiriki onesho husika lililoambatana na Kongamano la pili la Uwekezaji wa Sekta ya Utalii lenye washiriki takriban 300. Aidha, onesho hilo lilifuatiwa na ziara za mafunzo (Familiarization trips) kwenye vivutio 7 vya utalii ikiwemo Hifadhi za Taifa Mikumi, Milima ya Udzungwa, Nyerere na Ruaha; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; Hifadhi ya Msitu Pugu; Eneo la Kihistoria la Magofu ya Kilwa; Kisiwa cha Mafia; na Zanzibar. Onesho la SITE limeendelea kuwa fursa ya kuwakutanisha wadau wa utalii kutoka ndani na nje ya Nchi kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza ushirikiano wa kibiashara.

142. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano na Mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini Tanzania pamoja na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeratibu ziara ya mafunzo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Zanzibar. Kundi hilo la Viongozi Mashuhuri lilihusisha Waheshimiwa Mabalozi wa: Angola, Burundi, Comoros, Cuba, Denmark, Egypt, Ethiopia, Iran, Kenya, Korea, Morocco, Rwanda, Saudi Arabia, Somalia, Sudan, Syrian Arab Republic, Uturuki, Zimbabwe na Wawakilishi wa Mashirika ya: International Labour Organization, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization na United Nations Population Fund. Ziara hiyo imewezesha kuwajengea uwezo Mabalozi hao kuhusu utalii wa Tanzania ili waweze kuutangaza katika Nchi zao kwa lengo la kuvutia watalii na wawekezaji.

143. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Bodi imeratibu ziara nne (4) za mafunzo kwa washiriki 78 ikiwemo wakala wa utalii, waandishi wa habari, wazalishaji wa makala, makundi maalum na watu mashuhuri ili kuwajengea uelewa juu ya vivutio vya utalii wa Tanzania. Washiriki hao wametokea nchi za Brazil, Canada, India na Tanzania ambapo walipata fursa ya kutembelea Hifadhi za Taifa Serengeti, Kilimanjaro, Mikumi na Tarangire; Zanzibar; Kisiwa cha Mafia na Eneo la Hifadhi ya

Ngorongoro. Kwa kutambua mchango wa makundi ya watu makundi maalum katika uhifadhi na uendelezaji utalii, Bodi iliratibu ziara ya mafunzo kwa washiriki 50 makundi maalum kutembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi. Jitihada hizi zimelenga ushirikishwaji wa makundi maalum kutembelea na kutangaza vivutio vya utalii.

144. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi za Wizara na Sekta Binafsi imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani ya nchi kupitia maonesho, matukio na kampeni za utangazaji utalii. Bodi iliandaa kampeni moja ya utangazaji utalii "Funga Mwaka Kijanja, Talii" ambapo zaidi ya watalii wa ndani 103,785 walitembelea vivutio mbalimbali pamoja na kushiriki katika kampeni moja ya "Twenzetu Kileleni" ambapo zaidi ya watalii 400 wa ndani walishiriki katika kupanda Mlima Kilimanjaro. Bodi pia ilishiriki matukio mbalimbali ikiwemo "Churchill Comedy Show – Arusha" ambayo ilihudhuriwa na watu takriban 1,800, "Bata la Funga Mwaka – Arusha" iliyohudhuriwa na takriban watu 5,000, Uzinduzi wa Wiki ya Simba na Miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa Mikumi iliyohudhuriwa na takriban watu 1,232, "Great Ruaha Marathon-Iringa" iliyohudhuriwa na takriban watu 600 pamoja na "Rombo Marathon and Festival – Kilimanjaro" iliyohudhuriwa na takriban watu 1,200.

145. Mheshimiwa Spika, Bodi imeendelea kuratibu ushiriki wa wadau wa utalii katika maonesho ya ndani ya nchi kwa ajili ya kutangaza utalii ikiwemo: Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane), Simiyu Cultural and Tourism Festival, Zanzibar Tourism and Investment Show, Zanzibar Sports Bonanza, Usandawe Festival, Maonesho ya Wiki ya Vijana Mwenge, Serengeti Cultural Festival, Tamasha la Taifa la Utamaduni Ruvuma (Utamaduni Festival), Nyangumi Festival, Khanga Festival, Landrover Festival, Meru Forest Adventure Race Tourism Festival, Maasai Festival, Kizimkazi Festival, na Mafia Festival. Maonesho haya yameendelea kuwa chachu ya ongezeko la watalii wa ndani na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

146. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano na kutangaza utalii wa Tanzania sehemu mbalimbali Duniani, Bodi

imesaini Hati ya makubaliano (MoU) na mashirika ya ndege mawili ambayo ni Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Shirika la Ndege la Uturuki (Turkish Airlines). Kupitia makubaliano hayo, Bodi itapata fursa ya kutangaza vivutio vya utalii katika ndege 490 za Shirika la Ndege la Uturuki ambazo hufanya safari katika miji zaidi ya 350 Duniani. Aidha, Bodi ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wa makubaliano hayo ikiwemo kuandaa maudhui yatakayorushwa ndani ya ndege sambamba na kuratibu kampeni za pamoja. Vilevile, Bodi inaendelea na majadiliano ya utangazaji utalii na mashirika ya ndege ya Precision, Emirates, Ethiopian Airlines, Qatar Air na Air Asia, kukamilisha mazungumzo na vilabu mbalimbali vya michezo na kuendeleza misafara ya kimkakati ya kutangaza utalii (roadshows).

147. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mazao ya utalii wa meli na fukwe, Bodi imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuratibu mapokezi ya meli sita (6) za kitalii zilizokuwa na watalii 3,157 ambapo Meli ya OCI Riveira ilikuwa na watalii 1,160, Seabourn Sojourn (620), MS Europa (443) Hebridrean Sky (172), Ledumon't D'urville (278) na Le Bougainville (484). Watalii hao wametokea masoko ya kimkakati ikiwemo Ujerumani, Ufaransa, Canada, Uingereza, Australia na Marekani ambapo walipata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam (City Tour); Hifadhi ya Urithi wa Utamaduni wa Dunia ya Magofu ya Kale Kilwa Kisiwani na Songo Mnara; Mji wa Kihistoria Bagamoyo; na Hifadhi za Taifa Nyerere na Serengeti. Ujio wa watalii hao unatokana na jitihada za serikali za kuendeleza zao la utalii wa meli.

4.3.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

148. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii kina dhamana ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani za utalii na ukarimu. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimetoa mafunzo ya umahiri (Competence Based Education and Training - CBET) kwa jumla ya wanafunzi 1,398 katika ngazi ya Astashada na Stashahada sawa na asilimia 93.2 ya lengo la wanafunzi 1,500.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 214 walifanya mafunzo maalum ya programu ya Uanagenzi katika fani za ukarimu chini ya ufadhili wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

149. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha kiwango cha ubora wa huduma kwa watalii, Chuo cha Taifa cha Utalii kimeendelea na mkakati wa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa utalii. Hadi April 2025, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa jumla ya washiriki 1,377 ambapo washiriki 40 wamepata mafunzo ya umahiri wa uratibu wa matukio (Event Management Masterclass); 33 mafunzo ya umahiri wa Usafirishaji na Utalii (Travel and Tourism Masterclass); 15 Mafunzo ya umahiri wa Huduma za Ukarimu (Hospitality Masterclass); 14 Mafunzo ya Upishi wa Melini (Ship Cooks) kwa ushirikiano na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI); 100 Mafunzo ya huduma bora za vinywaji; 220 mafunzo kwa Maafisa Uhamiaji na 955 mafunzo ya Huduma bora kwa Watalii yaliyotolewa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari wa vyeo mbalimbali wa Jeshi la Polisi Tanzania. Aidha mafunzo haya ni njia muhimu katika kuboresha huduma kwa wageni ili kuimairisha sekta ya Utalii na kuongeza Pato la Taifa.

150. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza uwezo wa kudahili pamoja na kutoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira, Chuo kimeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo jipya la taaluma kwa kampasi ya Arusha, ambao umefikia asilimia 65 na kufanya ukarabati wa miundombinu ya jengo la mafunzo kwa kampasi ya Bustani uliofikia asilimia 30.

Kushoto ni hatua iliyofikiwa ya mradi wa ujenzi wa jengo la taaluma la Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Arusha na kulia ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea jengo hilo.

151. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea na jitihada za kujitangaza ili kufikia lengo ya udahili wa wanafunzi 1,500 kwa kutekeleza mikakati mbalimbali, ikiwemo kufanya huduma mkoba (Outreach programs) za uhamasishaji, kushiriki maonesho pamoja na kuandaa vipindi vya televisheni na redio kwa ajili ya kutangaza programu za mafunzo kwa wanafunzi wa shule za Sekondari na wadau mbalimbali wa utalii. Aidha, Chuo kilipata ushindi wa pili kama banda bora la ubunifu kwenye maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa yaliyoandaliwa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Maonesho hayo yalihitimishwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Prof. Palamagamba Kabudi.

152. Mheshimiwa Spika, chuo kimeendeleza ushirikiano wa kimataifa na kubadilishana uzoefu kati ya wanataaluma na waendeshaji wa huduma za kitalii kwa kuandaa Kongamano la 3 la Kimataifa la Kuunganisha Wanataaluma na Wadau wa Utalii na Ukarimu katika Nchi Zinazoendelelea (The 3rd Conference in Linking Industry with Academia in the Tourism and Hospitality in Developing Countries (LIATH-DC). Kongamano hili lilifanyika jijini Arusha mwezi Novemba 2024 na kuhudhuriwa na washiriki takriban 250 kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, Kenya, Zambia, Malawi, Sweden, Korea, Ethiopia, Ujerumani, Zimbabwe na Tanzania. Matokeo ya Kongamano hilo ni pamoja na kuboresha mitalaa ya Chuo ili kuendana na mahitaji ya soko;

kuongeza nafasi za mafunzo kwa vitendo, na kusaidia maamuzi ya msingi katika sekta kutokana na tafiti mbalimbali zilizowasilishwa. Aidha, kongamano hilo limeimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kuchochea ubunifu, kuboresha huduma, na kuhimiza maendeleo jumuishi kupitia utalii unaojumuisha jamii na unaozingatia mazingira.

153. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha watumishi wanakuwa na ujuzi stahiki, Chuo kimeendelea na utekelezaji wa Mpango wa mafunzo kwa kuwezesha watumishi 42 kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi ambapo watumishi 12 wanapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Uzamili na wanne (4) Uzamivu. Aidha, watumishi 26 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utalii, Ukarimu na mbinu za ufundishaji.

4.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

154. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi, utafiti na uendelezaji wa rasilimali za malikale. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Malikale ya Mwaka 2008, Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Sekta hii inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale, Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania na Mfuko wa Mambo ya Kale.

4.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

155. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uhifadhi, kuboresha mazingira ya kibiashara na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Mambo ya Kale, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Tozo ya Usimamizi na Uendelezaji Malikale kwa Tangazo la Serikali Na. 873 la tarehe 25 Oktoba, 2024, imekamilisha Rasimu za Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura ya 333, rasimu tatu za miongozo ya usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malikale ambazo ni: Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malikale, Mwongozo wa Utafiti wa Malikale. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kutwaa na Kubadilisha Umiliki wa Malikale. Sambamba na hatua

hizo, Wizara imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale ya Mwaka 2008 na imeandaa rasimu mbili za Mipango Jumuishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa eneo la Urithi wa Dunia, Kilwa Kisiwani na Songo Mnara pamoja na Mji wa Kihistoria Bagamoyo.

156. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutekeleza Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale na Masalia ya Binadamu yaliyochukuliwa wakati wa Ukoloni, Wizara imeshiriki katika ziara ya Kamati ya Kitaifa ya Majadiliano kuhusu malikale na masalia ya binadamu iliyopo nchini Ujerumani ambapo Kamati hiyo imetembelea taasisi nne (4) za Ujerumani zinazohifadhi mikusanyo ya Tanzania. Lengo la ziara hiyo lilikua ni kuona na kufanya tathmini ya hali halisi ya malikale za Tanzania zilizopo nchini Ujerumani. Taasisi zilizotembelewa ni Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Fraas (Stuttgart); Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Berlin; Makumbusho ya ethnolojia ya Linden Stuttgart; Makumbusho ya Rothenbaum (Hamburg) na Taasisi za Humboldt Forum na Prussian Cultural Heritage Foundation na afya ya Charrite. Tathmini hiyo ilibaini kwamba mikusanyo ya Tanzania iliyopo katika taasisi hizo inajumuisha mabaki ya miili ya binadamu, paleontolojia (visukukuu vya wanyama na mimea), akiolojia na vifaa vya mila na utamaduni. Taarifa zilizizopatikana kutokana na ziara hiyo, zitatumika katika kuimarisha majadiliano baina ya Serikali za Shirikisho la Ujerumani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu namna ya kurejesha au kunufaika na malikale zilizopo nchini Ujerumani.

157. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa maeneo ya malikale yanalindwa kisheria, kuendelezwa na kutumika kiutalii, Wizara imekusanya taarifa za kiuhifadhi za maeneo 163 katika mikoa 10 kwa lengo la kuyatangaza katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo ambayo taarifa zake zimekusanywa ni katika mikoa ya Ruvuma (8), Iringa (3), Lindi (54), Tanga (44), Singida (13), Morogoro (7), Manyara (2), Kagera (5), Mwanza (10), Mbeya (1), Tabora (2) na Pwani (14).

158. Mheshimiwa Spika, kati ya maeneo 163 ambayo taarifa zake zimekusanywa, taratibu za kisheria zinazohusu maeneo 16

yaliyopo katika mikoa ya Morogoro maeneo (2), Lindi (1), Ruvuma (2), Tanga (3), Mbeya (1), Singida (4), Tabora (2) na Iringa (1) zimekamilika kwa ajili ya kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na kambi zilizotumiwa na wapigania uhuru wa nchi ya Afrika ya Kusini na Msumbiji zilizopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kampasi ya Solomon Mahlangu-Mazimbu – Morogoro, Kihesa Mgagao – Iringa na Shule ya Sekondari ya Samora Machel - Mbeya; Makazi ya Watemi Fundikira na Isike – Tabora; Jengo la Kihistoria la Hospitali ya Afya ya Akili na Kanisa la KKKT Lutindi, Korogwe na Jengo la Kanisa na kituo cha Hija Magila Msalabani, wilayani Muheza - Tanga; na eneo la Mnara wa Kumbukumbu ya Hayati Edward Moringe Sokoine, Mvomero-Mkoani Morogoro.

159. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine, imefanya tathmini ya hali ya uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo 18 ya malikale yaliyopo kwenye Orodha ya Urithi wa Taifa katika mikoa ya Dodoma (12), Singida (2) na Lindi (4). Maeneo yaliyofanyiwa tathmini yanajumuisha michoro ya miambani, miji na majengo ya kihistoria na maeneo ya palentolojia ambayo yamebeba ushahidi wa chimbuko na maendeleo ya binadamu katika ardhi ya Tanzania. Lengo la tathmini hiyo ni kuhuisha orodha ya maeneo ya Urithi wa Taifa, kuandaa mipango ya kuendeleza yaliyo katika hali mbaya na kuyakabidhi kwa wadau wenye uwezo na nia ya kuyatumia kwa maendeleo endelevu. Tathmini hiyo imebaini kwamba maeneo hayo, yapo katika hali nzuri ya kiuhifadhi isipokua manne (4) hayajaanza kutumika kiutalii. Katika kuhakikisha kuwa maeneo hayo manne (4) yanatumika kwa faida za kijamii na kiuchumi, Wizara imeyakabidhi kwa wadau ambao wameonesha nia ya kuyatumia kwa maendeleo endelevu. Wadau hao ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa maeneo (2) na Kanisa la Anglican Kilimatinde, wilayani Manyoni (2). Aidha, maeneo 14 yaliyobaki yanaendelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

160. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutatua migogoro ya mipaka kuhusu umiliki na uendeshaji wa maeneo ya malikale, migororo miwili (2) imefanyiwa kazi ambapo mgogoro wa kwanza

unaohusu Kijiji cha Engaruka ulikuwa ni utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta. Kwa sasa, Wizara na uongozi wa Kijiji cha Engaruka, mkoani Arusha wanaendelea na vikao kupata namna bora ya kupunguza eneo la kihistoria la Engaruka kwa ajili ya kuwapatia wananchi bila kuathiri uhifadhi. Katika mgogoro wa pili unaohusu Familia ya Mtwa Mkwawa, makubaliano yamefanyika kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Usimamizi wa eneo la Makumbusho ya Mtwa Mkwawa, Iringa ambao utabainisha wajibu na haki za wadau wa eneo hilo.

161. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na kusimamia matamasha manne (4) ya Kumbukumbu kwa lengo la kurithisha historia ya Taifa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kuhimiza matumizi endelevu ya malikale. Matamasha hayo ni Kumbukizi ya Vita ya Majimaji, Nandete – Lindi na Songea – Ruvuma; na Maadhimisho ya Kumbukizi ya Miaka 103 Mwl. Nyerere yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2024 Butiama – Mara na Aprili, 2025 jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa miaka kumi wa Kuenzi na Kutangaza Urithi wa Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akitazama onesho la Historia ya Vita vya Majimaji, katika Makumbusho ya Majimaji, Songea Mkoa wa Ruvuma.

162. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa kwenye uhifadhi wa maeneo yanye sifa za kipekee, Wizara ilishiriki Mkutano uliofanyika Paris, Ufaransa Desemba 2024 ambao ulijadili hifadhi za jiolojia za UNESCO (UNESCO Global Georpark) ikiwemo Eneo la Jiolojia la Ngorongoro Lengai. Kupitia mkutano huo, Eneo la Jiolojia Hifadhi ya Ngorongoro Lengai lilirejeshewa hadhi yake iliyokuwa imepotea tangu mwaka 2022. Urejeshwaji huo umetokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa ikiwemo kuzingatia vigezo vilivyowekwa na UNESCO kwa kuimarisha uhifadhi, kuboresha miundombinu, kukusanya taarifa, kulitangaza pamoja na kushirikisha jamii katika matumizi endelevu ya eneo hilo. Vilevile, Wizara imeshiriki mkutano wa tisa (9) wa wataalam wa fani ya akiolojia na paleontolojia uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Agosti, 2024 ambapo wataalam walijengewa uwezo katika fani za uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya paleontolojia na akiolojia.

4.3.4.2 Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA

163. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 kwa lengo la kuwezesha majukumu ya uhifadhi na utafiti wa malikale. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko umewezesha utekelezaji wa Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale na Masalia ya Miili ya Binadamu iliyochukuliwa wakati wa Ukoloni, uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maeneo 2 ya Malikale ya Mji wa Kihistoria wa Bagamoyo na Magofu ya Kaole; na kutambua maeneo 16 ya malikale ili yaweze kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa. Aidha, Mfuko umewezesha uratibu wa shughuli za uhifadhi wa malikale katika maeneo 18 nchini; kufanya vikao 2 vya wadau kujadili uhifadhi na ufukuaji wa Nyayo za Laetoli; na kuandaa Kanuni za Utafiti wa Malikale na Uanzishwaji wa Makumbusho Binafsi. Vilevile, Mfuko umewezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere.

4.3.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa – NMT

164. Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa lina jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kutoa elimu kwa umma

kuhusu mikusanyo ya kisayansi na kiutamaduni yenye hadhi ya urithi wa Taifa. Vilevile, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo saba (7) vya Makumbusho ya Taifa na maeneo 107 ya Malikale yaliyopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara.

165. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuimarisha uhifadhi wa malikale na makumbusho kwa kujenga nyumba za asili saba (7) kwa mfumo wa Kaya zinazojumuisha jamii za Waha (2), Wabembe (3) na jamii ya Wamasai (2) katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Aidha, ukarabati wa nyumba za asili 13 uliohusisha Kaya za Wangoni, Wazaramo, Wamakua, Wagogo, Jamii za Makete na Wabena umefanyika katika vituo vya Makumbusho ya Majimaji, Songea (2) na Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam (11). Vilevile, ukarabati wa majenzi ya kale tisa (9) umefanyika katika eneo la Lindi mjini (1), Mbuamaji (1), Majimaji (4), Mikindani (2) na Makumbusho ya Mwl. Nyerere, Butiama (1).

166. Mheshimiwa Spika, katika kulinda na kuhifadhi urithi wa malikale, Shirika limeongeza mikusanyo mipya 1,146 inayohusisha mila, historia na biolojia na kufanya idadi ya mikusanyo iliyopo Makumbusho ya Taifa kufikia 483,937. Kati ya mikusanyo hiyo, 15 ya mila imetolewa kwa hiari na wananchi wakati wa Tamasha la Utamaduni lililofanyika mwezi Septemba, 2024 Mkoani Ruvuma; 33 ni historia ya Mwami Theresa Ntare; 11 ni fedha za kale; 1,000 ni Masalia ya Mnyama aina ya Pomboo (Dolphine); 87 ni mikusanyo ya mila iliyotolewa kutoka kwa jamii za Waha na Wabembe kutoka Mkoani Kigoma na Jamii ya Wanyakyusa kutoka Mkoani Mbeya.

167. Mheshimiwa Spika, Shirika limeimarisha miundombinu ya uhifadhi na utangazaji wa utalii wa malikale kwa kuweka vibao elekezi vitano (5) katika maeneo ya Mtwara-Mikindani (3), Tendaguru (1), Azimio la Arusha (1) na kuanza taratibu za ujenzi wa kituo cha taarifa pamoja na ukarabati wa Mnara wa Mashujaa wa Vita ya Majimaji Nandete wilayani Kilwa.

168. Mheshimiwa Spika, Shirika limeboresha uhifadhi na ukusanyaji wa taarifa za mikusanyo kwa kuendelea kutumia

mfumo wa teknolojia ya kidijitali ujulikanao kama Digital Record Archive and Management System – DRAMPS. Mfumo huu umefanikisha usajili wa jumla ya mikusanyo 1,840, hivyo kufikisha jumla ya mikusanyo 10,115 iliyosajiliwa. Kwa upande mwingine, Shirika kwa kushirikiana na Taasisi ya CyArk ya nchini Marekani imeendesha warsha ya uchukuaji taarifa za Malikale kwa teknolojia ya kidijitali katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Hatua hiyo inalenga kutumia mifumo ya kidijitali katika kuhifadhi kumbukumbu za maeneo ya malikale nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa matumizi ya utafiti na utoaji wa elimu kwa umma.

169. Mheshimiwa Spika, Shirika limeratibu na kufanya tafiti sita (6) za kimkakati zinazolenga kuimarisha maendeleo ya sekta ya malikale kwa kuongeza mikusanyo na kushirikisha wadau katika uhifadhi na uendelezaji malikale nchini. Vilevile, Shirika limetoa machapisho matano (5) na kusimamia ufanyikaji wa tafiti saba (7) katika masuala ya paleontolojia, akiolojia na michoro ya miambani zilizofanyika katika maeneo ya Olduvai Gorge, Ziwa Natron na Makuyuni-Arusha, Luxmanda-Manyara, Hifadhi ya Taifa Saadani-Pangani, Ismila-Iringa na SiuyuSingida. Pia, miradi kazi (school projects) 291 imefanyika kwa wanafunzi wa shule za sekondari 109 katika mikoa ya Dar es Salaam (187), Arusha (85), Ruvuma (11) na Mara (8). Matokeo ya kazi na tafiti hizo, yamesaidia kuimarisha maendeleo ya sekta kwa kuongeza mikusanyo; kuongeza ujuzi kwa wataalam na kuboresha programu za ushirikishaji wadau.

170. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Shirika limeweka Onesho Jipya la kudumu la ndege ya kwanza ya Serikali aina ya Jet, Fokker-28-5H-CCM iliyotumiwa na Marais wa nchi kwa Awamu Tano kuanzia mwaka 1978 hadi 2018. Onesho hilo limebeba historia ya namna usafiri wa anga ulivyokuwa na mchango kwa viongozi wakuu wa nchi katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na shughuli mbalimbali za kujenga Taifa. Sambamba na hilo, Shirika limekusanya taarifa na kuandaa maudhui ya Onesho la kudumu la Dinasoria ambalo litawekwa katika Kituo cha Taarifa Tendaguru kwa lengo la kujenga uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa urithi wa asili, uendelezaji wa malikale, kujenga

uzalendo na kutambua fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya malikale.

171. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuhamasisha umma wa watanzania kuhifadhi historia zao na kuzirithisha kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limetoa ushauri kwa Taasisi (4) na jamii (4) kuanzisha na kuendesha makumbusho binafsi. Taasisi hizo zinajumuisha: Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uanzishwaji wa makavazi ya Muungano; Mamlaka ya Bandari kuhusu kuanzisha Makumbusho ya Historia ya Usafiri wa Majini; Ujiji Heritage Development Organization-UHDO inayotarajia kuanzisha makumbusho ya mji wa kihistoria wa Ujiji- Kigoma; na Nangwanda Sijaona Foundation ya Newala Mkoani Mtwara inayotarajia kuanzisha makumbusho itakayohifadhi historia ya Ndugu Lawi Nangwanda Sijaona ambaye ni miongoni mwa Wapigania Uhuru wa Tanganyika. Vile vile, ushauri umetolewa kwa jamii (4) ambazo ni Wamatumbi kutoka wilayani Kilwa kuhusu uhifadhi wa historia ya Vita ya Majimaji; Jamii za watu wa Njombe na Nachingwea kuendeleza uhifadhi kupitia makumbusho za utamaduni; na Familia ya Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa katika kuhifadhi, kuendeleza na kutangaza historia ya kiongozi huyo.

172. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Taasisi moja (1) na wamiliki wawili (2) wameanzisha makumbusho binafsi. Taasisi hiyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichoanzisha makumbusho ya historia ya Chuo hicho, na watu binafsi wawili (2) wameanzisha makumbusho za: Jiolojia iliyopo Bagamoyo, Pwani na Makumbusho ya Kata ya Kanyigo iliyopo Misenyi, Kagera. Vilevile, wadau wawili (2) wamekarabati majengo ya kale na kuhuisha matumizi yake. Wadau hao ni Taasisi ya Islamic Club ya Kigamboni - Dar es Salaam ambayo imekarabati Msikiti wa Kale wa Mbuamaji na Bwana Vasantsinh Champs amekarabati jengo la kale moja (1) katika Mji wa kihistoria Bagamoyo na kulitumia kwa ajili ya huduma za malazi.

173. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendesha matamasha na matukio makuu matatu (3) ya kuhamasisha uhifadhi na utalii wa

malikale ambayo ni Tamasha la Waha na Wanyakyusa yaliyofanyika Kijiji cha Makumbusho-Dar es Salaam, Tamasha la Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji-Nandete (Lindi) na Songea (Ruvuma). Aidha, programu 11 za kimakumbusho zimefanyika ikiwemo programu ya Museum Art Explotion, programu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu (Museum Hub), na programu ya simulizi za kimakumbusho Museum Talk zinazorushwa kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Vilevile, vipindi 74 vya kutangaza huduma na mazao ya utalii wa malikale vimerushwa kupitia vipindi vya Radio (24), Televisheni (16) na Makala (34) katika mitandao ya kijamii. Pia, programu 40 za uhamasishaji zimefanyika katika shule za sekondari zilizopo mkoa wa Dar es Salaam (17), Arusha (5), Ruvuma (12), Mara (4) na Mtwara (2). Kupitia matamasha, programu na matukio hayo, jamii imepata elimu kuhusu uhifadhi, matumizi endelevu ya malikale na kujenga uzalendo.

174. Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya Nchi kutembelea Makumbusho, Shirika limeandaa maonesho ya muda matano (5) ambayo ni Onesho la Kimataifa la Ushirikiano kati ya Tanzania na Italia; Fursa ya Soko la Utalii Bagamoyo, Mapishi ya Vyakula vya Asili, Siku ya Zinj Duniani na Mchango wa Wanawake katika Uhifadhi wa Utamaduni, Ukombozi na Maadili ya Taifa. Uandaaji na uwekaji wa maonesho hayo umefanikisha kuhamasisha utalii wa malikale kimataifa; kujenga uzalendo kwa wananchi; kutambua manufaa yatokanayo na shughuli za uhifadhi wa Malikale Nchini pamoja na kuleta watalii takriban 7,400; Hivyo, kuwezesha idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya makumbusho na malikale kuongezeka kutoka watalii 226,135 kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024 kufikia watalii 312,048 katika kipindi cha kufikia Aprili 2025.

175. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji kazi, Shirika limewezesha watumishi 35 kuhudhuria mafunzo ndani na nje ya Nchi. Kati ya hao, watumishi 18 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 17 wanapata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuongeza ufanisi. Vilevile kufikia mwezi Aprili 2025, watumishi 19 wamepandishwa vyeo na watumishi watatu (3)

wameajiriwa kwa masharti ya ajira ya kudumu na malipo ya pensheni.

4.3.5 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka

(i) Kuimarisha Utendaji wa Wizara (Utawala na Rasilimaliwatu)

176. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Nne. Aidha, Wizara imeendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kuwahimiza watumishi kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu, maadili ya utumishi wa Umma, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu wakizingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Sambamba na hilo, Wizara imetoa elimu kwa watumishi kuhusu rushwa na maadili ambapo jumla ya watumishi 1,347 wamepatiwa mafunzo.

177. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imeajiri watumishi 676 wa kada mbalimbali na inakamilisha taratibu za ajira za watumishi wapya 556. Aidha, Wizara imewawezesha watumishi 1,800 kupata mafunzo ambapo watumishi 425 kujiunga na mafunzo ya muda mrefu, watumishi 1,375 kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 872 kupata mafunzo ya jeshi la uhifadhi. Mafunzo hayo yamekusudiwa kuwajengea uwezo watumishi kumudu majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kupata sifa za kimuundo ili kuwawezesha kupata sifa za kupanda vyeo pamoja na kuwaandaa watumishi wanaotarajia kustaafu kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kumudu maisha baada ya kustaafu. Vilevile, watumishi wa kada mbalimbali 737 wamepandishwa vyeo.

178. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kwa kuwahudumia watumishi waathirika waliojiweka wazi kwa kuwapa posho maalum kwa ajili ya lishe bora na kuwahudumia watumishi wenye ulemavu. Pia, Wizara inaendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi wa Wizara na

kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza afya zao kupitia vipeperushi na vikao rasmi vya Wizara.

179. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kutoa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kufanya mazoezi mahala pa kazi, Wizara imeendelea kutekeleza mwongozo huo unaolenga kuimarisha afya za watumishi kwa kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Morogoro Oktoba, 2024; SHIMMUTA iliyofanyika Mkoani Tanga Novemba, 2024 pamoja na Bunge Marathon 2025. Vilevile, Wizara ilishiriki katika michezo ya maadhimisho ya Mei Mosi iliyofanyika Kitaifa Aprili, 2025 mkoani Singida. Katika mashindano hayo Wizara ilifanikiwa kutwaa makombe mawili (2) na medali 36 baada ya kuzigaragaza bila huruma timu za Wizara zingine. Ushiriki wa Michezo hiyo umekuwa chachu ya kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi ya viungo, kuimarisha afya na kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

(ii) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

180. Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 31 wa World Travel Awards Portugal uliofanyika mwezi Novemba 2024 na kufanikiwa kupata fursa ya kuwa mwenyeji wa tukio la utoaji wa Tuzo za Kimataifa za Utalii zinazotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya World Travel Awards kwa mwaka 2025 Kanda ya Afrika na Ocenic. Katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki Mkutano wa 46 wa Kamati ya Urithi wa Dunia, New Delhi-India uliofanyika Julai 2024 ambapo masuala mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia yalijadiliwa na kuonekana kwamba maeneo ya Urithi wa Dunia ya Tanzania yana hali nzuri ya kiuhifadhi. Vilevile, Wizara ilishiriki Mkutano wa 122 wa Baraza Tendaji la Shirika la Utalii Duniani uliofanyika nchini Colombia Novemba, 2024.

181. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa kwenye masuala ya uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii, Wizara imeshiriki mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa ikiwemo SADC,

EAC, IORA, UNESCO, CITES, UNFCCC, UNPFII, COP-29 na Mkutano wa tisa (9) wa wataalam wa fani ya akiolojia na paleontolojia uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Agosti, 2024. Ushiriki katika matukio hayo huchochea ongezeko la idadi ya watalii, kujenga uwezo kwa watumishi, kuitambulisha Tanzania katika medani ya utalii wa kimataifa, kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kwa muktadha wa kukuza Sekta ya Utalii, Malikale na Maliasili pamoja na ongezeko la mapato kwa ujumla.

182. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Wizara imeendelea kutekeleza mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira, maliasili, malikale na utalii. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya TabiaNchi (UNFCCC); Mkataba wa UNESCO unaohusu Uhifadhi na Ulinzi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia ya Asili na Utamaduni; Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES); Mkataba wa Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ukame (UNCCD); Mkataba wa Wanyamapori Wahamao (CMS); na Mkataba wa Uhifadhi wa Bioanuai (CBD). Kwa kutekeleza mikataba hiyo, Tanzania imeendelea kushirikiana na Nchi nyingine duniani katika uhifadhi wa maliasili, malikale na ulinzi wa urithi wa Dunia.

4.4 Miradi ya Maendeleo

183. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitengewa **Shilingi 176,392,513,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi** 97,225,838,000.00 fedha za ndani; na Shilingi **79,166,675,000.00** fedha za nje. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 52,753,101,479.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali chini ya Wizara na **Shilingi 123,639,411,521.00** za Miradi inayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA, NCT, TTB, NMT, TAWIRI, TAFORI, PWTI, FTI, FITI na BTI). Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 103,897,210,974.29** sawa na **asilimia 58.9** ya fedha zilizoidhinishwa kwa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,997,221,261.09** ni fedha za ndani na **Shilingi 52,899,989,713.20** ni

fedha za nje. Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

A. Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)

184. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya **Shilingi 1,501,044,606.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 1,501,000,000.00** zimetolewa ambazo ni sawa na asilimia 99.9 ya fedha zilizoidhinishwa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuhuisha teknolojia zilizotumika kutengeneza moduli mbalimbali za Mfumo wa MNRT Portal; kuongeza moduli mpya pamoja na kufungamanisha mfumo wa MNRT Portal na mifumo ya taasisi nyingine; kufanya manunuzi ya vifaa vya TEHAMA; Hadi sasa Wizara imefanikiwa kununua Storage mpya kwa ajili ya Data centre na DR site kwa gharama ya Shilingi 450,000,000.00; kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa maafisa sita (6) nchini India na Afrika Kusini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa uendeshaji na usimamizi wa mifumo pamoja na usimamizi wa usalama wa mifumo (cyber security); na Kuwezesha kukamilisha nyaraka mbalimbali za ujenzi wa mfumo wa Kupanga madaraja huduma za malazi (ASERT), ikijumuisha kutoa mafunzo ya mfumo huo wa ASERT pamoja na kufanya majaribio ya ukubali wa mfumo (User Acceptance Test – UAT).

B. Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)

185. Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi, Ruaha, Udzungwa na katika Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Kilombero. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, mradi ulitengewa jumla ya **Shilingi 40,972,672,655.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi 92,672,655.00** zilikuwa fedha za

ndani na **Shilingi 40,880,000,000.00** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia (WB). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 26,724,909,880.75** zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 65. Fedha hizo zilijumuisha **Shilingi 26,632,237,225.75** fedha za nje na **Shilingi 92,672,655.00** fedha za ndani. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege vinne (4) katika Hifadhi za Taifa Mikumi (1), Nyerere (1) na Ruaha (2) ambapo ujenzi wake umefikia wastani wa asilimia 87.7. Maboresho hayo yamewezesha kuongezeka miruko ya ndege katika Hifadhi ya Taifa Mikumi kutoka miruko 1,719 mwaka 2022/2023 hadi 2,705 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 57.

186. Mheshimiwa Spika, mradi umekamilisha ujenzi wa majengo 41 ya utalii na watumishi katika hifadhi za Taifa Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Nyerere ikiwemo malango matatu (3) ya kuingia na kutoka hifadhini, nyumba 32 za kufikia watalii, hosteli moja (1), vituo viwili (2) vya kutolea taarifa za utalii. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa Kituo cha ufuatiliaji wa ikolojia ambapo ujenzi wa majengo katika Hifadhi za Taifa Nyerere na Ruaha umekamilika na katika Hifadhi ya Taifa Mikumi ujenzi umefikia asilimia 92. Pia, ujenzi wa njia ya juu ya utalii "canopy walkway" katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Udzungwa umefikia asilimia 70 na ujenzi wa kambi za kufikia wageni katika Hifadhi ya Msitu Asilia Kilombero umekamilika. Majengo ya utalii yataongeza uwezo wa huduma za malazi katika hifadhi za kipaumbele kwa kupokea watalii kutoka 100 kwa siku hadi watalii 453 pamoja na ongezeko la makazi kwa watumishi kutoka familia 18 hadi 72.

187. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha utafiti wa wanayamapori katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa umekamilika ambapo utasaidia kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na wanyamapori katika hifadhi za kusini mwa Tanzania. Aidha, ujenzi huu umegharimu jumla ya Shilingi 1,554,918,738.00 kati ya fedha hizo, Shilingi 1,536,707,285.21 zimelipwa sawa na asilimia 99. Ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha utalii katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa unaendelea ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 33 Ujenzi huu utagharimu jumla ya Shilingi

21,395,440,150.62 kati ya fedha hizo, Shilingi 4,494,082,089.04 sawa na asilimia 21 zimelipwa.

188. Mheshimiwa Spika, kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za mabonde madogo ya mito Chimala na Kimani na ujenzi unaendelea katika skimu za Mbuyuni-Kimani na Makangarawe zilizopo Wilaya ya Mbarali kwa kuboresha mfereji wenye urefu wa kilometa 1 na ujenzi wa skimu hizi umefikia asilimia 38.5; ujenzi wa ofisi 10 za Jumuiya za Watumia Maji (WUA) katika wilaya za Mbarali (Mwakaganga, Madibira, Mambi, Masage na Mswiswi), Makete (Matamba na Ikuwo), Wanging'ombe (Ihai na Mdadu) na Mufindi (Ikiwela) ambapo ujenzi umekamilika na utawezesha jumuiya hizo kusimamia matumizi ya maji.

189. Mheshimiwa Spika, kuwezesha ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 1,050 kutoka vijiji 61 katika vyuo 50 vilivyopo nchini ambapo jumla ya Shilingi 7,715,169,120.00 zimetumika. Aidha, vijana 561 wamemaliza masomo na 16 kati yao wamepata ajira katika taasisi mbalimbali. Ufadhili wa masomo unawasaidia vijana kujiajiri au kuajiriwa katika utoaji wa huduma za utalii na kupunguza utegemezi katika rasilimali za hifadhi; na kuratibu upatikanaji wa vikundi vya awamu ya pili katika vijiji 46 kutoka wilaya 10 (Morogoro, Kilombero, Kilosa, Mvomero, Iringa, Kilolo, Chamwino, Mbarali, Rufiji na Kisarawe) ambapo jumla ya vikundi 397 vyenye jumla ya wanachama 7,701 (Me-2,612, Ke-5,089) vimekidhi vigezo kupata fedha mtaji ambapo jumla ya Shilingi 3,593,658,275 zimetolewa. Upatikanaji wa fedha mtaji kwa awamu ya kwanza na ya pili, umewezesha uwezo wa wanachama kupata mikopo kutoka Shilingi 2,466,425,360 hadi Shilingi 5,861,754,187 sawa na ongezeko la asilimia 58 na kumwezesha mwanakikundi mmoja mmoja kujikwamua kiuchumi ambapo baadhi yao wameanzisha biashara mpya, kuboresha makazi na kuanzisha miradi.

C. Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania)

190. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (Global Environmental Facility – GEF). Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 3,660,500,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 2,632,475,000.00** zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia **72** ya fedha iliyoidhinishwa. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa ruzuku Shilingi 337,500,000.00 kwa WMA (3) zinazoshiriki uhifadhi katika ikolojia ya Ruaha – Rungwa zikiwemo WMA za WAGA, UMEMARUWA na Chamwino na jumuiya za wafugaji nyuki za MUHESI na MWAKINTARU kwa ajili ya kuwezesha miradi ya kukuza kipato na kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu. Ruzuku hiyo imewezesha utengenezaji wa mizinga 2,190 ambapo Umemaruwa WMA imepata mizinga 250, WAGA Mizinga 300, Chamwino 135, jumuiya za wafugaji nyuki za MUHESI mizinga 880 na MWAKINTARU mizinga 740. Aidha, WMA ya WAGA imepatiwa vifaa vya kufugia nyuki na kuchakata mazao ya nyuki.

191. Mheshimiwa Spika, Mradi huu pia umewezesha ununuzi wa pikipiki 20 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ulinzi kwa vikosi maalum vya kudhibiti ujangili katika kanda 10 za kiikolojia na WMA za WAGA, UMEMARUWA na MBOMIPA. Sambamba na hilo, mradi uwezesha kikao cha wadau wa uhifadhi na himasheria kujadili utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu kuzuia ujangili. Miongoni mwa masuala yaliyoazimiwa ni kuanzishwa kwa utaratibu shirikishi (Public – Private Partnership - PPP) utakaowezesha wadau kuchangia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa mwaka 2023 – 2033.

192. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Mradi umewezesha mafunzo ya uchunguzi, utambuzi wa nyara, intelijensia na uendeshaji wa mashitaka kwa maafisa 56 kutoka Jeshi la Uhifadhi, Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili na Kanda za ki-

ikolojia za kuratibu Doria. Sambamba na hilo mradi umewezesha mafunzo ya mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii kwenye mfumo Ikolojia wa Ruaha – Rungwa katika Wilaya ya Itigi, Manyoni, Iringa, Mufindi na Mbarali.

193. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha ushirikiano katika uhifadhi wa ukanda wa Afrika Mashariki, mradi umewezesha mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kubadilishana taarifa za ujangili (EAC-TWIX) kwa maafisa 31 wa Idara ya Wanyamapori, TAWA, TANAPA, TFS na NCAA na kuwaunganisha na maafisa wengine kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC ili kubadilishana taarifa kupitia mtandao huo. Mradi pia umewezesha mtandao wa ufuatiliaji wa kijamii katika mfumo ikolojia wa Ruaha - Rungwa kwa kuwapatia mafunzo, vifaa (simu) na namba mbili (2) maalum za simu za kupiga bure kupokelea taarifa. Mtandao huo umewezesha ukusanyaji wa taarifa za vitendo vya ujangili na kufanyiwa kazi kabla madhara hayajajitokeza. Katika hatua nyingine mradi umewezesha mafunzo kuhusu uhifadhi na faida zake, utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori na uendeshaji wa doria kwa viongozi 127 wa WMA za WAGA, Chamwino na UMEMARUWA.

D. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)

194. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi wa kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 950,672,655.00** fedha za ndani. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 858,000,000.00** zimetolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya TAFORI na kuboresha miundombinu ya kufundishia katika Chuo cha Mafunzo ya Misitu Olmotonyi (FTI) na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi (FITI).

E. Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)

195. Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja

wa Ulaya. Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi kwa upande wa Tanzania Bara na mkoa wa Pemba upande wa Zanzibar. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 1,371,141,150.00** kati ya **Shilingi 1,587,948,290.00** zilizoidhinishwa zimepokelewa na kutumika kwa shughuli zifuatazo: kuwezesha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 148 pamoja na ununuzi wa samani (vitanda, meza na viti) katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora. Hadi sasa, ujenzi wa bweni umefikia asilimia 68 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2025. Vilevile, mradi umewezeha ujenzi wa vituo sita (6) vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika halmashauri za wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo, na Mlele. Katika hatua nyingine, ujenzi wa kituo cha kufundishia (Manzuki darasa) kwenye Chuo cha Kilimo Zanzibar umekamilika.

196. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Mradi umewezesha taratibu za uanzishwaji wa misitu ya vijiji 22 iliyotengwa kuwa Hifadhi za Nyuki katika mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma na Singida; na hifadhi za nyuki 7 kwa mikoa ya Pemba Kaskazini na Pemba Kusini. Aidha, katika maeneo hayo mradi umewezesha kuanzisha ukanda wa kufugia nyuki kwenye Pori la Akiba Moyowosi (Hekta 139,200); kuwezesha maandalizi ya Mpango wa Biashara wa Maabara ya Taifa ya Tafiti za Ufugaji Nyuki Njiro – Arusha; kuwezesha mapitio ya Sera ya Misitu ya Zanzibar kwa kujumuisha kipengele cha ufugaji nyuki; na kuwezesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwa wakufunzi sita (6) kutoka Chuo cha Kilimo Zanzibar. Vilevile, mradi umeandaa mwongozo wa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa Chuo cha Kilimo Zanzibar; kuwezesha maandalizi na uzinduzi wa Alama ya Asali ya Tanzania (Honey Trademark); vikao sita (6) vya wafanyabiashara ya Mazao ya Nyuki na Serikali ili kutatua vikwazo vya kibiashara; na vikao 10 vya kujenga uwezo katika usimamizi na uendeshaji wa taasisi au Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki.

197. Mheshimiwa Spika, Mradi pia umewezesha mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa vijana na wanawake 973 kutoka

Tanzania Bara na Zanzibar na kutoa mizinga ya nyuki 2,200 kwa vikundi 40 vya wafugaji nyuki; kuwezesha mafunzo ya kushona mavazi kinga ya nyuki kwa mafundi 20 kutoka Pemba; kuwezesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa wafanyabiashara 35 kuhusu Kanuni mpya za biashara ya mazao ya nyuki kwenye masoko katika nchi za Umoja wa Ulaya; mafunzo ya kuimarisha ushirika kwa wajumbe 25 wa bodi kutoka TABEDO na PEBA; na kuwezesha wafanyabiashara 35 wa mazao ya nyuki kushiriki katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) Jijini Dar es Salaam.

F. Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use nd Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR)

198. Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani "Global Environmental Facility – GEF". Mradi una lengo la kukuza usimamizi jumuishi wa rasilimali za ardhi, maji na misitu nchini, na unatekelezwa katika kongani ya Kilombero kwa upande wa Tanzania Bara na Kaskazini A na B kwa upande wa Zanzibar. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 2,474,900,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 1,422,400,000** zimetolewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: Kufanya maboresho ya ofisi za mradi zilizopo Kilombero na Zanzibar kwa kununua vifaa vya ofisi na vitendea kazi vya mradi; kuwezesha vikao vya mradi kwa ajili ya kujadili na kupitisha mpango na bajeti ya utekelezaji wa shughuli za mradi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kikao cha wadau cha utekelezaji wa mpango huo; kukusanya taarifa za msingi za mradi kuhusu maeneo mahsusi ya ikolojia kwa ajili ya uhifadhi, mnyororo wa thamani wa zao la mpunga na kuandaa mpango wa uhifadhi wa ikolojia ya Kiashange-Mokotoni na Kinyasini Zanzibar. Vilevile, mradi umewezesha kazi ya utambuzi wa fursa za uwekezaji, na maeneo ya kuhifadhi, kuanzisha na kuimarisha jukwaa la pamoja la wadau watekelezaji mradi katika ikolojia ya Kilombero na Zanzibar.

G. Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Marais - Dodoma

199. Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo katika mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 1,000,000,000.00** ziliidhinishwa na kupokelewa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni kuajiri Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu, kuandaa michoro na makadirio ya gharama za ujenzi. Mtaalam huyo, amekabidhiwa eneo la mradi mwezi Machi, 2025 na anaendelea na kazi ambayo itakamilika mwezi Julai, 2025. Aidha, taratibu za ununuzi wa vitendea kazi likiwemo gari la mradi zinaendelea.

H. Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii

200. Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za ndani. Mwaka wa fedha 2024/2025, **Shilingi 2,757,658,485.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mafunzo. Hadi Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 1,240,171,685.59** zimepokelewa na kutumika katika ujenzi wa jengo la taaluma lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 katika Kampasi ya Arusha ambapo ujenzi umefikia asilimia 65 pamoja na kufanya ukarabati wa jengo la taaluma katika Kampasi ya Bustani kwa kutumia fedha kutoka vyanzo vya mapato ya ndani (Own source) kiasi cha **shilingi 88,049,700.00** ukarabati huu umefikia asilimia 30.

I. Miradi ya TANAPA

201. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 (Julai 2024 – Aprili 2025) Shirika limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za nje ambapo miradi iliyotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Msaada wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Tanzania; Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti awamu ya kwanza na ya Pili pamoja na Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya Hifadhi za Taifa za Katavi, Mahale, na Ushoroba wa Uunganishi. Miradi hii yote inafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia benki ya

maendeleo ya KfW ambapo jumla ya **Shillingi 16,475,916,669.99** zilitumika kati ya **Shilingi 18,633,325,000.00** zilizotengwa.

202. Mheshimiwa Spika, kupitia mradi wa Msaada wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Nchini Tanzania (ERB) shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi wa malori 5 (Serengeti - 2 na Nyerere – 3), mitambo 5 ya kutengeneza barabara Hifadhi ya Taifa Serengeti (grader 2, compactor 1, excavator 1 na back hoe loader 1), kulipia gharama za doria za askari za magari na ndege zikiwemo posho, sare, mafuta ya magari, matengenezo ya magari 79 (Serengeti 51 na Nyerere 28), uwekaji wa mifumo mipya ya nishati ya jua katika vituo 12 vya askari hifadhi ya Serengeti, kufanya utafiti wa maji katika vituo 2 vya askari pamoja na kukarabati visima vinne (4) vya mafuta katika hifadhi ya Taifa Nyerere. Vilevile mradi umejenga karakana moja ya magari Arusha, umetoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 5,621 pamoja na kuendeleza vikundi vya kukuza uchumi katika Wilaya za Busega, Meatu na Itilima. Aidha, Mradi umefanikisha uandaaji wa mpango wa usimamizi mioto (FMP) katika hifadhi ya Taifa Nyerere.

203. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti (SEDCP I) - Awamu ya Kwanza umetekeleza miradi ya matengenezo ya barabara za mchepuko (rehabilitation of feeder roads) zenye urefu wa kilomita 73.52 (Wilaya ya Serengeti kilometa 27.82 na box culvert 5, Wilaya ya Ngorongoro kilometa 46.7), ujenzi wa kituo cha kutolea taarifa katika eneo la Seronera na miradi ya kijamii 18 pamoja na mabwawa 8 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti (SEDCP II) Awamu ya Pili umewezesha tafiti za topografia na haidrojia kwa ujenzi wa daraja la Kogatende, ukarabati wa jengo la Fort Ikoma, visima vya uvunaji maji. Aidha, mradi umewezesha ukamilishaji wa mipango ya matumizi bora ya Ardhi kwenye vijiji 18 na kutoa mafunzo ya COCOBA kwa vikundi 36 vyenye wanachama 659 katika Wilaya za Bariadi, Tarime na Bunda kupitia hifadhi ya Taifa Serengeti.

204. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya Hifadhi za Taifa Katavi, Mahale, na Ushoroba unaounganisha hifadhi hizi

mbili (KAMACO) umefanikisha kazi ya kuwekwa kwa vigingi 45 na mabango 15 katika Hifadhi ya Msitu ya Kijiji cha Lufubu, Wilaya ya Uvinza na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 18 (10 vya Wilaya ya Tanganyika na 8 vya Wilaya ya Uvinza); marejeo ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu kwa kushirikisha jamii katika vijiji vitatu: Kafisha, Kaparamsenga, na Songambele; uondoaji wa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 159; na kuzoesha na kufuatilia sokwe 63 katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale. Aidha, mradi umekabidhi mashine aina ya excavator, mahema, simu za mkononi katika hifadhi ya Taifa Katavi; na lori la tani saba (7) na injini za boti tatu (3) katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

J. Miradi ya TAWA

205. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ilidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 22,004,578,381.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha **Shilingi 11,479,826,671.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,524,751,710.00** fedha za nje. Hadi Kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 3,881,872,668.45** zimepokelewa ambapo **Shilingi 2,960,569,668.45** ni fedha za nje na **Shilingi 921,303,000.00** ni fedha za ndani. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Kufanya ukarabati wa kilometa 393 za barabara na viwanja vidogo viwili (2) vya ndege katika Pori la Akiba Selous; Kununua na kufunga injini mpya ya ndege (5H SGR); na kununua magari matano (5) ya doria.

206. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika Shule ya Ngumbu-Liwale, Shule ya Sekondari Mwaseni-Rufiji na Shule ya Msingi Miguruwe; ujenzi wa ofisi, nyumba ya wageni umefikia asilimia 46, bweni la watumishi ambao umefikia asilimia 76 na karakana ambao upo asilimia 41 katika Pori la Akiba Selous kanda ya Kingupira; ofisi katika Pori la Akiba Selous kanda ya Miguruwe ambao upo katika hatua ya kupiga plasta; Bweni la wasichana Shule ya Sekondari Mchengerwa ambao upo katika hatua ya kuezeka. Aidha, Miradi inayoendelea inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2025.

5.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

207. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge, maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

208. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi kupitia matangazo katika ligi kuu za michezo mashuhuri duniani, mashindano ya kimataifa, mashirika ya ndege; misafara ya utangazaji utalii; matamasha makubwa ya kimataifa na mitandao mbalimbali ya Kimataifa na Vyombo vya Habari;

(ii) Kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo maeneo ya malikale pamoja na utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo, tiba na utamaduni;

(iii) Kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi ikiwemo barabara, viwanja vya ndege na huduma za utalii;

(iv) Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi na rasilimali, ufuatiliaji, utangazaji na uendeshaji wa shughuli za utalii;

(v) Kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale;

(vi) Kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya Misitu na Nyuki;

(vii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu mbalimbali, kufanya tafiti za kimkakati na kutoa huduma za ushauri zinazohusu masuala ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori, misitu na nyuki, malikale na uendelezaji utalii;

(viii) Kuelimisha na kuhamasisha Jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, malikale, misitu na ufugaji nyuki;

(ix) Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na uhifadhi; na

(x) Kuandaa na kufanya Mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii.

5.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

209. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,183,584,115,330.55** kutoka kwenye Idara na Taasisi zake.

5.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

210. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 359,982,271,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000.00** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 105,749,922,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara **Shilingi 130,709,054,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 123,523,295,000.00.** Fedha za Miradi ya Maendeleo

zinajumuisha **Shilingi 32,476,051,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** fedha za nje.

211. Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 254,232,349,000.00 zinajumuisha Shilingi 32,527,989,914.00 kwa ajili ya Wizara na Shilingi **221,704,359,086.00** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 10,189,499,000.00** ni Mishahara na **Shilingi 22,338,490,914.00** ni Matumizi Mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 120,519,555,000.00** za Mishahara na **Shilingi 101,184,804,086.00** za Matumizi Mengineyo.

5.3 Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

5.3.1.1.1.1 Idara ya Wanyamapori

212. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya Shilingi **48,312,790,524** zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa helikopta 2 kupitia taasisi za uhifadhi za TANAPA (1) na NCAA (1); uchimbaji wa mabwawa 12 katika Mapori ya Akiba ya Rungwa (2), Kizigo (2) Muhesi (2), Maswa (1), SelousKingupira (1), Wami-Mbiki (1), Msanjesi (1) na Hifadhi za Taifa za Katavi (1), na Mikumi (1); uchimbaji wa visima vya maji 18 katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro (1), Mikumi (6), Mkomazi (2), Tarangire (7), Mto Ugala (1) na Milima ya Udzungwa (1).

213. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara kupitia taasisi za TANAPA na NCAA itajenga uzio wa umeme wenye jumla ya urefu wa Kilometa 53 ambapo Kilometa 38 ni kutoka Tabora B hadi Mto Mara katika Hifadhi ya Taifa Serengeti na Kilometa 15 kutoka lango la Loduare kuelekea Oldiani katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, Wizara kupitia taasisi zake (TAWA, TANAPA na NCAA) itajenga vituo 19 vya askari kwenye maeneo yenye changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya za Tunduru (2), Kiteto (1), Ikungi (1), Nkasi (1), Itilima (1), Manyoni (1), Kilosa (1), Rufiji (1), Babati (1), Morogoro (2), Karatu (1), Monduli (2) na hifadhi za taifa za Ibanda Kyerwa (1), Mto Ugala (1), Rumanyika Karagwe (2) na ujenzi wa

vizimba 50 katika maeneo yenye changamoto ya mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya za Nkasi (3), Sengerema (3), Buchosa (3), Kibiti (3), Rufiji (3), Morogoro (3), Namtumbo (2), Nanyumbu (2), Uvinza (2), Geita (2), Kibaha (2), Mkuranga (2), Busega (2), Mvomero (2), Nyasa (2), Songwe (2), Iringa (3), Kilosa (1), Tarime (2), Kalambo (2), Mkinga (1), Nanyamba (1), na Ukerewe (2).

214. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na wadau itawajengea uwezo Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 100 kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya 20. Vilevile, Wizara itafanya semina pamoja na kununua pikipiki 22 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya 22 ili kuendelea kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao na kuwawezesha kufika kwenye maeneo ya matukio kwa wakati, mtawalia.

215. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushiriki wa jamii katika uhifadhi, Wizara itaendelea kuwezesha uanzishaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori nne (4) katika wilaya za Uvinza, Mkalama, Kilolo na Ikungi. Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo kwa WMA mpya na zilizopo kwa kuziwezesha vitendea kazi zikiwemo pikipiki 12 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori. Vilevile, Wizara itaendelea kuandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutatua changamoto za usimamizi wa WMA nchini.

216. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege nyuki (drones) 12 na mikanda maalum ya mawasiliano 50 (GPS Satellite Collars) kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori hao. Mikanda hiyo itafungwa kwa tembo viongozi katika maeneo yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Wizara itanunua na kusambaza mabomu baridi 40,000 katika maeneo yenye changamoto ya Tembo. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kufanya tafiti za kimkakati kwa ajili ya kugundua mbinu mpya za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

217. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022 - 2026 kwa kuendelea kuelimisha jamii zilizopo kwenye maeneo ya shoroba za wanyamapori za: Ziwa Manyara, Kwakuchinja, Serengeti Complex – Yaeda Chini, Nyerere Selous – Niassa, Ruaha – Rungwa – Udzungwa, Ruaha – Rungwa – Katavi Complex, Kilombero – Milima ya Udzungwa, Nyerere Selous – Wami Mbiki, Serengeti Complex – Longido, na Udzungwa – Mikumi; pamoja na kuendelelea kufanya tathmini ya hali halisi ya maeneo hayo, kubainisha mipaka na kuweka mabango.

218. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi watakaoathirika na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011 na marejeo yake ya mwaka 2024.

219. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori, Wizara kupitia Taasisi zake za Uhifadhi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023-2033; Mpango wa Usimamizi wa Tembo wa Mwaka 2023-2033; na Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022-2026. Utekelezaji wa mipango na mikakati hii itawezesha kudhibiti matukio ya ujangili na biashara haramu ya nyara nchini pamoja na kuimarisha uhifadhi. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283 na Kanuni zake kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

5.3.1.2 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

220. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko utaendelea kuwezesha; utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu mbalimbali za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kulipa kifuta jasho na machozi kwa wananchi watakaoathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu; kuwezesha Kikosi kazi cha Taifa cha Kudhibiti Ujangili; utatuzi wa migogoro kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishaji hadhi maeneo yaliyohifadhiwa; na kujenga uwezo katika

usimamizi wa rasilimali za wanyamapori. Katika hatua nyingine Mfuko utawezesha vyuo vya mafunzo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tafiti za kimkakati za wanyamapori.

5.3.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

221. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za ulinzi katika hifadhi za Taifa kwa kufanya doria 99,291. Aidha, Shirika litaweka alama kwa faru 45 ili kufuatilia mienendo yao katika Hifadhi za Taifa Serengeti (25) na Mkomazi (20) pamoja na kufunga mifumo ya redio katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro (1), Milima ya Udzungwa (1), Ruaha (1), na Saadani (1) kwa ajili ya mawasiliano. Vilevile, Shirika litajenga vituo vinne (4) vya askari katika hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Mto Ugalla (1) na Rumanyika-Karagwe (2) na kukarabati vituo vya askari vitano (5) katika Hifadhi za Taifa Katavi (1), Kitulo (1), Milima ya Mahale (1), Milima ya Udzungwa (1) na Tarangire (1) ili kuimarisha ulinzi na kukabiliana na matukio ya ujangili.

222. Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha wanyamapori wanapata maji ya kutosha ndani ya hifadhi kwa kuchimba mabwawa (2) na visima virefu 18 na katika Hifadhi za Taifa (Kilimanjaro (1), Mikumi (7), Mkomazi (2), Tarangire (7), Mto Ugala (1), Katavi (1), na Milima ya Udzungwa (1). Sambamba na hilo, Shirika litaondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8,838.20 ili kuongeza nyanda za malisho kwa wanyama katika hifadhi za Taifa Arusha (1,105.6), Mikumi (4,800), Mkomazi (200), BurigiChato (300), Gombe (10), Katavi (6), Nyerere (50), Serengeti (500), Saadani (372), Rumanyika-Karagwe (25), Kisiwa cha Rubondo (400), Ziwa Manyara (40), Milima ya Udzungwa (39.6), Ibanda-Kyerwa (800), Tarangire (100), Ruaha (15), Kitulo (5), Kisiwa cha Saanane (22) na Mto Ugalla (48). Aidha, Shirika litaboresha eneo la malisho ya wanyamapori lenye ukubwa wa hekta 900 katika hifadhi ya Ziwa Manyara.

223. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye uhifadhi, Shirika litatekeleza miradi mbalimbali kwa jamii zinazopakana na hifadhi zote 21. Miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa mabweni saba (7) katika shule za Sekondari wilayani Namtumbo (1), Kyerwa (1), Serengeti (2), Moshi (1), Arumeru (1), na Tunduru (1) pamoja na hosteli ya wasichana wilaya ya Chunya; kuweka mifumo ya gesi ya kupikia katika shule sita (6) wilaya za Moshi (2), Hai (2) na Rombo (2); kujenga madarasa 24 wilayani Handeni (4), Busokelo (2), Monduli (2), Kilosa (2), Kyerwa (3), Serengeti (6), Lushoto (2) na Bariadi (3). Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha ujenzi wa nyumba 2 za walimu wilayani Simanjiro (1) na Babati Vijijini (1); kujenga matundu 30 ya vyoo katika shule za msingi Wilayani Busokelo (7), Simanjiro (7), Urambo (7) na Karatu (9) na kusambaza samani (viti na meza) 600 katika shule zilizopo katika Wilaya za Kaliua (200), Urambo (200), na Uvinza (200), pia ununuzi wa kompyuta 20 na kompyuta mpakato 24 katika shule ya sekondari Musati Wilaya ya Serengeti. Aidha, Shirika litawezesha miradi ya ufugaji nyuki kwa vikundi viwili wilayani Karatu kwa kugawa mizinga ya nyuki 200; Ujenzi wa mabwawa na Vizimba (3) kwa ajili ya ufugaji samaki Wilayani Mpanda (1), Chato (1) na Nyamagana (1). Vilevile, Shirika litawezesha ujenzi wa maabara katika zahanati mbili (2) Wilayani Karagwe (1) na Kigoma (1), jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kituo cha afya Mwakijembe wilaya ya Mkinga; pamoja na ujenzi wa jengo la "infusion unit" hospitali ya Mpanda. Sambamba na hilo, Shirika litawezesha ujenzi wa kituo cha polisi wilaya ya Iringa Vijijini pamoja na ujenzi wa ofisi ya kijiji wilaya ya Kilombero.

224. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za utalii, Shirika litajenga "Picnic Sites" 4 katika Hifadhi za Taifa Ziwa Manyara (1), Kisiwa cha Rubondo (1) na RumanyikaKaragwe (2); Cottages 18 katika Hifadhi za Taifa za Saadani (1), Arusha (1), Kilimanjaro (2), Ziwa Manyara (5), Katavi (2), Ibanda-Kyerwa (3), Milima ya Mahale (1) na Kisiwa cha Rubondo (3); majiko katika kambi za utalii na maeneo ya kulia chakula matano katika Hifadhi za Taifa za Mkomazi (1), Tarangire (1), Katavi (1), Kitulo (1) na Burigi-Chato (1); "Rest Houses" 3 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (2) na Ziwa Manyara (1) na vyoo vya wageni 15 katika Hifadhi za Taifa za Mikumi (2), Arusha (1), Kilimanjaro (5), Tarangire (4),

Nyerere (1) na Ruaha (2). Shirika litajenga malango 6 ya kuingilia wageni katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Saadani (2), Mikumi (2) na Mto Ugalla (1).

225. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Shirika litaboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga barabara ya kilomita 6.69 ya tabaka gumu ili kuunganisha Hifadhi ya Tarangire na barabara ya lami eneo la Minjingu hadi lango kuu la Hifadhi. Sambamba na hilo, Shirika litafungua barabara mpya kuu na barabara za utalii zenye urefu wa kilomita 1,027.19 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 2), Burigi-Chato (km 50), Milima ya Mahale (km 22), Nyerere (km 150), RumanyikaKaragwe (km 1), Serengeti (km 561), Tarangire (km 181.19), Milima ya Udzungwa (km 45) na Mto Ugalla (km 15). Sambamba na hilo, Shirika litafanya ukarabati mkubwa wa viwanja vya ndege 11 katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Serengeti (7), Katavi (1), Milima ya Mahale (1) pamoja na Kisiwa cha Rubondo (1); na kufanya ukarabati mdogo kwa viwanja 17 katika hifadhi za Nyerere (5), Kilimanjaro (5), Ugalla (2), Mikumi (1), Saadani (1), Serengeti (1) na Tarangire (1).

226. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Shirika litakarabati barabara za utalii na barabara kuu zenye urefu wa kilomita 2,596 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 104), Burigi-Chato (km 50), Ibanda-Kyerwa (km 90), Katavi (km 159.50), Kilimanjaro (km 286.80), Kitulo (km 25), Ziwa Manyara (km 341), Mkomazi (km 20), Nyerere (km 400), Ruaha (km 231), Kisiwa cha Rubondo (km 79), Saadani (km 16.5), Tarangire (km 220), Milima ya Udzungwa (km 93.8), Rumanyika-Karagwe (km 90), Mikumi (km 140) na Mto Ugalla (km 100). Vilevile, Shirika litakarabati njia za kutembea kwa miguu (trails) za kilomita 908.7 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 32), Gombe (km 10), Kilimanjaro (km 629.20), Ziwa Manyara (km 4.8), Milima ya Mahale (km 105), Kisiwa cha Rubondo (km 21), Saadani (km 30), Tarangire (km 1.7), Kitulo (km 1) na Kisiwa cha Saanane (km 0.4).

227. Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kutangaza fursa za uwekezaji ikiwemo malazi katika hifadhi kulingana na mpango wa ujumla wa hifadhi husika. Kadhalika, Shirika litaboresha na kuimarisha mazao ya utalii kwa kuendelea kuboresha mazao

yaliyopo na kubuni mazao mapya ya utalii ikiwemo kuanzishwa kwa utalii wa majini ndani ya Ziwa Viktoria unaounganisha Hifadhi za Taifa Kisiwa cha Saanane, Kisiwa cha Rubondo na Serengeti ili kufungua aina mpya ya utalii kupitia eneo la Ghuba ya Speke. Aidha, Shirika litaendelea na ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa gofu pamoja na hoteli ya Chato ili kuanza kutumika na kuongeza idadi ya wageni pamoja na mapato kwa ujumla. Vilevile, Shirika limetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa Samani na vifaa katika majengo yaliyojengwa na ufadhili wa mradi wa REGROW katika Hifadhi za Taifa Ruaha, Nyerere, Mikumi, na Milima ya Udzungwa ili majengo hayo yaliyokamilika yaweze kutumika na kufikia malengo tarajiwa.

228. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Shirika linaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato pamoja na kuboresha huduma kwa wageni, jumla ya "smart gates" 15 katika hifadhi za Serengeti (8), Manyara (1), Arusha (2), Mkomazi (2), Mikumi (1) na Tarangire (1) zitawekwa.

229. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, Shirika litajenga nyumba 3 za watumishi, na kukarabati nyumba 133 katika hifadhi za Ibanda-Kyerwa (1), Milima ya Mahale (36), Mkomazi (1), Nyerere (61), Ruaha (5), Rumanyika-Karagwe (1), Serengeti (1), Tarangire (2), Milima ya Udzungwa (7), Kitulo (2), TANAPA Makao Makuu (16), Southern Zone (1) na Mto Ugala (2). Aidha, Shirika litajenga ofisi 3 katika Kanda za Magharibi (1), Kaskazini (1), na Mashariki (1). Vilevile, Shirika litawezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi (6) na mafunzo ya muda mfupi ya nyanja mbalimbali kwa watumishi (1,500) ikiwa ni pamoja na kuwezesha watumishi kushiriki michezo katika ngazi zote. Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha upatikanaji wa vifaa vya utendaji kazi ikiwemo ununuzi wa magari 28, magari ya zimamoto 4 kwajili ya viwanja vya ndege vya Hifadhi za Taifa Mikumi (1), Nyerere (1) na Ruaha (4), ili kuongeza ufanisi.

5.3.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania–TAWA

230. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka itaendelea kudhibiti ujangili na biashara haramu ya nyara kwa kuimarisha doria ambapo jumla ya doria 18,920 zitafanyika. Aidha, Mamlaka itajenga vituo vitatu (3) vya askari katika mapori ya akiba ya Moyowosi, Luganzo na Pori Tengefu Ziwa Natron. Sambamba na hilo, Mamlaka itanunua injini 10 za boti, pikipiki 16, boti (1) na trekta (1) kwa ajili ya kuimarisha doria katika maeneo ya nchi kavu, maeneo yenye maziwa, mito na ardhioevu. Vilevile, Mamlaka itanunua ndege nyuki (drones) sita (6) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na mwitikio wa haraka kudhibiti na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu.

231. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Mamlaka itajenga kilomita 197 za barabara katika Mapori ya Akiba Wami-Mbiki (150), Mpanga Kipengere (30), Rukwa (17) na kufanya ukarabati wa kilomita 220 za barabara katika Mapori ya Akiba Kizigo (120) na Muhesi (100). Vilevile, Mamlaka itajenga kiwanja cha ndege katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere; kambi moja (1) ya wageni (campsite) katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni; maeneo ya kupumzikia wageni (picnic sites) matatu (3) katika Mapori ya Akiba Mpanga Kipengere (2) na Wamimbiki (1); na njia ya waenda kwa miguu kilomita 2 katika Bustani ya Wanyamapori Tabora.

232. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itashiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji pamoja na utalii wa picha na uwindaji. Miongoni mwa maonesho hayo ni Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2025), Dallas Safari Club International - USA, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane na Kizimkazi Festival (Zanzibar).

233. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Kanda ya Uhifadhi Magharibi mkoani Tabora; ujenzi wa nyumba ya watumishi (1) katika Pori la Akiba Piti; ununuzi wa magari 23 kwa ajili ya shughuli za doria (18), utawala (1) na usimamizi wa utalii (4); na ujenzi wa uzio kwa ajili ya ghala la silaha katika Pori la Akiba Lukwika-Lumesule. Vilevile, Mamlaka itawezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 163 katika fani mbalimbali; mafunzo ya ukakamavu na utayari kwa watumishi 351; na kuwezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMUTA.

5.3.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA

234. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori kwa kufanya doria 5,492, doria maalum mbili (2) na doria za mwitikio wa haraka wa kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga vituo viwili (2) vya askari katika maeneo ya Ndorobo na Mbulumbulu na kufanya ukarabati wa vituo vya askari vitatu (3) katika maeneo ya Naiyobi, Endamagha na Lemala. Aidha, Mamlaka itafunga visukuma mawimbi kwa faru 32 ili kufuatilia mienendo yao ndani ya Hifadhi pamoja na kuwapatia mafunzo askari 33 katika mfumo wa kufuatilia mienendo ya faru.

235. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Mamlaka itasafisha mpaka wenye urefu wa kilomita 200 na kuweka vigingi 150 kwa lengo la kuweka alama ya mipaka na kuepusha changamoto ya moto holela. Aidha, Mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano na jamii zinazopakana na hifadhi kwa kuwezesha miradi ya maendeleo na kufanya mikutano 108 ya ujirani mwema kwa lengo la kutoa elimu ya uhifadhi na kutatua migogoro. Sambamba na hilo, Mamlaka itafanya mafunzo kwa vikundi vitano (5) vinavyozunguka Hifadhi. Mafunzo hayo ni katika eneo la ufugaji bora wa nyuki, kuongeza thamani mazao ya nyuki na utafutaji wa masoko ya nyuki.

236. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kuondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,000 lililoathirika ndani ya hifadhi. Vilevile, hekta 8,000 zitachomwa moto kupitia moto mpango ili kuboresha nyanda za malisho katika maeneo hayo. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaotesha jumla ya miche ya miti 100,000 na kuigawa kwa wadau mbalimbali na jamii zinazopakana na hifadhi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa ikolojia wa Serengeti-Masai Mara.

237. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka itajenga barabara zenye jumla ya kilomita 64.5 ambazo ni Loduare hadi Golini kilomita 29.5 kwa kiwango cha tabaka gumu la zege, Enduleni hadi Olpiro kilomita 15 kwa kiwango cha changarawe na mtandao wa barabara za Ndutu kilomita 20 kwa kiwango cha changarawe. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa mtandao wa barabara wenye kilomita 346 na ukarabati wa viwanja viwili (2) vya ndege Ngorongoro na Ndutu. Sambamba na hilo, Mamlaka itachimba kisima kimoja (1) Laitole na kusimika pampu tano (5) za maji katika kisima cha Olduvai (1), Ndutu (1), kituo cha Askofu (1) na Lerai (2). Katika hatua nyingine, Mamlaka itafunga umeme wa nishati ya jua katika vituo vya askari vinne (4) vilivyopo maeneo ya Galusi, Ndolobo, Lostete na Olduvai na itafanya ukarabati katika vituo vya huduma za utalii sita (6) katika maeneo ya Lemala, Ngoitiktok, Viewpoint, Simba A, Lerai na Mumba.

238. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuongeza thamani vivutio vya utalii kwa kuboresha njia za watembea kwa miguu (walking trails) katika eneo la Endoro na Empakai; kuendelea na utangazaji wa vivutio na matukio mbalimbali kutoka hifadhini mubashara kupitia Ngorongoro live streaming na; kushiriki katika matukio na maonesho ya utalii na uhifadhi ndani ya nchi (15) na nje ya nchi (14) pamoja na misafara ya utalii mitano (5) na kampeni nne (4) za ndani kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani.

239. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea na jukumu la kutoa ufadhili wa ada, fedha ya kujikimu na nauli kwa wanafunzi wenyeji 1,347: katika ngazi za chuo kikuu wanafunzi 14, vyuo vya kati wanafunzi 167, na sekondari

wanafunzi 1,166. Aidha, Mamlaka itaendelea na huduma ya ugawaji unga wa uji na sukari kwa shule 26 za msingi zilizopo ndani ya hifadhi, ujenzi wa vyoo vitano (5) katika shule za msingi za Bulati, Ildonyo, Makao mapya, Meshili na Misigiyo. Vilevile, Mamlaka itaendelea na utoaji wa huduma za afya kwa wakazi ndani ya Hifadhi katika zahanati ya Mamlaka.

240. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi Mamlaka itakamilisha ujenzi wa ofisi ya Makao makuu wilayani karatu katika eneo la Kamny. Aidha, Mamlaka itawezesha watumishi 35 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 80 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Mamlaka itawawezesha watumishi 93 kuhudhuria katika mashindano ya SHIMUTA pamoja na mashindano mengine ambayo Mamlaka inaalikwa kushiriki.

5.3.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

241. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi itaendelea kufanya, kuratibu, na kusimamia tafiti za wanyamapori kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi na utalii endelevu. Maeneo ya kipaumbele katika tafiti zitakazofanyika ni pamoja na; tafiti za mahusiano ya viumbe na ikolojia zao; afya ya mifumo ikolojia; uhifadhi wa bioanuai na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia mbalimbali; matumizi ya teknolojia katika uhifadhi; na migongano kati ya binadamu na wanyamapori. Aidha, Taasisi itatekeleza zoezi la kuidadi wanyamapori aina ya Kanivora katika mifumo ikolojia 9 nchini. Vilevile, Taasisi itasambaza matokeo ya tafiti kwa Serikali na wadau wa uhifadhi na utalii, kuandaa Kongamano la 15 la Kimataifa la Kisayansi na kutoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

242. Mheshimiwa Spika, Taasisi itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 12 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 40 ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

5.3.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka – CAWM

243. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi wapatao 1,498 katika fani za Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii; na Usimamizi wa Mazingira na Uthibiti wa taka. Kozi hizo zitatolewa katika ngazi ya Cheti cha Msingi hadi Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi katika Nyanja za Usimamizi wa Wanyamapori, Utalii na Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa taka.

244. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kutoa mchango katika utatuzi wa changamoto zinazokabili Sekta ya Wanyamapori na Utalii, Chuo kitaendelea kufanya tafiti katika nyanja za bioanuwai, uhifadhi wa mazingira na jamii ya mimea, Uhifadhi wa wanyamapori, magonjwa ya wanyamapori na binadamu, Usimamizi wa utalii na Migongano baina ya wanyamapori na binadamu. Aidha, Chuo kitaendelea kutekeleza jukumu la kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani kwa wadau mbalimbali wakiwemo Serikali na Taasisi zake pamoja na Sekta binafsi.

245. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na wanafunzi, Chuo kitajenga jengo la Maktaba ya Kisasa, Darasa moja (1), ghala la silaha (1) na uzio wa ukuta katika Kampasi ya Chuo. Aidha, Chuo kitakarabati mabweni manne (4), madarasa mawili (2), nyumba tano (5) za watumishi, ofisi nane (8) na kujenga njia za ndani zenye urefu wa kiomita 1.5 katika Kampasi kuu ya Chuo. Vilevile, Chuo kitanunua na kufunga vifaa vya TEHAMA, kununua mabasi mawili (2) na mahema 100 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi. Sambamba na hilo, Chuo kitaweka miundombinu ya umeme na kuchimba kisima kimoja (1) cha maji katika eneo la mafunzo lililoko Arash, Tarafa ya Loliondo.

246. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Chuo kitaandaa mitaala mipya miwili (2) katika nyanja za Usimamizi wa Malikale (Cultural Heritage Management) na Uendeshaji wa Utalii na Safari (Travel and Tourism Management). Aidha, Chuo kitafanya mapitio ya program za mafunzo zilizopo ili kutoa elimu yenye tija katika kutatua changamoto za wanyamapori na utalii nchini.

247. Mheshimiwa Spika, ili kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Chuo kitawawezesha watumishi 36 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 85 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitaajiri watumishi wapya 22 ili kukidhi mahitaji ya utendaji na kuendelea kutoa stahiki kwa watumishi wa Chuo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo.

5.3.1.8 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC)

248. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo cha mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa wanafunzi 489, kati yao wanafunzi 169 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 320 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, kituo kitaendelea kushiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa ajili ya kutangaza shughuli za kituo na kutoa elimu.

249. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, kituo kitaendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga nyumba moja (1) ya watumishi, bweni moja (1), na kukamilisha ujenzi wa nyumba moja (1) ya watumishi. Aidha, kituo kitanunua vifaa vya mafunzo na malazi ikiwemo kompyuta (35), meza za kompyuta 35, vitanda 100, magodoro 200 na madawati 100. Sambamba na hilo, Kituo kitaweka mfumo wa maktaba mtandao (E- Library) pamoja na kufanya mapitio ya mtaala wa kozi ya Stashahada ya Utalii na Uongozaji Watalii. Vilevile, Kituo kitaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha watumishi sita (6) kushiriki mafunzo ya muda mfupi na watumishi wawili (2) wataendelea na masomo ya muda mrefu.

5.3.1.9 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi – PWTI

250. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi itadahili wanafunzi 670 katika fani za Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na Usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Vilevile, Taasisi itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 250. Katika hatua nyingine, Taasisi itaanza kufundisha Kozi za Stashahada ya Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji watalii na Usalama.

251. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Taasisi itawezesha watumishi watatu (3) kuendelea na masomo ya muda mrefu. Aidha, taasisi itakamilisha ujenzi wa maktaba na uzio; kujenga bweni la ghorofa mbili (2) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 240, madarasa manne (4) ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400. Vilevile, Taasisi itachimba kisima kimoja (1) cha maji katika kambi mpya ya mafunzo iliyoko Kata ya Matongo Wilaya ya Bariadi.

5.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

5.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

252. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya Mwaka 2002; Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) wa Mwaka 2007 na Mwongozo wa Uvunaji Endelevu katika Misitu ya Asili. Vilevile, Wizara itaandaa miongozo mitano (5) ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mashamba ya Miti, Mwongozo wa Bima ya Mazao ya Misitu na Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Mazao ya Nyuki Tanzania. Sambamba na hilo, Wizara itatafsiri na kusambaza Kanuni, Miongozo na Mikakati mbalimbali ya Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki kwa wadau.

253. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara itatekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora kwa kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki, kuwezesha mizinga ya nyuki 13,000 na mavazi ya

kinga 650 kwa vikundi vya wafugaji nyuki 130. Aidha, Wizara itawezesha uanzishwaji wa hifadhi za nyuki tatu (3) na hifadhi za misitu zenye ukubwa wa hekta 10,000 na kuandaa mipango mitano (5) ya usimamizi wa hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau 1,500 kuhusu mikakati ya mazao ya misitu yaliyohandisiwa, zao la mianzi na kilimo misitu, matumizi ya nishati safi ya kupikia na fursa za biashara ya hewa ya kaboni katika kanda tatu (3) za TFS. Kwa upande mwingine, Wizara itafanya mikutano miwili (2) baina ya Wizara za kisekta na wadau wa misitu na ufugaji nyuki kuhusu fursa na changamoto zilizopo katika sekta ya misitu na nyuki. Wizara pia itawajengea uwezo maafisa ufugaji nyuki pamoja na kununua pikipiki 20 kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za ufugaji nyuki.

254. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Wizara itafanya vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC); vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Vikao viwili (2) vya Kamati ya Uendashaji ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa na vikao viwili (2) vya Kamati Kuu ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa 50 wa Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA). Aidha, Wizara itaanzisha Baraza la Wataalam wa Misitu; na jukwaa la wadau wa biashara ya hewa ya kaboni na kilimo misitu.

255. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazao yatokanayo na misitu na nyuki, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya viwanda vya misitu na ufugaji nyuki, utekelezaji wa miradi na programu za misitu na ufugaji nyuki pamoja na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara itashiriki mikutano na warsha za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Mkutano wa 49 wa APIMONDIA; Vikao vya Ushirikiano katika Sekta ya Misitu na Nyuki baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Kamati ya Misitu ya Dunia (COFO); na kuratibu ushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Siku ya Kitaifa ya Upandaji Miti na Siku ya Misitu na Nyuki Duniani.

5.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

256. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala utaimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 16 yenye ukubwa wa hekta 221,825 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi 32. Aidha, Wakala utafanya jumla ya doria 16,688 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala utaimarisha mipaka ya misitu 170 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 554; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,394; kuweka vigingi 1,675; mabango 279; na kununua ndege nyuki (drones) 3.

257. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza kampeni ya Tanzania ya Kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu nchini, Wakala utaanzisha mashamba mapya mawili ya miti (Geita na Rwamgasa) yenye jumla ya hekta 28,000; kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za miti nchini kwa kuanzisha vyanzo vipya 12 vya mbegu; kuzalisha tani 27.5 za mbegu; na miche ya miti milioni 35.2. Aidha, Wakala utaendeleza mashamba 24 ya miti kwa kupanda miti katika eneo lenye hekta 7,052; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 2,084; kupalilia eneo lenye hekta 34,031; kupogolea hekta 9,447; na kupunguzia miti kwenye hekta 3,208. Vilevile, Wakala utapanda miche ya mikoko takriban 79,000 katika eneo la hekta 57 ili kurejesha uoto wa asili katika maeneo hayo.

258. Mheshimiwa Spika, Wakala utaimarisha miundombinu ya utalii katika misitu ya hifadhi kwa: kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 223 za kuwezesha kufika kwenye hifadhi; mabanda matano (5) ya kupumzika watalii katika hifadhi ya mikoko Wilaya ya Kinondoni; geti moja (1) katika kituo cha NAFRAC - Shinyanga; na kukarabati kilomita 301.6 za njia za watalii, kilomita 112.1 za barabara za kufika kwenye hifadhi, na kambi 21 katika hifadhi za misitu 33. Aidha, Wakala utaimarisha vituo vya utalii wa malikale kwa kujenga kituo cha utalii wa nyuki, na kukarabati makaburi 15 ya kihistoria katika vituo vya Michoro ya Miambani Kolo - Kondoa, Mji Mkongwe - Bagamoyo, Tembe la Kwihara - Tabora, Magofu ya Tongoni - Tanga na Kaole - Bagamoyo.

259. Mheshimiwa Spika, Wakala utaendeleza mashamba matatu (3) ya nyuki na manzuki 82; kuzalisha tani 45 za asali; tani 3 za nta; kusimamia viwanda vitatu (3) vya mazao ya nyuki; kutoa elimu kwa wafugaji nyuki 161; na kuchonga mizinga ya nyuki 2,500. Vilevile, Wakala utakusanya sampuli 126 za asali kutoka wilaya 30 na kuzipeleka Maabara ya kimataifa nchini Ujerumani kwa ajili ya kuhakiki viwango vya ubora wa asali inayozalishwa nchini Tanzania kwa lengo la kuongeza wigo katika masoko ya kimataifa.

260. Mheshimiwa Spika, Wakala utaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kukamilisha ujenzi wa vituo vitano (5) vya ulinzi (ranger posts); kujenga ofisi saba (7) ikiwemo jengo la Makao Makuu ya Wakala moja (1) Jijini Dodoma, Ofisi za Wilaya sita (6) za Simanjiro, Bahi, Ngorongoro, Mkinga, Rombo na Kakonko; vituo saba (7) vya askari, na nyumba tatu (3) za watumishi. Vilevile, Wakala utanunua magari nane (8), malori mawili (2), pikipiki 40, boti tatu (3) na trekta moja (1). Aidha, Wakala utawezesha watumishi 75 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 685 ya muda mfupi katika fani mbalimbali.

5.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

261. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, TAFORI itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Tatu wa Utafiti wa Misitu (2021 – 2031) na Mpango Kabambe wa Kwanza wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki (2020 – 2030). Aidha, TAFORI itafanya utafiti wa kuangalia jinsi wadudu wachavushao wanavyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwenye milima ya Uluguru na Udzungwa Mkoani Morogoro. Aidha, TAFORI itakamilisha tathmini ya miti dawa na matumizi yake kwa ajili ya kuboresha maisha na uhifadhi wa misitu katika eneo la Milima ya Tao la Mashariki. Vilevile, TAFORI itaendelea na utafiti wa kuchunguza athari za mizunguko ya uvunaji wa spishi za miti aina ya misindano na mikaratusi kwenye uzalishaji na ubora wa mbao; kufanya utafiti kuhusu gharama na faida ya uzalishaji wa utomvu unaofanywa na wakulima wadogo wa miti katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa. Sambamba na hilo, TAFORI itaendelea na utafiti juu ya kudhibiti mimea vamizi kwenye

maeneo ya hifadhi; na kufanya utafiti wa nyuki wasiodunga na aina ya mizinga inayofaa kwa kufugia katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, TAFORI itafanya utafiti wa namna bora ya kutumia tasnia ya ufugaji nyuki kuboresha utalii wa nyuki (Api-tourism); na kuanzisha manzuki za utafiti na mashamba ya kuzalisha mazao ya nyuki katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga na Singida.

262. Mheshimiwa Spika, Kwa upande mwingine, TAFORI itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kukarabati maabara na jengo la Ofisi ya Makao Makuu, kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Tabora na kuweka vitendea kazi kwenye jengo la Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Kibaha. Vilevile, TAFORI itaimarisha uwezo wa kitalu cha miti kilichopo katika Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Kibaha kwa kuboresha teknolojia ya uzalishaji wa miche ya miti ili kuongeza upatikanaji wa vipando bora vya miti katika maeneo ya Pwani ya Tanzania. Aidha, TAFORI itaendelea kuwezesha watumishi 11 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, 28 mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 25 wa kada mbalimbali.

5.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora – BTI

263. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitadahili wanafunzi 420 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa Sekta ya Nyuki kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam juu ya masuala mbalimbali ili kuendeleza na kukuza Sekta ya Nyuki. Vilevile, Chuo kitaendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa bweni la wanafunzi wa kike, ujenzi wa maabara, kujenga uzio kuzunguka eneo la Chuo; kukarabati nyumba mbili (2) za watumishi; kununua vifaa saba (7) na mashine tatu (3) vya karakana ya mbao kwa ajili ya kutengeneza mizinga ya nyuki; pamoja na kuimarisha mifumo ya TEHAMA. Katika hatua nyingine, Chuo kitawezesha mtumishi mmoja (1) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitashiriki katika maonesho mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

5.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

264. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kitakuwa na jukumu la kutoa mafunzo ya ujuzi na ufundi stadi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Chuo kitadahili wanafunzi 500 wa teknolojia ya viwanda vya misitu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada, pia wanafunzi 100 katika elimu ya ufundi stadi. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wananchi. Kwa upande mwingine, Chuo kitashirikiana na wadau mbalimbali kuandaa maandiko ya miradi ya maendeleo.

265. Mheshimiwa Spika, Chuo kitaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200; ukarabati wa madarasa mawili (2) na mabweni mawili (2) mjini Moshi; darasa moja (1) na bweni moja (1) katika kituo cha mafunzo kilichopo West Kilimanjaro. Vilevile, Chuo kitaendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kuboresha utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha watumishi wanne (4) kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 33 kupata mafunzo ya muda mfupi.

5.3.2.6 Chuo cha Misitu, Olmotonyi - FTI

266. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Misitu, Olmotonyi kitadahili wanafunzi 930 katika ngazi ya astashahada na Stashahada ya misitu. Katika hatua nyingine, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 200 na ushauri wa kitaalamu wa misitu na uhifadhi wa mazingira kwa wanafunzi katika shule 10 za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Arumeru na Jiji la Arusha. Sambamba na hilo, Chuo kitajenga miundombinu ya utalii ikolojia, kitakarabati bwalo la chakula la wanafunzi na maktaba. Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Chuo kitawezesha watumishi wanne (4) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 10 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitashiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

5.3.2.7 Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu - FWITC

267. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu cha Mafinga kitadahili wanafunzi 80 katika ngazi ya ufundi stadi wa misitu na viwanda vya misitu. Katika hatua nyingine, Kituo kitatoa mafunzo ya muda mfupi ya misitu na viwanda vya misitu kwa wakulima wadogo 200 wa miti. Sambamba na hilo, Kituo kitajenga bweni moja (1) la wanafunzi. Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Kituo kitawezesha watumishi wawili (2) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi nane (8) wa muda mfupi. Vilevile, Kituo kitashiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

5.3.2.8 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

268. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko utaendelea kuwezesha na kugharamia miradi ya kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki kwa kutoa ruzuku kwa miradi 183 ambayo utekelezaji wake unaendelea na miradi mipya 120 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti, upandaji miti, ufugaji nyuki na miradi ya nishati mbadala. Aidha, Mfuko utaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 katika Chuo cha FITI kwa lengo la kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa wanafunzi wa kike pamoja na kuendelea kugharamia ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kituo cha Utafiti wa Misitu mkoani Tabora. Vilevile, Mfuko utaendelea kugharamia tafiti mpya tano (5) za kimkakati zinazoratibiwa na TAFORI zenye lengo la kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu.

269. Mheshimiwa Spika, Mfuko utaendelea kugharamia masomo ya shahada ya uzamili na uzamivu kwa fani ambazo zina watalaam wachache hapa nchini ambazo ni uboreshaji wa vizazi vya miti (tree breeding) na utambuzi wa magonjwa ya miti na misitu (forestry pathology). Mafunzo hayo yataboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu hususani mazao ya misitu kutoka mashamba ya miti ya kupandwa.

270. Mheshimiwa Spika, Mfuko utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko katika eneo la Nzuguni 'C' Jijini Dodoma. Aidha, Mfuko utaendelea na utekelezaji wa muundo mpya kwa kuongeza watumishi katika kada za uchumi, sheria na mawasiliano pamoja na kuongeza watumishi katika vitengo vingine ili kuweza Mfuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, Mfuko utaendelea kuboresha utendaji kazi kwa kuwezesha watumishi wawili (2) kushiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 kushiriki mafunzo ya muda mfupi.

5.3.3 Sekta ya Utalii

5.3.3.1 Idara ya Utalii

271. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutanua wigo wa mazao ya utalii na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara itafanya ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne (4) za Kaskazini, Kusini, Mashariki na Kati pamoja na kufanya uhakiki wa wakala wa biashara za utalii. Vilevile, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora wa nyota katika mikoa 18 pamoja na kubaini vivutio vya utalii katika mikoa 16 kwa mujibu wa Sheria ya Utalii, Sura ya 65.

272. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau wa utalii kuhusu matumizi ya mfumo wa kusajili wageni MNRT Portal; na mafunzo ya mfumo wa kujitathmini na kupanga ubora wa nyota kwa huduma za malazi AserT. Wizara pia itaandaa warsha mbili (2) za kuhamasisha na kuwajengea uelewa wadau wa utalii kuhusu vigezo vya kupanga huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora wa nyota. Sambamba na hilo, Wizara itaandaa warsha (2) zitakazoshirikisha wadau kuhusu umuhimu wa utambuzi wa mazao mapya ya utalii. Hatua hizi zinalenga kuimarisha huduma za utalii nchini.

273. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Utalii nchini, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008; Kanuni za Usajili na Utoaji Leseni za Wakala wa Utalii za Mwaka 2015; Kanuni za Huduma za Malazi za Mwaka 2015 na Kanuni za Waongoza Wageni za

Mwaka 2015. Vilevile, Wizara itafanya mapitio ya Mwongozo wa Usajili na Utoaji wa Leseni kwa Wakala wa Biashara za Utalii pamoja na kufanya mikutano minne (4) ya kuwajengea uwezo wadau kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Utalii. Sambamba na hilo, Wizara itafanya mikutano mitatu (3) ya wadau wa utalii ili kujadili masuala yanayohusu uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati. Wizara pia, itashiriki matamasha, matukio, maonesho na mikutano ya mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kutoa elimu kuhusu shughuli za utalii.

5.3.3.2 Tozo ya Maendeleo ya Utalii – TDL

274. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) itawezesha Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya utalii katika maeneo ya hifadhi ikiwemo malango ya kuingilia wageni, maeneo ya kupumzikia, kambi za watalii, migahawa, mabanda ya watalii, vituo vya burudani vya utalii; picnic site, vituo vya taarifa na kumbukumbu pamoja na miundombinu ya michezo na burudani ikiwemo viwanja vya mpira na bwawa la kuogelea. Aidha, TDL itawezesha ujenzi na ukarabati wa majengo ya kihistoria na barabara katika maeneo ya hifadhi.

275. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha masoko ya utalii ndani na nje ya nchi, TDL itawezesha kutangaza vivutio vya utalii kupitia maonesho, matamasha na mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa na kuanzisha ushirikiano na vyombo vya habari vya Kimataifa na Klabu kubwa za michezo Duniani. Aidha, itawezesha utoaji wa mafunzo ya utalii na ukarimu, kufanya tafiti mbalimbali ili kutambua masoko mapya na mahitaji ya watalii pamoja na kufanya uhakiki wa huduma za malazi. Katika hatua nyingine, TDL itawezesha ufungaji wa mabango ya kidijitali ya taarifa kwa wageni pamoja na ununuzi wa vifaa vya shughuli za utangazaji utalii ikiwemo ununuzi wa vifaa vya maonesho.

5.3.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

276. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kutekeleza jukumu la kutangaza na

kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya Nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kutangaza utalii kupitia mashirika ya ndege ya kitaifa na kimataifa yakiwemo Air Tanzania Company Limited, Turkish Airlines, Emirates na Qatar Airways kwa kuweka matangazo mbalimbali; kutumia Ligi za michezo zenye wafuatiliaji wengi ikiwemo CHAN, AFCON na Ligi za mpira zilizopo nchini; kuendelea kuandaa na kurusha makala za vivutio vya utalii kupitia vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa kama Expedia Group. Pia, Bodi itaratibu utangazaji wa Filamu ya Amazing Tanzania kwenye vyombo mbalimbali vya habari vya Nchini China. Kadhalika, Bodi itakamilisha uandaaji wa maudhui ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii katika soko la India kupitia watu maarufu wa Nchini humo. Kwa upande mwingine, Bodi itaendelea kutumia treni za kisasa za Shirika la Reli Tanzania kutangaza na kusafirisha watalii wa kitaifa na kimataifa kutembelea vivutio vya utalii.

277. Mheshimiwa Spika, Bodi itaendelea kutumia Mabalozi wa Hiari na watu mashuhuri katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya Nchi. Pia, Bodi itaratibu Kampeni mbalimbali zinazolenga kuhamasisha utalii wa ndani hususan wakati wa mapumziko ya sikukuu za kitaifa, likizo na msimu wa mwisho wa mwaka.

278. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi zetu za Ubalozi zilizopo katika nchi mbalimbali kutangaza utalii kupitia misafara ya utangazaji utalii (Road Shows) kwenye Bara la Amerika, Asia, Ulaya na Mashariki ya Kati; ziara za mafunzo (Familiarization Trips) kwa waandishi wa habari, wakala wa utalii na watu wenye ushawishi kutoka kwenye masoko ya msingi na kimkakati. Vilevile, Bodi itaratibu ushiriki wa Nchi katika maonesho na matukio mbalimbali ya utangazaji utalii ndani na nje ya nchi. Aidha, Bodi itaandaa onesho la 9 la Swahili International Tourism Expo – S!TE 2025 kwa kushirikisha waoneshaji na wanunuzi wa Kimatifa wa bidhaa za utalii kwa lengo la kutangaza utalii na fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

279. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutangaza na kutoa huduma za utalii kidijitali, Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kujenga mfumo wa "Destination Portal" wenye huduma za akili mnemba, chatbot na booking platform; pamoja na kutengeneza na kusimika mabango matano (5) ya kutangaza utalii kidijitali kwenye Jiji la Dar es Salaam (1), Arusha (1), Dodoma (1), Mwanza (1) na Mbeya (1). Aidha, Bodi itaendelea kushirikiana na wadau kutangaza mazao ya utalii ikiwemo utalii wa meli, fukwe, mikutano na matukio, michezo, uwindaji wa kitalii, utamaduni, malikale, ikolojia, miamba, kilimo, matibabu, nyuki na vyakula. Vilevile, Bodi itaendelea kuhamasisha utalii wa ndani kwa kufanya kampeni za utalii wa ndani kwa makundi mbalimbali ikiwemo wanafunzi, wafanyakazi, taasisi za kidini, wasanii na watu mashuhuri.

280. Mheshimiwa Spika, Bodi itaongeza juhudi ya kutangaza mazao ya Utalii wa Utamaduni, Utalii wa Mikutano na Matukio, na Utalii wa Historia ili kukuza utalii wa ndani na kuvutia watalii wa kimataifa. Hatua hiyo itakwenda sambamba na uratibu na udhamini wa matamasha mbalimbali ya utamaduni; na utangazaji wa maeneo ya kihistoria ikiwemo sehemu zenye kumbukizi za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Pia, Bodi itakamilisha usajili katika Shirika la Mikutano Duniani (ICCA) ili kupata fursa ya kuitangaza Tanzania kama Kituo Bora cha Utalii wa Mikutano na Matukio sambamba na kuvutia mikutano mbalimbali ya kimataifa kufanyika nchini.

5.3.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

281. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Taifa cha Utalii kitaendelea na ujenzi wa jengo jipya la taaluma kampasi ya Arusha ambalo litafanikisha ongezeko la udahili wa wanafunzi kutoka 1,500 hadi 2,000. Aidha, Chuo kitapanua wigo wa huduma zake kwa: utoaji wa mafunzo; utafiti wa kisekta; na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa wadau mbalimbali walio katika mnyororo wa thamani wa utalii.

282. Mheshimiwa Spika, Chuo kitaendelea na mpango wa kuimarisha kampasi ya Mwanza, ili kujitanua na kufikia mahitaji ya

wadau mbalimbali, kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa majengo ya taaluma katika viwanja viwili (2) Shibula na Semba vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Sambamba na hilo chuo kitaimarisha mpango wa mafunzo ya Uanagenzi (apprenticeship) pamoja na mpango wa kurasimisha ujuzi kwa watoa huduma za ukarimu na utalii (Recognition of Prior Learning).

283. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza udahili wa wanafunzi na kuboresha utoaji huduma za utalii na ukarimu Nchini, Chuo kitaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya huduma mkoba (Outreach programs) kwa kutembelea shule za Sekondari 80, kushiriki maonesho mbalimbali pamoja na kuandaa vipindi vya televisheni (5) na redio (10) kwa ajili ya kutangaza programu za Mafunzo kwa Wanafunzi na Wadau mbalimbali wa Utalii.

284. Mheshimiwa Spika, Chuo kitaanza maandalizi ya Kongamano la 4 la Kimataifa (The 4th Linking Industry with Academia in the Tourism and Hospitality in Developing Countries (LIATH-DC)) litalokutanisha Wadau na Wanataaluma katika masuala ya Utalii na Ukarimu.

285. Mheshimiwa Spika, Chuo kitaendelea na utekelezaji wa Mpango wa mafunzo kwa Watumishi 46 kuwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya Nchi ambapo watumishi 8 watapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Uzamili (Masters) na Uzamivu (PhD) na watumishi 38 watawezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi. Utoaji wa mafunzo hayo utajikita zaidi katika fani za ukarimu, utalii na uratibu wa matukio.

5.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

5.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

286. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara itatangaza maeneo sita (6) ya malikale kuwa Urithi wa Taifa, kukusanya taarifa za kiuhifadhi za maeneo 25 ya malikale kwa ajili ya kuhuisha orodha ya Urithi wa Taifa; kufanya tathmini

ya hali ya uhifadhi wa maeneo nane (8) yaliyopo kwenye Orodha ya Urithi wa Taifa katika mikoa ya Mara, Geita, Kagera na Shinyanga; na kufanya ukaguzi wa hali ya uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 10 ya malikale, makumbusho saba (7), kusajili makumbusho binafsi pamoja na kuratibu utatuzi wa migogoro ya mipaka katika maeneo matano (5) ya malikale. Aidha, Wizara itafanya vikao viwili (2) vya wadau katika mikoa miwili (2) kwa ajili ya kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008, kuratibu vikao vinne (4) vya Kamati ya Majadiliano kuhusu masuala ya urejeshwaji wa malikale za Tanzania zilizopo nje ya nchi; na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba miwili (2) ya uhifadhi kati ya Wizara na wadau.

287. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara itafanya vikao viwili (2) vya wadau kwa ajili ya kupata maoni kuhusu mwongozo wa kutwaa na kuhamisha umiliki wa rasilimalikale na kufanya kikao kimoja cha wadau kwa ajili ya kutathimini utendaji wa sekta. Vilevile, Wizara itashiriki mikutano ya kikanda na kimataifa inayohusu uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Pia, Wizara itafanya tathmini na kuandaa andiko la kuorodhesha njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Katika hatua nyingine, Wizara itawezesha watumishi watano (5) kupata mafunzo ya muda mrefu na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo pamoja na kushiriki katika maonesho na matamasha ya kitaifa ikiwemo Sabasaba na Nanenane kwa lengo la kuhamasisha matumizi endelevu ya malikale.

5.3.4.2 Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale – NFA

288. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Mambo ya Kale utawezesha maandalizi ya kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura ya 333 na miongozo ya Uhifadhi wa maeneo ya malikale; ukusanyaji wa taarifa za uhifadhi wa maeneo 30 ya malikale ili yaweze kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa; maandalizi ya Mpango wa Uhifadhi wa Makumbusho ya Mtwa Mkwawa- Kalenga; na usimamizi wa hali za uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 45 ya Urithi wa Taifa.

289. Mheshimiwa Spika, Katika hatua nyingine, Mfuko utawezesha ushiriki wa Wizara katika maonesho kwa lengo la kubainisha na kutangaza shughuli za Mifuko; kufanya vikao vya wadau vya kujadili uhifadhi wa Nyayo za ZAMADAMU Laetoli na Engarasero; utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere; na kuwezesha mafunzo ya uhifadhi wa maeneo na majengo ya kihistoria.

5.3.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT

290. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika litaendelea kuhifadhi na kuendeleza urithi wa malikale na mikusanyo kwa kufungua kituo cha taarifa chenye historia ya kuanza kwa vita ya Majimaji, Nandete-Kilwa na kujenga nyumba za asili 3 kwa mfumo wa kaya katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Vilevile, Shirika litasimamia ukarabati wa majenzi ya kale 18 katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara pamoja na kutumia mifumo ya TEHAMA kuhifadhi kumbukumbu za maeneo hayo. Pia Shirika, litaendelea kushirikisha wadau binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale nchini.

291. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Shirika litaboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi kwa kuboresha maonesho manne (4) ya kudumu katika kituo cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni-Dar es Salaam, kufungua maonesho mapya matatu (3) ya kudumu katika vituo vya MbuamajiKigamboni (1), Mikumbi – Lindi Mjini (1) na Mkwajuni – Tendaguru (1). Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika shughuli za utalii na uhifadhi zikiwemo usajili wa mikusanyo na maonesho. Vilevile, Shirika litakarabati stoo mbili (2) za uhifadhi wa mikusanyo katika kituo cha MajimajiSongea (1) na Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni-Dar es Salaam (1).

292. Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kutangaza vivutio vya malikale na makumbusho ili kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia matamasha manne (4) ya urithi wa mtanzania, maonesho, matukio, warsha na programu zenye kujenga uelewa kuhusiana na utalii wa malikale. Vilevile, Shirika litafanya tafiti tano

(5) za masuala ya urithi wa utamaduni na kutoa vibali vya utafiti katika maeneo ya malikale; kukusanya na kuhifadhi mikusanyo 1,000 ya asili na kiutamaduni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa makumbusho binafsi. Aidha, Shirika litaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makumbusho ya Marais, Dodoma na kuratibu Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, 35 mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 41 wa kada mbalimbali.

5.4 Miradi ya Maendeleo

293. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 105,749,922,000.00** kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 32,476,051,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo **Shilingi 105,749,922,000.00** zinajumuisha **Shilingi 34,348,073,903.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara; na **Shilingi 71,401,848,097.00** za Miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, TAWA, TFS, NMT, NCT na TAWIRI).

294. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(A) Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)

Mradi wa Programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 57,476,764.00** fedha za ndani na **Shilingi 920,000,000.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kujenga jukwaa la kufungamanisha na kubadilishana taarifa za mifumo ya Sekta ya Maliasili na Utalii (MNRT Faru-Gateway);

(ii) Kuboresha miundombinu ya "datacenter" ya Wizara pamoja na "Disaster Recovery ya Wizara"; na

(iii) Kuwezesha mafunzo kwa watumishi tisa (9) kuhusu utafiti na ubunifu wa miradi ya maendeleo.

(B) Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 18,682,561,593.00** fedha za ndani kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) katika eneo la Kihesa Kilolo-Iringa;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliji katika skimu za mabonde madogo ya mito Chimala na Kimani kwa ujenzi wa Skimu za Mbuyuni-Kimani na Makangarawe katika Wilaya ya Mbarali;

(iii) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Madibira;

(iv) Kuwezesha huduma za ushauri elekezi katika ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania katika eneo la Kihesa Kilolo-Iringa;

(v) Kuwezesha ujenzi wa Malambo ya kunywesha mifugo (cattle troughs) katika vijiji vya Ikanutwa, Mabadaga, Mahango, Manienga na Itamboleo katika Wilaya ya Mbarali; na

(vi) Kuwezesha Usimamizi na Uratibu wa mradi kwa kufanya Tathmini na Ufuatiliaji, Usimamizi wa Fedha, Manunuzi na upatikanaji wa vitendea kazi kwa watekelezaji wa mradi.

(C) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves)

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani, Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 1,114,138,124.00** kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ukarabati wa miundombinu na Majengo chakavu PASIANSI; na

(ii) Ununuzi wa visukuma mawimbi 50 pamoja na mabomu baridi 20,000.

(D) Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania)

Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira "Global Environmental Facility – GEF" katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 2,586,276,000.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwezesha mafunzo ya mbinu za kisayansi za uchunguzi wa makosa ya ujangili na biashara haramu ya nyara kwa maafisa kutoka Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP) na Kanda za Ki-ikolojia za Kuratibu Doria (TCGs);

(ii) Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuwezesha utendaji wa mfumo wa kukusanyia taarifa na kuratibu doria;

(iii) Kuwezesha doria za ki-intelijensia za kupambana na ujangili katika mifumo ikolojia yenye changamoto ya ujangili;

(iv) Kuwezesha tathmini ya kisayansi kuhusu hali ya ujangili nchini na uwezo wa Serikali kukabiliana nao;

(v) Kuwezesha ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Chamwino;

(vi) Kuwezesha tathmini ya rasilimali za wanyamapori katika eneo la Ikungi na kuandaa Mpango wa Kanda wa Usimamizi WMA tarajiwa ya Ikungi;

(vii) Kuwezesha utekelezaji wa mbinu shirikishi za kukabiliana na Wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yanayopakana na hifadhi kwenye Wilaya ya Itigi;

(viii) Kuwezesha jamii katika Jumuiya za ufugaji nyuki za Mwakintaru, Muhesi na WMA ya WAGA mizinga na vifaa vya kusindika mazao ya nyuki ili kuongeza thamani;

(ix) Kuwezesha kampeni za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara za wanyamapori katika maeneo yanayozunguka hifadhi kwenye mfumo Ikolojia wa Ruaha – Rungwa;

(x) Kuwezesha mafunzo ya uongozi kwa Bodi ya Ushauri wa Maliasili pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa Askari wa Vijiji katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii Chamwino; na

(xi) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Kijamii wa Ufuatiliaji wa Vitendo vya Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara katika Kanda ya Kiikolojia ya Kuratibu Doria Moyowosi – Ugalla.

(E) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)

Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mradi utatumia **Shilingi 570,403,992.00** fedha za ndani kwa ajili ya

(i) Kujenga maabara ya kisayansi ya mafunzo kwenye Chuo cha Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI);

(ii) Kukarabati miundombinu na majengo chakavu FITI;

(iii) Kukarabati miundombinu na majengo chakavu FTI; na

(iv) Kukarabati miundombinu chakavu – TAFORI.

(F) Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 1,842,401,666.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kujenga vituo vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika Wilaya za Uyui, Urambo na Itigi;

(ii) Kuandaa mipango ya biashara (business plan) kwa ajili ya vituo vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo na Mlele;

(iii) Kuanzisha Ukanda wa kufugia nyuki kwenye Hifadhi ya Msitu Kigosi (hekta 923,904);

(iv) Kuwezesha mapitio ya Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya Mwaka 2002 na Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki za Mwaka 2005 ili ziendane na mahitaji ya sasa;

(v) Kuwezesha wadau wa ufugaji nyuki kushiriki makongamano ya kitaifa, kikanda na ya kimataifa kwa lengo la kuwaunganisha na masoko ya asali na mazao mengine ya nyuki;

(vi) Kujenga uzio na kuweka matenki ya maji kwenye vituo vya kukusanyia mazao ya nyuki vilivyopo katika wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo na Mlele;

(vii) Kuwajengea uwezo vikundi vya wafugaji nyuki wakiwemo vijana na wanawake na vyama vya ushirika juu ya huduma za kifedha na masuala ya teknolojia katika kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki;

(viii) Kujenga Kituo cha kuuzia asali na mazao mengine ya Nyuki (Marketing center) Wilaya ya Wete-Pemba Kaskazini;

(ix) Kuwezesha wafanyabiashara sita (6) wenye viwanda vya kuchakata asali kupata cheti cha uthibiti wa ubora wa chakula (HACCP);

(x) Kuwezesha makampuni manne (4) ya uuzaji wa asali kupata cheti cha uuzaji wa asali mahuluku (Organic Certificate);

(xi) Kukarabati kituo cha kuchakata mazao ya nyuki cha SIDO-Singida pamoja na ununuzi wa seti ya mashine za kuchakata asali;

(xii) Kuandaa mfumo wa ukusanyaji wa bei ya asali na kusambaza kupitia TANTRADE;

(xiii) Kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara 30 juu ya mbinu za utafutaji masoko ya asali; na

(xiv) Kutoa mafunzo ya kuongeza thamani mazao ya nyuki kwa wanawake wajasiriamali.

(G) Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR)

Mradi huu unafadhilia na Mfuko wa Mazingira wa Dunia "Global Enviromental Facility – GEF" na katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 3,664,636,331.00** fedha za nje kuendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufungamanisha mipango iliyopo ya usimamizi wa kisekta katika eneo la Kilombero kwa ajili ya kuandaa mfumo Shirikishi wa Usimamizi wa Ardhi;

(ii) Kutekeleza mpango kazi wa Usimamizi Shirikishi wa vyanzo vya maji katika Bonde la Kilombero na maeneo ya Kiashange-Mokotoni na Kinyasini-Kisongoni (Zanzibar);

(iii) Kuwezesha maandalizi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji katika maeneo ya kipaumbele Kilombero na Zanzibar;

(iv) Kutoa mafunzo na kujenga uelewa kuhusu usimamizi shirikishi wa ikolojia Kilombero na Zanzibar;

(v) Kuwezesha tathmini ya vihatarishi kwenye maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya uongoaji kwenye maeneo yaliyoharibiwa Kilombero na Zanzibar;

(vi) Kusimamia maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi katika ikolojia lengwa kupitia mbinu zilizofanya vizuri kwenye maeneo mengine kwa Kilombero na Zanzibar; na

(vii) Kuwezesha wadau wanaotekeleza jitihada za uongoaji wa maeneo yaliyoharibiwa kwa kujikita zaidi kwa wakulima wadogo na sekta binafsi Kilombero na Zanzibar.

(H) Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Misitu, Matumizi Bora ya Ardhi na Kuongeza thamani ya Mazao ya Misitu (Forestry Land Use and Value Chains Development in Tanzania- FORLAND)

Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Ufini (Finland) na katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 4,001,200,000.00** fedha za nje kuendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo kwa Jumuiya 30 za wakulima wa miti kuhusu upandaji, utunzaji na usimamizi wa mashamba ya miti;

(ii) Kuwezesha mapitio na maandalizi ya Mipango 20 ya matumizi bora ya ardhi katika Mkoa wa Iringa;

(iii) Kujenga uwezo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kuhusu biashara ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa pamoja na mikakati mingine ya biashara;

(iv) Kujenga uwezo kwa timu za vijiji za usimamizi wa moto kuhusu mbinu za kupambana na majanga ya moto; na

(v) Kujenga uwezo wa miundombinu ya kufundishia ya Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC).

(I) Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Uhifadhi wa Misitu ya Mikoko (Enhancing Management of State Forest Plantations and Mangroves Forest Reserve in Tanzania)

Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa na katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 32,253,375,989.00** fedha za nje uendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupanda miti kwenye eneo la hekta 4,500 katika Mashamba ya Miti ya Mtibwa (hekta 500), Silayo (hekta 3,000) na Wino (hekta 1,000) pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara katika mashamba hayo;

(ii) Kufanya tathmini ya maeneo ya Misitu ya Mikoko yaliyopo Wilaya za Kilwa, Rufiji na Kibiti na kuandaa Mipango ya Usimamizi ya hifadhi hizo;

(iii) Kununua magari 22, mitambo 9 na kujenga vituo vya ulinzi 5 ili kuimarisha usimamizi wa maeneo ya hifadhi; na

(iv) Kuwezesha miradi ya kiuchumi, kijamii na uhifadhi wa mazingira itakayoibuliwa na jamii zinazopakana na misitu ya hifadhi.

(J) Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project)

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 908,979,433.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuanza kwa ujenzi wa ukumbi wa mikutano na matukio; na

(ii) Kuendeleza Kituo cha Utangazaji Utalii Kidijitali kupitia mfumo wa "Travel Companion".

(K) Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi huu utatumia fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 1,654,595,091.00** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma kwenye Kampasi ya Arusha. Jengo hilo litakuwa na miundombinu ya madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa wakati mmoja, kumbi za mihadhara, kumbi za mikutano na vifaa vya mafunzo vikiwemo majiko, chumba cha kufulia, mgahawa na vyumba vya wageni.

(L) Uanzishwaji wa makumbusho ya Marais, Dodoma

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makumbusho ya Marais, jijini Dodoma.

(**M) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi Makao Makuu ya TAWIRI**

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Nchini (TAWIRI) katika kuimarisha mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa watumishi, Taasisi imetengewa fedha za ndani

Shilingi 1,000,000,000.00 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu. Jengo hili litakuwa na miundombinu ya Ofisi za watumishi, maabara za wanyamapori na kumbi za mikutano.

(N) Miradi ya TANAPA

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) litatumia kiasi cha **Shilingi 18,489,000,000.00** fedha za nje ili kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Ukarabati wa mradi wa usambazaji maji wa Naabi; uchimbaji wa visima sita lango la Ndabaka, uwanja wa ndege wa Lobo, ofisi ya Mkuu wa Hifadhi, Makoma, Mawe Meupe na uwanja wa ndege wa Kusini; pamoja na uwekaji wa mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua kwenye nyumba za Askari za Ndabaka, Kirawira A na B, Nyamuma, Kogatende, Lobo, Kuka Main Base, Naabi Hill Gate, Moru Main Base, Crater Sub-Base na Simiyu;

(ii) Ujenzi wa mabwawa nane katika wilaya za Serengeti (5) pamoja na Ngorongoro (3);

(iii) Ujenzi wa madaraja matatu (Kapilula – 1, Mongwe - 1 katika hifadhi ya Taifa Katavi pamoja na Kogatende – 1 katika hifadhi ya Taifa Serengeti);

(iv) Ujenzi wa gereji kubwa na ya kisasa katika hifadhi ya Taifa Katavi;

(v) Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa hifadhi, nyumba ya kupumzikia wageni, gereji ndogo pamoja na uzio katika vituo vya askari viwili vya Ikamba na Mabilibili katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale;

(vi) Kugharamia shughuli ya uzoeshaji wa Sokwe mtu katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale;

(vii) Ujenzi wa miundombinu ya kudhibiti mwenendo wa magari ikiwemo minara ya kuimarisha mtandao kutoka

TANAPA Makao Makuu kupitia Hifadhi za Taifa Arusha, Tarangire, Ziwa Manyara, Ngorongoro hadi Serengeti;

(viii) Kuunganisha mifumo ya umeme jua kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato katika malango yote ya kuingilia na kutokea wageni katika Hifadhi ya Taifa Serengeti;

(ix) Ununuzi wa magari mawili kwa ajili ya kuwezesha shughuli za tathmini na ufuatiliaji wa mradi;

(x) Ujenzi wa jengo la "control room" kubwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenengo wa magari ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti; na

(xi) Kuwezesha uandaaji mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 32 vilivyopo jirani na hifadhi katika wilaya za Bariadi (18), Bunda (7) na Tarime (7).

(O) Miradi ya TAWA

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori itatumia kiasi cha **Shilingi 17,004,877,017.00** ambapo kiasi cha **Shilingi 7,487,896,003.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 9,516,981,014.00** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa vivuko 96 katika Pori la Akiba Selous kanda ya Kingupira na Liwale;

(ii) Ujenzi wa madaraja mawili ya Lungónya Kanda ya Kingupira (1) na Matandu Kanda ya Miguruwe (1) katika Pori la Akiba Selous;

(iii) Ujenzi wa bweni la watumishi katika Pori la Akiba Selous kanda ya Miguruwe;

(iv) Kuwezesha ununuzi wa mafuta ya ndege pamoja na matengenezo ya mara kwa mara ya ndege katika Pori la Akiba Selous-Miguruwe;

(v) Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo GPS 80, ndege nyuki 6 na Kamera kwa ajili ya Mapori ya Akiba Selous na Lukwika Lumesule;

(vi) Ununuzi wa magari ya doria 14 kwa ajili ya Mapori ya Akiba Selous (10) na Lukwika Lumesule (4) na gari maalum moja (1) kwa ajili ya shughuli za uhamasishaji na utoaji elimu kwa Pori la Akiba Selous;

(vii) Ujenzi wa kilomita 197 za barabara katika Mapori ya Akiba Mpanga Kipengere (30), Rukwa (17), na Wami-Mbiki (150);

(viii) Ununuzi wa magari sita (6), boti 1, trekta 1, pikipiki 16, engine 10 za boti pamoja na ununuzi wa samani kwa ajili ya ofisi sita (6) za Mapori ya Akiba Maswa, Uwanda, Mpanga Kipengere, Igombe, Moyowosi na Pori Tengefu Ziwa Natron; na

(ix) Ujenzi wa ofisi ya Kanda ya Magharibi kwa ajili ya Mapori ya Akiba ya Rukwa, Ugalla na Inyonga.

6.0 SHUKRANI

295. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo, maelekezo na msukumo anayotupatia katika Sekta ya Maliasili na Utalii ambayo imeiwezesha sekta hii kuendelea kukua, kuimarika na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Pia, natumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

296. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mailiasili na Utalii kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu

Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo vya Wizara; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa ushirikiano wanaonipa na kujituma bila kuchoka katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya kila siku. Asanteni sana na Kazi Iendelee.

297. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa Wizara yetu ikiwa ni pamoja na Washirika mbalimbali wa Maendeleo, kwa mchango wao mkubwa katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Mchango wao umeendelea kuimarisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwaletea wananchi maendeleo endelevu.

298. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi marafiki, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali pamoja na wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa mchango wao mkubwa katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii. Ushirikiano wao umeendelea kuwa kichocheo muhimu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa letu. Vilevile, nazishukuru kwa dhati Serikali za Canada, China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya kwa kuendelea kushirikiana nasi.

299. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuyashukuru na kuyatambua Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo zimeendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na: EU, AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, RTI, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNTourism, IORA, USAID, Honey Guide Foundation, CIFOR, ICRAF, INBAR, GATSBY, FOREST- FARM FACILITY, SIX RIVERS, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Mchango wao umeendelea kuwa muhimu katika kulinda na kuendeleza rasilimali zetu kwa manufaa ya Taifa.

300. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa ndani wa Sekta ya Maliasili na Utalii wakiwemo: TCT, TATO, HAT, TAHOA, TLTO, TTGA, KGA, NTSGS, IGS, TGS, KTGA, NGTF, KPA, TPO, TACTO, TAOA, TAHA, TAWTO, TWEA, CWMAC, TABEDO, TAF, TTGAU, API-SUPPORT, HEAT, SHIVIMITA, Nature Tanzania na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale, uendelezaji na utangazaji utalii ikiwemo ofisi zetu za Ubalozi nje ya Nchi.

301. Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutambua mchango wa Viongozi wetu wa Dini na Viongozi wa Kimila katika kuelimisha jamii, kusimamia na kushiriki kikamilifu katika juhudi za uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi yetu zikiwemo wanyamapori, misitu na malikale. Viongozi hawa wamekua mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu, kuzuia ujangili, ukataji holela wa miti, uharibifu wa malikale pamoja na kuhimiza utalii wa ndani unaozingatia mila, desturi na utunzaji wa mazingira. Kwa upande mwingine, natambua mchango mkubwa unaotolewa na wenzetu wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Shule za Sekondari na Msingi kwa namna walivyojikita katika utunzaji wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuanzisha vitalu vya miti na miradi ya ufugaji nyuki katika maeneo yao. Vilevile, natambua mchango wa taasisi za tafiti kwa namna zinavyoshirikiana na Wizara kutafuta suluhisho la changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya Maliasili na Utalii.

302. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama, Taasisi za Himasheria pamoja na vyombo vya habari kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji Utalii.

303. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ninawahakikishia kuwa Wizara inatambua na kuthamini mchango wenu na itaendelea

kuimarisha na kufungua milango ya ushirikiano zaidi kwa maendeleo ya sekta yetu na Taifa kwa ujumla.

304. Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine kuzishukuru Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika utekelezaji wa majukumu yetu katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji Utalii na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026

305. Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 359,982,271,000.00** kwa matumizi ya Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 105,749,922,000.00** ni za Miradi ya Maendeleo.

306. Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 130,709,054,000.00** za Mishahara na **Shilingi 123,523,295,000.00** za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 32,476,051,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** fedha za nje.

8.0 HITIMISHO

307. Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushiriki katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji wa Utalii. Aidha, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

308. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.maliasili.go.tz

309. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea niombe taarifa yetu yote ya Kamati kama ilivyowasilishwa asubuhi Mezani iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu Tano kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa, msingi wa uchambuzi na mawanda ya uchambuzi;

(b) Sehemu ya Pili inayochambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Sehemu ya Tatu inayochambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya Nne inayofafanua maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(e) Sehemu ya Mwisho inahitimisha taarifa ya uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) na (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii baada ya ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha. Madhumuni ya sehemu hii ni kupata uelewa utakaolisaidia Bunge lako Tukufu katika majadiliano yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati; tarehe 31 Mei, 2024, wakati wa uwasilishwaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo tisa. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa na inapenda kuipongeza Wizara kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa yapo baadhi ya maoni na ushauri ambayo bado hayajafanyiwa kazi ipasavyo na uzingatiaji wake hauridhishi. Uzingatiaji usioridhisha wa maoni na ushauri wa Kamati katika kutimiza majukumu ya Wizara unaweza kupunguza ufanisi na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi, kinyume na lengo la Serikali kama inavyotakiwa na Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa miwili ya Manyara na Arusha ili kukagua miradi mitano ambayo ni miongoni mwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa kuhusu miradi hiyo inapatikana katika ukurasa wa saba mpaka ukurasa wa 13 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara; Wizara imeendelea kutekeleza vipaumbele na majukumu yake na kufanya sekta zinazosimamiwa na Wizara hii

kuendelea kuleta tija katika Taifa letu. Katika Taarifa ya Shirika la Utalii Duniani kuhusu ukuaji wa Sekta ya Utalii baada ya athari za ugonjwa wa UVIKO-19, inaonyesha kuwa idadi ya watalii kutoka nje imefikia watalii milioni 2,141,895 ikilinganishwa na watalii 620,867 mwaka 2020. Idadi hii ni sawa na ongezeko la takribani 245% na kuifanya Tanzania kushika nafasi ya kwanza Barani Afrika na nafasi ya sita duniani kwa ongezeko la watalii wa Kimataifa baada ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya fedha za nje yatokayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. Ongezeko hili ni sawa na 445.77% ambalo limeifanya Tanzania kuwa nafasi ya tatu Barani Afrika na nafasi ya tisa duniani baada ya athari za UVIKO-19. Haya ni mafanikio ya kujivunia kama Taifa na Kamati inapongeza juhudi za Serikali hasa juhudi binafsi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuikwamua sekta hii kupitia uwekezaji wa kibajeti na kuamua kutangaza utalii kupitia filamu ya *Tanzania- The Royal Tour* pamoja na *Amazing Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 968,842,018,480.00. Hadi kufikia Februari, 2025 hatua ya ukusanyaji wa maduhuli ilifikia shilingi bilioni 826,995,557,098.00 sawa na 85.4% ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli. Maelezo zaidi ni kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 17 - 19 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina; kwa upande wa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni 708,891,841,026.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 404,986,147,454.81 sawa na 57.13% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni

347,414,766,151.69 sawa na 65.24% zilikuwa za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 57,571,381,303.13, sawa na 33% zilikuwa za kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali isiyoridhisha ya upokeaji wa fedha kutoka Hazina kwenye utekelezaji wa shughuli za Wizara ni moja ya kikwazo kikubwa katika kuhakikisha kwamba Wizara na taasisi zake zinaendelea kukuza Sekta ya Utalii. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuhakikisha Wizara na taasisi zake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Mwenendo wa upokeaji fedha kutoka Hazina kwa ufafanuzi zaidi ni kama unavyoonekana kwenye ukurasa wa 19 - 21 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025 – 2025/2026. Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69 inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni 1,183,584,115,330.55. Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa shilingi 214,742,096,850.55 sawa na 22.16% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha unaokwisha.

Katika malengo ya makusanyo 90% yatakusanywa kutumia taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii huku 9.59% ya makadirio yatakusanywa kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kukabiliana na nakisi ya bajeti katika sekta zinazosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Uchambuzi zaidi ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 22 - 24.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) inakadiria kutumia shilingi bilioni 359,982,271,000.00 kulinganisha na makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 708,891,841,026.00 katika mwaka wa fedha unaokwisha. Makadirio ya matumizi ya Wizara hii yamepungua shilingi bilioni 348,909,570,026.00, sawa na 49.22% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaokwisha.

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo ya uchambuzi yanaonesha kuwa upungufu huo unatokana na uamuzi wa Serikali kuzingatia ushauri uliokuwa ukitolewa Bunge lako Tukufu juu ya kuziruhusu Taasisi za Ngorongoro na Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania *(TANAPA)* kuanza kubaki na makusanyo yake. Uamuzi huo utaongeza ufanisi wa utendaji katika taasisi hizo na kuleta manufaa katika nyanja za za kiuchumi, kiutamaduni, burudani na tafiti za kisayansi. Uchambuzi zaidi ni kama inavyoonekana ukurasa wa 25 - 27.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uchambuzi wa Mambo Mahsusi katika Sekta ya Maliasili na Utalii; changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu; migongano baina ya wanyamapori na binadamu ndiyo changamoto inayoongoza katika utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sasa. Changamoto hii imepelekea madhara ya uharibifu wa mali na miundombinu, ulemavu na upotevu wa maisha kwa baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge liliidhinishia Serikali kiasi cha shilingi bilioni 45,144,308,496.73, ambapo ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya

kukabiliana na changamoto hii. Taswira ya utekelezaji wa shughuli hizo dhidi ya mpango wa awali inaonekana katika kielelezo namba sita kilichopo kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kupitia kielelezo namba hapo juu, ni wazi kuwa utekelezaji wa shughuli hizo ulifanyika kwa kiwango kisichoridhisha ukilinganisha ukubwa wa changamoto yenyewe. Vilevile Serikali imeweka utaratibu wa kutoa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi waliokumbwa na changamoto hii. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa wananchi walioathirika na migongano hiyo kuhusu ucheleweshaji wa malipo hayo. Hali hii inachangiwa na mchakato mrefu wa kuthibitisha madai ya wananchi walioathirika na wanyamapori katika maeneo yao. Malalamiko ya wananchi na wawakilishi wao kuhusu migogoro hii ni mengi na madhara yake ni dhahiri. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatekeleza kwa ufanisi na ukamilifu shughuli zilizoidhinishiwa fedha na Bunge kwa ajili kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tozo ya Maendeleo ya Utalii *(Tourism Development Levy-TDL);* katika kutimiza azma yake ya kukuza na kuendeleza Sekta ya Utalii nchini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia kurejeshwa kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii nchini *(TDL)* ambayo ilikuwa imesitishwa kutokana na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020. Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 ili kuruhusu asilimia sita ya mapato ghafi ya taasisi za *TANAPA* na *NCAA* kuwa chanzo cha tozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake ambao unalenga kukuza sekta ya utalii nchini. Aidha, uamuzi wa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha unaonesha nia ya dhati ya Bunge lako Tukufu katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye kuleta maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kufanya uchambuzi wa taarifa kuhusu matumizi ya fedha za tozo hiyo tarehe 25

Machi, 2025 na tarehe 12 Mei, 2025. Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kukosekana kwa mpango wa matumizi ya fedha hizo. Kamati inaitaka Wizara kuandaa mpango mkakati ambao utaainisha vipaumbele ambavyo vitatekelezwa kupitia fedha hizo kabla ya kuanza kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali *(DDMCC);* kituo hiki kilianza ujenzi wake mwaka 2017 na kukamilika Disemba, 2021 na kiligharimu jumla ya shilingi bilioni 1,372,256,210.07. Kituo kilianza kazi kwa majaribio ya awali tarehe 5 Januari, 2022 kwa kuingia mkataba na mtoa huduma anayeitwa *Through Mobile Africa Limited*. Hata hivyo, Kamati ilifanya ziara na kukagua utendaji wa kituo hicho tarehe 17 Machi, 2024 ambapo ilikuta kituo hicho hakifanyi kazi kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake, Wizara ilisema kuwa kituo hicho kinafanya kazi kimajaribio na kwa sasa kinashindwa kuanza kazi kwa kukosa fedha. Vile vile taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ilionesha uzembe wa kituo hicho kutokufanya kazi licha ya manufaa yake kwa taasisi katika kuingiza mapato na kutangaza utalii nchini. Aidha, kituo hiki kilitarajiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 29,089,851,719 kwa mwaka wa fedha 2025 kama kingeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia sababu hizo, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 1,749,160,000.00 kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kituo hiki kinafanya kazi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Tarehe 23 Oktoba, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya utendaji wa kituo hiki ambapo Wizara ilionyesha bado kituo hakijaanza kazi. Katika taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyowasilishwa Bungeni tarehe 7 Februari, 2025, Bunge liliiagiza Serikali kufanya tathmini na uchuguzi wa kina ili kubaini sababu ya kituo hicho kushindwa kufanya kazi na iwasilishe taarifa kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025. Kamati ilipokea taarifa ya tathmini hiyo na kufanya majadiliano na Wizara tarehe 25 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Kamati inaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, taarifa hiyo ilibainisha uwepo wa uzembe na hujuma katika mchakato wa kuanzisha na kukiendesha kituo hicho. Hali hiyo imefanya uendeshaji wa kituo hicho kukwama licha ya faida zake katika kutangaza na kukuza Sekta ya Utalii nchini. Taarifa ya Wizara inabainisha kuwa Serikali imeanza kuchukua hatua za awali za kinidhamu kwa wahusika. Hata hivyo, Kamati haijaridhika na kasi ya Serikali katika kuwachukulia hatua wahusika wote na katika kuhakikisha kuwa kituo hicho kinafanya kazi kama inavyopaswa ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Utalii Tanzania; Bodi ya Utalii Tanzania ni taasisi ya umma iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura, 364 ikitakiwa kuchukua majukumu ya lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania *(Tanzania Tourist Corporation TTC)*. Bodi hii imepewa jukumu la kutangaza na kuendeleza shughuli mbalimbali katika Sekta ya Utalii nchini. Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali ikiwa ni pamoja na Sheria ya Uanzishwaji wa Bodi ili kupima ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Sheria ya uanzishaji wa Bodi hii ni ya muda mrefu na inayohitaji marekebisho. Pia Bodi hiyo inakabiliwa changamoto kadhaa ikiwemo muundo wake, ukosefu wa bajeti ya kutosha katika utekelezaji wa shughuli zake, pamoja na mwingiliano wa majukumu baina yake, Wizara na taasisi nyingine za Serikali. Vilevile, Bodi hii inakabiliwa na upungufu wa watumishi wenye weledi na utaaalam wa kutangaza utalii kidijitali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Changamoto ya Uendeshaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCAA)*. Sekta ya utalii nchini kama ilivyokuwa sehemu nyingine duniani ilipata mtikisiko mkubwa mwaka 2019 hadi 2020 kutokana na UVIKO-19. Kama taasisi za kipaumbele katika uhifadhi na utalii nchini, taasisi za

TANAPA na *NCAA* ziliathirika hali iliyotishia uwezo wao wa kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 Bunge lilifanya uamuzi kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, ambapo taasisi hizi zilitakiwa kukusanya maduhuli na kuyapeleka Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, taasisi hizi zilitakiwa kupewa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kujiendesha na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kunusuru Sekta ya Utalii nchini. Hatua hizo zimeleta ongezeko la watalii nchini ambao wanatembelea Hifadhi za Taifa na Eneo la Mamlaka ya Ngorongoro kama vivutio vya kipaumbele. Hali hii imechangia Taasisi za *TANAPA* na Ngorongoro kupata changamoto ya kujiendesha katika maeneo ya kutolea huduma kwa watalii na kushindwa kufanya shughuli za uhifadhi kwa ufanisi kutokana na nakisi ya bajeti kutoka Serikalini pamoja na kuchelewa kupokea mgao wa fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na madaraja katika maeneo yanayosimamiwa na taasisi hizo siyo nzuri. Hali hii inachangia watalii wengi nchini kushindwa kufika katika vivutio vingi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kurejesha utaratibu wa *TANAPA* na Ngorongoro kukusanya na kutumia ili kuwezesha taaasisi hizi kujiendesha kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa ushauri huu na Serikali iliahidi kutekeleza, hata hivyo Serikali haikutekeleza ushauri huo wakati wa bajeti kuu na kupitisha Sheria ya Fedha kama ilivyokuwa imeahidi. Kama ushauri huu hautatekelezwa, ni wazi kuwa hali hii itaendelea kuathiri Sekta ya Utalii na Uhifadhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii,

sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Jumla; Serikali ihakikishe itaendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio hivyo hali itakayochangia kuongeza mapato ya Serikali, kukuza uchumi na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani kwenye shughuli zitokanazo na utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kulinda na kuhifadhi rasilimali za misitu, wanyamapori na malikale kwa ajili ya kuendelea kupata manufaa ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie kikamilifu na kuongeza ufasini katika ukusanyaji wa mapato ili taasisi zinazokusanya mapato kupitia MNRT portal ziweze kufika malengo yaliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, Wizara inatakiwa kusimamia na kuzuia matumizi fedha yasiyo ya lazima katika taasisi zinazokusanya na kutumia ili kuhakikisha kunakuwa na tija katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Ushauri wa Kamati; Changamoto ya Uendeshaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; Kamati inashauri kuwa, kupitia Sheria ya Fedha Serikali ihakikishe inafanya marekebisho ili kuruhusu utaratibu wa kukusanya na kutumia kama ilivyokuwa awali. Uamuzi huo utaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya TANAPA na Ngorongoro pamoja na kuleta tija kwenye Sekta ya Uhifadhi na Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu; Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali itekeleze kwa ukamilifu mkakati wa Kitaifa wa kushughulika na mgongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupata utatuzi wa kudumu wa changamoto hiyo;

(ii) Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishiwa fedha na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kukabiliana na changamoto hali itakayopunguza na kuondoa madhara ya migongano hiyo;

(iii) Serikali iboreshe mfumo wa ulipaji wa kifuta machozi na kifuta jasho ili kurahisisha upatikanaji wake hali inayopunguza madhara yanayotokana na migongano hiyo; na

(iv) Serikali ishirikiane na wadau wa uhifadhi kutoka sekta binafsi kuweka uzio wa umeme (electrical fence) katika maeneo yenye changamoto kubwa ya tembo.

Mheshimiwa Spika, Tozo ya Maendeleo ya Utalii; Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iunde chombo cha usimamizi kinachojitegemea katika usimamizi na matumizi ya fedha hizo kama ilivyofanyika katika Mfuko wa Misitu Tanzania ili kuzuia kuingiliwa na kuongeza uwajibikiaji katika matumizi ya fedha hizo;

(ii) Isitishe baadhi ya shughuli zilizoonekana kutokuwa na tija kama ilivyoshauriwa na Kamati; na

(iii) Iandae mpango mkakati ambao utaonyesha shughuli na vipaumbele vitakavyotekelezwa kwa ajili ya kuendeleza na kuleta matokeo yaliyotarajiwa katika Sekta ya Utalii kupitia fedha za tozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za Jumuiya za Wanyapori (WMA); Kamati inaishauri Serikali kuwa, ifanye marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ili kuruhusu mgao wa fedha za WMA kwa mujibu wa Kanuni za WMA za mwaka 2018 ziende moja kwa moja kwenye Jumuiya hizo ikiwa ni pamoja na fedha zinazotokana na shughuli za utalii wa picha.

Mheshimiwa Spika, hoteli na lodge za Serikali zilizobinafsishwa; Kamati inashauri kuwa, Serikali iongeze kasi katika kuhakikisha kuwa majadiliano kati ya Wakili Mkuu wa Serikali na wawekezaji ambao wameshindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya uwekezaji yanafikia mwisho na kuzingatia sheria ili hoteli na lodge hizo ziweze kurejeshwa Serikalini hali itakayopunguza changamoto ya uhaba wa huduma za malazi kwa watalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha kutangaza utalii kidijitali (DDMCC); Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iwachukulie hatua za kinidhamu na kisheria wote waliohusika katika kuhujumu utendaji wa kituo hicho; na

(ii) Iongeze usimamizi ili kituo hicho kiweze kufanya kazi kama ilivyotarajiwa kwa ajili ya kutangaza kidijitali na kuongeza mapato ya Bodi ya Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025; Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali iongeze kasi ya usimamizi wa miradi ili ikamilike kwa wakati kwa ajili ya kutoa huduma iliyokusudiwa kwani miradi mingi ipo nyuma ya wakati; na

(ii) Serikali ipeleke fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuhakikisha wakndarasi wanalipwa kwa wakati hivyo kuepushia Serikali hasara inayotokana na riba ya kuchelewesha malipo kwa wakandarasi;

(iii) Kupitia timu za usimamizi na ukaguzi wa miradi, ihakikishe inafanya tathmini na kusimamia thamani ya fedha katika miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB); Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iandae mkakati wa haraka wa kufanya mapitio ya Sheria ya Bodi Utalii Tanzania Sura, 364 ili kubadili muundo wa Bodi na kuipa majukumu ya kutangaza, kuwezesha na kudhibiti shughuli za biashara ya uwekezaji katika sekta ya Utalii nchini;

(ii) Kuweka mikakati ya kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kuwa huru kujiendesha na kujitegemea kimapato; na

(iii) Ihakikishe inachukua hatua za haraka kutafuta watalaamu katika eneo la kutangaza utalii hasa utangazaji wa kidijitali ili kuiwezesha bodi hiyo kufanya majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Dkt. Tulia Akson, Mbunge wa Mbeya Mjini, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kazi kubwa na nzuri unayofanya ya kuliongoza Bunge letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunakutakia kila lakheri katika mchakato wa mwaka huu 2025 utakapotengua kitendawili kama ni Mbeya Mjini au ni Uyole basi Mwenyezi Mungu akutangulie. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia tunampongeza Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo wamekuwa wakitimiza majukumu yao kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa kuniamini na kwa ushirikiano walioutoa wakati wote wa shughuli za kamati yetu. Pia ninawashukuru kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha pamoja na uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake, ningependa kuwataja, lakini naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi H. Chana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hasa katika sekta hii. Aidha, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninawashukuru watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka I. Leonard, kwa kuongoza na kuratibu vyema shughuli za Bunge na Kamati. Pia, ninawashukuru Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Charles Wanyancha na Eunice Shirima kwa kazi kubwa waliyoifanya kuisaidia Kamati lakini pia kwa maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee, binafsi napenda kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi kwa usaidizi, ushirikiano na utulivu unaoniwezesha kutimiza majukumu yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, ninawashukuru wana CCM na wananchi wote wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kuendelea kuniamini, kunivumilia na kuniunga mkono katika majukumu yangu, kwa pamoja tumefanya mengi sana. Ninajua wanajua kwamba nguvu bado ninazo, uwezo bado ninao na utayari wa kuendelea kuwatumikia bado ninao. Tuombeane uzima, kheri na neema katika kuliendea jambo letu na kwa baraka za Mwenyezi Mungu jambo lipo na litakuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa, niliombe Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Sehemu ya tatu inayochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iv) Sehemu ya nne inayofafanua Maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya mwisho inahitimisha taarifa ya uchambuzi wa bajeti.

1.2 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Maliasili na Utalii ni Masharti ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, ambapo Kanuni ya 6 (8)(b) ikisomwa kwa pamoja na kanuni ya 7(1)(a) zinatoa jukumu hilo kwa Kamati. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa za Utekelezaji Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta za Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) na (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii baada ya ziara ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha. Madhumuni ya sehemu hii ni kupata uelewa utakaolisaidia Bunge katika majadiliano yake kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Aidha, sehemu hii inafafanua mambo matano yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushuri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge;

(iii) Utekelezaji wa majukumu na Vipaumbele vya Wizara;

(iv) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufanya uamuzi baada ya mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 31 Mei, 2024, wakati wa uwasilishwaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka fedha 2024/2025, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo tisa (09). Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Machi, 2025, Waziri wa Maliasili na Utalii alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuzingatia ushauri wa Kamati. Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao bado utekelezaji wake hauridhishi. Maoni na ushauri ambao utekelezaji wake hauridhishi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ndogo katika kuchukua hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori

wakali na waharibifu nchini kwa ajili ya kunusuru maisha ya watu, wanyamapori na kuzuia uharibifu wa mali unaotokana na migongano hiyo;

(ii) Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta ili kupima na kufanya utambuzi wa mipaka hali itakayoondoa migogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo ya hifadhi;

(ii) Serikali kufanya sehemu ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 ambayo imeruhusu fedha zinazotokana na shughuli ndani ya Jumuiya za Wanyamapori (WMAs) kulipwa moja kwa moja kwenye WMAs. Marekebisho ya Sheria yaliyofanyika hayakujumuisha mgawo wa fedha unaotokana na utalii wa picha kwenye maeneo ya WMAs;

(v) Serikali kushindwa kuchukua hatua za haraka kurudisha hoteli na loji toka kwa wamiliki waliobinafsishiwa hoteli na Loji za Serikali ambao wamekiuka masharti ya mikataba yao ya kuziboresha hali itakayopunguza uhaba wa huduma ya malazi ya watalii na kuleta tija iliyokusudiwa;

(vi) Serikali kushindwa kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC) ili kiweze kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na kuleta tija iliyokusudiwa ambapo hadi sasa kituo hicho hakijaanza kufanya kazi kama inavyotarajiwa; na

(vi) Serikali haikufanya marekebisho kwenye Sheria ya fedha ili kuruhusu taasisi za TANAPA na NCAA zikusanye maduhuli na kutumia kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji usioridhisha wa maoni na ushauri wa Kamati katika kutimiza majukumu ya Wizara, unaweza kupunguza ufanisi na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi

kinyume na lengo la Serikali kama inavyotakiwa na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili (2) ya Manyara na Arusha ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kamati ilikagua miradi mitano (05) kama ifuatayo:-

(a) Mradi Na. 4314: Mradi wa Ujenzi wa Barabara na Lango la Kuingilia katika Hifadhi ya Taifa Tarangire Eneo la Mamire

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulitekelezwa kwa thamani ya Shilingi 4,345,011,281.60 ikiwa ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 28 ikiwa ni kutoka tarehe 10 Machi, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2025. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 12 Machi, 2025, ambapo Kamati ilitembelea na kufanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umepokea kiasi cha Shilingi 1,708,175,348.65 sawa na asilimia 39.3 tu ya fedha zote za mradi. Kazi hii imetekelezwa kwa kipindi cha 25 sawa na asilimia 89.3 ya muda wote. Hali hii inaweza kuchangia utekelezaji wa mradi kuchelewa, kuongeza gharama za kukamilisha mradi kutokana na mfumuko wa bei na kuiingizia Serikali hasara kupitia malipo ya riba kwa mkandarasi kucheleweshewa malipo yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijionea utekelezaji wa mradi na kubaini kuwa mradi umetekelezwa kwa asilimia 60 na hivyo kuwa nyuma kwa takribani asilimia 29.3 ukilinganisha na muda halisi wa utekelezaji wa mradi. Aidha, Kamati iliitaka Wizara kuhakikisha inamsimamia mkandarasi ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

(b) Mradi Na. 4814: Mradi wa Ujenzi wa Majengo katika Makao Makuu Mapya ya Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulitengewa na kuidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 10,474,526,694.25 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na nyumba tatu kwa ajili ya makazi ya Kamishna wa Uhifadhi na Naibu Makamishna wa Uhifadhi wawili. Kwa mujibu wa mkataba wa mradi uliosainiwa tarehe 08 Julai, 2022, mradi huu ulitakiwa kutekelezwa ndani ya miezi 12 kuanzia tarehe 10 Oktoba, 2022 hadi tarehe 10 Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara na kukagua mradi huo tarehe 13 Machi, 2025 ambapo ilikuta mradi umefikia asilimia 85 huku muda wa utekelezaji wake ukiwa umepita kwa zaidi ya miezi 18 sawa na asilimia 150. Katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini mradi huo unakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati kwani hadi kufikia tarehe 26 Novemba, 2024 Mamlaka imepokea kiasi cha Shilingi 6,291,051,718.59 sawa na asilimia 60.1 tu kutoka Serikalini kwa ajili ya mradi. Aidha, Wizara ilikuwa imewasilsha hati Na. 7 ya malipo ya Shilingi 729,501,996.75 Wizara ya Fedha kiasi ambacho hakikuwa kimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini kuwa Serikali imeanza kupata hasara zinazotokana na ucheleweshaji wa mradi huo kwani mkandarasi aliwasilsha maombi ya fedha za ziada na kuidhinishiwa na msimamizi wa mradi kiasi cha Shilingi 133,906,616.04 kama riba inayotokana na kucheleweshewa malipo yake kwa wakati. Aidha, ucheleweshaji huo pia unachangia kupunguza ufanisi katika utendaji wa Mamlaka kwani inalazimika kutumia majengo ambayo awali yalitumika kama makazi ya watumishi wa mamlaka katika eneo la Kemny Wilayani Karatu. Hata hivyo, Kamati ilitarifiwa kuwa mradi huo unategemea kukamilika tarehe 30 Mei, 2025.

(c) Mradi Na. 4342: Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Taaluma katika Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Arusha

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni sehemu ya mikakati ya upanuzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Arusha ukiwa

umeidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi 5,045,927,551.256. Utekelezaji wa mradi huu ni miezi 22 kuanzia tarehe 25 September 2023 hadi tarehe 31/07/2025.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2024 ambapo Kamati ilifanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umefikia asilimia 59 na muda uliotumika kuwa asilimia 82 takribani miezi 18. Kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa na kutumika kwenye mradi kilikuwa Shilingi 1,673,974,784.72 sawa na asilimia 33 tu ya fedha zote za mradi. Wizara ilikwisha wasilisha hati Na. 3 kwa ajili ya malipo ya mkandarasi kiasi cha Shilingi 412,207,116.90 ambacho kilikuwa hakijapokelewa.
Mheshimiwa Spika, Katika ukaguzi wake Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi upo nyuma kwa takribani asilimia 23. Kamati inaitaka Wizara kupitia timu ya usimamizi wa mradi kumtaka mkandarasi kuongeza juhudi ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda uliopangwa. Pia, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa malipo kwa wakati ili kuepuka hasara inayoweza kutokana na riba ya kuchelewesha malipo kwa mkandarasi.

(d) Mradi Na. 4313: Mradi wa Ukarabati wa Barabara ya Jumuia Katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha

Mheshimiwa Spika, mradi huu uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha Shilingi 419,195,00.00 ukiwa na lengo la kutoa huduma kwa watalii na wananchi wanaoshi kuzunguka hifadhi ya Taifa ya Arusha. Mradi huu umehusisha ukarabati wa urefu wa Kilomita 16 za barabara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa wa miezi 3 tokea Agosti hadi Oktoba, 2024. Aidha mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na tayari umeanza kutumika hivyo kuchochea ubora wa huduma kwa watalii wanaotembelea hifadhi. Hali hiyo imeongeza ufanisi katika uwezo wa hifadhi hiyo kuhudumia watalii kwani wastani wa magari 170 hupita katika barabara hii kila siku, ambapo magari ya utalii ni takribani 100 na magari ya wananchi 70 yakiwemo malori na mabasi ya abiria.

(e) Mradi Na. 4817: Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji kwa Wanyama katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni moja ya mikakati ya Wizara katika kuhakikisha kunakuwa na maji ndani ya hifadhi wakati wote. Mradi huu umetengewa na Bunge Shilingi 125,729,000.00 na ulianza tarehe 24 Novemba, 2024 ulitarajiwa kukamilika tarehe 24 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ukaguzi katika mradi huu tarehe 13 Machi, 2025 na kubaini kuwa mradi umefikia asilimia 70. Pamoja na kazi hiyo kuwa imefanyika kwa kiasi hicho, Wizara ilikuwa haijapokea fedha yoyote kwa ajili ya mradi na kazi ilikuwa imesimama huku ikiwa imebaki takribani mwezi mmoja kabla ya kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea ufafanuzi toka Wizarani kuwa mkandarasi aliamua kuanza kazi bila hata kupewa malipo ya awali akitegemea atapokea malipo wakati akiendelea na kazi. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2025, Wizara ilikuwa imewasilisha hati Na. 1 ya Shilingi 77,000,000.00 kwa Wizara ya Fedha kiasi ambacho hakijalipwa na kufanya mkandarasi kushindwa kuendelea na kazi. Kamati inaitaka Wizara ya fedha kutoa kiasi hicho cha fedha ili kukwamua utekelezaji wa mradi uweze kukamilika kwa wakati.

2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimwa Spika, Katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika. Tathmini ya kina, imebainisha yafuatayo:-

(i) Kumekuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi mingi ya Wizara hali inayoweza kupelekea

kuongezeka kwa gharama na kupunguza tija inayotokana na miradi husika;

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha za miradi kutoka hazina sio ya kuridhisha na tayari Serikali imeanza kupata hasara ya kudaiwa riba na wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo. Mathalani katika utekelezaji wa Mradi Na. 4814: Ujenzi wa Majengo manne katika eneo la makao makuu mapya ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, mkandarasi amepeleka na kuidhinishiwa madai ya Shilingi 133,906,616.04 kama riba ya kucheleweshewa malipo yake; na

(iii) Kukosekana kwa uwiano wa thamani ya fedha na miradi mingi ya Wizara iliyofanyiwa ukaguzi na Kamati. Katika eneo hili, Kamati inapenda kuipongeza timu ya usimamizi wa Mradi Na. 4342: Ujenzi wa Jengo la Ghorofa 5 katika Chuo cha Taifa cha Utalii ambapo utekelezaji wa mradi na thamani ya fedha vinaonekana wazi tofauti na miradi mingine ambayo Kamati ilifanya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo hayo mahsusi yaliyobainika, Kamati pia ilibaini kuwa hali ya miundombinu ya barabara katika hifadhi za Taifa sio ya kuridhisha hali inayofanya vivutio vingi kushindwa kufikika hasa nyakati za mvua. Mathalani, katika hifadhi ya Taifa ya Arusha yenye mtandao wa barabara zenye urefu wa Kilomita 236.7, Serikali imefanya ukarabati wa Kilomita 16 ambazo ni sawa na asilimia 6.7 tu ya mtandao mzima barabara. Kamati inaitaka Serikali kuandaa mpango mkakati ambao utahakikisha barabara zilizo ndani ya hifadhi zinakarabatiwa ili ziweze kupitika wakati wote hivyo kuongeza tija katika sekta ya utalii nchini.

2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) unaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi

(CCM) ya mwaka 2020 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) mwaka 2021/22 – 2025/26. Aidha, miongozo mbalimbali ya Kimataifa pia imekuwa ikizingatiwa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu chini ya Umoja wa Mataifa, Malengo ya Utalii Endelevu chini Shirika la Utalii Duniani na maelekezo mengine.

Mheshimiwa Spika, sekta za kipaumbele katika Wizara ya Maliasili na Utalii ni Wanyamapori, Utalii, Mambo ya kale, Misitu na Nyuki. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imeendelea kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali zinazopatikana katika sekta hizi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Aidha, sekta hizi zimendelea kulinufaisha Taifa kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuchangia pato la Taifa, kutoa ajira na kupunguza umasikini wa kipato miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) kuhusu ukuaji wa sekta ya utalii baada ya athari za ugonjwa wa UVIKO-19, inaonyesha kuwa sekta ya utalii nchini imekuwa kwa kasi, hali ambayo imeifanya sekta hii kuendelea kuwa kinara katika kuchangia fedha za nje na kulinda thamani ya sarafu yetu hivyo kuhakikisha uchumi wa Taifa letu unakuwa himilivu. Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa hiyo na kubaini kuwa, idadi ya watalii kutoka nje imefikia watalii 2,141,895 mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 620,867 mwaka 2020. Idadi hii ni sawa na ongezeko la takribani asilimia 245 na kuifanya Tanzania kushika nafasi ya 1 barani Afrika na nafasi ya 06 duniani kwa ongezeko la watalii wa kimataifa baada ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya fedha za nje yatokayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 445.77 ambalo limeifanya Tanzania kuwa nafasi ya 3 barani Afrika na nafasi ya 9 duniani baada ya athari za UVIKO-19. Haya ni mafanikio ya kujivunia kama Taifa na Kamati inapongeza juhudi za Serikali hasa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuikwamua sekta hii kupitia

uwekezaji wa kibajeti na kuamua kutangaza Utalii kupitia filamu ya Tanzania- the Royal Tour pamoja na Amaizing Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na mafanikio haya makubwa ya kujivunia kumekuwepo na changamoto zinazoikabili sekta hii muhimu katika ustawi wa Taifa letu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na matukio ya migongano baina ya wanyamapori wakali na waharibifu, ubovu wa miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege, upungufu wa huduma bora za malazi na upungufu wa bajeti ya kutosha katika kutangaza vivutio vya utalii nchini. Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuchukua hatua madhubuti ya kukabiliana na changamoto hizo ili sekta hii iweze kuongeza tija katika uchumi wa Taifa na ustawi wa wananchi.

2.4 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa. Aidha, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutumia uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 968,842,018,480.00. Hadi kufikia Februari, 2025 hatua ya ukusanyaji wa Maduhuli ilifikia Shilingi 826,995,557,098.00 sawa na asilimia 85.40 ya lengo la makusanyo liliodhinishwa na Bunge. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli ulionyesha yafuatayo:-

i. Ukusanyaji wa kutumia MNRT portal, umefikia asilimia 68.04 ya lengo lililoidhinishiwa, huku ukusanyaji wa kutumia TRA imefikia asilimia 93.40 ya lengo. Kupitia takwimu hizi, Kamati imewianisha muda wa utekelezaji wa bajeti na hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na kubaini

kuwa malengo ya ukusanyaji kwa kila njia yatafikiwa kama ilivyoidhinishwa na Bunge; na

ii. Wakati wa makadirio, makusanyo kwa utaratibu wa MNRT portal yalitarajiwa kuchangia kwa asilimia 31.80 huku yale ya TRA yakitarajiwa kuchangia kwa asilimia 68.20. Hata hivyo, katika makusanyo halisi njia ya MNRT portal imechangia pungufu kwa asilimia 6.50 wakati njia ya TRA imechangia ziada kwa asilimia 6.50. Kwa takwimu hizi zinaonyesha kuwa njia ya TRA ina ufanisi zaidi katika kukusanya mapato ukilinganisha na ile ya MNRT portal. Taswira kamili ya ukusanyaji inaonekana katika Kielelezo Na. 1.

Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2025

Fungu 69	% ya Makadirio	Makadirio (A)	Makusanyo (B)	% ya Makusanyo Ufanisi	Lengo vs Makusanyo
MNRT Portal	**31.80**	**307,977,820,000.00**	**209,545,623,569.32**	**25.30**	**68.04**
TRA (TANAPA & NCAA)	**68.20**	**660,864,198,480.00**	**617,449,933,528.68**	**74.70**	**93.40**
JUMLA	**100**	**968,842,018,480.00**	**826,995,557,098.00**	**100**	**85.40**

Chanzo: Randama ya Wizara ya mwaka 2025 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mchanganuo huo ni dhahiri kuwa, Makusanyo taasisi za TANAPA na NCAA ndio yaliyofanikisha kwa kiasi kikubwa makusanyo kufikia asilimia 85.40. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ya makusanyo iliyofikiwa. Vilevile, Kamati inaitaka Wizara kuboresha mfumo na kuongeza usimamizi katika kukusanya mapato kwa njia ya MNRT Portal hali itakayoongeza ufanisi wa njia na kuongeza tija katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 708,891,841,026.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 404,986,147,454.81 sawa na asilimia 57.13 tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Katika fedha hizo, Shilingi 347,414,766,151.69 sawa na asilimia 65.24 zilikuwa za matumizi ya kawaida na Shilingi 57,571,381,303.13 sawa na asilimia 33 zilikuwa za kugharamia miradi ya maendeleo. Taswira ya Upatikanaji wa Fedha inaonekana katika Kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2025

Matumizi		Kilichoidhinishwa	Kilichopokelewa	Asilimia
Kawaida	OC	302,241,676,000.00	192,891,778,311.05	63.82
	Mishahara	230,257,652,026.00	154,522,987,840.64	67.11
	Jumla (A)	**532,499,328,026.00**	**347,414,766,151.69**	**65.24**
Maendeleo	Ndani	97,225,838,000.00	31,648,137,420.67	32.55
	Nje	79,166,675,000.00	25,923,243,882.45	32.75
	Jumla (B)	**176,392,513,000.00**	**57,571,381,303.12**	**32.64**
JUMLA KUU (A+B)		**708,891,841,026.00**	**404,986,147,454.81**	**57.13**

Chanzo: Randama ya Wizara 2025 na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti, Kamati uchambuzi wa kina katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina ambapo unaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2025:-

(i) Upatikanaji halisi ulitakiwa uwe usiopungua asilimia 66.67 ya Bajeti yote iliyoidhinishwa ili kuendana na muda wa utekelezaji wa bajeti, lakini Wizara ilikuwa imepokea asilimia 57.13 tu. Hali hii inaweza kuchangia kushuka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara; na

(ii) Katika asilimia 32.64 ya bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha za Ndani ni asilimia 32.55 tu, huku fedha za nje zikiwa ni asilimia 32.75 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hatua hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha za maendeleo sio wa kuridhisha hali ambayo imechangia katika baadhi ya miradi mbalimbali ya maendeleo na wakandarasi kushindwa kuendelea na kazi na sehemu zingine wameanza kuidai Serikali riba kwa kucheleweshewa malipo.

Mheshimiwa Spika, hali isiyoridhisha ya upokeaji wa fedha kutoka hazina kwenye utekelezaji wa shughuli za Wizara ni moja ya kikwazo kikubwa katika kuhakikisha Wizara na taasisi zake zinaendelea kukuza sekta ya utalii. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuhakikisha Wizara na taasisi zake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii.

3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na Matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,183,584,115,330.55. Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 inaonekana katika Kielelezo Na. 3.

Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026

Fungu 69	2024/2025	2025/2026	% Ongezeko
Maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali	105,558,757,000.00	113,536,198,276.65	7.56
Maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi	863,283,261,480.00	1,070,047,917,053.90	23.95
JUMLA	**968,842,018,480.00**	**1,183,584,115,330.55**	**22.16**

Chanzo: Randama ya Wizara 2025 na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa shilingi 214,742,096,850.55 sawa na asilimia 22.16 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, kwa mtiririko wa makusanyanyo kwa miaka 3 mfululizo, ni wazi kuwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli haya litafikiwa;

(ii) Makadirio ya Makusanyo ya maduhuli yanayokwenda mfuko mkuu wa Serikali yameongezeka kwa asilimia 7.56 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Hata hivyo, ili kufikia lengo hili, Wizara iimarishe usimamizi wa mikataba ya uwekezaji katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA hususani SWICA, usimamizi wa shughuli za kitalii na kuboresha mfumo wa MNRT portal ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli;

(iii) Makusanyo ya maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi yameongezeka kwa asilimia 23.95 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Ongezeko hilo limetokana na uamuzi wa Serikali kuruhusu baadhi ya taasisi kubaki na makusanyo yake ili kuongeza ufanisi katika kujiendesha; na

(iv) Katika lengo la Makusanyo ya Wizara, asilimia 90.41 ya makusanyo, yatakusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, huku asilimia 9.59 makadirio yatakusanywa na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kukabiliana na nakisi ya bajeti katika sekta zinazosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa ukuaji wa sekta ya utalii nchini umechangia ongezeko la makadirio ya maduhuli. Aidha, utekelezaji wa mkakati wa wizara wa kuimarisha sekta ya utalii baada ya athari za UVIKO-19 ni sehemu ya sababu za ongezeko la makadirio ya maduhuli. Hata hivyo, lengo hilo la maduhuli litaweza kufikiwa iwapo Serikali itatekeleza ipasavyo mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii kwa ufanisi na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) inakadiria kutumia Shilingi 359,982,271,000.00 kulinganisha na makadirio ya matumizi ya

Shilingi 708,891,841,026.00 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kulinganisha makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taswira ya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 inaonekana katika Kielelezo Na. 4.

Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026

Mwaka	**Matumizi ya Kawaida**		**Maendeleo**	
	PE	**OC**	**Ndani**	**Nje**
2024/25	230,257,652,026	302,241,676,000	97,225,838,000	79,166,675,000
2025/26	130,709,054,000	123,523,295,000	32,476,051,000	73,273,871,000
Pungufu	99,548,598,026	178,718,381,000	64,749,787,000	5,892,804,000
Asilimia -%	-43.23	-59.13	-66.60	-7.44

Chanzo: Randamba ya Wizara 2025 na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonyesha kuwa:-

(i) Makadirio ya matumizi ya Wizara hii yamepungua kwa Shilingi 348,909,570,026.00 sawa na asilimia 49.22 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Fedha za mishahara zimepungua kwa Shilingi 99,548,598,026 sawa na asilimia 43.23 ilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Fedha za matumizi ya mengineyo yaani (OC) zimepungua kwa Shilingi 178,718,381,000 sawa na asilimia 59.13 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Fedha za miradi ya maendeleo zimepungua kwa Shilingi 70,579,591,000.00 sawa na asilimia 60 ikilinganishwa na mwaka 2024/2025. Aidha, fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo zimepungua kwa asilimia 66.60 huku fedha za nje zikipungua kwa asilimia 7.44.

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo ya uchambuzi yanatokana na uamuzi wa Serikali kuzingatia ushauri uliokuwa ukitolewa Bungeni juu ya kuziruhusu Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kuanza kubaki na makusanyo yake. Uamuzi huo utaongeza ufanisi wa utendaji katika taasisi hizo na kuleta manufaa katika nyanja za za kiuchumi, kiutamaduni, burudani na tafiti za kisayansi.

3.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, sekta ya maliasili na utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi, hivyo ulinganisho wa bajeti ya Wizara hii dhidi ya bajeti ya Taifa ni jambo linalosaidia kuweka msingi wa ushauri kuhusu sekta husika. Kwa kuzingatia hilo, sehemu hii inatathmini mambo yafuatayo:-

(i) Uwiano wa bajeti ya Wizara kwa bajeti ya Taifa; na

(ii) Ulinganisho wa hali ya uwiano kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka wa fedha 2025/2026. Taswira ya ulinganisho huo unaonekana katika Kielelezo Namba 5.

Kielelezo Na. 5: Bajeti ya Wizara (Fungu 69) dhidi ya Bajeti ya Taifa

BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2024/2025			
AINA	**BAJETI TAIFA**	**BAJETI YA MALIASILI**	**ASILIMIA**
OC	5,822,535,000,000	302,241,676,000	5.19
MISHAHARA	11,997,752,000,000	230,257,652,026	1.92
MAENDELEO NDANI	12,148,283,000,000	97,225,838,000	0.80

MAENDELEO NJE	3,640,838,000,000	79,166,675,000	2.17
DENI LA SERIKALI	15,736,280,000,000	-	-
JUMLA	**49,345,688,000,000**	**708,891,841,026**	**1.44**
BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2025/2026			
AINA	**BAJETI TAIFA**	**BAJETI YA MALIASILI**	**ASILIMIA**
OC	6,444,293,900,000	123,523,295,000	1.92
MISHAHARA	13,174,240,500,000	130,709,054,000	0.99
MAENDELEO NDANI	13,320,501,900,000	32,476,051,000	0.24
MAENDELEO NJE	6,150,902,600,000	73,273,871,000	1.19
DENI LA SERIKALI	17,950,311,400,000	-	-
JUMLA	**57,040,250,300,000**	**359,982,271,000.00**	**0.63**

Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 na 2025/2026, Randama ya Wizara ya Maliasili na Utalii 2024/2025 na 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kwa tathmini hiyo, uchambuzi umeonyesha mambo yafuatayo:-

Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya Bajeti ya Taifa imepungua kutoka asilimia 1.44hadi asilimia 0.63;

(i) Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka asilimia 5.19 hadi asilimia 1.92;

(ii) Bajeti ya mishahara imepungua kutoka asilimia 1.92 hadi kufikia asilimia 0.99;

(ii) Bajeti ya Maendeleo kutokana na fedha za ndani imepungua kutoka asilimia 0.88 hadi asilimia 0.24; na

(iv) Bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za nje imepungua kutoka asilimia 2.17 hadi asilimia 1.19.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa viashiria vya kibajeti katika mwaka wa fedha 2025/2026 ukilinganisha na ile ya mwaka

2024/2025 kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 5 imetokana na taasisi za TANAPA na NCAA kuanza kujitegemea katika makusanyo na matumizi, hivyo kufanya bajeti zake kuwa si sehemu ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

3.4 Uchambuzi wa Mambo Mahsusi katika Sekta ya Maliasili na Utalii.

(i) Changamoto ya Wanyamapori wakali na Waharibifu

Mheshimiwa Spika, migongano baina ya wanyamapori na binadamu ndio changamoto inayoongoza katika utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii. Changamoto hii imepelekea madhara ya uharibifu wa mali na miundombinu, ulemavu na upotevu wa maisha kwa baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bunge liliidhinishia Serikali kiasi cha Shilingi 45,144,308,496.73 ambapo ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hii. Taswira ya utekelezaji wa shughuli hizo dhidi ya mpango wa awali unaonekana katika Kielelezo Namba 6.

Kielelezo Na. 6: Utekelezaji wa Shughuli za kukabiliana na Migongano baina ya Wanyapori na Binadamu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia Februari, 2025

SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA HADI FEBRUARI, 2025			
SHUGHULI	**MPANGO**	**UTEKELEZAJI**	**ASILIMIA YA UTEKELEZAJI**
Ununuzi wa Helkopita	02	0	0
Uchimbaji wa mabwawa	30	08	26
Ujenzi wa vizimba	50	08	16
Ujenzi wa vituo	10	4	40
Ununuzi wa pikipiki 39	39	9	23

Ununizi wa ndege nyuki	16	17	106
Ununuzi na Ugawaji wa mabomu baridi	35,000	12,072	34
Ajira kwa Askari wa Uhifadhi	850	473	55
Mafunzo kwa askari **wa vijiji (VGS)**	200	33	16
Ununuzi na Usambazaji wa mikanda ya Satelite Collars	100	18	18

Chanzo: Randama ya Wizara 2025 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kupitia kielelezo Na. 6 hapo juu, ni wazi kuwa utekelezaji wa shughuli hizo ulifanyika kwa kiwango kisichoridhisha ukilinganisha ukubwa wa changamoto yenyewe. Vilevile, Serikali imeweka utaratibu wa kutoa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi waliokumbwa na changamoto hii. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa wananchi walioathirika na migongano hiyo kuhusu ucheleweshaji wa malipo hayo. Hali hii inachangiwa na mchakato mrefu wa kuthibitisha madai ya wananchi walioathirika na wanyamapori katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi na wawakilishi wao kuhusu migogoro hii ni mengi na madhara yake ni dhahiri. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatekeleza kwa ufanisi na ukamilifu shughuli zilizoidhinishiwa fedha na Bunge kwa ajili kukabiliana na changamoto hii.

(ii) Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy-TDL)

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza adhma yake ya kukuza na kuendeleza sekta ya Utalii Nchini Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia kurejeshwa kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii nchini (TDL) ambayo ilikuwa imesitishwa kutokana na Sheria ya Fedha ya mwaka 2020.

Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2024 ili kuruhusu asilimia 6 ya mapato ghafi ya taasisi za TANAPA na NCAA kuwa chanzo cha tozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake ambao unalenga kukuza sekta ya utalii nchini. Aidha, uamuzi wa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha unaonesha nia ya dhati ya Bunge lako Tukufu katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye kuleta maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kufanya uchambuzi wa taarifa kuhusu matumizi ya fedha za tozo hiyo tarehe 25 Machi, 2025 na tarehe 12 Mei, 2025. Katika uchambuzi wake, Kamati haikuridhika na baadhi shughuli zilizotekelezwa kupitia matumizi ya fedha hizo. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibainisha kukosekana kwa mpango wa matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara kusitisha mara moja matumizi yote yanayoonekana kutokuwa na tija katika kuendeleza sekta ya utalii nchini. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuandaa mpango mkakati ambao utaanisha vipaumbele ambavyo vitatekelezwa kupitia fedha hizo kabla ya kuanza kwa mwaka ujao wa fedha.

(iii) Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC)

Mheshimiwa Spika, kituo hiki kilianza ujenzi wake mwaka mwaka 2017 na kukamilika kufikia Disemba 2021 kwa jumla ya Shilingi 1,372,256,210.07. Kituo kilianza kazi kwa majaribio ya awali tarehe 5 Januari, 2022 kwa kuingia mkataba na mtoa huduma anayeitwa Through Mobile Africa Ltd. Hata hivyo, Kamati ilifanya ziara na kukagua utendaji wa kituo hiki tarehe 17 Machi, 2024 ambapo ilikuta kituo hicho hakifanyi kazi kama ilivyotarajiwa. Katika taarifa yake, Wizara ilisema kuwa kituo hicho kinafanya kazi kimajaribio na kwa sasa kinashindwa kuanza kazi kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ilionesha uzembe wa kituo hicho kutokufanya kazi licha ya manufaa yake kwa taasisi katika kuingiza mapato na kutangaza utalii nchini. Aidha, kituo hiki kilitarajiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 29,089,851,719 hadi mwaka 2025 kama kingeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia sababu hizo, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi 1,749,160,000.00 kwa ajili ya kuhakikisha kito hiki kinafanya kazi katika mwaka wa fedha 2024/2025. Tarehe 23 Oktoba, 2024 Kamati ilipokea taarifa ya utendaji wa kituo hiki ambapo Wizara ilionyesha bado kituo hakijaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyowasilishwa Bungeni tarehe 7 Februari, 2025, Bunge liliiagiza Serikali kufanya tathmini na uchuguzi wa kina ili kubaini sababu ya Kituo hicho kushindwa kufanya kazi na iwasilishe taarifa kwa Katibu Wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025. Kamati ilipokea taarifa ya tathmini hiyo na kufanya majadiliano na Wizara tarehe 25 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Kamati inaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, taarifa hiyo ilibainisha uwepo wa uzembe na hujuma katika mchakato wa kuanzisha na kukiendesha kituo hicho. Hali hiyo imefanya uendeshaji wa kituo hicho kukwama licha ya faida zake katika kutangaza na kukuza sekta ya utalii nchini. Taarifa ya Wizara inabainisha kuwa Serikali imeanza kuchukua hatua za awali za kinidhamu kwa wahusika. Hata hivyo, Kamati haijaridhika na kasi ya Serikali katika kuwachukulia hatua wahusika wote na katika kuhakikisha kuwa kituo hicho kinafanya kazi kama inavyopaswa ili kuleta tija iliyokusudiwa.

(iv) Bodi ya Utalii Tanzania (Tanzania Tourist Board - TTB)

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania ni taasisi ya umma iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura, 364 ikitakiwa kuchukua majukumu ya lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania (Tanzania Tourist Corporation- TTC). Bodi hii imepewa jukumu la kutangaza na kuendeleza shughuli mbalimbali katika sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali ikiwa ni pamoja na sheria ya uanzishwaji wa Bodi ili kupima ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Sheria ya uanzishaji wa Bodi hii ni ya muda mrefu na inayohitaji marekebisho. Pia Bodi hiyo inakabiliwa changamoto kadhaa ikiwemo muundo wake, ukosefu wa bajeti ya kutosha katika utekelezaji wa shuhuli zake, muingiliano wa majukumu baina yake, wizara na taasisi nyingine za Serikali. Vilevile, Bodi hii inakabiliwa upungufu wa watumishi wenye weledi na utaaalam wa kutangaza utalii kidijitali.

(v) Changamoto ya Uendeshaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii nchini kama ilivyokuwa sehemu nyingine duniani ilipata mtikisiko mkubwa mwaka 2019 hadi 2020 kutokana na UVIKO-19. Kama taasisi za kipaumbele katika uhifadhi na utalii nchini, taasisi za TANAPA na NCAA ziliathirika hali iliyotishia uwezo wao wa kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 Bunge lilifanya uamuzi kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, ambapo taasisi hizi zilitakiwa kukusanya maduhuli na kuyapeleka mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, taasisi hizi zilitakiwa kupewa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kujiendesha na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kunusuru sekta ya utalii nchini. Hatua hizo

zimeleta ongezeko la watalii nchini ambao wanatembelea Hifadhi za Taifa na Eneo la Ngorongoro kama vivutio vya kipaumbele. Hali hii imechangia taasisi za TANAPA na NCAA kupata changamoto ya kujiendesha katika maeneo ya kutolea huduma kwa watalii na kushindwa kufanya shughuli za uhifadhi kwa ufanisi kutokana na nakisi ya bajeti kutoka Serikalini pamoja na kuchelewa kupokea mgao wa fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na madaraja katika maeneo yanayosimamiwa na taasisi hizo sio nzuri. Hali hii inachangia watalii wengi nchini kushindwa kufika katika vivutio vingi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kurejesha utaratibu wa TANAPA na NCAA kukusanya na kutumia ili kuwezesha taaasisi hizi kujiendesha kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa ushauri huu na Serikali iliahidi kuutekeleza hata hivyo Serikali haikutekeleza ushauri huo kama ilivyoahidi. Kama ushauri huu hautatekelezwa, ni wazi kuwa hali hii itaendelea kuathiri sekta ya utalii na uhifadhi nchini.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

4.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali ihakikishe inaendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio hivyo hali itakayochangia kuongeza mapato ya Serikali, kukuza uchumi na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani kwenye shughuli zitokanazo na utalii nchini;

(b) Serikali iendelee kulinda na kuhifadhi rasilimali za misitu, wanyamapori na malikale kwa ajili ya kuendelea kupata manufaa ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(c) Serikali isimamie kikamilifu na kuongeza ufasini katika ukusanyaji wa Mapato ili taasisi zinazokusanya mapato kupitia MNRT portal ziweze kufikia lengo lililoidhishwa na Bunge. Aidha, Wizara inatakiwa kusimamia na kuzuia matumizi fedha yasiyo ya lazima katika taasisi zinazokusanya na kutumia ili kuhakikisha kunakuwa na tija katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo.

4.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii

(a) Changamoto ya ya Uendeshaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)

Kamati inashauri kuwa, kupitia Sheria ya Fedha Serikali ihakikishe inafanya marekebisho ili kuruhusu utaratibu wa kukusanya na kutumia kama ilivyokuwa awali. Uamuzi huo utaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya TANAPA na NCAA pamoja na kuleta tija kwenye sekta ya Uhifadhi na Utalii nchini.

(b) Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Itekeleze kwa ukamilifu Mkakati wa Kitaifa wa kushughulika na mgongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupata utatuzi wa kudumu wa changamoto hiyo;

(ii) Iongeze kasi ya utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishiwa fedha na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kukabiliana na changamoto hali itakayopunguza na kuondoa madhara ya migongano hiyo;

(ii) Iboreshe mfumo wa ulipaji wa kifuta machozi na kifuta jasho ili kurahisisha upatikanaji wake hali inayopunguza madhara yatokanayo na migongano hiyo; na

(iv) Ishirikiane na wadau wa uhifadhi kutoka sekta binafsi ili kuweka uzio wa umeme (electrical fence) katika maeneo yenye changamoto kubwa ya tembo.

(c) Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iunde chombo cha usimamizi kinachojitegemea katika usimamizi na matumizi ya fedha hizo kama inavyofanyika katika Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ili kuzuia kuingiliwa na kuongeza uwajibikiaji katika matumizi ya fedha hizo;

(ii) Isitishe shughuli zisizokuwa na tija kama ilivyoshauriwa na Kamati; na

(iii) Iandae mpango mkakati (strategic plan) ambao utaonyesha shughuli na vipaumbele vitakavyotekelezwa kwa ajili ya kuendeleza na kuleta matokeo yaliyotarajiwa katika sekta ya utalii kupitia fedha za tozo hiyo.

(d) Changamoto ya Ucheleweshaji wa Fedha za Jumuiya za Wanyapori (WMAs')

Kamati inaishauri Serikali kuwa, ifanye marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ili kuruhusu mgao wa fedha za WMAs' kwa mujibu wa Kanuni za WMA za mwaka 2018 ziende moja kwa moja kwenye Jumuiya hizo ikiwa ni pamoja na fedha zinazotokana na shughuli za utalii wa picha.

(e) Hoteli na Loji za Serikali zilizobinafsishwa

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi katika kuhakikisha kuwa majalidiliano kati Wakili Mkuu wa Serikali na Wawekezaji ambao wameshindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya uwekezaji yanafikia mwisho kwa kuzingatia sheria ili hoteli na loji hizo ziweze kurejeshwa Serikalini hali itakayopunguza changamoto ya uhaba wa huduma za malazi kwa watalii nchini; na

(ii) Kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Msajili wa Hazina zifanye ufuatiliaji wa mara kwa mara katika hoteli ambazo zinafanya kazi kwa mujibu wa masharti ya uwekezaji ili kuhakikisha zinatoa huduma katika ubora unaotakiwa.

(f) Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC)

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iwachukulie hatua za kinidhamu na kisheria wote waliohusika katika kuhujumu utendaji wa kituo hicho; na

(ii) Iongeze usimamizi ili kituo hicho kiweze kufanya kazi kama ilivyotarajiwa kwa ajili ya kutangaza kidijitali na kuongeza mapato ya Bodi ya Utalii nchini.

(g) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha mwaka 2024/2025

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi ya usimamizi wa miradi ili ikamilike kwa wakati kwa ajili ya kutoa huduma iliyokusudiwa kwani miradi mingi ipo nyuma ya wakati; na

(ii) Ipeleke fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuhakikisha wakndarasi wanalipwa kwa wakati hivyo kuepushia Serikali hasara inayotokana na riba ya kuchelewesha malipo kwa wakandarasi;

(iii) Kupitia timu za usimamizi na ukaguzi wa miradi, inahakikisha thamani ya fedha katika miradi inayotekelezwa na Wizara inazingatiwa.

(h) Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iandae mkakati wa haraka wa kufanya mapitio ya Sheria ya Bodi Utalii Tanzania Sura, 364 ili kubadili muundo wa Bodi na kuipa majukumu ya kutangaza, kuwezesha na kudhibiti shughuli za biashara na uwekezaji katika sekta ya Utalii nchini;

(ii) Kuweka mikakati ya kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kuwa huru kujiendesha na kujitegemea kimapato; na

(iii) Ihakikishe inachukua hatua za haraka kutafuta watalaamu katika eneo la kutangaza utalii kidijali ili kuiwezesha bodi hiyo kufanya majukumu yake kwa ufanisi na kupata

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na uchambuzi wa bajeti ya wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wake, ningependa kuwatambua Wajumbe wa

Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
5. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
6. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
10. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
11. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
12. Mhe.Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb
13. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Ask. Dkt Josephat Mathias Gwajima, Mb
20. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
21. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi, Mb
22. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hasa katika sekta hii. Aidha, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee nawashukuru watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

19 Mei, 2025

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Waziri kutusomea hotuba yake, lakini pia Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Sasa kinachofuata hapa ni Wabunge mbalimbali ambao wameonesha nia ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri na hivyo tutaanza na hao, lakini kabla hatujaanza kuwasoma wale waliokusudia kuchangia ninalo tangazo moja hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu baada ya aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni kufariki akiwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, basi kipindi kile ninyi nyote mlishiriki Mheshimiwa Rais alionesha nia ya kwamba Tanzania bado tungeweza kushiriki katika huo mchakato na kwa kweli lile alilokuwa amelisema wakati ule basi sasa mchakato ule umekwenda, sasa umetimia na maneno ya Mheshimiwa Rais ya kiti hicho kurejea Tanzania kimerejea na sasa tumepata

Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, Profesa Mohamed Yakub Janabi.(Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kumpongeza sana kwa hatua hii ambayo ameifikia na kumtakia kila la kheri tutapata nafasi ya kumpongeza sawasawa atakapokuja hapa Bungeni, tutakapomtangaza kama ambavyo tumekuwa tukifanya hivyo huko nyuma. Kipekee kabisa niishukuru Timu yote ikiongozwa na Mheshimiwa wetu Waziri wa Afya Jenista Mhagama na wote waliohusika, lakini pia Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wote kwa kweli na Watanzania wote kwa sababu wengi walishiriki kwa hali, wengine kwa maombi, kwa hiyo, kila mmoja alishiriki, lakini hawa viongozi nimewataja kwa sehemu tu ili tuone kwa kweli wote tumeshiriki.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wengine waliungana na Mheshimiwa Rais katika kusafiri na Profesa Janabi kwenda kwenye kampeni kwenye nchi mbalimbali. Kwa hiyo, hao nao tunawashukuru lakini wengi mlifanya maombi ili jambo hili liende sawasawa. Ahsanteni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hapa nimemtaja Mheshimiwa Rais, na yeye tutumie fursa hii kama Watanzania kumshukuru sana kwa nguvu aliyoweka katika kuhakikisha kiti hiki kinarejea Tanzania kwa mara ya pili. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua hii, lakini pia tunamshukuru sana kwa kujitoa kwake yeye binafsi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wengi wetu hata yeye mwenyewe ilibidi aseme maneno ya kwamba, ninamuunga mkono, huyu ni kijana wangu na mmeona mwaka jana alifanya hatua ya ujasiri kabisa, akampa cheo ofisini kwake. Hicho nacho kimesaidia kwa kweli kwamba huyu ndiye Mshauri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo la afya hapa nchini. (Makofi)

Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo nafasi hizi zinapojitokeza basi yeye mwenyewe anakuwa mbele kabisa kuhakikisha nchi yake inapata heshima. Tunamshukuru sana kwa kazi hiyo na ninaamini siku tutakapokuwa

tukisikiliza hotuba ambayo itakuwa inaletwa na Mheshimiwa wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naamini tutapata pengine orodha ya kuonesha nafasi mbalimbali ambazo zimepatikana katika kipindi hiki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa Rais kwa sababu ya mahusiano aliyoyaweka vizuri kabisa kimataifa kushirikiana na Serikali za Nchi zingine lakini kushirikiana na Marais wenziwe, basi inaturahisishia vyeo hivi kuendelea kuja hapa nchini. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nimesema kwamba Mheshimiwa Waziri atatutajia kwa sababu hata mimi ningeanza kuorodhesha hapa sina uhakika nitavipata vyote, lakini kwa sababu tunayempongeza hapa yupo kwenye eneo la afya Profesa Janabi, lakini hapohapo Muhimbili miezi michache pia pametoa Mkurugenzi wa Masuala ya Tiba ama inaitwa Afya Umoja wa Afrika *(AU)*, inaongozwa na Mtanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunafanya vizuri na nirejee tena kauli yangu ya kwamba tusijidharau, Watanzania tunafanya vizuri na haya yote yanaendelea kupatikana si kwa bahati mbaya yanapatikana kwa sababu ya mambo mazuri yanayofanyika hapa nchini ikiwa ni pamoja na eneo la utawala bora. Kwa hiyo, mlishike hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimesikia kicheko kimetoka mahali lakini ndiyo hivyo, yaani kwamba tuko vizuri kwenye utawala bora na ndiyo maana watu wetu wanaaminiwa kwenye hayo maeneo ambayo wanaweza kuongoza sehemu nyingine pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hili jambo tutalirejea atakapokuja Mheshimiwa (naona nimekazana sana kumwita Mheshimiwa itakuwa anaelekea huko) Profesa Janabi atakapokuja hapa tutafanya hiyo kazi kwa ukamilifu zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo sasa, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka ajiandae. Uchangiaji ni dakika saba.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Pindi Chana pamoja na Katibu Mkuu, lakini na Wakuu wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia kwa hatua hii ya ukuaji wa Sekta ya Utalii kama ambavyo hotuba ya Waziri imesema. Kwa kweli tunafarijika sana na hasa tukiamini kwamba huu ni mchango mkubwa sana wa mwana diplomasia namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye dhamira yake ya dhati katika kukuza sekta hii kila Mtanzania anaiona na kwa kweli tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezai Mungu basi aendelee kuboresha huduma na ustawi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maeneo mahsusi kama matatu hivi niyachangie kwa haraka kutokana na changamoto ya muda. Eneo la kwanza; pamoja na ukuaji wa Sekta ya Utalii lakini bado tuna changamoto ya wanyamapori hasa sisi ambao tunakaa pembezoni mwa hifadhi. Kule Lushoto tuko pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na hifadhi hii inapatikana katika Mikoa miwili ya Kilimanjaro na Tanga, lakini kwa kweli wenzetu wa TANAPA sehemu kubwa sana wamelalia katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa huku Tanga haionekani sana kiasi kwamba sisi tunakumbana tu na athari za hawa wanyama hasa ndovu na mbogo ambao wakikimbizwa maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro wengi wanakimbilia katika wilaya zetu hasa Lushoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwamba yale yote ambayo tumezungumza hapa kama mbinu za kwenda kuwadhibiti zifanyike kwa uwiano. Haipendezi sana kuona kwamba tunajenga vituo vya kuwakimbiza katika wilaya zingine halafu tunaacha wilaya zingine katika ushoroba uleule kiasi kwamba maana yake ni kwamba unapowafukuza eneo moja kwa njia rahisi tu ni kwamba wanaenda kwenye eneo lingine. Kwa hiyo, hilo ni muhimu sana kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa sisi tumepoteza zaidi ya wananchi wanne, wamevamiwa na ndovu na wamepoteza maisha na mwananchi mmoja yeye amevamiwa na mbogo. Kwa ujumla wananchi watano katika Halmashauri ya Lushoto Tarafa ya Umba.

Mheshimiwa Spika, hawa wananachi takribani 1728 wanaendelea kusubiri malipo yao ya fidia mbalimbali ambazo wamechukuliwa taarifa zao zote, lakini mpaka sasa hawajalipwa fidia na hili lilikuwa agizo la Mheshimiwa Rais alivyokuja kwenye Wilaya ya Lushoto tarehe 24 Februari, alitoa maelekezo mahsusi kwamba fidia hii ikalipwe kwa haraka ili wananchi hawa waweze kunufaika angalau na hayo malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Sekta ya Kilimo imeathirika zaidi ya hekari 5,178 katika hiyo Tarafa ya Umba na sehemu kubwa hapa ni zao la mkonge, zimeathiriwa vibaya na wanyama hawa waharibifu na hii inasababisha umaskini watu wetu kwa sababu kilimo kama cha mkonge kupanda mpaka kuvuna ni zaidi ya miaka mitatu minne, sasa umeshapanda unafikia katika hatua ya kuanza kuvuna tembo wanakuja wanafyeka shamba zima hiyo kwa kweli ni kuwarudisha nyuma wananchi, tunaomba jitihada ziongezeke ili kuhakikisha kwamba wananchi hawa wananufaika na rasilimali zinazowazunguka.

Mheshimiwa Spika, hapa ninapozungumza nina barua ya Wizara ambayo ilikuwa inazitaka halmashauri zaidi ya 44 ambazo zinazungukwa na hifadhi zipeleke vijana wasiopungua watano ili wakapewe mafunzo maalum ya uhifadhi, lakini katika Mkoa wa Tanga kwa maana sisi tunaozunguka Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kuna Wilaya ya Mkinga, Wilaya ya Korogwe na Wilaya ya Lushoto. Vijana wa Wilaya ya Mkinga na Wilaya ya Korogwe wamechukuliwa, lakini kule Lushoto vijana watano mpaka sasa hivi hawajachukuliwa na tumepeleka barua yetu na nakala yake ninayo hapa vijana hawa watano kutoka Kijiji cha Kivingo hawajaitwa kwenye yale mafunzo na wenzano sasa wanakaribia kukamilisha mafunzo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara hili jambo imeomba yenyewe na imeenda kuwasaili hawa vijana ni muhimu sana kuleta usawa katika Taifa letu. Kama ambavyo nimetangulia kusema haitapendeza majirani zetu wao wanafukuza tembo maana yake wakiwafukuza watakuja kwenye maeneo yetu, sisi bila mafunzo tutawezaje kuwaondoa katika maeneo yetu? Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tungeomba sana lifanyike haraka vijana hawa na wenyewe wakapate mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika ziara ya Mheshimiwa Rais, hivyo hivyo aliahidi kutumegea eneo kupitia msitu/shamba la *TFS* pale Lukozi takribani ekari nne ambazo tumeomba. Barua zote tumezipeleka Wizarani tangu mwaka 2023, Katibu Mkuu nimewasilisha kwake, Waziri nimekutumia nakala Naibu Waziri nimekutumia nakala. Tunaomba sana Mheshimiwa Rais siku ile ameeleza kwa ufasaha sana kwamba ombi hili lishughulikiwe haraka kwa sababu kata hii ni kata ya kimkakati ambapo tunakusudia kujenga soko la Kimataifa la mbogamboga ili mbogamboga zote zinazotoka katika Wilaya ya Lushoto zianzie katika eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumeshafanya maongezi ya awali na wenzetu wa shamba wameridhia na wamezileta barua kwenye mamlaka zao ambapo ni ofisini kwako Mheshimiwa Waziri, basi tunaomba kwa msisitizo huu na ile ahadi ya Mheshimiwa Rais hili nalo liende likakamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, siyo kwa umuhimu ni jambo la uvunaji wa hewa ukaa (*carbon*). Kama Mheshimiwa Waziri utakumbuka Mheshimiwa Rais alitupongeza wananchi wa Lushoto kwa kuwa watunzaji wazuri wa mazingira. Kwa hiyo, nasi tungependa tunufaike na utunzaji ule na uhifadhi ule wa misitu kwa kuvuna hewa ya ukaa. Tunaiomba sana Wizara iwe msaada kwetu kutusaidia kupata elimu na mafunzo mbalimbali kwa sababu misitu tunayo ya kutosha na wananchi wako na utayari wa kutosha ili na sisi tuweze kushiriki katika fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia, lakini kutokana na muda nitagusa maeneo mawili suala la Nyatwali na uharibifu wa wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ipo kwenye *top ten* ya halmashauri ambazo zinaathirika na wanyamapori, lakini tuna upungufu wa vifaakazi kwa ajili ya doria na hiyo inasababisha athari kubwa kwa wananchi kudhuriwa na wanyamapori hususani tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza hekari 5,398 za mazao mbalimbali zimeathiriwa na tembo. Hivi ninavyozungumza wananchi 1,483 mashamba yao yameathirika na hawajalipwa mpaka leo, hivi ninavyozungumza ng'ombe 800 wameuawa wananchi hawajalipwa, hivi ninavyozungumza ng'ombe 355 wameathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaoathirika hawa ni wananchi maskini kabisa, ni wananchi wa kawaida, lakini mpaka leo hakuna kifuta jasho, hii athari iko kwenye Kata mbalimbali za Halmashauri na Jimbo la Bunda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwatajie haya maeneo ili myafanyie kazi na mkitaka hata nyaraka nitawaletea. Kunzugu, Ichamu, Kiharagweta, Changuge, Bukore, Mashujaa, Nyamatoke, Tairo, Mitimirefu, Balili, Rubana, Mcharo, Utakare, Idara ya Maji, Nyasana, Guta, Makongeni, Stooni, Kunanga, Gushigwamala, Nyabehu, Kurugongo, Kunzugu, Bukore, Tairo, Ihale, Guta Mjini, Kinyambwiga na Guta B. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wananchi wa maeneo haya wamekaa zaidi ya miaka miwili wananchi zaidi ya 1400 hawajalipwa hekari zaidi ya elfu tano mia tatu tisini na zimeteketezwa, ng'ombe zaidi ya 800 wameuwa, ng'ombe zaidi ya 355. Hivi Mheshimiwa Waziri tunataka wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini waone kuwa na mbuga isiwe fahari tena?

Mheshimiwa Spika, ninaamini tukitengeneza mazingira mazuri ya kulinda wananchi wanaozungukwa na hifadhi, hifadhi hizi hazitahitaji zilindwe na mtutu. Hifadhi hizi zitalindwa na raia wema ambao wataona thamani ya mbuga yao na wao kunufaika. Dada yangu Mheshimiwa Pindi Chana na kaka yangu ninaomba watusaidie wananchi wa Halmashauri ya Bunda Mjini wapate haki yao, ninaomba sana hali ni mbaya! Huku kumesababisha njaa sasa hivi, watu wanalima, ngombe wanafuga, ng'ombe zinauliwa, zinajeruhiwa mashamba yao yanaliwa na tembo, wana zaidi ya miaka miwili hawajalipa fidia. Wapo akina mama, wapo vijana, wapo wazee wangu, tafadhali sana leo naongea kwa upole hili jambo ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wananchi wameteseka sana wanahitaji fidia tumechoka sisi watu wa Mara hatupendi kuomba chakula, lakini hii njaa inasababishwa na wanyama wakali. Kama wameshajua kwenye halmashauri kumi hizi wanaathirika na wanyamapori kwa nini hawafanyi doria ya mara kwa mara? Leo hii mifugo ikienda hifadhini ni shida, mnyama akidhurika ni shida, lakini wananchi pia wanaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapenda mbuga zetu tunajua zinachangia pato kwenye Serikali yetu, lakini lazima tu-*balance* wananchi walindwe, wananchi wahakikishiwe mazao yao, mifugo yao ili mambo yaende, kuwe kuna furaha kotekote kusiwe na furaha kwa upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la Nyatwali na amesema watu zaidi ya 3000 wamelipwa na amesema kuna makaburi yamehamishwa. Ni kweli kabisa malipo yapo, lakini malipo hayo ni yaleyale waliyokuwa wakilalamikia, leo wamewatoa kwenye eneo ambalo wanalipwa

square meter 480 wamehamia kwenye eneo ambalo wameenda kununua *square meter* zaidi ya 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo sawa bado wananchi wa Nyatwali wanalia na wanalalamika na mimi leo wazee wangu wananchi wa Nyatwali wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Nyatwali wanakuja Dodoma nitawaleta ofisini kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu zaidi ya 384 vilevile hawajlipwa na kuna taarifa kwamba tayari fedha zimetokoa Wizara ya Fedha zimekwama Maliasili. Wale wengine wamewaondoa kwa kidogo na hawa watu bado wako pale, miundombinu wameshaibomoa, wamebomoa shule, wamebomoa mahospitali, watoto hawaendi shule. Siyo sawa, hata hayo makaburi wameyahamisha hawakuhamisha kwa staha, watu wameenda kwa mitutu ya bunduki wanafukua miili wanaichanganya na aliyefanya ni Mkuu wa Wilaya ambaye ninaona sasa hivi amehamishwa. Hatuwezi kuvumilia mambo kama haya tunataka kila mtu alindwe kutokana na utu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo watu hawana sehemu za kuishi, wanafunzi wengine hawaendi shule, lakini kwenye huko kuhamisha Halmashauri yetu ya Mji ilikuwa imejenga majengo pale yamebomolewa, lakini kuna baadhi ya wale waliohama wamewahamishia kwenye maeneo mengine, fidia ya halmashauri yetu kwa ajili ya kwenda kuendeleza miundombinu kwa idadi ya watu wale ambao wamewapeleka kule ikoje? Maana watoto wameenda kwenye shule zingine wanahitaji madarasa! Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri nilikuwa ninahitaji nipate majibu sahihi, wananchi wangu kwenye suala la fidia, wananchi wangu kwenye suala la Nyatwali na hili nililizungumza tangu nikiwa kijana kabisa mpaka sasa hivi mtu mzima na Brighton ana miaka 20 sasa. *(Makofi)*

SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, ajiandae.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na timu yetu ya Mawaziri Dkt. Pindi Chana na Naibu wake Kitandula lakini bila kuwasahau watendaji wakuu wanaoongozwa na Katibu wetu Mkuu Dkt. Abbas. Kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana ya kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Spika, siyo kidogo kutoka asilimia ambazo tulikuwa tunazipigia kelele huko nyuma kwamba sasa utalii Tanzania hauko vizuri leo tumefika asilimia 132, siyo kitu cha kawaida ni kwa sababu ya juhudi kubwa ambayo anafanya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia *program* mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri amezisoma ikiwemo na *Royal Tou*. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na sisi tutaendelea kumuunga mkono katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine mazuri ambayo Mheshimiwa Rais anafanya kwenye Sekta hii ya Utalii, kwa mara ya kwanza kabisa kuna maombi ambayo yapo hata kwenye taarifa ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Mnzava amewasilisha, kuna fedha ambazo alitoa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya maendelezo ya utalii (*TDL),* fedha zile ni nyingi na zinahitaji umakini mkubwa sana halijaongelewa hapa hilo suala lazima niliongelee kidogo. Fedha zile zinahitaji umadhubuti na umakini mkubwa katika kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zile Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amezitoa kwa nia njema ili kuendeleza utalii, yako mambo mengi ndani mle kwa ajili ya kuendeleza utalii, lakini zipo taasisi ambazo zimeshaanza kutumia fedha hizo wanaendelea kuzitumia kwa ajili ya kuendeleza utalii, lakini zipo ambazo ninafahamu, karibu bilioni 17 bado hazijatumika na kuna baadhi ya maneno mengi ya mashaka kuhusiana na fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia Katibu wako Mkuu Dkt. Abbas wanafanya kazi nzuri sana fedha hizi kwa sababu mama amezitoa kwa nia njema ziende kutumika kwa nia njema hiyo hiyo. Maana kuna watu wakiishaona fedha zimetoka basi wanapeleka vitu vingine havijafanyiwa hata

tathmini ya kutosha, uchambuzi wa kutosha, wanapeleka kuomba fedha zile. Zile fedha ni nyingi na huko ndiko kunaweza kukatokea upigaji, fedha hizi zilindwe ziende kwa madhumuni ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametarajia zitafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu pia hizi fedha hazijakaguliwa bado na *CAG*, ikiwezekana *CAG* atakapoanza kufanya kazi basi apitie kuangalia hizi fedha alizoweka Mama za kuendeleza utalii je, zitatumika ama zinatumika kama ilivyokusudiwa? Ili yale malengo ambayo Mama anayatarajia katika Sekta ya Utalii ambayo tunafanya vizuri sana yaweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la pili, katika hayo hayo mambo ya kitalii tulikuwa Arusha kama ripoti ya Kamati inavyosema kwenye mambo ya vyakula, tunafanya kazi au tuna sifa kubwa kwenye maeneo mengi, lakini kwenye chakula bado kidogo. Kwenye hoteli zetu za kitalii alikuwepo hivi karibuni Balozi wa India, alikuja kule Arusha na alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha kuna baadhi ya vyakula hasa vya Kia sia nikichukulia mfano wenzetu Wahindi siyo wengi sana kama walivyo wazungu na mataifa mengine kwenye utalii wetu kwa sababu ya vyakula, kwa hiyo waangalie kuhusu vyakula wanafanyaje.

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu wapo hata kule Tabora Igombe kule tunalo ongezeko kubwa la viboko wananchi wanaathirika, ninaomba sana kwenye kulipa fidia wasikawize fidia zao kwa sababu wanakuwa wamejeruhiwa na wengine wamepata madhara ya vifo, lakini tusisahau pia wapinzani wanatumiaga sana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanyama hawana uzazi wa mpango, kule wao wanazaliana na wamedhibitiwa ni wengi hata barabarani tunakutana nao, hata Arusha tulivyoenda tembo wako barabarani, tuangalie namna gani tutawavuna ili kupunguza makali yao kwa sababu wanaendelea kuongezeka na ni wengi kweli na ndiyo ilikuwa matarajio yetu kwamba

waweze kuongezeka ili watu waweze kuwaona wanyama wakiwa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kuwasikiliza sana wapinzani hawa kunakuwa na shida, mimi huwa ninapenda kuwafananisha na mtoto mdogo wakati mwingine. Unajua mtoto mdogo huwa akianguka kwenye watu wengi hivi kanainuka kanaangalia huku na huku halafu kakiona mko kimya kanaendelea na shughuli zake, kosa useme pole, ukisema pole huwa kanaangua yowe. Ndiyo sawa na hawa wenzetu kila wanalotimiziwa na Mheshimiwa Rais wanalalamika, jamani hatuendi hata Ikulu wanakaribishwa mpaka chai, wengine hawa wengine wako sijui wamefungiwa wapi saa hizi, walionwa hata walipokuwa wagonjwa, lakini wao wanapenda kelele tu, uki-*pay attention* tu tayari wanapiga kelele kama yule mtoto mdogo na *attention* yao mojawapo saa hizi ndiyo hiyo wanaenda mpaka Bunge la Ulaya na kwingine, sisi kwetu kumetulia. Hawa wanapenda kelele, tusiwasikilize na Mama aendelee kukaa kimya.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya na Mwenyezi Mungu amjalie ampatie afya njema aweze kufanya kazi kwa utulivu na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe kwa kazi kubwa unayoifanya ya kutuongoza katika Bunge ambalo limetulia na linakwenda kwa kasi ya kidigitali vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi anayoifanya ya

kuliweka Bunge letu kuwa Bunge la kisasa na lenye kueleweka. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Pindi Chana, Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Hassan Abbas kwa kazi kubwa sana ya kulisukuma hili gurudumu ambalo lilikuwa linalegea, lakini sasa hivi tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatuna cha kusema zaidi ya kusema Mwenyezi Mungu azidi kumlinda Rais wetu, kupitia *Royal Tour* tunaona sasa hivi watalii wameshafikia milioni tano angalau tunaonyesha *speed* kubwa ya utalii inaonekana. Hili ongezeko la utalii linaongezea ongezeko la mapato, inaongezeka ongezeko la ajira Tanzania. Hivyo kwa kupitia sekta hii kwa kupitia ma-*tour operators* na wengine Sekta ya Utalii inakuwa na kuingizia mapato katika fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana *TANAPA* Ngorongoro kwa kazi kubwa sana na kwa kweli wamesimamia mifumo yao leo tunaona ongezeko la mapato yanapatikana kwa vile wana umahiri na wana weledi mkubwa wa kusimamia mapato ya Kitanzania. Mwenyezi Mungu awabariki na aendelee kuwalinda kwanza wanao uzoefu na uzoefu huu umewafanya mpaka leo tunaona *TANAPA* haiyumbi kwa kupitia kiongozi wake Alhaji Juma Kuji na hata huko Ngorongoro mapato yanaongezeka yote mifumo ni mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda ni mdogo, ninamshukuru sana Mkurugenzi Mkuu wa *TFS,* kwa kweli amemuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya leo, *TFS* inapanda miti Tanzania nzima na upandaji huu wa miti wa Tanzania nzima tunaiona Tanzania yenye kijani inaonekana na tunaona mvua ambazo tulikuwa tayari tunaingia katika ukame Tanzania inaingia kutokana na kazi anayoifanya Dosantos Mwenyezi Mungu amjalie azidi kusimamia suala hili la Sekta ya Misitu ambayo sasa hivi ni kioo cha jamii katika mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia tozo ya *TDL (Tourism Development Levy)*. Kwa kweli katika Bunge la Kumi nililizungumzia hili. Tanzania tunahitaji ku-*brand tourism* na ku-

promote marketing ya *tourism*. Kuna baadhi ya maeneo kama Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ilikuwa nyuma, haijakuwa *promoted*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi pesa zikipatikana nina imani kabisa Selous itakuwa inatangazwa kwa weledi ili angalau haya mapato tunayoyapata shilingi bilioni 900 na ushee yaongezeke zaidi. Mikoa hii ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ni kivutio kikubwa cha utalii katika nchi hii. Hiyo ndiyo mikoa ambayo inaizunguka Selous kwa asilimia kubwa, lakini bado Selous haijatangazwa vya kutosha. Kwa hiyo pato la Selous likitangazwa kwa kupitia huu Mfuko, kwa kweli mabadiliko makubwa tutaweza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi; mimi ni balozi wa utalii na huu ubalozi nilitunukiwa tuzo na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenyewe, lakini utalii wangu huu na ubalozi wangu huu sitakuwa na furaha nao kama mjusi wangu hajaleta mapato katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kunyamaza na suala la mjusi hata siku moja. Ni haki yetu ya msingi na toka mwaka 2007 ninamzungumzia mjusi ambaye yuko Ujerumani mpaka leo hii, lakini kwa miaka yote hii bado kuna kizunguzungu cha mjusi. Wenzetu Namibia walifanikiwa katika kudai mapato, lakini leo Tanzania tumekwama wapi na mjusi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda kaangalie mahali alipotoka mjusi. Hakuna msaada wa aina yoyote ambayo tumepewa na Wajerumani; hii haikubaliki. Wananufaika na yule mjusi kwa matangazo ya kibiashara. Leo tunaona sinema kubwa za kidunia za kutumia *dinosaur* lakini wale *dinosaur* wanatoka Lindi, eneo la Tendaguru na Vijiji vya Tendaguru ambavyo nitavitaja: Namapwia, Mipingo, Matapwa, Makangaga na Mnyangara; vijiji hivi vyote havijafaidika na Wajerumani hata kwa kutujengea shule. Kwa kweli ni masikitiko makubwa ambayo sitaridhika bila kuona kwa nini pato la mjusi limeachwa mpaka leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiachana na *film,* wale wanaoingiza mule kuna *exhibition* kila mwaka inafanyika ndani ya Ujerumani

na ile *exhibition* wanapata mapato makubwa. Nia na makusudi siyo kumleta mjusi. Tunataka tugawane tozo toka wameanza kumfanyia biashara mpaka leo. Ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kwa mjusi ili mapato yale Serikali Kuu ifaidike, ufaidike Mkoa wangu wa Lindi, lakini na vile vijiji vipate barabara, shule, maji na vipate zahanati. Hawajatusaidia kwa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema kitu kimoja kwa Waheshimiwa Wabunge, huu ni msiba mkubwa kwetu. Pato letu linachezewa Ujerumani sisi wenyewe hatuna faida na kila siku wanakuja wananiambia mama mjusi mjusi mjusi. Hakuna faida ya mjusi. Ninachosema, ninasikia sasa hivi wameandaa Kamati, lakini unaandaaje Kamati ya mjusi bila kumweka balozi wa utalii ambaye amesimama na mjusi toka mwaka 2005? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, mimi ni balozi wa mjusi toka nimeanza kuingia Bungeni nimesimama na mjusi mpaka leo. Sasa wanapounda Kamati bila kuniweka mimi, hiyo Kamati ni batili kwa vile nina uelewa mpana na anapotoka mjusi kuliko hata watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja niliwauliza watu wa Wizara; je, mjusi anapotoka mnapajua? Wengine hawapajui nimekuja kuwazibua mimi masikio. Hivi wanaandaa Kamati mimi Riziki sipo? Haiwezekani! Wanakuwa wanafanya vitu ambavyo ni batili. Tunataka maendeleo ya mjusi yafike Lindi na Halmashauri ya Lindi ipate tozo na sisi tupate *revenue collection* wanayoipata kule. Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, Mwenyezi Mungu akubariki. Muda umenipa mdogo, ukinipa nafasi nina uwezo wa kutiririka na suala la mjusi na tujue mapato kiasi gani yanapatikana na Kamati yangu ninataka tuisimamie tena tuhakikishe pato letu la mjusi ndani ya Bunge linawezekana.

Mheshimiwa Spika, sina la kusema, ninaunga mkono hoja ila muda ni mdogo na ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Lulida ninaona unabatilisha Kamati hapo iliyoundwa, lakini kwa sababu sijui hiyo Kamati imeundwa kwa mazingira gani na haijaundwa na Bunge, kwa hiyo, haiwezi kuwa batili. Ninaamini huyo aliyeunda anayo mamlaka ya kuiunda na ameiunda sawasawa tu. Inawezekana wapo wenzio ambao nao wanazungumzia mjusi ila hawamo humu Bungeni.

Kwa hivyo, hilo la kubatilisha mimi ninakusaidia; Mbunge huwezi kubatilisha hiyo Kamati ambayo imeundwa kwa sababu simjui ni nani ameiunda. Nimeona niliweke sawa hapo nisije nikaanza kuambiwa jamani Bunge leo limebatilisha Kamati iliyoundwa huko nje. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtangaza anayefuatia lakini kuna wageni wengine ambao waliingia baada ya tangazo la awali. Yupo Ndugu Seraphine Lusala, Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo, kutoka Serena Hotel, Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge: wageni wengine ambao hawakutangazwa asubuhi wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, kwanza ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Idara na Maafisa kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii. Wote wasimame kwa pamoja. Wako upande gani hawa? Ahaa, wameshaelekea huko? Haya karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo makamanda wa Kanda ya Jeshi la Uhifadhi kutoka Taasisi za *TANAPA, TAWA* na *TFS;* wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wadau kutoka Sekta Ndogo ya Utalii na Wawakilishi wa Vyama vya Utalii; Wadau wa Sekta Ndogo ya Wanyamapori, Viongozi na Wawakilishi wa Mashirika na Vyama mbalimbali; Wadau wa Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki na Wawakilishi wa Mashirika na Vyama vya Misitu na Ufugaji Nyuki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri umetualika huko kwenye Siku ya Nyuki, ninaamini hao nyuki wamewekwa mazingira ambayo hawatatusababishia madhara tutakapofika huko.

Tunao vilevile wadau wa Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale wakiongozwa na Chifu Adam Abdul Sapi Mkwawa, Chifu wa jamii ya Wahehe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wadau kutoka Benki ya *NMB;* wadau wa Habari za Utalii kutoka Nipashe, *Crown Media* na Tumaini *Media;* na wanafunzi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara, Kampasi ya Dodoma, wanaosomea utalii. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ambao ni familia ya Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba wakiongozwa na mke wake Ndugu Rozina Maganga. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 20 wa Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, hawa ni Maafisa Tarafa, Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji kutoka Wilaya ya Mkinga wakiongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkinga, Ndugu Salum Palangyo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: wadau nane wa Sekta ya Misitu, watengenezaji na wauzaji wa *furniture* za mbao kutoka Leka *Investment* ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu na kuchangia katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kupitia Wizara au taasisi zote ikiwemo taasisi hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi kubwa ya kutuletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze vile vile Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya hadi kuhakikisha kwamba mapato ya nchi yetu kupitia sekta hii yanaongezeka mara dufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia katika pato la Taifa kwa 17% na zaidi. Awali kabla ya kipindi cha *Royal Tour* cha Mheshimiwa Rais, Sekta hii ya Utalii ilikuwa inachangia dola za Kimarekani bilioni moja, lakini kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais, Sekta hii imeweza kukua na sasa hivi tunajivunia kusema kwamba inachangia dola bilioni 3.9 katika mapato ya nchi. Hongera sana Mheshimiwa Rais na watendaji. Hongereni sana kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kwamba mapato ya nchi yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sekta hii ya Utalii, taarifa ya Wizara na Kamati zimesema. Ninaungana na Kamati kwamba Mfuko wa *TDL* lengo lake ni kutangaza vivutio vya utalii na kuimarisha utalii Tanzania. Kama ni hivyo, ni lazima tuangalie vigezo vya nchi ambazo zimefanya vizuri kupitia Sekta hii ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri, moja ni Nchi ya Singapore ambayo imefanya vizuri katika Sekta hii ya Utalii. Nchi ya Singapore ina Bodi ya Utalii kama ya kwetu, lakini kila mwaka inaingiza dola bilioni 22. Pia Bodi hiyo hiyo imesambaa katika nchi tofauti zinazofanya vizuri. Katika masoko ya Kimataifa imefungua ofisi 19 kila nchi. Pia, ina watumishi 514. Bodi yetu sisi ya Utalii hatujaipa nguvu ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, ninaomba sana kwa sababu Bodi yetu bado ni tegemezi. Hatujaipa mamlaka ya kisheria kuweza kutangaza vivutio vya utalii Tanzania. Tuipe mamlaka bodi, siyo kila sekta tu itangaze vivutio. Bodi hii ina uwezo wa kutangaza vivutio, ina uwezo wa kujenga miundombinu na ina uwezo wa kutangaza na kukaribisha uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi hii kama tutaiimarisha na tukasema kwamba fedha za *TDL* zielekee moja kwa moja kwenye Bodi ya Utalii, matokeo yake watayaona. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri kuleta Bungeni hapa mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Utalii. Bodi yetu bado ni tegemezi, inategemea fedha za *OC* za Wizara. Mpaka Wizara iseme sijui ni kiasi gani, hawana uwezo wa kufanya kazi wala kuweka watumishi wenye weledi na walio bora.

Mheshimiwa Spika, Bodi hii kama tutaiimarisha vizuri na tukafuata vigezo kama vile, Mheshimiwa Waziri wewe unajua vizuri tu, tutaweza kuongeza mapato ya nchi kuliko. Fedha zinazotokana na utalii katika nchi hii zitaweza kuendesha mapato yote ya nchi kwa mwaka mzima kwa sababu nimesema kwamba dola bilioni 22 zile za Kimarekani ni sawa na shilingi trilioni 64, ambapo sisi tunaweza kutumia na kubaki ziada. Sisi tunataka twende mbele zaidi hatutaki tuwe nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefika hatua nzuri, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Tumsaidie Mheshimiwa Rais ili tuweze kwenda vizuri. Tuongeze mapato kwa kupitia Sekta hii ya Utalii. Wizara zote zilizopo nchini zitashindwa na utalii kutokana na ukubwa wake na kutokana na sasa hivi wasafiri walivyo wengi kwa sababu wakipitia kwenye mitandao wakiona mwenendo wa nchi ulivyo, wakiona amani na utulivu wa nchi ulivyo, wakiona miundombinu, huduma mbalimbali na mambo mengine kupitia mitandao wataweza kuongezeka zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya marekebisho ya Bodi ya Utalii aje atoe majibu kwamba ni lini tunafanya marekebisho ili Bodi iweze kuwa

na nguvu na mamlaka ya kusimamia na kuendesha utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Nchi ya Singapore ambayo ninasema imeendelea katika masoko ya Kimataifa, ilileta mikataba mitatu ya kibiashara ya utalii ambayo lengo lake ni kufanya biashara na nchi ya Tanzania kupitia Sekta ya Utalii, iwe miundombinu, uwekezaji au vitu vingine, lakini mpaka leo mikataba hiyo haijasainiwa. Tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwenda kuona, kule ukiingia unakwenda sehemu moja tu ya utalii. Kila mtu analipa dola 20, lakini angalia ni watu wangapi wanaingia katika eneo moja la utalii? Watu 4,000 kwa siku. Kila mmoja analipa dola 20 au 15 na sehemu nyingine unakwenda hadi dola 35. Maendeleo yamekua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wao wenyewe wametushangaa wanasema: "Ninyi mna uwezo, mna vitu *artificial* na mna kila kitu." Yaani sisi tunashangaa tumetembea Tarangire, Ngorongoro na kwingineko; ninyi mna vitu *natural* kabisa. Ndiyo maana sisi tukasema tuingie mkataba na ninyi. Leo wanakuja kufanya nini? Hivi mlirogwa wapi? *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante sana.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe matokeo ya mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Utalii. Pia, atuambie mikataba hii imekwama wapi iweze kusainiwa ili tuweze kuingia mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Pindi Chana na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote. Kusema ukweli kazi wanayofanya inaonekana. Tunaona Sekta ya Maliasili na Utalii kuna mahali imetoka na kuna mahali inakwenda. Kwa hiyo, ninawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema Mungu alivyoiumba Tanzania alikuwa na makusudi yake. Aliiweka Tanzania hapa ilipo na akatupa 32.5% kama rasilimali za maliasili. Alikuwa na nia njema kabisa kwa ajili ya Watanzania na katika hizi rasilimali ambazo ametupa kuna vitu vingi vizuri ambavyo Mungu ametukabidhi; Mlima Kilimanjaro ukiwepo, mbuga za wanyama, na taja vitu vyote vizuri ambavyo Mungu ameviumba akaviweka Tanzania na vitu vyote hivi vinavutia utalii. Kwa hiyo, ni tegemeo langu kubwa kabisa hii 32.5% ya eneo letu utalii na maliasili zilizopo ziendelee kutupa faida na tija katika kukuza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshauona utalii una faida nyingi sana. Waziri ametupa *data* nyingi nzuri na tumeona imechangia kikamilifu na vizuri kwenye pato la Taifa. Ukichanganya maliasili pamoja na utalii ni kwenye 21.5% ya pato la Taifa ambapo utalii umechangia 17.2%.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua nzuri na idadi ya watalii imeongezeka kama ulivyosema kutoka kwenye 900,000 wale wa nje mpaka karibu milioni mbili na wale wa ndani pia wameongezeka kutoka laki ngapi mpaka milioni tatu. Kwa hiyo, lile lengo la kufikisha watalii 500,000 lililo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumelifikia. Hongereni sana, hapo ninawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwe mkweli Daktari ninamsifu amefanya kazi nzuri, lakini bado nitampa changamoto. Sekta ya Utalii na Maliasili ina mchango mkubwa sana kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, bado tunahitaji tujitathmini na tutafakari tuangalie ni kwa namna gani Sekta hii hasa Utalii inaweza ikachangia kwenye pato letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu bado idadi ya watalii wanaokuja nchini kwa mawazo yangu bado ni wachache (ndiyo changamoto ninayokupa). Nilitegemea sawa tumeshafikisha *5.3 million;* kwa hiyo, ndiyo tumefika au bado? Ninafikiri bado sana tulitakiwa twende mpaka kwenye milioni 10. Nina uhakika tukijipanga vizuri na kujitathmini tunaweza tukafikia watalii milioni 10 kwenye nchi hii na kama yule mchangiaji wa mwisho alivyoongea, watachangia kwa kiasi kikubwa kabisa katika pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba ni vyema kuboresha vitu vifuatavyo ili tuweze kuchangia kikamilifu kwenye pato la Taifa letu hasa Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza ninachoomba tukiangalie tukiwekee mkazo ni kuweka mkazo kwenye kutangaza soko la watalii hapa nchini ili watalii waweze kuja. Bado idadi ni ndogo kwa mawazo yangu na tumeona mafanikio makubwa ambayo tumepata kutokana na filamu ya *Royal Tour* ambayo Rais ameshiriki na ile ya *Amazing Tanzania* ambayo pia Rais ameshiriki.

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe kama Wizara, Serikali iendelee kufanya vitu kama hivi kutangaza masoko, kukamata nchi mbalimbali ambazo ni wateja wetu kwenye Sekta ya Utalii. Kwa mfano, tunaweza tukamshirikisha tena Rais, tukamwomba na nina uhakika hatakataa twende kwa Waarabu pale tucheze filamu inayofanana fanana na wao wataifurahia, watairusha kwenye dunia ya Waarabu na mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwa Wajapani, Wafaransa, turushe filamu kule kwa Kifaransa, tutumie wakalimani; tuipeleke kule kwa sababu, hizi ndiyo nchi ambazo zinashiriki sana kwenye Sekta ya Utalii dunia nzima. Pia, twende India, Australia tuoneshe vitu ambavyo tunavyo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara, imeshaanza kampeni nzuri kwa kutumia mashirika ya ndege, tujiongeze zaidi, hapo wamefanya vizuri. Tuendelee kutumia vyombo vya habari vikubwa duniani kutangaza utalii wetu hapa nchini, tutumie watu maarufu. Kwa mfano, wachezaji wa mpira; ninajua wamesema kwenye ligi zile wanapeleka huko, lakini wachezaji maarufu wa mpira wakiwaleta hapa, hata wasipolipa; wamlete Lionel Messi hapa, wamlete Ronaldo au tutumie watu wengine maarufu duniani. Kwa mfano, wakimleta Bill Gates, ni rafiki yetu, akija hapa akionekana yupo kwenye mbuga zetu za wanyama ama Serena Williams na watu wengine wote maarufu, tukiwatumia wale nina uhakika tutakuwa tumeitangaza Sekta yetu ya Utalii vizuri na mambo yetu yatatunyokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika matangazo ya soko letu pia, ninashauri tushiriki kwenye maonesho ya kimataifa na ya kikanda, tuoneshe vitu ambavyo nchi yetu inavyo. Kwa mfano, kule kwenye maonesho najua kuna kitu kinaitwa *ITB* Berlin, kwa Wajerumani kule, twende kwenye maonesho yao. Kuna kitu kinaitwa *IFTM,* ya Wafaransa, kuna kitu kinaitwa *East African Tourism EXPO,* vyote hivi tushiriki na ikiwezekana, ikitupendeza pia, tuwe na maonesho yetu ya ndani; tuite hawa *giant* waje washiriki waone vitu ambavyo tunavyo, tutakuwa tumelipanua soko letu na tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu kuboresha miundombinu ya barabara na usafirishaji. Kuna tatizo kubwa; kwanza niipongeze Serikali, mtalii anapotoka Ulaya mpaka Dar es Salaam mpaka *KIA,* mambo ni safi. Kutoka *KIA* kwenda mjini mambo ni safi, barabara ni safi, lakini hotelini kwenda kule *site* ambako kuna vivutio vyetu vya utalii, hali ni mbaya, barabara ni mbaya. Nitawapa mfano, kuna mti mrefu kuliko yote Afrika uko Kata ya Mbokomu kule Jimboni kwangu Moshi Vijijini, yaani sasa hivi ukisema unapanda kwenda kuuona ule mti haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kuna kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia *route* ya Umbwe, haiwezekani, barabara ni mbaya. Sasa sisi tunahitaji pesa kutoka kwa hawa jamaa, lakini anapokuja, akipanda gari akienda kule, anarudi ameugua, hatarudi tena. Akifika kule tena atawaambia watu wengine wasije kwa sababu, hali ya barabara ni mbaya. Tukubaliane, hawa watu wametoka kwenye mazingira mazuri ambako barabara zao ni nzuri, anapokuja hapa akiwa *subjected* kwenye shida kama hizo na kuugua inakuwa siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali tutumie hata ule mfuko wa kusaidia jamii, *CSR*. Badala ya kufanya vitu vingine, watengeneze hizi barabara ili tuendelee kupata kipato kutoka kwenye barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, naona umeshaniwashia taa. Nilikuwa nina mengi, lakini nitawasilisha kwa maandishi.

SPIKA: Haya ahsante.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ikiwa muda wetu utaruhusu, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenijalia na mimi kuwemo miongoni mwa wachangiaji.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya kuhakikisha utalii wetu unasonga mbele. Pia nitumie nafasi hii kipekee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya. Mheshimiwa Rais ana nafasi kubwa, ukiona Mheshimiwa Rais anaacha enzi yake pale Ikulu, anaacha mamlaka yake, anaenda

kushinda msituni kutangaza utalii na kwa kweli, tumeona matokeo makubwa sana. Kipekee tunampongeza na tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunajua wanafanya kazi kubwa na nzuri ya kumsaidia sana Mheshimiwa Rais. Nianze na neno hili, Mheshimiwa Rais nia yake ni njema, niwaombe sana wazingatie ushauri na maoni ya Kamati. Pia, tuone nia njema ya Mheshimiwa Rais aliyonayo, kupitia utalii wetu, leo hii tunajivunia mafanikio makubwa, ambayo tumeyapata kutoka watalii 922,692 mpaka watalii 2,141,895 ni mafanikio makubwa. Pia, ukiangalia fedha ambazo tumeziingiza kutoka shilingi bilioni 1.3 mpaka kufika shilingi bilioni 3.9, saw ana 200%, haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Wizara tujipange tuendelee kutangaza utalii wetu. Biashara ni matangazo, huwezi ukajifungia ndani ukasema biashara yako itajulikana. Kwa hiyo, niombe sana, kama tulivyoshauri Kamati, hiki kituo cha utangazaji, mambo ambayo yamefanyika, hatua zinazochukuliwa na huu uzembe ambao tumeuona ni sehemu ya kufifisha na kurudisha nyuma hatua ambazo Mheshimiwa Rais anazichukua. Kwa hiyo, tuwaombe sana, lazima wahakikishe kituo hiki kinafanya kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana wanyama waharibifu pamoja na wanyama wakali. Tukubaliane, Tembo wanapopita wamekuwa wakiacha uharibifu mkubwa na umaskini, wananchi wengi wamekuwa walemavu na wengine kufa, lakini ukija kuangalia kifuta jasho, kwanza kinachelewa pia, kifuta jasho chenyewe ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, niwape mfano, kuna wananchi walikuwa kwenye kitongoji kimoja kule kwenye Kata ya Businde, kitongoji kizima wananchi hawa walikuwa ni wakulima, wana mashamba yao; wamehamishwa kabisa, tembo wameharibu mashamba yale na nyumba. Wale wananchi leo hii ni maskini wa kutupwa,

lakini ndiyo waliokuwa wanazalisha ndizi, wanazalisha viazi, wanazalisha na mazao mengine ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, sasa lazima hili tuliangalie. Pamoja na juhudi za Serikali zinazochukuliwa, njia mbalimbali wanazotumia kuhakikisha wanadhibiti hao wanyama waharibifu na wakali, niombe sana, kama Kamati tumeshauri kujenga fensi hizi za umeme, zinaweza zikawa suluhisho. Tunaona maeneo mengine wamewekeza nguvu kubwa, lakini kwenye suala hili la fensi bado hawajawekeza nguvu kubwa. Kwa hiyo, tuombe sana Wizara hili waliangalie, vinginevyo tunaleta umaskini, tunaleta uharibifu mkubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni, tumekuwa tunasema wananchi wanavamia maeneo ambayo ni ya wanyama. Hawa tembo walishapita, lakini huyu mwananchi anapokuja kwenye hili eneo, anapewa na kijiji, anafuata taratibu zote, hakuna alama inayomwonesha huyu mwananchi hapa alipita tembo, baada ya miaka 20 mpaka 30 huyu mwananchi ana shamba lake, ameshawekeza, tembo wanakuja kuvamia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana, Serikali waweke alama waainishe maeneo yote ambayo bado wananchi hawajawekeza ili yajulikane. Mwananchi anapokuja kuomba eneo, kama ni kununua shamba, ijulikane kwenye kijiji, kitongoji na kwenye kata husika, maeneo haya walipita tembo, ili kuondoa uharibifu huu ambao unaendelea kwa wananchi wetu, tunaendelea kuwafanya kuwa maskini. Kwa hiyo, niombe sana Serikali hili iliangalie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunaomba, kama Kamati, hizi fedha za *TBL* zisimamiwe vizuri, nia ya Mheshimiwa Rais ni njema. Sasa Mheshimiwa Waziri akae vizuri na wataalam wake waone namna ya kuzisimamia zilete tija kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru. Ninawatakia kila la heri Wizara ya Maliasili na Utalii na Mungu awabariki. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii na Hotuba ya Waziri. Kabla sijatoa mchango wangu, Mheshimiwa Riziki Lulida amekuwa akisema sana kuhusu hilo jusi. Nnimsaidie, ifike mwisho sasa lirudi kwa sababu, faida ni kwa wote sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, baada ya kufanya Filamu ya *Royal Tour* sisi watu wa Hai ni mashuhuda namba moja kwa sababu, Uwanja wetu wa Kilimanjaro, pale *KIA,* tumekuwa tunapokea ndege karibu kila siku. *KLM* wanaingia kila siku na mashirika makubwa ya ndege yanazidi kuongezeka. Hii idadi wanayoiona, tumetoka kwenye 992,000 mpaka 2,141,000 na bado ninaamini kule kwenye 5,000,000 tunaweza kufika, kama haya nitakayosema hapa yatazingatiwa na mengine waliyosema wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kufikia idadi hii tunatakiwa kufanya maandalizi ya mazingira yote na hapa mchango wangu nitajielekeza kwenye Wizara mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri anahitaji sana zimsaidie ili kutengeneza mazingira rafiki ya kuwezesha watalii, wakifika hapa, waende wao wenyewe kutangaza kwa watu wengine. Moja ya mazingira ni kuhakikisha kunakuwepo na hoteli za kutosha kwenye mazingira haya, ambayo kuna vituo vya utalii. Kwa mfano, sisi wa Ukanda wa Kaskazini, kuanzia Arusha mpaka kwenda Tanga, je, idadi hii ikifikiwa wameshafanya tathmini kujua hawa watu watapata sehemu za kukaa?

Mheshimiwa Spika, sasa nimwoneshe kona ambayo anaweza kupita ukapata hoteli. Sisi kule kwetu Hai tuna maeneo mazuri sana ya kuweza kujenga hoteli za vivutio vya kitalii. Niliwahi kuzungumza na Kamishna wa *PPP* - Ndugu David Kafulila, kumwambia atembelee eneo la Wilaya yetu ya Hai kwa mashamba yake ya ushirika, ili tuweze kuyatumia kwa kufanya tathmini na kutafuta wadau ambao wanaweza kujenga hoteli za

kisasa kwa kushirikiana na vyama vyetu vya ushirika vilivyopo pale. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, nimkaribishe apokee wazo hili. Tuna maeneo mazuri sana ambayo ukijenga hoteli za kitalii, mtalii akikaa pale, yeye mwenyewe anafanya utalii kwenye mazingira yale na vivutio vingine.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni barabara za kwenda kwenye maeneo ya utalii. Amesema Profesa Ndakidemi nami niseme, bahati nzuri nilishatembea na Mheshimiwa Waziri nikamwonesha barabara zile tatu ambazo zinaenda Mlima Kilimanjaro. Barabara zile zikipitika mwaka wote, kipindi cha jua na mvua, kwa maana ya Januari mpaka Desemba, zitatengeneza mazingira mazuri ya utalii kuweza kufikika, ikiwa ni sambamba na maeneo ya vivutio, hasa ya biashara. Pale Bomang'ombe, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, zimejengwa barabara; kuna Barabara ya Cheki Maji – Bomang'ombe *TPC*.

Mheshimiwa Spika, pale katikati tukiweza kuweka vibanda vizuri vya utalii, maana yake ni mtalii anaposhuka *KIA* anaweza kuanza kupata huduma kuanzia pale Bomang'ombe, kuliko ilivyo sasa hivi, mpaka afike Moshi Mjini au aende Arusha, lakini pale angeweza kupata huduma. Eneo hili nimwombe Waziri alitazame, lakini pia, atushauri kwa sababu, Halmashauri ya Wilaya ya Hai tayari tumeshaanza mchakato wa kufanya pale, ni eneo la kitalii. Tupate wataalam wake watutembelee ili tuzungumze lugha moja inayofanana, sambamba na ujenzi wa hoteli pale eneo la *KIA*.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa tunapopisha eneo la *KIA* moja ya sababu ni kwamba, zitajengwa hoteli za *five* star. Tuombe basi na yeye atusaidie kusukuma huo mradi ukamilike, ili eneo lile la *KIA* liwe na hoteli za kujitosheleza, ni pamoja na Mradi wa *Geopark*. Mradi wa *Geopark* watalaam wako walitueleza kwamba, watapita kwenye vivutio vya utalii, vile vidogo vidogo, kule Mronga tuna vipepeo ambao Tanzania na duniani kote hawapatikani.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo ya zamani, malikale nyingi. Afisa wetu wa Halmashauri alitembelea maeneo yale yote, ili mtalii anapokuja Mlima Kilimanjaro kuwe na *package,* aende

Temka, aende kwenye hivyo vituo vingine, tutaboresha utalii wetu, tutawavutia zaidi na tutamuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa Mlima Kilimanjaro siyo wa Ofisi ya Makamu wa Rais peke yake na anayehusika na utalii aone. Walifanya tathmini ya kinachosababisha theluji ya Mlima Kilimanjaro kuyeyuka ni kitu gani? Mvua kubwa iliyonyesha, ya mawe, inasababishwa na kitu gani?

Mheshimiwa Spika, tungeomba hii taarifa ya tathmini iliyofanyika itolewe kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya kuwajengea uwezo kujua mabadiliko ya tabia nchi, ili tutunze Mlima wetu wa Kilimanjaro huu. Sambamba na hilo ni upandaji wa miti, lisiwe ni suala tu la kupanda miti na kuiacha. Kumekuwa na utamaduni sasa hivi watu wanaenda wanasema taasisi fulani imetoa miche 100,000 wanapiga picha wanaondoka. Wanapanda ile miche inaliwa na mbuzi inaishia hapo.

Mheshimiwa Spika, nadhani tutengeneze kanuni, kama mtu anayetaka kutupa miti, apande, aitunze, ikifika angalau 30% au 50% ndiyo aite vyombo vya habari sasa kwenda kutukabidhi, kuliko hiki kinachofanyika sasa hivi. Tunapoteza hela na uoto wa asili bado unazidi kuteketea.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, pia, niombe kutengeneza mahusiano mazuri na sisi tunaotunza Mlima Kilimanjaro, *CSR* Mheshimiwa Waziri, alituahidi hapa. Ni kweli, kuna maeneo tumepata majiko ya gesi, ujenzi wa madarasa, lakini sisi tulioko kule Mlima Kilimanjaro, nilisema tena hapa mwaka jana, tunafahamu nchi yetu yote fedha zinakusanywa zinaenda kwenye *central pool,* lakini *CSR* maeneo mengine wanapata. Walioko kwenye migodi huku tunaona namna ambavyo wanapata *CSR,* inawasaidia wananchi wanaozunguka maeneo yale. Sisi *CSR* yetu ya Mlima Kilimanjaro mbona hatuioni na sisi ndio tunaotunza huu mlima?

Mheshimiwa Spika, moto ukiunguza, tunapanda kule kwa upendo kabisa, lakini tofauti na maeneo mengine ambapo

wanakimbizana na watu. Sisi tunaupenda mlima wetu na tunautunza kwa upendo. Niombe fedha ya *CSR* tuletewe.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa pia nikisema suala la vijana wanaopanda Mlima Kilimanjaro wasitoke tu maeneo mengine. Ni kweli, tunajua ni biashara huria, nchi yetu yote ni yetu sisi, lakini kutengeneza upendo, wale vijana wanaozunguka Mlima Kilimanjaro na wenyewe ni vizuri wakapewa kipaumbele kuliko tu mtu anakuja na watalii; kampuni inakuja inapanda mlimani moja kwa moja, hakuna hata mtu mmoja wa pale ameshirikishwa. Niwapongeze pia, kampuni zinazohusika na utalii, hasa Kampuni ya *Alteza*; tumeona imeongoza kwenye kampuni ambazo zinalipa kodi, tuendelee kuwatia moyo ili tushirikiane kwenye sekta hii kuhakikisha inainuka.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine dogo sana; pale, Uwanja wetu wa Kilimanjaro umekuwa tembo wanaingia uwanjani. Sasa niombe, uwanja ule ni *sensitive,* waone namna ya kudhibiti jambo hili, tofauti kabisa na maeneo mengine, tusije tukapata taharuki pale.

Mheshimiwa Spika, nimekuona umeshawasha na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii na kwa sababu muda umekwenda, niende tu moja kwa moja. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na *staff* wote pia, Kamati ya Kisekta kwa mchango mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na eneo lile la *OC* na *retention,* hapo hapo niguse miundombinu. Mwaka jana nilichangia, niliongelea barabara na katika barabara niliongelea, hasa, hii Barabara ya kutoka Ngorongoro kwenda Serengeti, ambayo sasa imetengenezwa vizuri, lakini barabara, zile *feeder roads* kule kwenye mbuga kwa kweli, zina hali mbaya sana, sana. Hebu tusaidieni.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo limeonekana, ukiangalia ripoti ya *CAG* ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeonesha kabisa kwamba, ile *OC* ambayo ilikuwa inatakiwa ije; kwa mfano, Ngorongoro, *OC* ya maendeleo ilikuwa ije shilingi bilioni 28, lakini kwa mwaka huo ilienda zero. Kwa *TANAPA,* kwa ujumla wake, ilikuwa iende shilingi bilioni 23, lakini ilienda bilioni moja tu.

Mheshimiwa Spika, wanasema ng'ombe anayekamuliwa hachinjwi, ng'ombe anayekamuliwa analishwa vizuri, anapewa *molasis*. Sasa hawa ng'ombe ambao tunawakamua, lakini kwenye *retention,* kwenye hizi *OC* hatuwapelekei! Pamoja na kwamba, kwenye Taarifa ya Kamati wameonesha kwamba, kutakuwa na *retention,* lakini inaonekana uendaji wake hauendi na hawapati hizi fedha. Sasa hii kwa kweli tunawaua.

Mheshimiwa Spika, tuangalie tu unapokuwa na barabara mbovu, zile siyo tu kwamba, unamtesa mtalii, lakini hata mfanyabiashara, magari yake yale yanakuwa yanachoka kwa haraka na magari haya yanayokuja, *model* mpya, hayana ugumu kama yale ya zamani, kwa hiyo, niombe sana. Kwenye Ripoti ya *CAG* wameelezea kabisa, kuanzia ukurasa wa 156 mpaka 158 na kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameongelea, ukurasa wa 20, Kamati pia, kwenye ukurasa wa 16, ninaomba sana.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane hii *OC* inayoenda ya mshahara peke yake, tukumbuke pia, kwenye *OC* ya Maendeleo kuna miradi imesimama, ipo imekuwa *listed* pale, lakini mbele zaidi kuna suala la ulinzi ambao *rangers* wako pale wana mahitaji mengi. Kwa hiyo, ninaomba hilo niliongolee kwa uzito wake kwa kweli na ninajua pengine siyo la kwako moja kwa moja, Mheshimiwa Waziri, lakini ni la Serikali kwa sababu, hii inatakiwa irudi kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni, eneo la *manpower. Manpower* kwenye eneo la uhifadhi na ma-*guide* tumepiga hatua sana na nikipongeze sana *Chuo cha Mweka Wildlife,* kimekuwa kina *standard* za Kimataifa, lakini fedha tuliyoweka kwenye Chuo cha *VETA,* kwa ajili ya watumishi wa hoteli ninaona

haijaweza kutupa tija. Kuna haja ya Serikali ku-*review,* aidha mitaala au *attitude* peke yake, tuna shida kubwa sana kwa watumishi wa hoteli. Kuna mzungumzaji mmoja amesema, hata kwenye chakula; chakula ni eneo moja, lakini *customer care* na namna ya ku-*handle* wageni, pamoja na lugha za kigeni, tuna shida sana.

Mheshimiwa Spika, kazi zetu nyingi zimechukuliwa na majirani hapa na hawa majirani wana chuo kimoja tu, kama cha kwetu. Sisi tunakuwaje tunashindwa na tuko karibu kupata watu watakaotoa elimu bora, hasa kwenye hoteli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ma-*guide* na ma-*porter,* nimeliongelea kwa muda mrefu. Sasa ninaomba tuwe na *mechanism,* Mheshimiwa Waziri anaifahamu ile *Kilimanjaro Porters' Association Program,* ni kama *NGO,* inaweza ika-*endorse* kampuni za *tours* ambazo zinawalipa vizuri wale *porters,* kuendana na mwongozo wa Serikali, lakini inatumia hiyo hiyo *website* kwa kampuni ambazo zime-*default* kuwafanyia *marketing,* ambayo ni *negative* kule na wanapoteza utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa tunashindwaje, kama Serikali, kuwa na chombo cha kusimamia hayo maslahi ambacho kitakuwa badala ya kwamba, huyu ame-*default,* unatangaza dunia nzima kwamba, huyu hafai, halipi hawa vizuri; kukawa kuna makubaliano, watu wakarekebishwa, badala ya kuharibu biashara kwa sababu, unapokuwa umesha-*recommend negatively* mtu kuja ku-*recover* tena hiyo *market* inachukua muda mrefu. Kwa hiyo, ningeomba tuangalie namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Saashisha ameongelea suala la hoteli na ametaja maeneo mengi. Mimi nitoe tu mfano, ni kweli kwamba, Serikali imeshindwa kuwa na *bailout mechanism* kwa kampuni kubwa kipindi zinaposhindwa kujiendesha, kwa ajili ya ku-*rescue* kodi, ambayo tunapata pale na zile ajira?

Mheshimiwa Spika, mfano, nimetolea Hoteli ya Ngurdoto. Juzi nimepita tena pale kulikuwa kuna mkutano wa *airport* zote Afrika, ulikuwa unafanyika pale. Kuna eneo zuri, ni sehemu pekee

Marais wanaweza wakaenda wakalala, zaidi ya 10, 20, inaingia kwenye mchanganyiko, Serikali kweli, inashindwa ku-*bailout* hata kwa kununua *share* au kutafuta mbia wa kuiendesha, mwisho wake inaenda inakuwa mabweni ya wanafunzi?

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie namna, kama Serikali kwa sababu, yule naye ni ng'ombe ambaye tunamkamua, ni vizuri akatunzwa. Hii iwe ni kwa biashara nyingine zote ambazo zimeshakuwa kwa kiwango kikubwa kama ile Hoteli ya Ngurdoto.

Mheshimiwa Spika, kuna *fee* mpya ambazo ziliwekwa kwenye *scenic flight,* zile ndege ambazo zinapita karibu na mlima na maeneo yenye mandhari nzuri, kwa ajili ya watu kuangalia na kupiga picha. Kumekuwepo na kodi zilizowekwa mpaka wadau walikuja mpaka hapa na ninashukuru baadhi ya watendaji Wizarani walinisaidia kuangalia kuzirekebisha. Zile *scenic flight* ni aina mpya ya utalii, sasa inapokuwa imewekewa kodi kubwa inaua mandhari nzima ya kuwa na *product* nyingi za watalii. Ninaomba sana tuangalie namna ya kurekebisha zile kodi, ili watu hawa waweze kufanya biashara yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niendelee kukumbusha lile la ku-*integrate* mikutano, ku-*integrate* michezo na utalii wetu. Nilishatoa ile *tournament ya* golf, ilikuwa ifanyike kule Kili *Golf*, ambayo ni *PGA tour,* ni ya Kimataifa, ingetuweka kwenye ramani ya dunia, lakini watu pia, wangeweza kwenda kwenye vivutio vyetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana leo. Nitawataja baadhi ya Wabunge ambao tutaanza nao michango alasiri tutakapokutana tena. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka,

Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga na wengine wataendelea kutajwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni, leo.

(Saa 7.04 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Nitawaita wachangiaji ambao tunao mchana wa leo. Tutaanza na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hii Wizara ya Maliasili na Utalii. Shukurani zangu za dhati kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza tu nimshukuru *Allah Subhanahu wataala* kwa kutujalia uzima na uhai, lakini hali

kadhalika nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Hazara Pindi Chana kwa utekelezaji wake mzuri wa bajeti, uwasilishaji ulikuwa mzuri. Hali kadhalika Mheshimiwa Naibu Waziri amefanya kazi nzuri amekuwa akijibu maswali yetu hapa kwa ukakamavu na ufanisi mkubwa. Pia nimpongeze Katibu Mkuu na timu yake kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri na uandaaji wa taarifa hii ambayo leo tumewasilishiwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye mchango wangu na kwanza nimshukuru *Allah* kwa sababu katika kipindi changu cha mwaka wa tano hapa Bungeni toka mwaka 2020 nimekuwa nikichangia hii bajeti ya maliasili na utalii. Hali kadhalika taarifa zote za Kamati nimekuwa vilevile nikichangia. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo nimeyaona ambayo tumekuwa tukiyazungumza hapa yametekelezwa vizuri na yale ambayo ni changamoto na kwamba bado hazikupata ufumbuzi ni mategemeo yetu kwamba katika bajeti ya awamu hii basi Wizara itajitahidi kuweza kuzishughulikia na kuweza kuleta ufanisi na utekelezaji wa ilani uwe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, changamoto ya kidunia ya upoteaji wa misitu inazikabili nchi nyingi kwa sababu sasa hivi dunia nzima inapoteza takriban hekta milioni 23 za misitu kila mwaka. Katika upoteaji huo sisi Tanzania tunachangia karibu hekta zaidi ya laki nne kwa mwaka zinazopotea kutokana na ukataji na utumiaji mbaya wa misitu yetu. Sababu kubwa za upoteaji wa misitu kwa Tanzania, kwanza ni uvamizi wa maeneo kwa sababu za kilimo pamoja na ujenzi. Sababu nyingine kubwa ni utumiaji mbaya kutokana na ukataji wa shughuli za kuni, makaa pamoja na harakati za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upoteaji huu wa misitu umekuwa na athari kubwa sana na kama Wizara, zile ambazo ni Wizara mtambuka hazikukaa pamoja zikazishughulikia kwa pamoja basi tutaendelea kupoteza misitu na tutafika wakati basi Zanzibar na Tanzania kwa ujumla itakuwa ni jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeziomba tu zile Wizara, kwa sababu tukiangalia ukataji wa misitu huu tusiiangalie Wizara

ya Maliasili na Utalii peke yake, tuziangalie Wizara za Maji; kwa sababu misitu ikipotea maana yake vyanzo vya maji vinapotea; misitu ikipotea vilevile maeneo ambayo yanazalisha nishati kama vile Bwawa la Mwalimu Nyerere nalo linakuwa ni hatarini. Vilevile misitu ikipotea vyanzo vya utalii ambavyo tunahangaika hivi sasa kuhakikisha kwamba watalii wanaongezeka navyo vilevile tunaenda kuvurugika.

Mheshimiwa Spika, kuna bajeti kubwa ya kilimo imetengwa nayo kama tukiendelea hivi hivi misitu kupotea, mabwawa, mito na hata ile *reserve* yetu ya maji ya chini nayo inakwenda kuathirika kwa sababu kilimo cha umwagiliaji nacho kitakuwa vilevile, kazi ni bure kwa sababu inategemea maji ambayo yanapotea kutokana na uharibifu wa misitu. Hata Sekta ya Mifugo nayo itaathirika kama misitu itaendelea kupotea kwa sababu na wao wanategemea maji kuweza kunywesha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu sasa, ni lazima sekta hizi zikae kwa pamoja, wasiangalie sekta zao tu wakajifungia kwenye Wizara zao au ofisini kwao wakasahau kwamba na wao tatizo la uharibifu wa misitu pia linawaathiri. Sasa, mapendekezo yangu, la kwanza ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri tukajitahidi kwanza kuangalia uwezekano wa kuhakikisha sana utawala wa sheria unaimarika. Kwa sababu Tanzania tunasifika kwamba tunatunga sheria vizuri, lakini shida tuliyonayo ni kwamba utekelezaji wa sheria hizi ndiyo mgumu. Kwa hiyo ningeliomba hili nalo tukalitia maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba, tuweke mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kuweza kushughulikia suala la uharibifu wa misitu. Kwa sababu tumekuwa tukizungumza hapa *TFS (Tanzania Forest Service)* itapandishwe iwe mamlaka; lakini nalo hili kwa mwaka wa tano nalo limeshindikana pia. Sasa na hili pia linakuwa gumu? Tunataka tuweke umadhubuti wa uhifadhi wa misitu yetu. *TFS* kuipandisha hadhi ni suala la usiku mmoja tu wakatuletea sheria hapa tuhakikisha hili linakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Jeshi la Uhifadhi, tumezungumza kwamba Jeshi la Uhifadhi kuna vijana

wengi wanamaliza chuo kule Olmotonyi pamoja na Chuo cha Mweka; tuongeze idadi ya Jeshi la Uhifadhi, lakini pia maslahi yao tuyaangalie. Kwa sababu sasa hivi *TANAPA* wanalipa kivyao, *TFS* wanalipa kivyao na *WMA* wanalipa kivyao. Sasa, tuangalie haya maslahi ya Jeshi la Uhifadhi ambayo vijana wetu hawa wanapata athari za uharibu, wanaumia, wanauliwa lakini hatimaye ukiangalia maslahi yao si mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine vilevile ni kuongeza wigo wa elimu na ushirikishaji wa jamii. Tukiongeza wigo wa elimu kuhusu uhifadhi wa jamii; na Mheshimiwa Rais amekwishatupa dira kwa sababu yeye amekwenda kwenye ku-*act* ule mchezo wa *Royal Tour* pamoja na *Amazing* Tanzania kama kutupa dira kuhusu tunashughulikia masuala ya kutoa elimu kwa jamii. Sasa twende na sisi tuongeze wigo wa elimu, tuielimishe jamii. Tutumie vipindi vya redio na *TV*; Hali kadhalika twende kwa jamii kama vile zamani ambapo kulikuwa na *cinema* maalum zinakwenda vijijini kuweza kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeliomba tu, suala la uharibu wa misitu na ni suala nyeti ni suala la kushughulikiwa haraka ili Tanzania iwe endelevu katika sekta zake mbalimbali za uzalishaji pamoja na za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Soud. Nilikwishamwita Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa hii kwa ajili ya kuweza kuchangia kwenye Wizara yetu ya Maliasili na Utalii, Wizara ambayo tunajua kwa asilimia kubwa mapato wanayapata kutokana na Kanda ya Kaskazini na Arusha ikiwemo. Nitazungumza mambo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kilio chetu ni kile kile kama cha mwaka jana. Tumeona kuna changamoto kubwa sana tangu Serikali ilipoamua kuchukua fedha za Ngorongoro na *TANAPA* na kuzipeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Fedha zinakwenda kule, lakini hazirudi kama ambavyo inavyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa tuliyosomewa hapa leo, tunaambiwa kwamba Serikali imeweza kurudisha 32.55% kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Hata hivyo, ukienda hali ya barabara ni mbaya, miradi mbalimbali kule inasuasua kwa sababu Serikali inakusanya fedha na hatimaye hairudishi kwenye taasisi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ombi letu, tunaomba Serikali irudishe utaratibu wa zamani, Mamlaka ya Hifadi ya Ngorongoro na *TANAPA* pamoja na taasisi nyingine zote za Wizara ya Maliasili wakusanye wenyewe halafu warudishe gawio kama walivyokuwa wanafanya miaka mingine iliyopita. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuboresha barabara zetu, miradi mbalimbali ya maendeleo, lakini pia tutaweka taswira nzuri zaidi kwa watalii wetu kwa sababu biashara ile ni biashara ya *leisure*. Mtu amesafiri anakuja ku-*enjoy* anakutana na makologesheni na vitu vingine. Ninadhani ni jambo ambalo haliendani na maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameipigia debe *Royal Tour* akitegemea kwamba wageni wakija wanufaike na fursa ambayo ametutengenezea kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumekuwa tukisema kila siku, kwamba Sekta ya Utalii ni sekta ambayo lazima iwe *predictable,* ni sekta ambayo akitaka kuingiza tozo ni lazima uiandae jamii. Hata hivyo ni sekta ambayo tumeona inaonewa sana. Serikali kila ikikaa kutafuta fedha inakwenda kuangalia kwenye vilevile vya utalii. Badala ya kutafuta vyanzo vipya wanarudi kule kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, safari hii tumeona wameleta *introduction of new environmental management* ya *fees and charges* kwa wenzetu hawa wa *NEMC*. *NEMC* kupitia

kanuni ya tarehe 14 Mei, 2021 walikuwa wana-*charge* kwa kupitia *facility*. Kama una hoteli unalipa kwa hoteli nzima. Kwa mfano hoteli ya nyota tatu mpaka tano walikuwa wanalipa milioni mbili kwa hoteli ambazo ziko ndani ya hifadhi au karibu na hifadhi. Kwa nyota moja hadi mbili ni milioni moja na nyota ambazo hazijawa *graded* ilikuwa ni laki saba na nusu. Sasa hivi wanataka na wao kulipa kwa kitanda. Yaani kila mtalii anapolala pale na *NEMC* naye pia anataka apate fedha. Kwa maana ya kwamba kila kwenye holeli ambazo ziko karibu na hifadhi au ndani ya hifadhi kila kitanda elfu hamsini, kama ni *guest house* kila kitanda ni elfu thelathini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza yule mtalii akilala pale ndani kwenye kile kitanda yaani *role* pale ya *NEMC* inakuwa ni kitu gani? Ninadhani mwanzoni ile kufanya kwa *facility* ilikuwa angalau ina-*make sense*. Ni vizuri Wizara ya Fedha, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na watu wa mazingira wakae chini waangalie. Tozo kama hivi zinawakatisha tamaa wale ambao wanamsaidia Rais Samia kwenye *Royal Tour* kwenye ku-*boost* utalii kwa sababu kila siku ni changamoto kubwa na zinakuwa ni nyingi zaidi. Kwa hiyo ninadhani hili jambo lina hitaji jicho la ziada la Serikali; na kwamba tozo kama hizi zinatakiwa ziondelewe na tubaki na kanuni ya zamani ambayo wala haikuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye upande wa matumizi ya dola, kwa maana ya fedha za kigeni. Sina tatizo na maelekezo ya Serikali kwamba tutumie shilingi yetu katika nchi yetu, lakini biashara ya utalii ni biashara ambayo ni *very sensive*. Leo ukiangalia *BOT* pale wanatumbia dola moja unaweza ukanunua kwa 2,670 unaweza ukauza kwa 2,697, lakini mtalii anayekuja Tanzania leo ana *book one year in advance* wengine hata miaka miwili kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ume-*quote* umeambiwa dola moja ni 2,670, umebadilisha hiyo fedha ukamtumia kule mtalii wako akalipia leo halafu anakuja baada ya mwaka mmoja, pengine dola imefika 2,900 au 3,000 au 2,800. Sasa, ile tofauti inayojitokeza pale itakwenda kumuathiri mfanyabiashara wa utalii

wa ndani. Sisi tulikuwa tunadhani, kwa sababu hii biashara ni ya kimataifa inasaidia pia kuleta *forex* ni vizuri wakaruhusiwa kuendelea ku-*quote* kwa dola wakapokea fedha kutoka nje huko kwa dola na mwisho wa siku hata mtu akibadilisha vile hata baada ya miaka 10 ijayo bado dola moja itabaki kuwa ni dola moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiigawa kwa shilingi mabadiliko yoyote yakitokea changamoto itakuwa ni kubwa zaidi, kwa hiyo tuinaomba Wizara, kwa sababu kwenye ile kanuni hawajatoa ufafanuzi kwenye Sekta ya Utalii hili jambo linakwenda kuangaliwa kwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa kweli, wameweza kufuta tozo ile kwa wale ambao wanaongoza utalii. Hata hivyo wamesahau kitu kimoja, wafanyakazi wa Sekta ya Utalii ambao wanaingia ndani ya hifadhi kila siku wanachajiwa fedha na Serikali. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba, pamoja na kufuta tozo hii kwa wale wanaoongoza utalii na wafanyakazi wote ambao wanafanya ndani ya hifadhi, pamoja na yale ya magari na wenyewe pia wakafute tozo zao kwa sababu wao si watalii, wao ni wafanyakazi, wameajiriwa; na ule mzigo wote hauendi kwa wafanyakazi peke yake, pia unakwenda kwa mwenye kampuni ya utalii. Kwa hiyo tunaomba Serikali ikaangalie uwezekano pia wa kufuta na hii ili wafanyakazi wale Tanzania ambao wamepata fursa ya ajira wasipate changamoto kama hiyo ya kulipishwa wakati wanatumikia ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo nyingine wanasema ya kupanga hoteli nyota tano, tatu, nne wamepunguza kutoka dola 2,500 kwa nyota tano hadi 1,500. Hii tozo ni kufuta kabisa; hii ni kazi ya Serikali kuzi-*grade* hoteli zetu kwamba hii ni nyota tano, ni nyota nne, nyota ngapi. Kwa nini wakam-*charge* mtu ambaye anafanya kazi ya utalii? Sasa wanakusanya kodi, kodi kazi yake ni nini? Wanalipwa mishahara, kazi yake nini? Sasa si wakafanye kazi kama hiyo ya kwenda ku-*grade* hizo hoteli na vitu vingine? Isiwe kila kitu kwenda kuwakamua tu hawa watu wa Sekta ya Utalii, kitu ambacho kwa kweli kinarudisha nyuma jitihada za Rais Samia za masuala ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye upande wa wale wanaofanya biashara ya kuwapandisha watalii mlimani, tumeona na wenyewe pia wamepunguza kama Serikali kutoka dola 2,000 hadi milioni tatu; ya nini yote hiyo? Hiyo ni leseni tu ya biashara. Leseni inakusaidia kumtambua huyu mfanyabiashara ukishamtambua; ana kodi nyingine zaidi ya 53 hapa ambazo anazilipa. Sijui analipa huko *TRA,* analipa *concession fee,* wanalipa sijui *bed night levy;* wanalipa *conservation fee,* sijui *digit services,* wanalipa kodi kibao zaidi ya 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kileseni cha kumtambua tu kwa nini kinakuwa na gharama kubwa namna hiyo? Kwa hiyo ninashauri na hii yenyewe kama tunataka ku-*charge* basi angalau kwa kampuni ndiyo angalau milioni moja ambao wanapandisha utalii; lakini kwa mtu binafsi ingekuwa angalau shilingi elfu hamsini ili vijana wengi wa Kitanzania ambao hawana ajira waweze kupata fursa ya kupata ajira na hatimaye fedha isiwe kikwazo cha kuwaingiza sekta hiyo rasmi…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante…

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kumalizia…

MWENYEKITI: Muda wako tayari Mheshimiwa Mrisho Gambo.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana…

MWENYEKITI: Sijui kama umeunga mkono hoja?

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nimezitoa, ninadhani nikipata ufafanuzi wake nitakuwa na fursa nzuri zaidi ya kuweza kuunga mkono.

MWENYEKITI: Haya, ninashukuru sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa

Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana hii Wizara ambayo pia ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi na Maliasili, kwa hiyo hii ni moja kati ya Wizara ambayo tuko nayo. Kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri iliyoko mezani, lakini pili niunge mkono maoni ya Kamati yangu ambayo tunaisimamia yale ambayo tumeyatoa kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninaomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kaka yangu Abbasi na viongozi wote wa Wizara hii, akiwemo Naibu Katibu Mkuu na Makamishna wote wanaoisimamia Wizara ya Maliasili kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na kwa kuhakikisha kwamba maliasili za nchi yetu na Sekta ya Utalii inaendelea kukua; kwa hiyo tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo tu ambalo ninatamani nilizungumze; ni kwenye sekta ya hiki ambacho kimezungumza na Kamati kuhusu *TDL.* Niipongeze Serikali kwanza kwa kuwa na huu Mfuko wa Tozo, kwa maana ya *Tourists Development Levy;* ni Mfuko ambao kwa kweli umekuwa na manufaa, kwa maana ya upatikanaji wa fedha kwenye Wizara yetu. Pili, tunachokitamani ni kwamba fedha hizi zikafanye kazi ambayo Wizara inakusudia kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kwamba, ukiangalia makusanyo ya kutoka mwezi Mei kama sikosei hadi mwezi wa Desemba ni karibu bilioni 33.4. Ni fedha nyingi na ni fedha ambazo tunatamani kwamba ziende kwenye utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokitamani ni nini; ni kwamba Sekta ya Utalii ni sekta ambayo ina changamoto mbalimbali. *For instance,* kuna kuna *issue* ya miundombinu ya barabara, mawasiliano na pia uelewa; elimu ya watu kuhakikisha kwamba Sekta ya Utalii inakua. Kwa sasa niombe sana Serikali na Wizara yetu, kwamba tunapopata fedha kama hizi tujikite kwenye

kutatua changamoto zile ambazo tunatamani zihakikishe utalii unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *TTB* wanatangaza utalii, lakini hawawezi wakawa wanajikita kutangaza utalii bila pia kugundua ni changamoto zipi tuzitatue ili utalii wetu ukue? Kama changamoto ya kwanza ni miundombinu, kama wachangiaji wengine walivyosema, basi ni vema tukajikita kwamba fedha ambazo zinapatikana muda mwingine kwenye ku-*support* na kukuza utalii zijikite kwenye ku-*support* na kujenga miundombinu ambayo ni rafiki ili watalii waweze kuja kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikwishawahi kuzungumza hapa, kwamba kama tunatamani utalii pia ukue ni kuhakikisha kwamba tuna *invest* zaidi pia kwenye kutoa elimu na kuutangaza utalii wenyewe. Tunatamani kabisa kwamba kama fedha inapatikana Wizara ikiamua kwamba haya mambo matatu yanatatuliwa yawe yametatuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho yakaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani nilisema kwamba unaweza ukakuta mtalii ametoka nje amefika Dar es Salaam, amefika *KIA,* lakini wale watu wanaoanza kumpokea hadi anafika kwenye hifadhi mpaka anaondoka kuanzia kwenye huduma za hoteli. Je, hawa watu wana elimu kiasi gani na uzalendo kiasi gani kuhusu utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi ambayo inatakiwa tuhakikishe kwamba Wizara hii ambayo inasimamia jukumu zima la utalii inatumia fedha hizi pia kuelimisha na kuwajenga Watanzania ambao wapo kwenye mnyororo wa kuhakikisha kwamba mtalii anaenda na kurudi, anapata ile *taste,* uzalendo na anapata vionjo vya eneo tofauti tofauti kabisa katika kuhakikisha utalii wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi unaweza ukakutana na watu ambao ni dereva *tax* wapo barabarani ambao wanabeba watalii wetu, lakini je, wana elimu kuhusu utalii wetu? Hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwamba Wizara ione fursa wanapopata fedha kama hizi za *TDL* kujikita; kama wanajikita kwenye kuelimisha utalii, kuweka miundombinu sawa kwenye hifadhi, kujenga mahusiano mazuri kati ya sekta binafsi na Wizara. Basi wafanye hivyo ili ile fedha iweze kuleta tija kama ambavyo sisi Kamati tulitamani kwamba iendelee kuleta tija kwa ajili ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unakuta hawa watu wa sekta binafsi ambao wanasimamia utalii, kwa sababu 90% ya Sekta ya Utalii inaongozwa na sekta binafsi. Wanatamani kuona pale ambapo wanatoa hizi tozo zinaleta *return* ya kutatua changamoto ambazo wanakutana nazo kwenye hifadhi au sekta yao ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri kazi nzuri ambayo wanaifanya pamoja na Makamishna wote wa *NCCA*, *TANAPA* na wengine wote wahakikishe kwamba fedha hizi ambazo zinapatikana kwa ajili ya *TTB* ziweze kufanya kazi husika ili ziweze kusaidia kwenye kukuza utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye suala la *orientation*. Sisi kama Kamati nia na kilio chetu kama Bunge na ninalishawishi Bunge pia waendelee kuomba kwamba *retention* ya fedha kwa ajili ya *TANAPA* na *NCCA* ziweze kufanyika, ili wenzetu waweze kukusanya na kutumia wao wenyewe. Hii inaweza kutusaidia kabisa katika kutatua changamoto ambazo wamekuwa wakikutana nazo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumepata fursa ya kuzunguka kwenye hizi taasisi, maeneo ya Ngorongoro na hifadhi mbalimbali tunaona kabisa uendeshaji wa taasisi hizi muda mwingine unakuja kuwa ni mgumu, kwa sababu ya kusubiria fedha kutoka serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukirudi kwenye ule mfumo mwingine ambao unaweza ukaisaidia taasisi ikaendelea itakuwa kwetu ni nia njema na ni jambo zuri kwa Serikali

kuhakikisha kwamba taasisi ambazo zinakusanya na kutumia fedha zinatumia vizuri. Ukitumia ule mfumo wa *eyes on, hands off* Serikali inaweza ikawasaidia wenzetu wakapata fedha na wakatumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba nilikuwa ninazungumzia hivi kwenye *TDL*. Pia, kwenye *TDL* kuna ule mradi tuliokuwa nao wa *REGROW* ambao ulileta changamoto kidogo na sasa Serikali imejiweka tayari yenyewe kwamba, sasa itatangaza utalii Kusini mwa Tanzania ambapo mojawapo ni Kitulo na maeneo mengine Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kama hizi Fedha za *TDL* ambazo tunazipata kama wanaenda kuongeza kwenye *effort* ambayo *REGROW* ingefanya, basi wao waende kuweka hiyo *effort* kuhakikisha kwamba hatupati changamoto tena kuona utalii wa kusini umelala. Wanaenda kutumia pia fedha hii kuhakikisha kwamba wanainua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha Utalii wa Kusini mwa Tanzania ikiwemo Kitulo kwa kweli wanatuunga mkono. Tuna uhitaji wa *accommodation*, barabara na kuhakikisha kabisa tuna *airport* ndani ya eneo la hifadhi yetu na tunashukuru kwamba walikuja eneo la Matamba wakapima eneo kwa ajili ya kujenga *airport*. Tunatamani vile vitu vitokee kwa sababu hii *project* ya *REGROW* imefika sehemu imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia huu Mfuko wa *TDL,* Wizara wahakikishe kwamba wana-*support* ukuaji wa utalii Kusini mwa Tanzania na sisi watu wa kusini tujisikie afadhali na ahueni kuhakikisha kwamba tunaungwa mkono kwenye Taifa letu. Ukienda Mbeya, Rukwa, Njombe, Morogoro na maeneo mengine ya kusini yana vivutio vingi ambavyo vingeweza kuingiza fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Wizara yetu ya Utalii inakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maoni yangu kwa sababu ninatamani pia changmaoto kubwa Nyanda za Juu Kusini ni miundombinu ya barabara mvua zinanyesha sana. Kwa hiyo,

watalii wakienda, wakirudi muda mwingine wanakuwa wakija hawawezi kurudi tena kutokana na changamoto ya barabara, wanasema kule kuna changamoto. Kwa hiyo, tunatamani wajikite kwenye kutatua changamoto ambazo zitafanya Bodi ya Utalii ukue, lakini changamoto ziweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hapo niseme wazi ninalishawishi Bunge waunge mkono bajeti hii na Serikali Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa na kusema kweli kabisa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anastahili pongezi kwenye sekta hii ambayo sisi tunaisimamia. Wizara ya Maliasili wamefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba utalii unarejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita Arusha leo, Vijana wa Arusha wanasema Waheshimiwa Wabunge Rais alichotufanyia hapa ndani ya Arusha, imebadilika hatuna haja ya kuhangaika na mambo mengine kwa sababu uchumi umerejea. Wanaona kabisa uchumi umerejea na hifadhi zinaleta matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Wabunge wenzangu wote tuunge mkono bajeti hii, tuiunge Serikali ikafanye kazi, pia niwaombe tu Waziri na…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sanga muda wako umeisha.

MHE. FESTO R. SANGA: ….watumishi wa Wizara hii kwamba tunawatia moyo sisi kama Wabunge tunaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana niseme wazi kwamba, ninaunga mkono hoja na ninawapa kila pongezi nikiamini wataenda kufanya kazi vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph

Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kukushukuru wewe jioni hii ya leo kunipatia nafasi nichangie Wizara hii muhimu ya Utalii na Maliasili. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyopambania maisha ya Watanzania kuhakikisha wanaishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu kweli nifikishe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya utalii, vilevile Naibu Waziri wake wa Utalii alishakuja Liwale, changamoto zetu tulimpatia na ametekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi vilevile ziende kwa vijana wale Makamanda, Kamanda aliyepo pale Liwale wa *TAWA* pamoja na *TANAPA* wanafanya vizuri. Pamoja na changamoto kubwa tuliyonayo wanafanya vizuri wakiongozwa na Bi. Hadija, Mhifadhi Mkuu wa Kanda. Kwa kweli ni watu ambao ukiwapatia taarifa wanafanya kazi kwa wakati kwa maana wana-*act* kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba nifikishe salamu, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja Liwale moja ya changamoto alizopewa ni kuhusu kifuta machozi. Ni kweli tangu mwaka 2021 Liwale tulikuwa hatujapata kifuta machozi, lakini kilio hiki kimepata ufumbuzi baada ya mwezi uliopita. Watu takribani 2,496 wamepata kifuta machozi. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanavijiji walionituma nifikishe hizo salamu; Kijiji cha Ngumbu, Mirui, Ngunja, Mangirikiti, Mtawatawa, Mtawango, Nayuru, Kiangala, Kitogolo, Makinda, Ngorowele Nambinda Lilombe, Nanjegeja, Ngorowopa, Mihumo, Chimbuko, Kikuyungu, Kigwema, Namahonga, Nampigamiti, Namtungunyu. Hawa wote wamenipatia salamu wanashukuru, lakini kushukuru ni kuomba tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo limesababishwa na hao wanyamapori. Kuna dalili ya kuwepo kwa njaa kwenye vijiji hivi nilivyovitaja. Hili jambo ni mtambuka lipo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Liwale tuna janga la njaa. Miongoni mwa sababu za njaa kwenye vijiji hivi nilivyovitaja, ziadi ya vijiji 34 hapa nimetaja vichache tu ni kwa sababu ya hawa wanyamapori. Kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe vyakula kwa ajili ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye uhifadhi tunashukuru kwamba sisi kule ndiyo waathirika wakubwa wa wanyamapori kwa sababu tuna ile Hifadhi ya Nyerere, Selous, Msitu wa Hangai, Msitu wa Nyela - Kipelele; hii sehemu yote ni makazi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Waziri, nisikitike tu pale uliposema kwamba kuna ile *fence* ya umeme. Sikusikia ukitaja hifadhi hizi zote, hakuna hifadhi hata moja iliyotajwa kwamba itapata hii *fence* ya umeme kuzuia wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo vilevile ahadi ya Waziri aliyepita kwamba tutapewa vile vituo vitatu vya askari. Tukapata kituo kimoja cha Ngumbu, lakini bado tuliahidiwa kutakuwa na Kituo cha Lilombe na Kituo cha Ndapata. Ninaomba iwe kwenye kumbukumbu ya Mheshimiwa Waziri hivi vituo tuvipate, vitusaidie kuongeza idadi ya askari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninawashukuru wale Makamanda wetu pale Wilayani wanafanya vizuri, lakini wana changamoto kubwa ya usafiri. Unajua jiografia ya wilaya yetu imetawanyika sana, kwa hiyo gari lile walilonalo kama moja halitoshi. Kwa hiyo, suala la usafiri ni jambo la muhimu sana. Wanaweza wakapata lawama kwamba hawafiki kwenye matukio mapema, kumbe sababu ni usafiri na idadi yao vilevile ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule nina *WMA* yangu ya Magingo**.** Hapa napo ninaomba sheria tulishapitisha kwamba zile fedha za *WMA* ziende moja kwa moja kwenye jumuiya hii. Jambo hili halijatekelezwa. Miongoni mwa maombi yetu ni maombi ya hizi

fedha. Fedha za *WMA* zinachelewa kufika na zinapochelewa wale kule wahifadhi na wao wanashindwa kulipwa mafao yao. Wasipolipwa askari wale kwa wakati maana yake hawaendi ku-*patrol* kule hifadhini. Kwa hiyo, ili fedha zile zije mapema ziweze kusaidia uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule fedha za *Covid,* Hifadhi ya Mwalimu Nyerere walipata milioni 700 kwa ajili ya kutengeneza barabara ya ulinzi. Ninaomba sana hii barabara ya ulinzi ambayo imetajwa ndiyo barabara ambayo mimi siku zote nimeipigania ndiyo inatuunganisha na watu wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niombe kila ukiuliza watu hawa wa ujenzi wanakwambia mpaka waongee na watu wa Maliasili. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wafanye hayo mazungumzo yaishe ili ile barabara yetu ya Mkoa wa Lindi na Morogoro ipatikane pamoja na kwamba inapita hifadhini. Inaonekana kikwazo kikubwa ni kwa sababu tu inapita hifadhini, lakini zipo barabara nyingi tu zinapita kwenye hifadhi zetu mbalimbali kama vile Serengeti na Mikumi huko zipo barabara zinapita. Kwa nini hii Barabara ya Liwale – Morogoro ishindikane eti kwa sababu tu inapita hifadhini? Ninaomba jambo hili lifike mwisho wajadiliane, wakubaline ili barabara hii ya ulinzi iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, jambo lingine la *TFS,* nayo tunawashukuru kwamba wanafanya vizuri wanatulindia misitu yetu. Hapa ninaomba nichangie mchango mmoja waone namna *TFS* wanaweza kushiriki kwenye ile Biashara ya Hewa Ukaa kwa sababu miongoni mwa sisi halmashauri tumeshatenga baadhi ya misitu kwa ajili ya kuingiza kwenye hii Biashara ya Hewa Ukaa lakini misitu mingi inayomilikiwa na *TFS* pale Liwale kwa mfano, kama huo Msitu wa Nyela – Kipelele au Mahangai wameweka mabango mengi. Sasa, sijaelewa ushiriki wao kwenye hii Biashara ya Hewa Ukaa, *TFS* wana nafasi gani? Ushauri wangu hawa watu wangeweza kufika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, kuna hii Idara ya Malikale. Sisi pale Liwale ukizungumzia Vita vya Majimaji

lipo Jengo la Mjerumani lina ghorofa moja. Lile jengo lina historia kubwa sana na ukifika pale kwa wazee watakuelezea historia ya hili jengo. Mawe waliyojenga lile jengo ni matumbawe yanapatikana Kilwa kilomita zaidi ya 250, babu zetu walibeba na unaona na picha kabisa pale babu zetu wamebeba yale mawe kutoka Kilwa kwa ajili ya kwenda kujenga lile boma. Juzi nimeuliza swali hapa tukaambiwa kwamba kuna mazungumzo halmashauri na Idara ya Malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili hebu tuharakishe hili jambo ili nalo liwemo kwenye vivutio vya utalii. Kwa kweli kama tukiamua kweli kujikita kwenye kuibua utalii kwa Kanda ya Kusini. Kusini kuna vivutio vingi mno, lakini ni vivutio ambavyo vimelala kwa sababu vingi havijaibuliwa. Kwa hiyo, hapo mchango wangu ni kuhakikisha kwamba Idara ya Malikale, waende Liwale waangalie lile boma namna ya kutushauri nini tufanye ili boma lile nalo liingie kwenye urithi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu biashara yoyote ya utumwa ukiizungumzia kabla ya wale watumwa hawajafika Kinyonga ina maana walikuwa wanakusanywa pale Bomani Liwale. Wakishakusanywa pale wanabebeshwa wanapelekwa Kilwa kwenye Soko la Watumwa. Kwa hiyo, Biashara ya Utumwa na Vita ya Majimaji huwezi kuitenganisha na lile Boma la Mjerumani lililopo pale Liwale.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Joseph Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia.

Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya, tumeona mapato yameongezeka, hongera sana kwa Waziri pamoja na wataalam wake, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake. Hongera sana kwa kuifanya Wizara hii kuwa rafiki na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea Geita, ninaomba kuchangia. Geita ninayo hifadhi inaitwa Rubondo. Hii Hifadhi ya Rubondo ni ya kihistoria ipo katikati ya Ziwa. Umri wangu wote Makao Makuu ya hifadhi ile mlango wa kuingia ulikuwa upo sehemu moja inaitwa Nkome, wahifadhi wanafahamu. Kuna majengo, ofisi na kila kitu cha ku-*park boat* na kila kitu. Miaka miwili au mitatu iliyopita nyuma Wizara iliamua kuhamisha mlango wa kuingia kwenye hifadhi na kuupeleka Chato Muganza. Cha ajabu zaidi Mheshimiwa hifadhi hii inapiga kura kwenye Jimbo la Geita maana yake ipo Kata ya Jimbo la Geita haipo Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninachotaka kujiuliza ni kwa nini kilitokea hicho kitu watu wa Wizara wanafahamu, sitaki kupingana na maamuzi waliyoyafanya lakini ombi langu kwanza; tunachezea vitu vya Serikali. Pale tuna ofisi za kutosha kabisa, kila kitu kipo mpaka na magari, lakini vimekuwa vikichakaa baada ya kuhama watu wote kwenda Muganza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba vivutio vyote vya ile hifadhi vipo kilomita nne tu kutoka kwenye Mlango wa Nkome, lakini ukiingilia Muganza inabidi uzunguke zaidi ya kilometa 30 ndiyo uje ukutane na hivyo vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaomba Mheshimiwa Waziri anisaidie hatuna sababu ya kuufunga ule mlango na sina sababu ya kuufunga Mlango wa Muganza kusema mhame, hapana! Kwa sasa kwa sababu utalii umeongezeka na hilo eneo lipo kwenye Jimbo la Geita, ninaomba ule Mlango Mkuu wa zamani wa Nkome ufunguliwe. Kama kutakuwa na milango miwili sawa, sidhani kama Wizara inakosa wafanyakazi wawili au watatu wa kuanzia kurudisha ile heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawapatumii basi ninaomba sisi pale Nkome tuna upungufu wa Shule za Msingi. Ninaomba yale majengo na lile eneo basi Waziri aturudishie tuweze kugawa tuwapatie watoto waweze kukaa pale walau wapate kusoma kuliko kuteketeza yale majengo, hakuna mtu anafanyia kazi, watumishi wote wamehamishwa, *radio call* zipo pale hazifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana na hakuna sababu ya kutukwepa kwamba hakuna sifa ya kupita kule. *Hotels* nzuri za kitalii tumejenga tunazo wanaweza kulala barabara inapitika. Niombe sana watalii hawaji kuangalia lami, kinachowaleta ni kuangalia vitu vya asili ikiwemo na maisha halisi ya Wasukuma wanaokaa maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani warudishe ule mlango ili watu wangu wa Jimbo la Geita waweze kwenda kutalii, kuona watalii wanaenda wanapita Nkome maisha yanaendelea. Ninakushukuru sana Mheshimiwa kama hili atalizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nami ninatoka Mkoa wa Geita kuna shamba linaitwa Silayo lipo pale Bwanga. Mheshimiwa Waziri shamba hili lina historia na Silayo nimemwona yumo humu. Mgogoro wa shamba lile, eneo la hifadhi lilimwondoa Waziri, Mheshimiwa Vuai Nahodha, anafahamu wale waliopo kwenye hifadhi operesheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kile Kitongoji cha Nyakayondwa Kijiji cha Bwanga ni kikubwa Mheshimiwa Waziri kina watu karibu 40,000. Lile shamba hatuna tatizo nalo, watu wanalilinda vizuri miti ya Silayo imepandwa imeota vizuri shamba kubwa. Sasa, kadri wananchi wanavyoongezeka, sisi bahati moja mbaya ukienda kulia unaenda ziwani, ukija huku unakuja kwenye hifadhi. Sisi sifa yetu Wasukuma tunazaa sana na mtu anapozaa watu wanataka kujitegemea hamuwezi kurundikana kwa baba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kama itampendeza baada ya bajeti yake hebu

akatembelee hicho Kijiji kinaitwa Nyakayondwa Bwanga. Kumeenda operesheni, watu wanakata ng'ombe wa watu, wanachoma vyakula. Sasa, hii haiwezi kuwa sawa na haya mambo yote yanafanyika purukushani, tunajua kabisa tunaenda kwenye uchaguzi, halafu zinaanza operesheni za kwenda kufukuza watu, kukata ng'ombe wa watu na kunyang'anya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, ikimpendeza aende pale akakutane na wale wanakijiji, aone namna ya kuumaliza ule mgogoro, ili wananchi waendelee kulilinda lile Shamba la Silayo. Kwa kweli ni shamba la kihistoria, tunahitaji kulilinda, lakini na sisi tunahitaji kuona kwamba tunaongezeka tunahitaji kuongezwa maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Geita. Tumempelekea maombi Mheshimiwa Waziri ninadhani toka ameingia amekuta *documents* zipo mezani. Watu wa Geita kama ninavyosema sisi tuna bahati kubwa sana ya kuzaa na miji yetu inakua, tunaongezeka. Ukifika Geita Mjini katikati ya mji kulia ni Ofisi za Mkuu wa Mkoa, kushoto kuna Hifadhi inaitwa Usindagwe eneo ambalo lipo mjini huhifadhi chochote hata fisi hawezi kukaa mle, ni vichaka tu vinafuga vibaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishamwomba muda mrefu atupatie baraka tuanze kujenga, watu wapime tupate viwanja. Katikati ya mji utahifadhi kitu gani? Sana sana tunahifadhi vibaka na mambo mengine. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili suala la Usindagwe limechukua muda mrefu sana. Ninajua mwenye maamuzi ni Waziri, akitamka hata leo watu wapo tayari kuanza kugawa viwanja pale tujenge, ili na sisi miji yetu ifanane na miji mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na miji inayoonyesha ghorofa halafu kulia inaonyesha vichaka vya vibaka. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri alichukulie hili suala kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninampongeza Mheshimiwa Rais: Mheshimiwa Rais, wakati anafanya Filamu ya *Royal Tour* Watanzania wengi tulisikia maneno yaliyopita. Ikifika hapo ninaanza kuona faida ya shule, tunahitaji mawazo mapya na ubunifu. Hakuna mtu alitegemea, sisi watu wenye akili tulinyamaza, tukijua tusubiri tuone wazo litakapofikia mwisho, lakini watu waliponda; Rais anaenda ku-*act* filamu, anafaya kazi za wasanii. Leo hii tunaona faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hata Arusha kwa Mheshimiwa Gambo kumetulia kwa sababu ya *Royal Tour* ya Mama Samia. Huu utalii tunaojisifu leo tumeongeza mapato ni sababu ya ubunifu wa Rais wetu alioufanya kutengeneza filamu ya *Royal Tour*. Kwa hiyo, ninawaomba Watanzania, watu wazuri wanapokuja na mawazo mazuri, mawazo mapya, tusikatishane tamaa, tuunganane mkono, tumeona faida kwenye *royal tour*, tunamwomba Mama asikate tamaa, aendelee kuleta mawazo mapya na sehemu zingine ili tuweze kupata matunda zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Nilishamwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nianze kwa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake mengi kwenye hii sekta na yana tija kubwa. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yao yote ya Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba na uwasilishaji mzuri ambao umeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika maeneo mawili. Eneo la kwanza, umuhimu wa jumuiya za hifadhi zinazoshirikisha wananchi kuanzishwa katika maeneo mengi. Kwangu kule

Sikonge kwa kweli kuna matatizo makubwa sana ya uhifadhi. Watumishi wa *TAWA* na *TFS* ni wachache mno kuweza kudhibiti maeneo waliyokabidhiwa. Kwa mfano, *TFS* Sikonge inatakiwa ihifadhi misitu minne. Msitu wa Itulu, Iswangala, Inyonga na Nyahua, ambapo maeneo yote haya yana kilometa za mraba 14,712 au hekta 1,479,208, eneo hilo ni kubwa sana, lakini watumishi ambao wameajiriwa na Serikali wako chini ya *TFS*, wako 17 tu na wengine 10 ni watumishi wa mikataba ya muda mfupi mfupi. Hivi hawa watu 27 ndiyo wanaweza wakadhibiti eneo lote hilo? Jibu ni kwamba haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge nayo ina misitu mitano ya hifadhi; Ipembampazi, Ugunda, Wala, Sikonge, na Goweko. Jumla ya kilometa za mraba 5,175 au hekta 517,560. Halmashauri nayo ina watumishi 17 tu wa Maliasili, kati ya hawa, watatu tu ndiyo Maafisa Wanyamapori. Hivi unategemea hawa watumishi wachache namna hiyo ndiyo wadhibiti eneo lote hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaishauri Wizara ianzishe jumuiya za hifadhi kwenye Kata za Kitunda na Kiloli, jumuiya moja; Kata za Kipili na Kilumbi jumuiya ya pili; na Kata za Nyahua, Igigwa, Kisanga mpaka Kiloleli nao wawe na jumuiya moja kubwa. Hizi jumuiya tatu ndiyo zitawasaidia hawa Maafisa wa Serikali Kuu, *TAWA* na *TFS*, pamoja na Maafisa wa Halmashauri kuweza kudhibiti na kutunza vizuri hizo hifadhi, vinginevyo *encroachment* ya wananchi itaendelea na hakutakuwa na udhibiti mzuri kwa sababu ya eneo kuwa kubwa na watumishi wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *encroachment* hii inaharibu mpaka mazalia ya nyuki na inaathiri mpaka Sekta ya Asali na Nta. Kwa hiyo, ninashauri Wizara ishirikiane na halmashauri kuanzisha hizi jumuiya za wananchi. Tunayo jumuiya moja kwenye *Game Reserve* ile ya Ipole, hiyo jumuiya moja ndiyo inasaidia hifadhi angalau kidogo, lakini kwingine kote kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo la pili, tunao Mradi wetu wa Umwagiliaji wa Uluwa, huu ni mradi ambao

ulianzishwa na Mwalimu Nyerere mwenyewe. Mwaka 1972 Mwalimu Nyerere alikuja na Sera ya Siasa ni Kilimo ambayo ilikuwa ni sera rasmi ya *TANU*. Mwaka 1975 zilipatikana fedha za kuchimba mabwawa 1,000, miongoni mwa mabwawa 1,000 yaliyochimbwa ni Bwawa la Uluwa kule Kiloleli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hili bwawa kuchimbwa likakamilika, mwaka 1977 Mwalimu Nyerere mwenyewe ndiye alikuja akalizindua hili bwawa. Siku ya kuzindua hilo bwawa akatoa hotuba akisema Wizara ya Kilimo ikamilishe miundombinu ili wananchi waanze Kilimo cha Umwagiliaji wa Mashamba. Sasa, kilichotokea kwa nini hayakujengwa mwaka 1978? Fedha zote zilielekezwa kwenye vita baada ya kuzuka Vita ya Uganda, ndiyo maana mradi ule haukujengwa wakati wa Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mradi ulikuja kuanza kujengwa mwaka 2007/2008, baada ya Wizara ya Kilimo kukumbuka maagizo ya Mheshimiwa Rais Nyerere kipindi kile, wamejenga mradi ule umekamilika....

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha au ni kengele ya kwanza?

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aah bado bado!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili bwawa limejengwa na miundombinu ikakamilika, wakati wanajiandaa kwa uzinduzi wa mradi tarehe 27 Januari, 2010 ilikuwa mradi uzinduliwe mwezi Februari, 2010, akaja Afisa Maliasili akatoa katazo la kuzuia. Hii Hifadhi ya Ipembampazi ni hifadhi ya Halmashauri, lakini sasa kwa nini Afisa Maliasili wa kutoka Wizarani amekuja akazuia ule mradi na mpaka leo haujawahi kufanya kazi? Serikali ndiyo iliwekeza na Serikali ndiyo imezuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kwa sababu Afisa Maliasili yule alisema ipatikane ridhaa ya Waziri wa Maliasili na

tumemfuatilia sana. Waziri Maige alikuja akatembelea pale akasema hakuna tatizo lolote, akaja Naibu Waziri Mheshimiwa *Eng*. Dkt. Ramo Makani akatembelea pale akasema hakuna tatizo. Akaja Waziri Mheshimiwa Profesa Magembe mwenyewe akafika pale akasema hakuna tatizo, akaja Waziri Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla akasema hakuna tatizo, tatizo ni kwamba, barua tu ya idhini ya Waziri ndiyo haijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba leo Mheshimiwa Waziri atoe tamko la kuruhusu. Pale kinachochukuliwa ni hekta 550 tu, wakati mbuga yenyewe ya Ipembampazi ina hekta 133,000. Hebu angalia ukubwa wa mbuga hekta 133,000 na hawa wakulima watafaidika na hekta 550 tu. Kwa nini Wizara imekataa kuruhusu mradi huu kwa miaka yote hii; ambao ni mradi unaomuenzi Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, ninaomba Waziri atoe ufafanuzi wa kueleweka, vinginevyo tusije tukafika mpaka tunashika shilingi wakati wa kupitisha mafungu ndiyo tueleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda. Nilishamwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu; pili, ninawashukuru wapigakura wa Urambo pamoja na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa; na tatu, kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu, kwa miradi mikubwa aliyotupa Urambo, lakini kwa sababu ya muda sitapata nafasi ya kuitaja yote. Ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Wizara, Waziri Mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mheshimiwa Dunstan kitandula, Katibu Mkuu Dkt. Abbas na wengine wote walioko ndani ya Wizara hiyo, Idara zote zinafanya kazi vizuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilikuwa ninapita nikitoka kwangu, nikapita pale Chinangali *Park* nikaona kaulimbiu nzuri sana, ninawapongeza Wizara ya Maliasili na Utalii. Inasema, "Nyuki ni Uhai na Uchumi Imara, Tuwahifadhi". Nilikuwa nimepanga kuja kuchangia, kwa kweli hiyo kaulimbiu imenifurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, nyuki ni kwa uhai, uchumi imara, tuwahifadhi na ndicho ninachokizungumzia leo kwa niaba ya wananchi wa Urambo, hususan Kata Nne ambazo zimo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla. Ninaomba niliweke wazi ndani ya Bunge hili kwamba, sisi kama wananchi wa Urambo tunaheshimu sana Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla. Tunajua madhumuni yake kwa faida ya sasa na ya baadaye. Kwa hiyo, tunaunga mkono, tatizo letu sisi ni hilo moja tu ambalo linatokana na kaulimbiu hii hapa, kwamba nyuki ni uhai, hata ukisema nyuki kwa uhai na uchumi imara, tuwahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghafla tu tulisikia kwamba Serikali imegeuza sasa eneo lote lile la pale kwetu Urambo, ambalo ndani yake kuna Kata Nne ambazo ni Nsenda, Ukondamoyo, Kasisi na Ugalla. Ghafla limeshageuzwa lile umekuwa Msitu wa Hifadhi ya Taifa. Kimsingi wazo ni zuri, tatizo lilitokea tu kwamba, wazo zuri, lakini lilifikishwa kwa utaratibu usioeleweka, tulishtukia tu ghafla kwamba sasa wananchi hawawezi kuingia hapa kwa sababu tayari imeshakuwa Hifadhi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, kitu kikubwa ambacho kilikosekana pale ni elimu kwa wananchi, kwamba maana ya Hifadhi ya Taifa ni nini? Wao watabaki na nini? Kitu gani watakuwa nacho, kitu gani watakosa, hapo ndiyo palipokosewa, elimu na ushirikishwaji wa wananchi. Wazo lilikuwa zuri, lakini utaratibu uliotumika ndiyo ninasema Mheshimiwa ulitakiwa ufanyie kazi vizuri kwa kuwaandaa wananchi waliomo mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo Kata Nne zina maeneo mengi ambayo ninapenda niyataje ili wajue kwamba kwa kweli maeneo mengi sana yameguswa. Kuna eneo la Kangeme, Lunyeta

yenyewe, Kangeme, Mpola, Mtakuja, Magimagi, Holongo, Itewe na Msumbiji. Ni maeneo mengi ambayo yameguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiria kwamba, kwa sababu tunatambua kwamba ni muhimu kuwa na Hifadhi ya Taifa, lakini wakati huo huo tunaamini kwamba kuna umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi, ninaomba nilete maombi manne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la kwanza, bado Wizara ya Maliasili na Utalii iandae utaratibu wa kukusanya hawa watu wanaohusika, wawe na kikao chao ili waone kweli Serikali inawathamini lakini wakati huo iwaelezee maana ya hifadhi na wao watabaki na nini na kitu gani kitakwenda kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosikia nilivyosema kaulimbiu, nyuki ni uhai. Kwanza asali yenyewe ni dawa, ni chakula, lakini ni uchumi imara tuwahifadhi, kwa miaka yote maeneo haya yalikuwa yanafuga nyuki. Ombi letu la pili, baada ya kuwashirikisha na kuwapa elimu, ombi letu la pili tugawiwe eneo hili angalau kilometa tano ili wananchi waendeleze huu uchumi imara wa asali ambao pia ni chakula, kwa hiyo, tunaomba angalau kilomita tano za eneo lile, Serikali itufikirie waturudishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaomba hapa hapa Bungeni, tunaomba tu tuikumbushe Wizara kwa nia nzuri tu, kwa kuwa waliamini na wao maneno yetu kwamba ni uchumi imara, wakaahidi huu humu Bungeni kupata mashine ya kuchenjua asali, tunaomba na sisi tuchenjue. Baada ya kupata mizinga, tufuge nyuki, tuchenjue asali ili na sisi tuuze asali kutoka Urambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika haya maombi yangu makubwa manne, eneo la Lunyeta kuna lango ambalo lilikuwepo zamani tunaomba walifufue, kwa sababu kuna mindombinu ya umeme kuna miundombinu ya simu, kwa hiyo tunaomba nasi Urambo tuwe na lango ambalo watalii watapita

huko kwa sababu eneo ni kubwa, kuna wanyama na kadhalika, tunaomba Serikali yetu na sisi ituwekee lango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, Serikali yetu ni sikivu, Wizara Watendaji wazuri, ninaamini kabisa leo tutapata majibu mazuri ili na sisi wa Urambo tupate asali kwa ajili ya uhai, hatimaye uchumi imara na maendeleo oyeee! *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: *Oyee!*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simwanza Sitta. Nilimwita Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi jioni hii kuchangia juu ya hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ziara aliyoifanya Tunduru akishirikiana na Waziri Maliasili na Utalii, kwa maelekezo yake sasa angalau vurugu ya tembo imepungua kwa asilimia kubwa. Tunashukuru tumepata *VGS* 28 katika maeneo ya *TAWA*, *TANAPA*, pamoja na *TFS*, lakini tumeletea Ndege Nyuki wawili wanaosaidia kufukuza tembo, vilevile tumepata kituo kimoja cha kudumu na vituo viwili vya muda katika Kijiji cha Mbesa na kule Matemanga ambavyo vinasaidia kuwafukuza tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo kubwa tunaomba sana tusaidiwe kuongeza Askari, Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla tuna hifadhi nyingi na tembo wanasumbua kutoka Selous, wanasumbua kutoka Msumbiji, *at least* kila Tarafa ingepata *camp* moja kwa ajili ya kufukuzia tembo ingetusaidia sana, hasa Tarafa ya Nalasi, Tarafa ya Lukumbule na Tarafa ya Namasakata, ingeweza kutusaidia kufukuza hawa wanyama wakali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika Hifadhi yetu ya Mwambesi, ni ya muda refu sana, ni hifadhi ya kijamii.

Mwanzo lilikuwa ni eneo la uwindaji, lakini sasa hivi limebaki kama hifadhi na hifadhi ile imekaribiana sana na wananchi wa vijiji 12 katika Tarafa ya Namasakata na Tarafa ya Lukumbule. Ni muda mrefu sana wananchi wa Vijiji vya Mchesi, Jiungeni, Kazamoyo, Imani, Angalia, Mwenge, pamoja na vijiji vingine 12 waliomba kupata maeneo ya kulima kutokana na idadi kubwa ya wananchi walioongezeka ili wapate namna ya kujikimu kwa njia ya kilimo. Kwa hiyo, tunaomba sana tufikiriwe mpango huu wa Mwambesi kugawa sehemu angalau watu wetu wapate maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niongelee kuhusu *TAWA*. Nimesikiliza hotuba ya Mwenyekiti katika mapendekezo aliyoyatoa ya kufanya *retention* ya pesa ya makusanyo yao, ninawaona *TAWA* wamesahaulika, lakini hawakusahaulika kwa bahati mbaya, *TAWA* tangu miaka ya nyuma kama sijasahau kwa sababu kipindi hiki si kipindi cha kumbukumbu sana. Ninakumbuka Kamati ilipendekeza iletwe sheria ya kuifanya *TAWA* iwe *independent entity* kama ilivyo *TANAPA* pamoja na Ngorongoro ili kuifanya *TAWA* iwe taasisi inayojitegemea na bodi yake iwe na mamlaka halisi ya kufanya maamuzi badala ya kushauri, mpaka kusubiri Mkurugenzi wa Wanyamapori apitishe *then* waende kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli *TAWA* wana matatizo mengi sana, moja ya matatizo ni eneo lao la *operation* ni kubwa ukilinganisha na Ngorongoro, ukilinganisha na *TANAPA*. Wanyama wote wakitoka *TANAPA*, wakitoka Ngorongoro, nje ya maeneo ya mipaka yao wanakuwa wanamilikiwa na *TAWA*. Kwa hiyo, *TAWA* nchi nzima hii wana maeneo makubwa ya *operation* kuliko *TANAPA* ilivyo na hawa wenzetu wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza wanatakiwa wafikiriwe kuwa taasisi kamili, jambo la pili waongezewe mishahara. Katika taasisi za hifadhi hawa watu wa *TAWA* ndiyo dhalili wana mshahara mdogo kuliko *TANAPA*, kuliko Ngorongoro. Kwa hiyo, hata *TFS* nao wamewazidi mishahara wakati wote wanaajiriwa katika mtindo mmoja, wote ni Askari USU ambao wanapaswa wale walioko kwenye *rank* moja, basi

wapate mshahara kulingana na wenzao pia kazi kubwa ya uhifadhi ya kutunza wanyamapori wanao hawa *TAWA*. Kwa hiyo, ninaomba jambo hili la kisheria lifanyiwe kazi ili mapungufu haya ya mshahara na *operation* yaweze kufanya *TAWA* ifanye kama wanavyofanya wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto za *TAWA*, kwa Jimbo letu la Tunduru Kusini kwa kweli ninawashukuru *TAWA*, kwa sababu ndiyo wanaosaidiana na Halmashauri yetu kwa asilimia kubwa kufukuza wanyama wakali ambao wanasumbua wananchi wetu. Juzi tu hapa Jumamosi kutokana na matumizi ya Ndege Nyuki, tembo walikimbia wakamwacha mtoto, mtoto yule akabaki anahangaika kwenda huku na kule, bahati nzuri akakutana na watu wakamfunga kamba tembo mtoto wakaondoka naye mpaka kijijini, kitu ambacho ni hatari, lakini watu wa *TAWA* wakamchukua yule tembo mtoto wakamrudisha kwenye hifahdi. Hili jambo linafanyika kwa sababu wale wako karibu, sasa, wakiwepo *VGS* kila eneo, itatusadia changamoto kama hizi kuzitatua kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninadhani ni suala la malipo ya fidia au kifuta jasho. Katikati hapa mlianzisha mtindo wa kutumiwa kwa mtandao. Kidogo lile jambo lilikuwa linaenda vizuri, lakini linachelewesha, wameamua kurudi kwenye mfumo ule wa zamani wa *manual*. Jambo hili linachelewesha malipo ya wananchi wetu, lakini kipekee ninaishukuru Serikali kuongeza kiwango cha kulipa kifuta jasho, kutoka shilingi laki moja mpaka shilingi laki mbili kwa hekta na mtu yeyote aliyeathirika kutokana na ukubwa wa shamba basi afanyiwe hesabu kulingana na ukubwa wa shamba kuliko ilivyokuwa zamani kwamba chini ya heka moja Serikali ilikuwa haiwezi kulipa fidia ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru tena kwa ile fidia ya wale ambao wameuawa na wanyama wakali au kudhurika, kwa malipo ya shilingi milioni mbili ingawa hayalingani na uhai wa binadamu, *at least* itaendelea kufuta jasho kwa hawa ndugu zetu ambao wanaathirika na hao wanyama wakali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninawashukuru Serikali wameona umuhimu wa kuondoa baadhi ya tozo ambazo zilikuwa zinazuia kuendeleza au wananchi wazawa kufanya shughuli za uwekezaji katika utalii. Ninaipongeza sana Serikali kuhusu jambo hili ninaomba lisiishie hapo, waangalie hata yale maeneo ambayo sisi wadogo tunaoanza kwenye Sekta ya Utalii wapunguze zaidi ili kuvutia Watanzania washiriki katika suala la utalii wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Daimu Mpakate.

Nilimwita Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ajiandae. *(Makofi)*

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na uzima, kuweza kusimama katika Bunge hili Tukufu, katika bajeti hii ya Maliasili ambayo ni ya mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili12 na mimi kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara watuambie, maana nilikuwa ninajaribu kupitia hotuba yao. Tangu baada ya *Royal Tour* sijaona Wizara ikija na mkakati wowote wa kuendeleza utalii. Baada ya *Royal Tour* sijaona jambo lolote jipya lenye kuvutia ambalo litatufanya tuondoke kwenye *Royal Tour* tuje tuingie kwenye jambo hilo lingine ambalo litavutia hata watalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mapungufu makubwa sana kwa Wizara ambayo tayari ilikuwa imewekwa juu kabisa na Mheshimiwa Rais, katika suala zima la kutangaza utalii wetu. Sasa kama wao wenyewe bado wanasubiri tena mbeleko ya namna

hiyo, sidhani kama tutafika tunapotakiwa kufika kwa sababu lazima tuongeze mapato kupitia utalii wetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tunasema, Tanzania kwa masuala ya utalii vivutio vyetu ni vingi kweli kweli, lakini bado Wizara haijafanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba kwenye eneo hili tunapata fedha za kutosha kupitia utalii wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nikumbushe hilo ili wenzetu hawa tuwaamshe kwamba jamani, sasa *Royal Tour, Royal Tour, Royal Tour* tena sasa hatuwezi kuendelea nayo miaka yote. Tutaisema ilikuwepo na imefanya vizuri kwelikweli kuliko kipindi kingine chochote, lakini mje sasa na mkakati mwingine au jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nilikuwa ninajaribu kupitia hapa. Leo Tanzania na sisi ni sehemu ya watu ambao tutakuwa wenyeji wa mashindano ya *AFCON* na *CHAN* lakini Wizara ya Maliasili mpaka sasa mbona hatuoni nini ambacho wanataka kufanya katika masuala mazima ya ku-*promote* utalii wetu nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda wenzetu hawajui ama kwa sababu tumezoea mambo ya zima moto, tunataka sasa tuanze tena yale mambo yetu ya *last minutes* ndio tunaanza kukurupuka, tunaanza kufanya aje, tunaanza kuchezea hela tu bila sababu zozote. Twende polepole wakati tukielekea kwenye mashindano hayo ili tuweze kuutangaza utalii wetu sawasawa na utalii huu utaweza kutuingizia kipato kikubwa kuliko hata hiki ambacho tunakipata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wetu wa Tabora ni mkoa ambao una mapori mengi sana. Eneo ni kubwa la Tabora na Tabora ndio mkoa mkubwa nchini. Nchi hii ya Tanzania, Mkoa wa Tabora ndio mkoa mkubwa ambao una eneo kubwa, lakini eneo kubwa la mkoa wetu ni pori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba wakati ule Kamati ya Mawaziri Nane inapita, tukasema tusaidiwe, watu wetu wameongezeka. Leo kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022, sisi ni wa tatu kwa wingi wa watu katika nchi hii. Kutokana na hilo tusaidike basi kwenye maeneo yetu mbalimbali tuweze kuongezewa maeneo ya watu wetu kuishi na kufanya shughuli zao za kila siku na hii itapunguza migogoro ya hifadhi na wananchi kwenye hayo maeneo ambayo yapo karibu na mapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona muda sio rafiki sana, lakini pamoja na kuwa tuna ukubwa wa mapori haya, lakini bado hata askari wetu wanaolinda mapori haya: moja; ni wachache na hawatoshi, pili; askari hawa wa *TAWA* bado hata vipato vyao haviridhishi. Hili jambo ninalirudia tena, ninasema; kwa nini kunakuwa na matabaka? Nawauliza Maliasili na Utalii kwa nini kunakuwa na matabaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani haya majukumu hawayaoni ama hawayajui, kwamba hawa watu wanafanya kazi ya aina moja? Wanaolinda mapori na wanaolinda hifadhi, hawa wanafanya kazi ya aina moja, hawana kazi tofauti. Kwa hiyo ni lazima waangalie uwezekano wa kuweza kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho lakini sio kwa umuhimu, ni kuhusu huu Mfuko wa Maendeleo ya Utalii. Nilikuwa ninajaribu kupitia baadhi ya viambatanisho, lakini ninaomba niseme jambo dogo kwa Wizara na huu ni ushauri. Baada ya kupitia hii na haya ambayo nimekutana nayo hapa, ninaomba nishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii waunde chombo maalum ambacho kitasaidia kudhibiti matumizi ya fedha hizi; kwa sababu gani ninasema hivi? Sisi Wabunge nami nikiwa miongoni mwao, tulipambana kuiomba Serikali iweze kusaidia zipatikane fedha ili tuweze kusaidia hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema hapa *TANAPA* imeongezewa hifadhi, kutoka zilizokuwepo zikaongezeka zaidi. Hawa wenye hifadhi zilizoongezeka hawana uwezo wa kujiendesha. Kwa hiyo, kukiwa na fedha ambayo itasaidia wataweza kufanya zile hifadhi nyingine zianze kufanya kazi zao bila kutegemea watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe na nimwambie Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii, unda chombo maalum. Wakati tutakapokuja kwenye bajeti ijayo, maana tutakuwepo wote *(Inshallah, Inshallah* tutakuwepo wote humu ndani *Inshallah)*, tukute hiki chombo kimeundwa ili muweze kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha hizi. Hizi fedha ni nyingi na zinakwenda bila utaratibu. Hili jambo si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKIT: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa. Nilishamwita Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ambaye pia atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu ambaye kupitia *Royal Tour* ameweza kuhakikisha kwamba ameongeza idadi ya watalii nchini, lakini pia pato limeongezeka kupitia utalii kutokana na Mheshimiwa Waziri alipotusomea hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya kusimamia Wizara hii. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi

nzuri anayoifanya katika Wizara hii, Katibu Mkuu Dkt. Abbas na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza Serikali kuhusu na Mradi wa *REGROW*. Kwanza, ujenzi wa barabara ile ya Msembe, inayokwenda *Ruaha National Park;* tunashukuru sana. Pia, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Iringa tunajua kwamba sasa utalii utakwenda kwa kasi kubwa lakini pia na ujenzi wa jengo la *TAWIRI* katika kituo cha Kihesa Kilolo, mimi nawapa maua yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, majengo mengine wanakamilisha lini? *TTB, TFS, ISCC* na Chuo cha Utalii cha Taifa lini sasa majengo yao wanakuja kuyajenga pale eneo la Kihesa Kilolo ili huu Utalii sasa hii *REGROW* iweze kwenda vizuri? Tutaomba majibu watakapokuwa wanajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni elimu kiasi gani sasa wananchi wa Iringa au wa Nyanda za Juu Kusini wameweza kupata katika kuendeleza huu utalii ili pia waweze kujiajiri kupitia utalii? Kwa sababu mradi huu wa zaidi ya shilingi bilioni 23 ninafikiri ulitakiwa uishie Januari 25 mwaka huu, sasa tupo mwezi wa tano; je, ukiisha huu mradi tutapatiwa mradi mwingine kwa ajili ya kuendeleza utalii Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee kuhusu maonesho ya utalii Kusini. Tunatambua kuwa Mkoa wa Iringa ni kitovu cha utalii kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Songwe, Katavi, Morogoro, Lindi na Mtwara. Mwaka 2019 Wizara ikishirikiana na mikoa hii ilianzisha Maonesho pale katika eneo la Kihesa Kilolo na kumpatia heshima Spika, wetu Dkt. Tulia Ackson, ambaye alikuwa ndiye mgeni rasmi na Maonesho hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wananchi 58 elfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niwaulize maswali yafuatayo: je, ni kwa nini Wizara imeiachia mikoa wakati ikijua bajeti yao haiwezi kukidhi maonesho hayo ya kitalii ya kimataifa, kwa sababu wao wanatumia OC tu kwa ajili ya maonesho hayo?

Je, kwa nini Wizara isichukue jukumu la kusimamia maonesho hayo kama ilivyofanya mwaka 2019 wakati huo najua Katibu Mkuu alikuwa Profesa Mkenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je kwa nini Bodi ya Utalii wasiratibu maonesho hayo ili hadhi ya kimataifa iweze kudumishwa na kurahisisha kuunganishwa Mikoa ya Kusini kuendeleza utalii wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba nishauri kwamba, Wizara iyasajili hayo maonesho kama yalivyo *CTITE* ili iyape kipaumbele kuyasimamia ili Nyanda za Juu Kusini tuweze kufanya vizuri kupitia utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee kuhusu wanyamapori waharibifu. Hili tatizo la wanyamapori hasa tembo na mamba kwa kweli katika Mkoa wetu wa Iringa wananchi wanateseka sana. Kuna baadhi ya maeneo kama Mahenge, Magana, Msosa, Ikula, Udekwa, Utalisoli katika Wilaya ya Kilolo wananchi wanateseka mno. Mashamba yao yanaliwa, wameuawa na kuna watu karibu sita wameshapoteza maisha kwenye Kijiji cha Msosa na Kijiji cha Mtandika, lakini hawa wote bado hawajaweza kupata hata kifuta jasho wala kifuta machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali juzi kwamba hawa wananchi walioharibiwa mashamba yao bado hawajalipwa kutoka mwaka 2020 mpaka 2025 na majina yao nimeomba wameshaniletea ninayo hapa na leo baada ya kuchangia nitakukabidhi ili wananchi hawa waweze kulipwa kifuta jasho na kifuta machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika maeneo mengine ya Idodi, Pawaga, Izazi na Migoli - Iringa vijijini na kwenyewe watu wanapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilikuwa na mpango wa kuanzisha hizi *WMA* lakini ule mpango ukoje? Ninataka tujue kwamba, tulijua kwamba hizi jumuiya ndio zitasaidia uharibifu

ambao unajitokeza lakini na ulinzi wa hawa wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuuliza pia; hifadhi ya Udzungwa 75% ipo katika Milima ya Udzungwa katika Wilaya ya Kilolo na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo wanaitwa Wazungwa lakini hii hifadhi inatajwa kutokea Morogoro. Sasa ninataka nijue; je, wananchi wa eneo hilo na halmashauri zinafaidikaje, zinapata nini kutokana na kuwepo 75% katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niombe sasa Wizara ijaribu kuangalia Nyanda za Juu Kusini tuna vivutio vingi sana ambavyo bado havina matangazo, havitangazwi kiasi cha kutosha. Mheshimiwa Sanga amesema, lakini pia miundombinu ya kwenda kwenye hivyo vivutio wala sio vizuri. Kwa hiyo tunaomba Nyanda za Juu Kusini ukiwepo Mkoa wa Iringa sasa iangaliwe kwa ukaribu ili pia wananchi waweze kujiajiri kupitia utalii na vilevile tuweze kupata pesa nyingi kupitia utalii wa Nyanda za Juu Kusini ili na sisi tuchangie pato kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaomba sasa Mkurugenzi wa Utalii au Waziri au Katibu au Naibu Waziri hebu waje watembelee Kihesa Kilolo, Kihesa Mgagao - Kata ya Ng'uruhe Wilaya ya Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa nimeelezea hapa kwamba kule kuna eneo zuri sana waliishi wale wapigania uhuru wakimbizi, ambapo katika eneo hilo kuna vyumba ambavyo waliishi maraisi. Lile eneo, kuna ambalo waliishi watu wa *South Africa*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kengele ya pili ilikuwa umalizie.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba waje waangalie kuna utalii mkubwa na

wenzetu Gereza alilolala Nelson Mandela, limekuwa utalii mkubwa na wanaingiza pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKIT: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao wapo ndani ya ukumbi wa Bunge, hawa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, (Mbunge), hawa ni wanafunzi 120 na walimu wanne wa Shule ya Sekondari ya Kiislamu Vuchama Ugweno kutoka Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro. Hebu tuwaone, simameni tuwaone, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile, tuna wageni wengine ambao wametembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 71 na walimu 11 wa Shule ya Awali na Msingi Rahma kutoka Jijini Dodoma, hebu tuwaone mlipo, karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na michango na kabla ya mchangiaji wa mwisho nilikuwa nimemwita mchangiaji mwingine (Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane), ningeomba achangie sasa halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Kisau, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kufanya kazi kubwa kupitia sinema ya *Royal Tour* na *Amazing Tanzania* ambayo imeweza kuchechemua Sekta hii ya Utalii na kuongeza mapato maradufu na idadi ya watalii maradufu katika nchi yetu (watalii wa ndani na wa nje).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Wizara nzima ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa wanayoifanya, sambamba na taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wilaya ya Kilwa tuna sehemu kubwa ya mafanikio ambayo yamepatikana. Tumepata *GN* Na. 163 na 166 zilizotambua mnara wa mashujaa wa Majimaji pamoja na mapango ya Nang'oma na Namaingo. Pia, tuliweza kuletewa boti ya kitalii pale Wilayani Kilwa Masoko ambayo imetumika kuongeza idadi kubwa ya watalii maradufu ya ilivyokuwa hapo kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru pia juhudi zimefanywa na taasisi ya *TAWA* katika kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi wetu. Wananchi wetu zaidi ya 2,000 wamepewa elimu ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa Sekta ya Utalii imepanda kiwango cha uchangiaji baada ya kuwa mapato mengi yamepatikana hadi kufikia 21%. Ni imani yangu kuna mambo ambayo ninakwenda kuishauri sasa Serikali, ikiyatekeleza nina hakika tutapandisha sehemu ya pato la Taifa kufikia hadi 40% mpaka 50% kutokana na vivutio vya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni katika maeneo yafuatayo kwenye Kumbukizi za Majimaji sambamba na yale mapango yaliyopo Kilwa, ninashauri *GN* itolewe na uwekezaji ufanyike katika mapango 17 yaliyopo sambamba na yale matatu, ambayo tayari yametolewa *GN* Namba 163. Ninaomba pia, Serikali itekeleze ahadi na mkakati wake wa kujenga Nyumba ya Makumbusho, Nandete, ambayo inahusiana na Vita vya Majimaji, lakini pia, iweze kujenga ngazi kushuka kwenye pango kubwa kuliko yote la Nang'oma, ambalo limepewa *GN* Namba 163. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali yetu, kupitia Wizara hii ya Maliasili na Utalii, imeweza kuanza kutoa tuzo. Sisi Wanakilwa tulianza kutoa tuzo tangu Majimaji iliyopita,

tulipotimiza miaka 119. Tulimtunukia Mheshimiwa Zakia Meghji, kama ambavyo mmefanya kwa sababu, yeye ndiye alikuwa Waziri wa kwanza wa Utalii kuingia katika pango kubwa kuliko yote la Nang'oma, mwaka 2001. Pia, tulitoa kwa Mashujaa wengine wa Majimaji na Waziri Mstaafu wa Utalii, dada yangu, Mheshimiwa Angellah Kairuki. Kwa hiyo, tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri katika maadhimisho ya mwaka 2025 naye tuje tumpe tuzo yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nitoe ushauri kwa Serikali, pia, kule kuliko na Boma la Wajerumani, Kibata, kutolewe *GN* kuliko kuwa na shamba la pamba, pale Kikwetu. *Ginnery* ya pamba ilikuwepo pale enzi za Wajerumani, nako kutolewe *GN*. Kuna *GN* katika Mlima Imbiliya ambao mtu wa kwanza katika Vita vya Majimaji aliuawa pale, ninaomba pia *GN* itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia, kuzungumzia yale ambayo wamezungumza wenzangu kuhusiana na kadhia ya wanyama aina ya ndovu. Mheshimiwa Waziri, tuna vijiji zaidi ya 12 katika Wilaya ya Kilwa, ambavyo vinakumbwa mara kwa mara na vingine kila siku kila kukicha. Hivi, ninapozungumza muda huu, tayari kuna vijiji tembo wameshaingia toka alfajiri; kuna Kijiji cha Zinga Kibaoni, Mitole, Mtepera, Kikole, Ruhatwe, Nakiu, Mkarango, Kandawale, Ngarambi, Namatewa, Kipindimbi na Kisimamkika. Hivi vijiji watu wetu wamekuwa wakisumbuliwa sana na wanyama wakali na wasumbufu aina ya ndovu, ambao kila kukicha wamekuwa wakivamia katika hivyo vijiji. *(Makofi)*

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Ngassa.

TAARIFA

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Ninapenda kumpa Taarifa Mheshimiwa Ndulane, hata sisi pale Igunga, Maeneo ya Itumba, Mtunguru, kule tumekuwa tukisumbuliwa na tembo mara kwa mara na

kusababisha maafa kwa wananchi, lakini tumeshatoa Taarifa Wizarani. Kwa hiyo, tunaona pia, na sisi tusaidiwe maeneo ya Mtunguru na Itumba. Ninampa Taarifa hiyo Mheshimiwa. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndulane, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimeipokea kwa mikono miwili kwa sababu, hilo ni tatizo la Kitaifa. Kwa hiyo, kumekuwa na shida kubwa na kwa bahati mbaya katika eneo letu sisi tembo huwa wanaingia jioni wanatoka alfajiri. Wamekuwa wakiharibu miundombinu mbalimbali ikiwemo nyumba za wananchi, mazao yao na pia, hata mazao yaliyohifadhiwa kwenye hifadhi nayo wamekuwa wakivunja nyumba wanakwenda kuchukua yale mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wananchi wengi wamepata vilema, wengine wameuawa kwa nyakati tofauti, lakini tunashukuru Serikali imeanza kuchukua hatua. Vijana wetu 10 wameshafundishwa *VGS* katika ule mpango wa kila vijiji vitano kuweza kupelekwa kwenye mafunzo katika Chuo cha Likuyu kule Namtumbo na tumeshaletewa mabomu 125, lakini pia, tunatarajia kuletewa ndege nyuki mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi vyote ambavyo tumeletewa, sambamba na mafunzo ya uhifadhi, bado havijaleta tija ya kutosha kwa sababu, vimekuwa vichache. Kuna Kijiji kama Mkarango, Kijiji kama Kandawale, Kipindimbi na kule Mtepera yaani sasa hivi tembo wameshaingia tayari. Kwa hiyo, udhibiti wao umekuwa mdogo kwa sababu, hata *VGS* wamekuwa wachache, lakini pia, hayo mabomu bado hatujayaona, japokuwa yalizunduliwa tangu mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iongoze *VGS* kuwapeleka kwenye *training* kule Namtumbo, lakini pia, iweze kuleta ndege nyuki wanaoweza kukabiliana na hao wanyama aina ya ndovu hata usiku kwa sababu, nina mashaka kwamba, huenda hata…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kidogo la kumalizia.

MWENYEKITI: Sawa, malizia.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa pia, kule Malinyi katika Kata za Itete kuna Pori la Akiba la Hifadhi ya Kilombero imezunduliwa, lakini kuna maeneo ya wananchi yamechukuliwa na mpaka wakati huu bado hawajalipwa fidia, lakini hawaruhusiwi kuingia kuhudumia mazao ya kudumu yaliyopo mle; kuna mazao kama miti ya mitiki na kakao. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iweze, aidha kuwaruhusu wananchi waingie kwenda kumalizia kulima yale mazao yao ili yakikomaa waweze kuvuna au waweze kulipa fidia kwa wale wananchi kwa sababu, hifadhi imefuata wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa za kufanya nchi yetu iongeze watalii, *potential* ya kuongeza watalii ni kubwa, nchi imebarikiwa ina vivutio vya kila aina kwa hiyo, ni Wizara kuwa *creative* zaidi kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Naibu Waziri na timu yetu. Leo sitakuwa mkali sana kwa sababu ya tukio walilofanya asubuhi la ile *GN,* Serikali yetu ni sikivu, wanapozungumza wananchi wanachukua hatua haraka sana. Kwa hiyo, kwa kweli, leo tena ninawaombea warudi kabisa kwenye Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii na uhifadhi ili uwe mzuri ni lazima ujali haki za wananchi na kwa sababu tumepata uhuru ni vyema watu wetu wanaohifadhi wakawa wanafahamu kwamba, Watanzania hawa ndiyo wahifadhi namba moja na kila wakati ni vyema kujenga mahusiano zaidi, ili tulinde maeneo yetu ya hifadhi, lakini Watanzania wakiwa wana furaha. Siyo kuwa, wapoteze mali zao, ama mifugo yao, ama maisha yao kutokana na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi karibu cha miezi miwili, mitatu hivi, Watanzania wa Kiteto karibu watano wamepoteza maisha kwa sababu ya tembo huko mashambani. Watanzania hawa ambao wanahangaika kila wakati kulima hawalali usiku na mchana. Tembo wamekuwa ni kadhia kubwa na binadamu wanapopoteza maisha kwa sababu, si sawa. Kwa hiyo, kila wakati waongeze nguvu na teknolojia, ili Watanzania hawa wasipoteze maisha, kwa ajili ya tembo hawa. Vijiji vya Makame huko wameshafariki wananchi karibu watatu, Ndorokoni, Ndaleta, Olpopong'I, karibu kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ni vyema kila wakati timu zenu zikawa *quick* ku-*respond* kwenye vitu kama hivi, lakini ni lazima nimpongeze Naibu Waziri, amekuwa *very quick* kujibu meseji kila wakati na ametuma timu hata kuna tembo mmoja ameshauawa, ambaye ni mkorofi sana, tunashukuru, kila wakati wawe wana-*respond,* lakini bado kuna mmoja anasumbua sana. Wananchi wamesham-*identify* kwa mkia wake, ninasikia ana mkia mfupi hivi, sasa wanapopata taarifa hizi na wao wawe *quick* kufanya hivyo ili tuendelee kuokoa maisha ya binadamu. Wananchi wetu wanahangaika, kila wakati wanapopoteza mazao yao, siyo sawa. Hatutaki tuwatengeneze Watanzania wanaokuwa maskini kwa sababu ya kupoteza mifugo yao, mazao na maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia limezungumzwa hapa, sheria zetu hazipo vizuri sana kwenye kutoa fidia, inaitwa kifuta jasho, lakini hata hicho kifuta jasho hakiji. Kwanza, inachukua muda mrefu sana, kesi za Kiteto zimeshaletwa, fomu zaidi ya 300, lakini fidia haziji kila wakati. Mheshimiwa Waziri kuna kesi ya

Mahakama, kesi ya Lenina, nimeshazungumza ni kesi za Mahakama Kuu, hukumu ya mwisho ya 2020 mpaka leo. Wananchi hawa Mahakama ilishawapa haki yao, lakini mpaka leo hawajalipwa na Mheshimiwa *Attorney General, I am very glad* unanisikiliza; hizi hukumu za Mahakama, Mahakama zinapofika mwisho na kutoa hukumu wananchi wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Mheshimiwa Waziri tafuteni mpango wa mtu anapofanya kosa ng'ombe wakaingia kwenye maeneo haya, badala ya kuwakamata na kukaa nao watengeneze namna ya ng'ombe kukaa nje ya hifadhi waendelee kuhudumia watu kwa sababu, ni vyakula vya watu. Sasa leo hivi ng'ombe wakitoka wakaenda kwenye hifadhi na wakawakamata, ndama wanabaki nyumbani na sisi tunasubiri tunywe maziwa jioni. Kwa hiyo, tusubiri kweli miaka mitatu ndio tunywe maziwa! Kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ni wakili, kwenye eneo hili lazima wafanye vizuri zaidi, tudumishe mahusiano. Ukikamata ng'ombe wangu, kwani ukisema wakae kijijini wakati wanaendelea na kesi na huyo asiondoke, kwani kuna shida gani? Ukishinda si utakuja kuwachukua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ya *WMA,* Wabunge wengi wameongea hapa na Kamati ya Bunge imezungumza kwamba, pesa za *WMA* ziende haraka. Wewe *imagine* tu, wao wana-*struggle* baada ya zile hela kwenda Hazina, lakini angalau wanapata mshahara, si ni kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni pesa tu za *operation* zina-*frustrate* mambo mengi, ndiyo maana wanataka pesa zirudi. Sasa *imagine* za *WMA,* za mishahara, za *operation,* zote zipo kule ni kwa sababu, tulishatengeneza Kanuni za *WMA* na wakaandika vizuri, kila mtu apate chake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi ninafikiri wao walikuwa wakiomba hizo fedha zitoke Hazina, kuna kipindi nilikuwa ninataka zisitoke, ili na wao wapate joto kidogo. Sijui ndio ile akina

Mheshimiwa Shangazi wanasema ubaya ubwela ili na wao wapate *pinch,* ili waelewe kwamba, pesa zinaweza zika-*frustrate* mambo yasipoenda vizuri na Waziri ni Wakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *WMA* ikiingia mkataba na mwekezaji halafu anayeweka hela ni mwingine, halafu huyu anashindwa ku-*meet* zile *obligations* za mikataba eti kwa sababu, pesa zipo mahali. Waziri wa Fedha, kama yupo hapa, pesa za *WMA* haziruhusiwi kwenda Hazina, hizi ni pesa za wananchi, ile *cut* inayooenda maliasili, pengine nwao ndiyo wapambane huko, lakini za *WMA* zinatakiwa ziende moja kwa moja kwenye *WMA*.

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako umeisha, malizia.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya. Basi kwa kuwa, leo nina furaha, ninaunga mkono hoja na niwatakieni kila la heri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilishamwita Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, baada ya Mheshimiwa Tadayo, watafuatia wachangiaji wanne wa dakika tano, tano, kengele itakuwa moja tu kwa wale wa dakika tano.

Mheshimiwa Tadayo endelea. Kwa hiyo, atafuatia Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshihimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Maboto.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote, kwa ridhaa na hisani yako, ninaomba uniruhusu kwa niaba ya Wana-Mwanga wote, kwa vile leo ninasimama mbele ya Bunge lako hili mara ya kwanza toka tumalize shughuli nzito ya kumsindikiza na kumuhifadhi Muasisi wa Wilaya yetu, Mzee Cleopa David Msuya, ninaomba uniruhusu nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo alitusindikiza kuanzia Dar es Salaam, kwenye kumuaga mzee wetu mpaka Mwanga na Kijijini kabisa, nyumbani kule Usangi, kwenye kumhifadhi mzee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini pia, tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson, tunamshukuru sana Jaji Mkuu, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, pamoja na Mawaziri, Wabunge na wote ambao kwa kweli, walitukimbilia na kutupa faraja kubwa katika kipindi kile. Tunawashukuru sana, Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu, Watanzania Wana-Mwanga pamoja na Chama Cha Mapinduzi kwamba, ni kweli tumepata pigo, lakini mzee wetu alituwekea misingi mizuri na hakuwa mchoyo katika kutufundisha jinsi ya kuendeleza mambo. Kwa hiyo, mimi bado ninaona mwanga mkubwa mbele ya Mwanga, sioni giza lolote, ninaamini mambo yatakuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda niende haraka. Nieleze tu kwamba, kwa kweli, Jimbo langu la Mwanga ni moja kati ya wanufaika wakubwa wa miradi mbalimbali ya Wizara hii, pamoja na taasisi zake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu na timu yako tunawashukuru sana kwa jinsi ambavyo mmeihudumia Wilaya yetu, wametupatia lango la Kaskazini la Hifadhi ya Mkomazi kwa heshima kubwa kabisa, alikuja kufungua Mheshimiwa Waziri Mkuu na sasa limeshaanza kufanya kazi. Ninaendelea kutoa wito kwa Wana-Mwanga kulitumia, kama fursa ya Uchumi, lakini pia, kuwaomba wadau wa utalii walitangaze sasa, ili liweze kupata wateja wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru pia, Wizara ya Maliasili, kupitia *TANAPA* kwamba, walitupatia bweni katika Shule ya Sekondari ya Kigonigoni na kuna mradi unaoendelea wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Kwangu na kuna mradi wa madarasa mawili katika Shule Sikizi ya Mgigili, tunawashukuru sana. Maeneo yote haya, ambayo wametupatia miradi hii ni yale maeneo ambayo yana changamoto ya wanyama wakali. Kwa hiyo, tunasisitiza wanafunzi kupata mabweni na kuwa na shule shikizi, kwa ajili ya watoto wadogo wasiende mbali sana

wakaathiriwa na hawa wanyama wakali. Kwa hiyo, tunawashukuru kwa kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanamwanga ni wahifadhi wazuri sana, pamoja na changamoto zote za wanyama wakali, lakini wamekuwa wavumilivu, wametoa ushirikiano kwa Serikali kwa kutokuleta madhara wala hasara kubwa kwa wanyama hawa, wamekuwa wakiishi nao na kufuata masharti. Kwa hiyo, basi Mheshimiwa Waziri na timu yake, pamoja na yote mema sana ambayo wametutendea, bado niwasilishe kwako maombi matatu tu; la kwanza ni, Serikali imetujengea shule nzuri sana inaitwa Toloha *Secondary School,* ni Kata ambayo ilikuwa haijapata shule, lile eneo ni la wafugaji, tunaomba Mheshimiwa Waziri, kupitia taasisi yako nzuri sana ya *TANAPA* au nyingine yoyote, watusaidie tupate bweni kwenye ile Shule ya Toloha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Kivisini, Serikali imetujengea shule nzuri sana na mabweni ya kidato cha kwanza mpaka cha nne. Tunaomba *TANAPA* kwa vile eneo lile ni lenye changamoto ya wanyama, basi watuongezee bweni, kwa ajili ya kidato cha tano na cha sita, tunawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi wa ile Shule ya Msingi Mgigili, ambayo wametujengea madarasa mawili pamoja na vyoo, ikiwapendeza, basi watuongezee madarasa matano pale, ili tuweze kukamilisha darasa la kwanza mpaka la saba. Wale watoto wasome kwenye yale madarasa yenu bora kwa sababu, ukweli kabisa ni kwamba, madarasa waliyotujengea mabweni ni ya viwango vya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mwanga imetunza mazingira vizuri na kwa namna moja au nyingine hiyo imesababisha matatizo ya wanyama. Eneo la tambarare, Tarafa ya Jipendea, yote ina tatizo la wanyama wakali ambao wanadhuru maisha na kuzuia uzalishaji, lakini maeneo ya milimani kuna wanyama wadogo sana, lakini nao wanaleta hasara kubwa, tumbili. Tunaomba mwongozo Mheshimiwa Waziri kwamba, ni namna gani watu wawa-*treat* wale wanyama kwa

sababu, kwa kweli, sasa hivi hata kupika chakula inabidi ukae hapo na fimbo ushikilie kwa sababu, watakuja waipue sufuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mwongozo wa Serikali wa kitaalam jinsi ya ku-*deal* na hao Wanyama, ili watu waweze kuishi. Tunapata hofu sasa kwamba, inawezekana hata haya magonjwa ambayo, pengine yanabebwa na wanyama, kama haya, yasije kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni juu ya suala zima la kifuta jasho na kifuta machozi. Katika harakati hizi za wanyama wakali katika Tarafa hii ninayosema ya Jipendea, wapo watu wengi ambao wengine ndugu zao wamepoteza maisha na wengine wameharibiwa mazao yao na walishahakikiwa tayari, malipo yamefanyika mpaka mwaka 2023, baada ya hapo bado hawajalipwa. Tunaomba kipaumbele katika eneo hili, ili katika miaka iliyofuata, baada ya 2023 basi, yale madai yaweze kulipwa, wale watu waweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa kipindi hiki cha mvua changamoto ya tembo kule kwetu imepungua, hii inatudhihirishia kwamba, tatizo kubwa ni maji. Ninadhani sasa ni wakati umefika, Serikali ichukue hatua ya kuhakikisha kule kwenye hifadhi tunapata mabwawa ya kutosha, hawa tembo wakae kwao na sisi tukae kwetu tuendelee na maisha yetu. Ninaunga mkono hoja, siyo tu kwa sababu nimependa, lakini kwa vile Wizara imefanya kazi nzuri. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri na Naibu, wamemwakilisha sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Sekta hii ya Utalii. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kajege, kwa dakika tano, tano.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2025. Kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na Naibu wake Mheshimiwa Kitandula. Pia ninapenda

nimpongeze Mheshimiwa Katibu Mkuu Mheshimiwa Abbas, Watendaji wote wa *TANAPA*, Ngorongoro, *TFS* na *TAWA* pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nichukue nafasi kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha utalii Nchini Tanzania. Sisi wenyewe ni mashahidi, bila filamu ya *Royal Tour* nchi yetu ilikuwa bado haijafahamika huko ughaibuni. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais alilichukua jambo hili kwa uwezo wake na kutoa ile filamu ya *Royal Tour* ambayo sasa hivi inatuuza huko nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo ninaliona hapa ni suala la upungufu wa hoteli. Watalii wengi wamekuwa wanakuja nchini kwetu Tanzania, lakini hatuna vitanda vya kutosha kwa sababu hoteli nyingi zilibinafsishwa. Kama mtakumbuka Serikali ilibinafsisha hoteli kwa mikataba mbalimbali lakini wapo wawekezaji ambao hawakutimiza masharti ya ubinafsishaji. Hoja hii imekuwa ni hoja ya Kamati tangu mwaka 2021, lakini Serikali haijaweza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Azimio la Bunge ambalo lilipitishwa humu ndani ya Bunge, kwamba zile hoteli ambazo hazijatimiza masharti ya ubinafsishaji ziweze kurudishwa. Mfano mzuri ni hoteli ya *Embassy* Dar es Salaam, ina takribani miaka 17 haijaweza kufanya kazi. Zipo hoteli nyingine za Kunduchi *Beach*, Mikumi na kadhalika. Hoteli Hizi zilibinafsisha lakini hazifanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije kwenye hoja ya kuzichukua hoteli hizi. Hatuwezi kuwa tunalalamika hatuna vitanda vya watalii kuja kulala wakati tulibinafsisha hoteli zetu na sasa tunashindwa kuzirudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hiyo ningependa niende moja kwa moja kwenye suala la Maafisa Maliasili walioko kwenye halmashauri zetu nchini Tanzania. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie hawa Maafisa Maliasili, Maafisa Wanyamapori waliopo kwenye

halmashauri vitendea kazi vyao vinatakiwa kununuliwa na nani? Kwa sababu wengi waliopo kwenye halmashauri hawana magari, wengine hawana risasi na wengine hawana bunduki. Utakuta ofisi imewekwa Afisa Wanyamapori hana gari la kwenda kuangalia wale wanyama msituni, hana bunduki, hana risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, waje na ufafanuzi na watueleze; je, huyu Afisa Wanyamapori aliye halmashauri anatakiwa kuhudumiwa na nani? Anahudumiwa na halmashauri au anahudumiwa na Wizara? Ili tufahamu, kwa sababu jambo hili limekuwa likileta shida. Unakuta wanyama wakali wamevamia mahali halmashauri ina Afisa Wanyamapori lakini anashindwa kwenda kule kwa sababu hana gari, anashindwa kwenda kumpiga yule tembo au mnyama yeyote mkali kwa sababu hana risasi. Sasa tuombe ufafanuzi, risasi za hawa Maafisa Wanyamapori walioko kwenye halmashauri, ni nani anayepaswa kuzinunua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nimeona wanapokuja wanyama wakali na waharibifu kwenye vijiji vyetu tunatumia *VGS*. *VGS* ni *temporary measure,* hata hizi ndege nyuki ambazo zimevumbuliwa sasa *is temporary measure, is not a permanent measure*. *Permanent measure* ilikuwa ni kuchimba mabwawa kwenye hifadhi zetu. Hata hivyo, mpaka sasa *TAWA* wamechimba mabwawa nane tu kwenye hifadhi zetu, hifadhi nyingine hazina maji. Tembo wanatoka kwenye hifadhi wanakwenda kutafuta maji, wanakwenda kutafuta chakula kwa sababu kwenye zile hifadhi hakuna maji…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ninaomba umalizie, muda wako umekwisha.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja zote za Kamati na ninaunga mkono hoja ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimwite sasa Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, dakika tano.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kukuza Sekta yetu ya Utalii Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala machache; la kwanza ni kuhusu vizimba. Katika hotuba ya wizara inaonesha katika mwaka ujao wa fedha watajenga vizimba vitatu tu katika Wilaya ya Bunda; hivi vizimba ni vichache sana. Kwa mfano nikiangalia ukubwa wa Jimbo langu, urefu wa ufukwe peke yake katika Ziwa Viktoria ni zaidi ya kilometa 100, lakini vilevile tuna zaidi ya mialo 40. Sasa, hivi vizimba vitatu vitajengwa wapi? Nilikuwa ninaomba Serikali ifikirie kujenga zaidi ya vizimba 40 katika jimbo langu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu fidia au kifuta jasho, ninasema ni fidia. Kwanza haitoki mapema, lakini vilevile ni kidogo sana kama walivyozungumza wenzangu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze kwamba ni hatua gani sasa Serikali inachukua ili kuhakikisha kwamba wale wananchi ambao wanapata madhara na wao wanapata kifuta jasho kwanza mapema, lakini vilevile kiwe ambacho kinawasaidia katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu vituo vya askari. Kutokana na mashambulizi ya wanyamapori katika jimbo langu nilikuwa ninaomba sasa tupate vituo vya askari wanyamapori katika maeneo yafuatayo: Kwa mfano, Buzigwe, kila mara kumekuwa na tatizo la mamba, ninaomba kuwe na kituo kingine Buzigwe; kingine katika Vijiji vya Mayolo; Kasaunga; Kisolya; Nampindi; Bulomba; Nchigondo; Mugala; Isikilo; na Namuhula. Hivi vyote ni vijiji ambavyo kila wakati kila mwaka kunakuwa na matukio ya mamba au matukio ya tembo kukanyaga watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie muda wangu kuunga mkono hoja, lakini nitapenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufunga hoja yake aje na majibu yatakayotosheleza ili nisiweze kukamata shilingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, dakika tano.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii. Pia ninataka kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya mpaka tumepata matunda haya makubwa ya utalii; na muda mchache uliopita Mheshimiwa Rais ametoka kulihutubia Taifa na kusema kwamba tulinde amani yetu ili wageni katika dunia nzima waendelee kuikimbilia Tanzania. Mheshimiwa Rais ametoka kusema kwamba hatoruhusu watu hata wa nchi jirani ambao wamevuruga kwao waje wavuruge kwetu; na Mheshimiwa Rais amesema kwamba hapa Afrika Mashariki na Afrika ambao hatujavurugwa ni sisi peke yetu. Kwa hiyo ikikupendeza hii hoja ya Mheshimiwa Rais ambayo ameihutubia leo ni muhimu sana ikaja kwenye Bunge lako tukaiunga mkono ili iendelee kukuza utalii na kulinda maliasili za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara pamoja na askari wetu, Wakuu wa Mikoa wetu na Waheshimiwa ma-*DC;* wanafanya kazi kubwa ya kulinda rasilimali zetu. Ninataka kusema Wizara hii ni kama wizara moja ya mfano kwa sababu imekusanya zaidi halafu inaomba fedha kidogo. Wamekusanya trilioni moja na bilioni moja nukta moja nane, lakini wanaomba bilioni 359. Ninaunga mkono hoja na ni imani yangu kwamba Wabunge wote wataunga mkono hoja; na tunapenda Wizara zote zingekuwa hivi, yaani anakusanya trilioni moja halafu yeye anaomba bilioni 359. Kwa kweli ni mfano mzuri sana ambao tunapaswa kuiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kilombero tuna Hifadhi ya Nyerere na Udzugwa; ninataka kuwa mmoja ya wahifadhi wazuri katika nchi yetu kwa sababu katika jimbo langu kuna mambo haya. Hata hivyo, ili tuendelee kuona kuwa tunanufaika na maliasili hizi watukumbuke sana sisi watu ambao tuna hifadhi. Kule kwenye Kata zangu za Mang'ula, Mwaya na Kisawasawa bado tembo ni tatizo kubwa sana tunaomba sana watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tunaomba wawaangalie wavuvi wetu. Wanaingia wakiingia kuvua mtoni wanatozwa. Ninashukuru *TAWA* wamepunguza tozo; lakini baiskeli inatozwa, tenga linatozwa na mvuvi anatozwa. Tulikuwa tunaomba; kwa sababu hawawezi kwenda kukata miti tena, hawawezi kwenda kulima basi wapate nafuu kwenye kwenda kuvua kwa gharama ya chini zaidi ili iweze kupata matunda makubwa *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na la msingi ambalo ninataka kusemea ni kuhusu mgogoro wa Kitula. Ninataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri hapa alitutumia timu, kuna wananchi walikuja hapa wakaa muda mrefu; na juzi ile timu ambayo imekuja walipata ajali, ninataka nitoe pole kwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Utatuzi wa Migogoro katika Wizara yake. Alipata ajali Mr. Kauzeni na sasa anaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanda mpaka kwenye eneo la mgogoro kule Itula, mimi mwenyewe nimejionea; sijafika kabisa Itula lakini nimejionea na ninataka niseme kwa kifupi hapa kwa sababu kulikuwa na vyombo vya habari vya wananchi hapa. Sisi sote tunaunga mkono uhifadhi na ukienda kule unaona kabisa ni mazingira ambayo yanakusanya maji, lakini wananchi wana hoja zao. Ninaomba Mr. Kauzeni atakapopata nafuu na timu twende pale tukawaambie wananchi ukweli, tuwasikilize kutokana na ramani yao ya kijiji, tuwasikilize kutokana na hoja zao za kijiji ambazo zimewauzia maeneo, tukae kwa pamoja tuwaambie ukweli wale wananchi; kwamba kama hapa ni hifadhi na kama kweli kuna mazao kama wanavyosema kwa sababu hatujafika. Basi, Mheshimiwa Waziri amesema kwenye hotuba yake kuwa analipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Kilombero wale watu ambao wanawatoa wana makaburi yao yapo kule na wanasema kwamba kokoa yao ipo kule. Kama ni lazima watoke basi walipwe fidia ili kuondoa nongwa wakati huu. Jambo hili ninalisema kwa ufupi sana, nimeona wananchi wameongea katika lugha kali, wanawasema askari wetu ambao wanafanya kazi ya kulinda kule kwa hali ya ukali, hawaamini tena Polisi wa

TANAPA, wanazungumza mpaka wanawalazimisha kuimba nyimbo ambazo sio nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, ninamwomba Mheshimiwa Waziri baada ya kupitishiwa bajeti yake hapa anipatie watu twende tufike hadi Itula. Wale wameomba mwezi mmoja waisome ramani, waitafsiri ramani, waweze kuweka mipaka. Tukawaambie ukweli wananchi wetu kama ni eneo la hifadhi basi kinachotakiwa kufanyika ni kwamba tuanze kuomba sasa kama linafaa kwa kilimo. Kama Serikali itatunyima basi wapewe fidia wale ili watoke, kuliko wanavyosema, kwamba mazao yao yamekatwa, wanasema kwamba kuna mazao yamepigwa dawa, wanasema wamepigwa mpaka alama huko mgongoni. Ninazungumza katika lugha ya kujenga kwa sababu tunataka Bonde la Kilombero lijaze maji Bwawa la Mwalimu Nyerere na pia tunataka tuendelee kulinda hifadhi yetu. Kama kweli tunataka kutoka kwenye hifadhi basi wananchi wetu walipwe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa muda huu mfupi wa dakika tano ulionipa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, nimwite Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, dakika tano.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa sana kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye Jimbo langu la Bunda Mjini, hasa kwenye Kata ile ya Nyatwali. Wananchi wa kata ile wameishi pale zaidi ya miaka 30 na sintofahamu kwa sababu wamekuwa wakiishi pale hawajui kama wataishi pale ama watahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja kutatua changamoto hiyo. Amelipa zaidi ya

shilingi bilioni 50 kwenye Kata ya Nyatwali na wananchi wale wote wamepata malipo yao. Kilichobaki ni fedha ndogo ndogo kwa ajili ya kuhamisha makaburi na fedha hizo zipo kwenye halmashauri yetu. Wiki iliyokwisha wananchi waliokuwa wamebaki zaidi ya wananchi 40 fedha zao zipo na sasa hivi wanaendelea kulipwa kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ametatua changamoto hii kubwa ambayo imewasumbua wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwa muda mrefu na wamekuwa wakiishi katika maisha ambayo kwa kweli walikuwa hawajui kwamba wanaanza vipi na wanamaliza vipi. Kwa kweli Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sehemu ya kutatua changamoto za Watanzania. Ametatua changamoto hii kubwa ambayo ilikuwa inatukabili kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu kuiomba Wizara ya Maliasili na Utalii. Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda ilitoa eneo la kujenga Ofisi za *TANAPA* Kanda ya Magharibi na wakawapa eneo bure na lipo na watu wa *TANAPA* wamepanga kwenye majengo ya wananchi wetu pale. Tunaiomba Wizara wawape watu wa *TANAPA* fedha kwa ajili ya kujenga ofisi zao za Kanda ya Magharibi kwenye Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa sababu eneo lipo. Wajenge na zile ofisi ndizo zitakazopunguza changamoto kubwa za wanyama kwenye maeneo hayo. Hata Wabunge wenzangu wanavyozungumzia kuhusu changamoto hizo wanazozipitia kwenye maeneo yao, ofisi zile zikijengwa pale Bunda Mjini changamoto nyingine zote tunazozizungumza zitakwisha kwa sababu kutakuwa na usimamizi madhubuti kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara ya Maliasili na Utalii, niwaombe na kwa sababu jambo hili tumekwishalizungumza hapa, leo ni zaidi ya miaka mitatu na lile eneo wamepewa zaidi ya miaka mitatu, lipo na lipo salama, halina mgogoro wa aina yoyote ile. Kwa hiyo, waje wawekeze pale, wajenge ofisi zao pale, zitasaidia kutatua changamoto mbalimbali kwenye maeneo yale na kanda nzima ya maeneo hayo kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kwenye eneo hilo. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maboto, Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo atakuwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na yeye alikuwa kwenye orodha tangu asubuhi, kwa hiyo atapewa dakika zake 10.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara maalumu katika nchi yetu. Ninamshukuru Waziri Mheshimiwa Pindi Chana, anafanya kazi nzuri sana tangu amepewa Wizara hii. Naibu wake Mheshimiwa Kitandula anafanya kazi nzuri, Abbas ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara anafanya kazi nzuri sana, Naibu Katibu Mkuu wake, Makamshina wote watatu wakubwa wale, Kamishna wa *TAWA*, Kamshina wa *TANAPA* na Kamishna wa *TFS* wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais; tumezungumza hapa sana mambo ya *Royal Tour* kwamba amefanya kazi vizuri na tumepata wawekezaji wengi kwenye maeneo yetu. Ninajua, wakati fulani mtu anaweza kusema tuwekee Wizara iwe na fedha nyingi kwa ajili ya kujenga hoteli; hapana, wakati fulani ni kutengeneza mazingira mazuri ya nchi yetu ili watalii waje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kwanza wa nchi ya utalii duniani ni kuweka amani, mkakati wa kwanza. Kwa hiyo pamoja na kwamba kuna *Royal Tour* ya Rais Samia, lakini kwa diplomasia yake ya nchi zote duniani ameleta watalii wengi kwenye nchi yetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa diplomasia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliona, maana mimi sielewi, ni kweli au sio kweli. Hivi Profesa Janabi amekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, ni kweli au sio kweli? Kama ni kweli kwani, Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani huwa tuna zamu? Kwamba

zamu hii Kanda ya Afrika, kwamba zamu hii tuliweka Mkurugenzi ambaye anatoka Tanzania, Mungu akamchukua akaenda, kwa sababu ni zamu yao Watanzania tuwape tena? Hapana, maana yake ni kwamba diplomasia na Mama Samia imefanya uteuzi wake na Profesa Janabi ametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukubali kwamba huyu mama katika makocha ni kocha bora duniani. Maana ukiteua mtu akaenda akafanya vizuri kwenye mechi maana yake unasifiwa kwamba ulifikiri vizuri zaidi. Kwa hiyo tunampongeza Profesa Janabi kwa cheo alichokipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninamshukuru Waziri Pindi Chana kwa sababu mgogoro wa wafugaji na mapori ya akiba umepungua sana. Nilikuwa ninajiuliza maswali mengi sana, hivi inatokeaje mimi kwa bahati mbaya nipo mpakani mwa hifadhi, ng'ombe wangu ameingia hifadhini, unawafilisi wote ng'ombe 500, 400, halafu mimi nimekaa nimerudi nyumbani, nikifika nyumbani ninaanza kukodisha ng'ombe wa kulimia, ninapata shamba ninalima, nikishalima heka kumi au tano, tembo anakuja anamaliza zote, hivi inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachunga ng'ombe wangu, wewe unachunga tembo porini lakini wewe unaachia anamaliza mazao, mimi nikija unanifilisi, hivi inakuwaje? Sasa kwa diplomasia ya Mama Samia amefanya kumteua Mheshimiwa Pindi Chana, hii diplomasia sasa imeenea kwa wananchi, migogoro imepungua, tunawapongeza sana Serikali na iendelee kufanya hivyo. Ikiwezekana huko mbele tunakokwenda kuwe na sheria kwamba, kama ni ng'ombe mmoja anatozwa elfu 50 atozwe, kama ni elfu 30 atozwe, ili ng'ombe wakiingia porini tumalizane huko huko na sisi turudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi inakuwaje unakuwa na ng'ombe, una kesi wanakaa pale ng'ombe 500, unakaa na kesi kwa miaka miwili, unakuta ng'ombe 20 wamebaki. Hivi tunamfilisi nani? Si Mtanzania huyu huyu? Tutengeneze mazingira, wewe uliyepeleka ng'ombe porini, tumalizane hapo hapo, lakini sio kumfilisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niipongeze diplomasia ya sasa hivi, naona wanafanya kazi nzuri na Makamshna wote, sasa hivi wana diplomasia, mambo yanakwenda vizuri, wanaweka huruma na mambo mengine yanaenda vizuri, niwashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *fence*. Suala la *fence* kama *Grumeti Fund* wamekubali kuweka *fence*, kama kuna maeneo yanachengachenga kutokuwekewa *fence* njooni Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye vijiji vile vya Bunda ambavyo ni Vijiji vya Kunzugu, Nyamatoke, Mihale, Bukore, Hunyari, Mariwanda, Kihumbu, Sarakwa, Mugeta, Kyandege na Tingirime. Waje kwenye maeneo haya waweke *fence,* sisi tumekubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aende akaongee na watu wanaoweka *fence*, sisi mpaka wetu na Bunda ni Mto Rubana. Sasa ili *fence* ipite inatakiwa iwe *zig zag*, siyo wapige *fence* ndani ya mto sisi tukose pa kwenda, hapana! Twende tuweke *zig zag* ili wanyama wafaidi na sisi tufaidi. Tunaomba tukaweke hiyo *fence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Mugeta – Kilawila, nimeona *TANAPA* mmefanya kazi nzuri sana kwa kuilima Barabara ya Mugumu ambayo inakuja Maeneo ya Natta huku. Mmefanya kazi nzuri na sisi sasa tunaomba Barabara ya kutoka Mugeta kwenda Mto Rubana, kwenda Kilawila**.** Haiwezekani watu wetu wanalima mchicha, wana maziwa na wanalima chakula hawaendi porini kuuza mpaka wazunguke Serengeti au waende Lamadi. Tunaomba hiyo Barabara ya Mugeta muweze kuilima iwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kifuta machozi na kifuta jasho. Sasa pale Bunda kuna Vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta, Kyandege, na kuna Tingirime. Karibu watu 540 wanadai kiinua mgongo na wengine wale waliouwawa na tembo wapo wanadai, wako 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, kuanzia kesho nitakwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri unisaidie hata hao ambao wanalipwa kifuta machozi wakalipwe. Haiwezekani jamani wameua, siku moja amenisaidia kazi nzuri sana, ninakukumbuka kazi nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Mama mmoja aliuawa na mtoto na nini, akaamuru wakamlipa hapo hapo. Tunampongeza sana na Mungu ambariki. Kwa hiyo, hawa wengine waliobaki, tuje tuwalipe wafanye kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* imejenga Kituo cha Afya kinaitwa Hunyari kwa 60%, asilimia nyingine Serikali ilimalizia. Sasa walijenga jengo la upasuaji *(theatre),* sasa limebakia madirisha na *finishing*. Tunaomba sasa waje walimalizie lile jengo ili kile kituo sasa kiweze kufunguliwa kifanye kazi vizuri sana. Ninawashukuru sana kwa moyo huo wa kujenga hicho kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la njaa la Jimbo la Bunda lisiwe kwa wakulima wa Jimbo la Bunda. Tatizo linaletwa na tembo, haiwezekani watu wakawa wanalima kila mwaka chakula kinaliwa chote. Sasa watu wa *TANAPA* na watu wa Wizara ya Maliasili watusaidie, tunapokuwa tunaomba chakula Serikalini waingilie kati tupewe. Kwa sababu wanyama weo au wanyama wetu ambao sisi hatuwezi kuwalinda ambao ni tembo wanakuja kumaliza mazao. Watusaidie wakati tunaomba chakula kuja kusaidia watu wa Jimbo la Bunda wanaoathirika na tembo ili wale wananchi sasa waweze kupata chakula.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere, muda wako umekwisha, malizia.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mbambamba na hii Wizara, ninaipenda sana, wanafanya kazi nzuri. Ninawaunga mkono na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wake na jitihada za kuhakikisha anaendelea kutangaza na jitihada za kukuza utalii kwenye nchi yetu. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa uchapakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Wizara kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa kuhakikisha utalii wa nchi yetu unakuwa hivyo Wizara nayo ifanye jitihada kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu kuhakikisha barabara zote zinazoingia kwenye mbuga zetu zinapitika mwaka mzima. Kwa mfano, barabara inayotoka Mandela kuingia kwenye mbuga yetu ya Saadani wakati wa mvua haipitiki kabisa. Hivyo Wizara iendelee kufanya jitihada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto ya tembo kuendelea kuvamia makazi ya wananchi bado ni kubwa sana. Kwa mfano kwa Jimbo la Mkinga katika maeneo ya Mwanyumba, Mavovo mpaka Mwakijembe changamoto bado ni kubwa sana. Hivyo niiombe Wizara kuendelea kuchukua hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Katibu Mkuu Dkt. Hassan A. Said, Naibu Katibu Mkuu (Maliasili) Ndugu Benedict M. Wakulyamba - CP, na Ndugu Nkoba E. Mabula (Utalii), wataalam wa Wizara, taasisi zilizo chini ya Wizara na wadau wa maendeleo kwa mchango wao mkubwa kwenye kujuza Sekta za Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye ni nini kifanyike ili kukuza Sekta ya Utalii hapa Tanzania. Utalii, ni

kitendo cha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa lengo la kujiburudisha au kujifunza. Tanzania ni moja kati ya nchi zenye vivutio vingi vya utalii hapa duniani na ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa nchi zenye utalii mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii hapa Tanzania umekuwa na faida nyingi kwa Watanzania wote, ikiwa ni pamoja na kutoa ajira, kuongeza kipato cha Taifa, kuleta fedha za kigeni na kutangaza utamaduni wa nchi yetu Tanzania. Utalii peke yake huchangia karibu 17.2% katika pato la Taifa na huko Zanzibar ni 30%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida zote, Sekta ya Utalii nchini mwetu imekua ni sekta inayosuasua kwani inaingiza idadi ndogo ya watalii kinyume na matarajio. Tanzania ni nchi yenye vivutio vingi na tukijipanga vizuri tunaweze kuingiza watalii millioni 10 kwa mwaka wakati kwa sasa bajeti hii ikisomwa tumeshaingiza watalii 5,360,247 (wa ndani - 3,218,352 na wa nje 2,141,885) na lengo letu kwa mwaka 2025 ilikuwa watalii 5,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma, watalii wa kimataifa walioingia nchini waliongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 2,141,895 mwaka 2024 sawa na ongezeko la 132.24%. Ili kufikia lengo letu la kuongeza watalii wa nje, ni lazima Tanzania tujitathmini wenyewe na kufanya mabadiliko ili kukuza Sekta ya Utalii na kuingiza watalii wengi watakaolinufaisha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha Sekta ya Utalii Tanzania, yafuatayo ni mambo muhimu ya kufanya ili kukuza sekta yetu hii: -

(i) Kuweka mkazo kwenye kutangaza masoko ya utalii na kuhamasishaji watalii kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tumejionea umuhimu wa kutangaza soko letu la utalii kupitia filamu za *The Royal Tour* na *Amazing Tanzania* zilizotengenezwa na kumshirikisha Rais wetu kuonesha vivutio vya utalii katika Taifa letu. Filamu hizi zimekuwa mkombozi mkubwa katika Sekta ya Utalii kwani watalii

wameongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 2,141,895 mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ni muhimu kufanya kampeni za matangazo kwenye vyombo vya habari vya kimataifa na majukwaa ya kidijitali kama vile mitandao ya kijamii, tovuti za utalii na blogu za usafiri kuelezea vitu vya kitalii tulivyojaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kutangaza masoko yetu ya utalii, nchi ijizatiti kushiriki kwenye maonesho ya kimataifa ya utalii ili kuongeza ufahamu na kuvutia watalii kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Ushiriki wetu kwenye maonesho ya kitalii ya kimataifa kama yale ya Afrika Mashariki *(East African Tourism Expo), Internationale Tourismus-Boerse (ITB) Berlin, World Travel Market (WMT) London, Group Leisure & Travel Show (GLT)* ya Uingereza, *FESPO* ya Zurich, *World Tourism Forum* ya Lucerne, *Stockholm Luxury Travel Fair, Fitur International Tourism Trade Fair* ya Madrid, *Tourisma & Caravaning* ya Magdeburg na *International French Travel Market (IFTM)*. Maonesho haya ni muhimu kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la utalii linaweza kutangazwa hapa nchini kwa kuandaa maonesho ya ndani na kimataifa yanayolenga kuonesha utajiri wa vivutio vya utalii vya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko letu la utalii linaweza kufanikiwa ikiwa tutawatumia baadhi ya watu maarufu katika jamii duniani kwenye kushawishi na kuvutia watalii kuja kutembelea mbuga zetu au kupanda Mlima Kilimanjaro. Kwa mfano, wachezaji maarufu wa mpira duniani kama Ronaldo au Lionel Mesi au watu maarufu wenye ushawishi duniani kama Barack Obama, Serena Williams, Bill Gates, Rashida Jones, Patrice Motsepe na wengine wanaojulikana wanaweza kutumika kutangaza soko letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabalozi wetu wanaweza kutumika na kusaidia kutangaza utalii wetu. Hawa wanatakiwa kupewa elimu ya utalii na mbinu madhubuti za kuutangaza utalii

wa nchi yetu popote watakapokuwepo. Wote hawa wanaweza kutumia mitandao kuonesha vitu vya kitalii tulivyonavyo Tanzania.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wetu utaboreka sana ikiwa Serikali yetu itaweka mkazo kwenye kutengeneza na kuboresha miundombinu ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kama vile barabara ni muhimu sana katika Sekta ya Utalii. Barabara hutumika kuwapeleka watalii katika maeneo ya utalii. Kwa sasa barabara zetu nyingi zinazopeleka watalii *site* ni mbovu sana kiasi cha kuumiza watalii wakati wa safari kuelekea katika vituo vya utalii. Kutokana na ubovu wa barabara, watalii huishia kuchoka sana baada ya safari. Jambo hili hupelekea kuwakatisha tamaa na kupunguza idadi ya watalii, kwani wengi hawajazoea barabara mbovu kama za kwetu. Ikumbukwe kwamba watalii wengi hutoka katika nchi zilizoendelea na zenye miundombinu bora sana ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ni muhimu kuimarisha na kujenga barabara za lami kuelekea kwenye mbuga na hifadhi za Taifa, barabara za kupanda milima iliyopo nchini na barabara zote zinazounganisha maeneo muhimu ya kitalii na miji mikubwa. Katika barabara hizi, ni jambo jema kuweka nakshi za asili kama za mawe kwa maeneo yenye miamba, madaraja ya kibunifu ya mbao kwa maeneo yenye miti mingi na kuweka kila aina ya sanaa za kibunifu zenye kuitangaza sanaa na utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji, Serikali iwekeze na kupanua na kuboresha viwanja vya ndege vya kimataifa na vile vilivyo karibu na maeneo ya utalii kama vile Uwanja wa Ndege wa Arusha, Kilimanjaro, Iringa na kadhalika. Ubora wa huduma za ndege utasaidia kuwafikisha watalii karibu na maeneo ya utalii kwa wakati muafaka na kwa ufanisi mkubwa.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utalii tunahitaji kuboresha huduma za msingi kama vile huduma za afya, mahoteli yenye hadhi na mawasiliano bora ya simu na *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma bora za afya ni moja ya sababu zitakazowapa watalii ari ya kuja kutalii hapa nchini. Ninaishauri Serikali iendelee kujitahidi kuboresha huduma za kiafya kwa kujenga au kushawishi wadau kujenga hospitali zenye hadhi ya nyota tano *(five stars)* kwa sababu inasemekana Tanzania hatuna hospitali yenye hadhi ya nyota tano *(five stars)* inayopendelewa kutumiwa na watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana, watalii kutoka nje wanaofika Mbuga za Ngorongoro, Manyara, Kilimanjaro, Mkomazi, Nyerere, Tarangire, Mikumi, Saadani, Gombe, Katavi, *Arusha National Park* na Serengeti wakipata changamoto kubwa hukimbilia kupata huduma ya afya mjini Nairobi, Kenya kwa sababu Tanzania hatuna hospitali yenye hadhi ya nyota tano *(five stars)*. Kwa sababu hiyo watalii wanaokuja na kuugua hupata hofu ya kurudi tena au husita kushawishi wengine kutembelea Tanzania, hivyo basi idadi ya watalii wanaotembelea Tanzania hupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wakija hapa nchini wanahitaji kulala kwenye nyumba safi na zenye hadhi. Ni vyema Serikali ikahimiza wawekezaji wajenge hoteli za aina mbalimbali zikiwemo zile za nyota tano zitakazotoa huduma nzuri za malazi, chakula na za kuwasafirisha watalii kutoka mahotelini kwenda maeneo mbalimbali kutalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yote wanakopita, kulala na kutembelewa na watalii, ni vyema upatikanaji wa mawasiliano bora ya simu na *internet* ukawa ni wa uhakika. Serikali iweke minara kwenye maeneo yote haya ili watalii wapate mtandao kila watakapokuwa.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupanua wigo wa maeneo mapya, ninaishauri Serikali iongeze ubunifu wa kuboresha na kukuza vivutio vya utalii. Pamoja na kuwa hapa Tanzania kuna vivutio vingi vya utalii, lakini ubunifu katika kuboresha vivutio hivyo bado uko chini. Vivutio vya utalii tulivyonavyo sasa ni vilevile tulivyokuwa navyo miaka nenda rudi, hivyo ni lazima tuwe wabunifu katika kuboresha vivutio vya utalii au kuongeza vingine

kwa sababu watalii wetu kila wanapokuja wanatukuta na vivutio vilevile na hakuna tulichoboresha wala kuongeza. Hii inawafanya wasipate hamu ya kurudi tena mara nyingine kwa kuhisi kuwa wamemaliza kutalii Tanzania hivyo hupelekea kupungua kwa idadi ya watalii katika misimu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayotakiwa kuboreshwa ni yale yenye maporomoko makubwa na ya kuvutia kama yale ya *Materuni Waterfalls, Marangu Waterfalls, Choma Waterfalls, Mount Meru Waterfalls, Engare Sero Waterfalls, Ndaro Waterfalls, Soni Waterfalls, Kinole Waterfalls, Nduruma Waterfalls* na *Mwalalo Waterfalls*, maeneo ya kihistoria kama vile Olduvai Gorge, *Kondoa Rock Paintings*, Miji ya Kihistoria ya Bagamoyo, Lindi na Mikindani, Magofu ya Kilwa na Bagamoyo, Mapango ya Amboni Tanga, Mahandaki yaliyokuwa yanatumika na wazee wetu wakati wa vita, Jumba la maonesho la Taifa lenye nyara mbalimbali kama mafuvu ya machifu wetu, Mti mrefu kuliko yote barani Afrika ulioko Kata ya Mbokomu, Mkoani Kilimanjaro na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kufanya ubunifu mbalimbali katika kila eneo. Kwa mfano, wawepo watu wa kuuza vitu mbalimbali kama vinyago, nguo, *t-shirt*, kanga, skafu zinazotangaza bidhaa mbalimbali za utalii katika sehemu husika. Katika maeneo haya, ufanyike ubunifu wa kuonyesha na kutangaza tamaduni zetu (kupitia nadharia ya Utalii wa Utamaduni) ambapo tutaonyesha na kunadi ngoma, vyakula vya asili na vitu vingine vya kuvutia vya asili.

(v) Mheshimiwa Spika, ili kuboresha Utalii hapa nchini, ni vizuri nchi ikaweka Sera na Sheria rafiki za kulinda Utalii. Kufanikisha hili, ninapendekeza yafuatayo yafanyike:-

(1) Kuboresha na kuimarisha Sheria za Usalama kwa Watalii wanaokuja kututembelea ili kujenga mazingira salama kwa wageni wote;

(2) Kuhakikisha kuwa Sheria na Sera zinazingatia uhifadhi wa mazingira na haki za wenyeji ambao ni walinzi wa kudumu waraslimali za kitalii katika maeneo yao;

(3) Kutunga Sheria na Sera madhubuti zinazovutia wawekezaji wa nje na wa ndani katika Sekta ya Utalii, ikiwa ni pamoja na uwepo wa vivutio vya kodi na motisha za kifedha;

(4) Kuweka Sheria kali za kupambana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori ili kulinda Maliasili za Kitalii;

(5) Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ya kuboresha ni ile ya huduma za utalii kwa Kundi la Waongoza Watalii. Tanzania inaweza kupokea watalii wengi zaidi ya tunavyopokea sasa ikiwa tutaelimisha waongoza Watalii wetu *(Tour guides)* na kuwaongezea ujuzi zaidi katika kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Ili kufanikisha hili, ninapendekeza kuwepo na Sheria ambayo itawalazimu Waongoza Watalii kuwa na cheti cha fani hii kitakachotolewa na vyuo vilivyothibitishwa na mamlaka za Serikali.
Sehemu ya mafunzo yao ijikite kwenye kwenda kujifunza namna ya kufanya majukumu yao na kuiga mifano kutoka nchi nyingine zenye mafanikio ya kupokea watalii duniani. Kupitia hili tutaongeza ubora wa huduma katika utalii na kufanya watalii kutoka nje kupenda zaidi kutalii Tanzania hivyo kuongeza idadi ya watalii. Kwa nyakati tofauti warsha na semina za mara kwa mara zitolewe kwa Waongoza Watalii ili wawe na ujuzi wa kisasa wa kutoa huduma bora kwa watalii;

(6) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania siku za mbele, ninaishauri Serikali iboreshe Sera ya Visa kwa kupanua Msamaha na Masharti ya Visa za Wageni ili kuwavutia watalii zaidi wa kigeni. Hii ni pamoja na kurefusha muda wa kukaa nchini kwani kufanya hivyo kutasababisha ongezeko la

watalii wa kigeni na Sekta ya Utalii itachochea fursa nyingi za kibiashara na kutia nguvu mpya katika maendeleo ya kiuchumi kwani kila wakiwa Tanzania watakuwa wanatuachia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, ikiwa tutaziangalia kwa umakini na kutatua changamoto hizi, Sekta ya Utalii itaimarika na watalii wengi wataitembelea Tanzania na hivyo kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza kwa kuimarisha utalii kusini na nchini. Kipekee kama Mbunge wa Iringa Mjini ninawashukuru kwa kuanza ujenzi wa Kituo cha Utalii Kusini, uwezeshaji wa kikundi cha ufugaji wa nyuki wa ukanda wa kijani toka Kata ya Kitwiru pamoja na mambo mengi mliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Maliasili waharakishe ujenzi wa Kituo cha Utalii Kusini kinachojengwa eneo la Kihesa kilolo ndani ya Manispaa ya Iringa. Kwani, tayari Uwanja wa Ndege wa Iringa umepanuliwa na kuanza kazi, idadi ya watalii imeongezeka kitakwimu kusini. Hii inasababisha sasa watalii wengi kukosa sehemu ya kupata taarifa sahihi za utalii kusini. Hivyo, tunaomba sasa kituo hiki kikamilike mapema ili kutengeneza muunganiko wa utalii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Utalii isimamie na kuendesha maonesho ya Utalii Kusini, ambayo huwa yanafanyika ndani ya Mji wa Iringa katika eneo linalojengwa kituo cha utalii kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Wizara ianzishe Maonesho ya Nyama Pori au *Nyama Pori Festival.* Sisi Iringa Mjini tuko tayari kushirikiana na Wizara katika Maonesho hayo ya *Nyama Pori Festival.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia mradi mwingine ukitokea kama wa *REGROW*, basi eneo la Iringa Manispaa liwe linaingia kama lango la utalii kusini. Ili kuwaandaa wananchi wa Iringa kuupokea utalii kusini. Ninaomba pia ili kutunza mazingira mazuri ya utalii, basi uwezeshaji wa vikundi vya ufugaji nyuki viwe vingi ili kusaidia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ishirikiane na wadau waliopo Iringa Mjini ili kukuza utalii na kutangaza utalii. Pia, wakati wa *AFCON* wasisahau kuleta watalii kusini. Ahsante ninashukuru na ninawasilisha.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Pia ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Dkt. Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa

kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia Uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mhesimiwa Balozi Dk Pindi Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Hotuba Nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa Letu katika ya Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kusababisha Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *program* ya kutunza maliasili zetu, Serikali iweke usimamizi wa msitu hasa ya asili, ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya nishati. Katika kupangilia matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara zote zinazosimamia Maliasili, Ardhi, Kilimo, Wizara za Maji na pia Wizara inayosimamia Mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi mazingira yetu na kuwepo msukumo zaidi kwenye kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza hatua zinazo-chukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala. Kuna mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma, Kata ya Inyala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mgogoro huu kuchukua muda mrefu na kusabisha hata uvunjifu wa amani, kuna ahadi ya mwaka 2015 alitoa Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli na kumwelekeza Waziri wa Ardhi na pia Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo kupitia upya mipaka, ili wananchi wa Kata za Inyala, hususani Kijiji cha Mwashoma waachiwe maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenye mgogoro ni mashamba ya wananchi na wamekuwa walinzi wazuri wa misitu na vyanzo vya maji, ni imani yangu wakiachiwa hayo maeneo yanayogombewa na *TFS* kwa maslahi mapana kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza juhudi za Serikali kuweka umuhimu wa kipekee na kupewa kipaumbele kwa Sekta ya Utalii ili iendelee kuchangia pato la Taifa, uhifadhi wa mazingira na ustawi wa jamii kupitia fursa za matumizi endelevu ya rasilimali za utalii. Mheshimiwa Rais, amekuwa mstari wa mbele kutangaza utalii kwa kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo Programu ya Tanzania - *The Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025 umekuwa mzuri sana kwa Sekta ya Utalii nchini Tanzania. Kwa mara ya kwanza katika historia, nchi imefanikiwa kuvuka lengo lake la kufikisha idadi ya watalii 5,000,000 mapema zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Kwa jumla, watalii 5,360,247 wameitembelea Tanzania, ikiwa ni ongezeko kubwa lililochangiwa zaidi na watalii wa ndani ambao wamefikia 3,218,352, huku watalii wa kimataifa wakiwa 2,141,895.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2022, mapato yatokanayo na watalii yameongezeka kwa 93% hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,527.72. Mchango huu wa Sekta ya Utalii bado ni mdogo sana kulinganisha na nchi shindani na lakini umeanza kulingana na maoteo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*FYDP* III 2021/2022-2025/2026)

umeelekeza kufikia idadi ya watalii wapatao 5,000,000 na kukusanya mapato ya kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni sita kufikia 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Sekta ya Utalii unakabiliwa na changamoto ya ushindani mkubwa katika soko la utalii wa kimataifa hasa kutokana na miundombinu na hata mazingira ambayo siyo rafiki kwa wawekezaji ikiwemo utitiri wa tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya utalii ni sawa na biashara zingine za nje zinazotegemewa katika mapato ya fedha za kigeni, lakini inakabiliwa na utitiri wa tozo katika mnyororo mzima na kusababisha kuwa mzigo mkubwa kupambana na ushindani wa kimataifa. Watalii kama ilivyo kwa biashara zingine wanaangalia sana na ubora wa huduma pamoja na gharama katika mnyororo mzima wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nchi yetu kubarikiwa utajiri wa vivutio vya aina mbalimbali, inatakiwa kuwepo na mkakati madhubuti wa kuhakikisha uendelezaji wa vivutio ili kuongeza wigo wa shughuli za utalii na hata kuondoa tozo ambazo ni mzigo kibiashara. Serikali iangalie kuondoa kodi zote ambazo hazitozwi na nchi shindani na pia mnyororo wa biashara ya utalii ichukuliwe kama biashara ya nje *(export)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana na tunakushukuru sana. Basi kabla sijamwita mtoa hoja, nimwite sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, dakika kumi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kujaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kufuatia mjadala wetu unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia afya njema na kwamba leo tunaijadili hotuba ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninatumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake kwa Wizara yetu na kwa msaada mkubwa anaotupa katika Wizara hii. Yeye kama mtaalam wa mambo haya ya utalii anatusaidia sana katika kufanya kazi yetu. Tunamshukuru sana na siku zote amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Wizara hii inapata rasilimali zinazotuwezesha kufanya shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru vilevile Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana. Amekuwa na msaada mkubwa sana kwangu. Anajitahidi sana kunisaidia niweze kumudu majukumu yangu ya kumsaidia, uzoefu wake katika shughuli za Kiserikali kwa kweli ananisaidia sana, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninawashukuru sana Kamati yetu; wamekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wizara yetu. Ni watu makini ambao siku zote wanapenda kuona kwamba Wizara hii inafanya vizuri zaidi. Ninataka niwaahidi kwamba tutajitahidi ndani ya Wizara kwa uwezo wetu wote kusikiliza kwa umakini mkubwa yale wanayotushauri na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambazo zimeibuka, zipo hoja ambazo zimeibuliwa na Kamati yetu. Ninapenda nijielekeze kwenye maeneo hayo, lakini vilevile hoja hizo zimegusiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwenye maoni ya Kamati, Kamati yetu imetuelekeza au imetoa ushauri kwamba Wizara ihakikishe inaendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vya utalii ili sekta hii iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, kazi kubwa inaendelea kufanyika ndani ya Wizara yetu. Wengi wamesema kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika kutangaza

utalii kupitia Filamu ya *Royal Tour*. Mara baada ya Mheshimiwa Rais kufanya jukumu lile sasa ni jukumu la Wizara na wataalam wetu kuhakikisha habari ile inayafikia masoko yetu. Katika kufanya hivi, tumeweza kuyafikia masoko mengi ambayo yamekuwa na tija katika Sekta yetu ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi sana kufanya utangazaji kwa kutumia mifumo ya kidijiti ili kuyafikia masoko makubwa. Vilevile, katika misafara yetu ya kwenda kutangaza utalii nje, tumejitahidi sasa kuwa wabunifu; kwamba badala ya kuwapa maneno tu, kule ambapo tunakwenda, wenzetu kule wanakuwa na *access* ya kuweza kuona moja kwa moja vivutio vyetu kwenye hifadhi zetu. Hili limekuwa na tija sana kupitia mifumo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuratibu misafara ya namna hiyo kulifikia Soko la China, tumeweza kulifikia Soko la India na sasa tumeanza kuona matokeo ya jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivi hatukuishia kwenye Filamu ya *Royal Tour*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, alikubali kwa mara nyingine kushiriki kwenye filamu nyingine ya *Amazing* Tanzania ambayo tunamshukuru vilevile Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ambaye na yeye alishiriki kwenye filamu hii. Filamu hii nayo imezinduliwa kule China, lakini vilevile tumeizindua hapa Tanzania na tumeanza kuona manufaa ya filamu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejielekeza vilevile kwenye kutumia watu maarufu na tunajielekeza kutumia Sekta ya Michezo ili kuweza kutanua wigo wa maeneo ambayo tunaweza kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi, hivi karibuni tumekuwa na mazunguzo ya karibu na mmiliki wa ile Timu ya *Manchester United*. Tulikwenda kufanya mazungumzo kule Uingereza na yeye amekuja hapa na timu yake. Hii yote ni katika kutanua wigo wa jinsi ya kutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashirikiana na mashirika ya ndege katika kutangaza utalii wetu. Mtaona hivi karibuni jinsi ambavyo tunashirikiana na Shirika letu la Ndege la *Air* Tanzania. Vilevile, tunashirikiana na wenzetu wa Turkish *Air* na tuna mipango ya kushirikiana na *Emirates*. Hii yote ni katika kuhakikisha tunafikia soko kubwa zaidi katika kuutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi tunazo fursa za kutangaza utalii na tunazo rasilimali kubwa ambazo tumekuwa tukizitumia hapa nchini. Tukio la nyumbu katika nchi yetu ni tukio kubwa la kiutalii. Sasa tumeamua kutengeneza aina ya kulitangaza hilo tukio la wale nyumbu kuzaliana kwa mamilioni. Liwe ni tukio ambalo dunia inaweza kuja kulishuhudia. Katika mipango yetu, tutaandaa filamu maalum kwa ajili ya jambo hilo. Niseme tu, mikakati ya kutangaza nchi yetu iko mingi na sisi tumejipanga kuelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Kamati yetu ililisema kwa msisitizo mkubwa ni katika kuhakikisha kile Kituo chetu cha Utangazaji cha *DDMNC*, tuhakikishe tunawachukulia hatua wale wote ambao walifanya ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imeanza kuchukua hatua kwa ajili ya watu hao, lakini kama wanavyofahamu sheria zetu za kazi, zimeweka mfumo ambao ni *low boost* ambao unahakikisha kwamba yule ambaye anatuhumiwa, lazima na yeye atendewe haki ya kusikilizwa ili hatua zikichukuliwa zisiwe na mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tunachukua umakini mkubwa sana kwenye kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa sheria ili tusiende kwa pupa tukajikuta kwamba tumeliharibu jambo hili badala ya kulitengeneza. Ninaliomba Bunge lako Tukufu liwe na subira, tunaifanya kazi hii kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo yalisemwa; dada yangu Mheshimiwa Hawa alisema kwenye ubunifu. Ninataka nimpe mfano mmoja tu, kwenye mazao ya utalii, utalii wa kuwaleta watalii kwa meli lilikuwa siyo jambo linalozungumzwa

katika nchi hii, lakini ndani ya hii miaka miwili tumefanya kazi kubwa sana ya kuleta *cruise ships*, watalii wanakuja kwa meli kuja kutembelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwanzo wa mwaka huu mpaka kufika mwezi Aprili tayari tulikuwa na meli karibu saba ambazo zimefika katika nchi yetu na jumla ya watalii 936 walikuwa wametembelea. Mwamko wa meli za kitalii kuja kwenye nchi yetu unaendelea kuongezeka. Ninaomba tuendelee kuiamini Wizara yetu, jambo kubwa linafanyika katika kuhakikisha Sekta ya Utalii inaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo ambayo yamesemwa na dada yangu Mheshimiwa Ritta, katika kuhakikisha utangazaji wa utalii kwenye kanda ile anakotokea unaweza kufanyika. Sisi kama Wizara tumesikia, wenzetu wa *TTB* watakwenda kulifanyia kazi jambo lile ili kuhakikisha tunashirikiana na maeneo haya ambayo yameanzisha maonesho ya kiutalii. Tusiyapokee majukumu yao lakini tufanye kazi kwa pamoja ili kuweza kuongeza thamani katika shughuli hizi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninakushukuru kwa kunipa muda huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Balozi Pindi Hazara Chana ili aweze kuhitimisha hoja yake. Kabla hajaanza kuhitimisha hoja yake, niseme, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(5), ninaongeza muda ili tuweze kumaliza shughuli hii pale ambapo tutakuwa tuko tayari. Mheshimiwa Balozi Pindi Chana, endelea.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninachukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa kupata fursa hii ya kuhitimisha hoja. Pia ninatoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na ninasema,

kwanza michango imeingia kwenye *Hansard,* lakini pamoja na michango kuingia kwenye *Hansard,* tutahakikisha tutaweka kwenye maandishi kila mchango na kuwasilisha. Kwa hiyo, tunatoa shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa michango yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunatoa shukurani nyingi kwa Kamati yetu ya Bunge; Kamati ambayo imekuwa ikitushauri mambo mengi mazuri na imeweza kufanya hata mapato ya utalii yameongezeka, idadi ya watalii pia wameongezeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kuelezea suala ambalo limezungumziwa kwa kiasi kikubwa, ambalo ni suala zima la uhifadhi na hasa mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori. Kwa kweli eneo hili sisi kama Wizara tunazidi kutoa kupaumbele cha hali na mali kuhakikisha kwamba tunadhibiti wanyamapori na tunahakikisha kwamba takwimu za ajali *(injury)* na takwimu zingine zinazotokana na wanyamapori kuleta uharibifu kwa binadamu na mazao zinazidi kupungua au kutokuwepo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazidi kuweka mikakati thabiti kabisa ya kuhakikisha kwamba tunadhibiti eneo hili. Katika bajeti hii, tumesema tunakwenda kununua *helicopter* zipatazo mbili za *TANAPA* na *Ngorongoro NCAA*. Hii yote ni katika kudhibiti mwingiliano utakaokuwepo na kufika kwa haraka kuratibu. Pia, tumeshaelekezana kwamba, sasa wakati umefika wa kulinda maeneo yetu ya hifadhi kwa njia ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na teknolojia, maana yake unaweza ukaona eneo lako la hifadhi na unaweza ukaona kwamba, sasa tembo wametoka. Hii ni pamoja na kufunga *collar* maalum. *Collar* hizi unaweza ukaziona kwenye *computer* na ni rahisi kujua, katika hifadhi fulani, kuna tembo wanatoka kwenye hifadhi kwenda kwenye maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana tutakwenda kununua *collar* na tutakwenda kuchimba mabwawa katika bajeti

hii. Haya mabwawa yataweza kusaidia kuhakikisha kwamba maeneo ya hifadhi yana maji na hata Mheshimiwa fulani amezungumza hapa kwamba, wakati wa mvua imedhihirika kabisa tembo hawatoki zaidi katika maeneo ya hifadhi. Kumbe maji ni kipaumbele katika maeneo yetu ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda vilevile kuweka ujenzi wa vizimba ambavyo vitasaidia sana kudhibiti mamba na viboko katika maeneo yetu mbalimbali. Hivi sasa tumeshaanza kuweka vizimba na Waheshimiwa wengi wameomba vizimba. Tumesikia na tutakuja huko kuhakikisha kuna vizimba ili watoto wanapoenda kuoga na akinamama kufua, wawe salama. Kwa hiyo, tutakwenda kuweka vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda pia kuendeleza ujenzi wa vituo vya askari katika maeneo yetu ambayo ni korofi yanayoonyesha kwamba takwimu za mwingiliano ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunakwenda pia kununua pikipiki na magari kwa ajili ya kusaidia askari wetu. Tumewasiliana na Waheshimiwa, kuna Waheshimiwa wanasema maeneo yetu hayana vitendea kazi vya kutosha. Tutahakikisha maeneo hayo tunasogeza vitendea kazi ili askari wetu wapate vitendea kazi, iwe ni pikipiki, magari au iwe ni *ranger post*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda pia kununua ndege nyuki. Ndege nyuki hizi ni *drones* ambazo zinatoa sauti kama ya nyuki ambapo tembo akisikia anaikimbia ile sauti na mara nyingi tunatumia ndege nyuki kusogeza hawa tembo kurudi katika hifadhi ili wasilete madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu tangu nimeingia kwa kweli, takwimu hizi za ajali *(Injury)* na matatizo mengine ya mwingiliano, ni takwimu ambazo nimeelekeza na kukubaliana kwamba lazima zishuke. Tuweke mikakati, mipango imara na tuhakikishe kwamba takwimu za mwingiliano, ajali za wanyama na wananchi zinakwenda kushuka na hatimaye kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kununua mabomu na kugawa mabomu. Haya yanaitwa mabomu baridi ambayo yanasaidia kusukuma wanyama. Pia, Waheshimiwa wamesema kwenye baadhi ya maeneo kuna upungufu wa askari na hayo maeneo tumeshayachukua, lakini tunakwenda pia kuajiri askari wa kutosha ili kuona ni kwa namna gani tunakwenda kuwapeleka katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha tumeomba askari 850 na mpaka sasa mchakato wa kufanya shughuli za utumishi ili askari hao wafike unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na askari, kuna mafunzo ya wanyamapori kwa askari wa vijiji ambao tunawaita *Village Game Scout*. Mafunzo hayo hutolewa kwenye vyuo vyetu kama Likuyu Sekamaganga na vyuo vingine na mafunzo haya yanasaidia sana vijana wetu hawa wanapopata mafunzo ili kuhakikisha kwamba wanaweza kudhibiti pale inapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, tayari kwa kushirikiana na *TAWIRI,* tunakwenda kuhakikisha kwamba na mikanda inanunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunakwenda kuweka mkakati wa kukabiliana na wanyamapori, mkakati huu tunakwenda kuuanzisha 2025 – 2030. Tulikuwa na mkakati wa awali wa 2020 – 2024, na sasa tunakwenda kuhuisha na kuwa na mkakati mwingine ambao utaanza Julai, 2025 – 2030, lakini tumesikia changamoto ya tembo, changamoto ya nyani katika maeneo ya Rombo, Kyela na wanyama wengine kama mamba, kiboko tumesikia na haya yote tunakwenda kushughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine ambayo tumeyazungumza hapa ni suala zima la fedha za utalii *(Tourism Development Levy)*. Awali ya yote nichukue nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa Serikali kuridhia tuwe na asilimia sita ya *TDL*, asilimia sita hizi wakati wa UVIKO tulikuwa hatuzipati na mnamo

2021/2022 kutokana na hali ya UVIKO hatukuwa na na fedha hizi za *TDL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi tunalishukuru Bunge lako, tunamshukuru Mheshimiwa Rais tumeanza kupata mnamo bajeti iliyopita Julai, mwaka jana. Tunatoa shukrani za dhati kabisa kwa fedha hizi ambapo Kamati pia imezungumza na Wabunge wengi, fedha hizi zimesaidia katika sehemu kubwa sana. Fedha hizi za *TDL* ni kwa manufaa ya kuendeleza utalii nchini. Tuseme kwamba katika kipindi hiki tumeweza kupata fedha hizi hadi mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimesaidia maeneo mengi kama walivyosema Kamati na mpaka sasa bado tunazo fedha takribani bilioni 22 hatujazitumia na tutazitumia kwa maelekezo ya Kamati ya Bunge. Kamati ya Bunge imeelekeza vizuri kwamba ili kutumia fedha hizi ni lazima tuwe na vipaumbele. Kamati imeeleza vizuri kabisa kwamba, ni vizuri tunapotumia fedha hizi tutumie kama ilivyo Mfuko wa Tanzania *Forest Fund*, nasi tunasema haya ni masuala ya msingi na ndiyo maana tumekuwa tukijadiliana na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata kiasi kisichopungua takribani bilioni 33 na sasa bado tunazo bilioni 22. Kwa hiyo, tunatoa shukrani kwa mawazo mazuri. Fedha hizi ni lazima zitumike kwa mujibu wa utaratibu ambao tumejiwekea na utaratibu ambao ni wa wazi. Kwa hiyo, tunashukuru sana, kwa mawazo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwanza tutakuwa na Mratibu maalum, Mratibu ambaye atakwenda kusimamia fedha hizi vizuri, pia tutakuwa na Kamati ya Ushauri, tunaweza tukasema ni Kamati ya Ushauri kwa mujibu wa *GN*, tunaweza tukasema ni bodi ambayo hata yale mashirika yanayochangia katika fedha hizi za *Tanzania Tourism Development Levy* asilimia sita ambapo zinatoka, *TANAPA,* Ngorongoro, *Conservation Commissioners* wote wanakuwa ni sehemu ya ile bodi ya kukubaliana kwamba fedha hizi ziende wapi. Hii ni Kamati ambayo ipo kwa mujibu wa Kanuni na Sheria na ni Kamati ambayo ni lazima itoe ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushauri wa Kamati tumesema kwamba, maoni mengi sana katika fedha hizi yamekuwa ni miundombinu, hivyo tuangalie ni namna gani fedha hizi zinaelekezwa katika suala zima la miundombinu, iwe ni masula ya madaraja, iwe ni masuala ya barabara tuone ni namna gani tunakwenda kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu inasaidia sana kuongeza Watalii. Watalii wanapokuja wanataka kuona barabara nzuri, hapa tumeona maoni ya Waheshimiwa Wabunge, wanasema "barabara zifunguliwe" na sisi tunaunga mkono hizi ni hoja za msingi sana. Barabara zetu ni lazima zipitike, tena zipitike kwa wakati wote siyo tu wakati wa kiangazi au wakati wa kipupwe. Kwa hiyo, fedha hizi kimsingi zitakuwa na chombo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu UVIKO hii ni mara ya kwanza tumepata, tangu baada ya UVIKO 19, hapo katikati zilikuwa hazijatoka kutokana na hali ya UVIKO, kwa hiyo tunatoa shukrani sana kwa Kamati, shukrani nyingi kwa Bunge na sasa tuendelee kuboresha mikakati na hizi fedha zitasaidia. Kama tulivyosema safari hii tunakwenda kukusanya bilioni za kutosha takribani trilioni moja, kwa hiyo fedha hizi zitasaidia masuala mazima ya kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka mfano wa 60%, 70% miundombinu, asilimia chache kidogo inayobaki tunaweza tukasema kuimarisha masuala ya masoko ya mafunzo na utafiti, tunahitaji utafiti, asilimia kidogo tunaweza tukasema 10% kwenye *tourism marketing, training and research* na masuala ya uwekezaji katika vifaa vya teknolojia, lakini asilimia kubwa ni miundombinu, tukiweza kufanikisha barabara, madaraja kama walivyosema Waheshimiwa "barabara yangu huku" wamezungumza hapa, malango, kwa mfano kufungua lango ambayo yapo karibu na hifadhi. Mheshimiwa Musukuma amezungumzia lango na Mheshimiwa Mama Sitta amezungumza lango. Maeneo ya umwagiliaji Mheshimiwa Kakunda kazungumza, kuongeza na kufungua Utalii Kusini, hii yote inahitaji miundombinu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi za *TDL* kwa kweli zitakwenda kusaidia na tunakwenda kuweka mikakati thabiti, ambapo zitakuwa na uwazi, zitakuwa na ushirikishwaji na kuhakikisha tunaweka kwenye vipaumbele ambavyo kimsingi vitasaidia kurudisha tena mapato. Hivyo tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ile filamu ya *Tanzania the Royal Tour*, *Amazing Tanzania* na mikakati mingi ya amani na utulivu katika nchi na ndiyo maana tumeweza kufikisha wataliii milioni 5.3 kama tulivyoelekezwa na mapato ya bilioni 3.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hii, Wabunge wamezungumzia suala la *retention*, tunaunga mkono suala hili, ni lazima kuwepo na *retention*. Katika maeneo haya ya hifadhi tunahitaji marekebisho iwe ni madaraja, sasa kama hakuna *retention* maana yake tutasubiri *OC* na tukisubiri *OC* yamkini daraja linabidi lirekebishwe haraka mara moja. Kwa hiyo, tunaendelea kushukuru kwa *political will* na maelekezo bayana kabisa kwamba sasa *TANAPA* na Ngorongoro kutakuwa na *retention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshalijadili hili jambo kwa kina na sasa tutaona mapendekezo haya katika *Finance Bill* inayokuja, kutakuwa na *retention* katika Shirika letu la *TANAPA* pamoja na *NCAA* (Ngorongoro) kwa kuanzia na baadaye kadri tunavyoenda tutaangalia na mashirika mengine jinsi ya kuwa na *retention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la Jumuiya za Wanyamapori za Jamii *(Wildlife Management Area)*. Haya ni maeneo ambayo yapo pembezoni mwa hifadhi, baada ya hifadhi pembezoni. Wananchi wanasema sisi tunaachilia eneo letu litumike kama Jumuiya ya Wanyamapori ya wananchi, maeneo haya yanasaidia sana. Kwanza kupunguza changamoto kati ya wanyama wakali na wanadamu, wanyama hawajui mipaka anatoka kwenye hifadhi, anapotoka kwenye hifadhi kunapokuwa na *WMA* maana yake anaingia katika eneo lenye *grade* nyingine ya hifadhi, lakini siyo kama maeneo ya *TANAPA*, *TAWA* au Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya wananchi wenyewe wanasema tuna-*surrender* kwa ajili ya manufaa yetu, wananchi wanawaalika wawekezaji wanaweka *camp*, wanaweka *lodge*, wanapata mapato, vijana katika maeneo hayo wanapata ajira za ulinzi kama vile *Game Scout*, wanapata ajira mbalimbali na fedha nyingi za utalii zinakuwa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wamezungumza fedha za *WMA* zinazotokana na masuala ya picha, kwa maana utalii wa picha una mapato, lakini kuna baadhi ya *WMA* wanafanya shughuli za uwindaji *(hunting)* na wao pia wanastahili haki yao. Hivyo, maoni ya Waheshimiwa wamesema fedha hizi, sheria zirekebishwe na zipatikane kwa wakati na kwa haraka. Hili ni eneo ambalo tumeshaanza mjadala ili fedha hizi ziweze kupatikana kwa wakati na kwa haraka. Kwa hiyo, eneo hili tunaendelea kuliboresha na niwashukuru sana wananchi. Yale maeneo ambayo yana hifadhi, yana maeneo ya wanyamapori ambayo hayana maeneo ya Jumuiya ya Wanyamapori, tuone ni namna gani ya kuanzisha haya maeneo, tayari Wizara yangu inaenda kutoa elimu, umuhimu wa kuwa na *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimetoa fedha kwa *WMA*. Eneo ambako kuna *WMA*, kwanza Halmashauri inapata mapato kama halmashauri yanayorejeshwa, lakini ile *WMA* yenyewe inapata na Serikali ya Kijiji inapata. Tumeshuhudia baadhi ya *WMA* wanapata hadi bilioni 1.3 ambazo zinasaidia maendeleo, zinasaidia uhifadhi, lakini Serikali za Vijiji zinapata mpaka milioni 600. Haya ni maeneo ambayo kwa lugha ya kitaalam wanaita shoroba (*corridor* za wanyamapori) maeneo haya huwezi kuweka makazi, maeneo haya huwezi kuweka mashamba. Kwa hiyo wakati umefika wa kuridhia kwamba maeneo kama haya nje, kijiji chenyewe kinaamua kwamba haya tunayahifadhi kama *buffer zones* na wanaweka *WMA*. Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo yanasaidia sana na tayari nimeshaongea na baadhi ya Wakurugenzi tuone ni namna gani ya kuendelea kutoa elimu ili tupate maeneo ya *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tayari tumeshaanza kurekebisha Sheria ya Kifuta Jasho na Kifuta

Machozi. Hivi sasa kifuta machozi tumeoongeza 100%, kifuta jasho tumeongeza 50%. Hivi sasa tupo katika Mfumo wa *PAIS*, huu ni mfumo ambao utasaidia fedha hizi kama walivyosema Waheshimiwa zipatikane kwa haraka na kwa wakati. Mfumo huu unaitwa *Problem Animal Information System*. Tumeshakaa na Maafisa wa Wanyamapori katika Wilaya zetu zote nchini na kuwaelekeza jinsi ya kuweka *data* katika maeneo haya. Sambamba na hilo, tunaanza na *pilot* katika Wilaya 10 kuona ni namna gani ya kutumia huu Mfumo wa *PAIS* kwa ajili ya suala zima la kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, lipo suala la geti, suala la geti ni miongoni mwa vipaumbele vyetu. Tumesema sambamba na njia mbalimbali tuone ni namna gani tunakwenda kuweka geti au kwa lugha nyingine tunaita *fence*, *fence* zinasaidia sana kuhakikisha kwamba wanyama hawa hawapiti kwenda kudhuru wananchi, tayari tumeshaweka makadirio ya kujenga hizi *fence*, *fence* ambazo zitazuia mwingiliano kati ya wanyama wakali pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa kushirikiana na wadau tumeshajenga kilometa takribani 61 za uzio wa umeme katika bajeti hii na katika bajeti ijayo tumesema tunakwenda kujenga takribani kilometa 53, ikiwa ni kutoka Loduare kuelekea Oldeani kilometa 15 katika Wilaya ya Karatu ili kudhibiti wanyama hawa. Pia, Hifadhi ya Ngorongoro, pia kilometa 38 kutoka Tabora 'B' hadi Mto Mara ili kudhibiti wanyama wanaotoka Hifadhi ya Serengeti, hii ni *corridor* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kabisa tukiweka mikakati hii uhifadhi utakuwa na manufaa, wananchi watakuwa na amani, watachangia uhifadhi, lakini sisi wenyewe wahifadhi tutaona kwamba wananchi wetu wako salama, wanaendelea vizuri na kuhakikisha kwamba uhifadhi unachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mengine yote tutaleta kwa maandishi, kunaomba kuwasilisha kama nilivyotoa ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, bado unatoa hoja yako.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono. Sasa tunakwenda kwenye hatua nyingine.

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*……..…….Sh. 7,055,621,550
Kifungu 1002 - *Finance and Account Unit*……..Sh. 1,248,926,356
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……..….Sh. 1,861,202,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.….Sh. 609,032,988
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……...….Sh. 837,288,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*…....Sh. 873,627,917
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*……..……..Sh. 619,996,000

Kifungu 1008 - *Management Information System Unit*……..Sh. 1,096,629,000
Kifungu 1009 - *Research and Training Unit*……...Sh. 36,342,330,996
Kifungu 1010 - *Paramilitary Coordination Unit*…..…Sh. 1,437,088,000
Kifungu *1011 - Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh.797,616,000
Kifungu 2001 - *Wildlife Development*…..……Sh. 114,400,430,216
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*…..……Sh. 59,864,665,503
Kifungu 4001 - *Tourism*……Sh. 15,212,109,126
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit*…..……Sh. 11,975,785,348

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit*……...….Sh. 977,476,764
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……..….Sh. 18,682,561,593
Kifungu 2001 – *Wildlife*……..……..….Sh. 40,194,291,141
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping*……..…Sh. 42,332,017,978
Kifungu 4001 – *Tourism*……..Sh. 2,563,574,524
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit*.....Sh. 1,000,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa, tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)*(a)* na *(b)* ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi, ikubaliwe na Bunge. Ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Sasa, nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki kwamba Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya ninyi kuhojiwa na kuafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, sasa ninatangaza rasmi kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Nitumie pia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo wamewaahidi Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba

wanaenda kuyafanyia kazi, ikiwa ni pamoja na zile hoja ambazo zimeletwa na Kamati, ushauri uliotolewa na Kamati na pia ushauri ulitolewa na Wabunge, wameonyesha kwamba wameupokea, hivyo tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wetu tunakupongeza sana na tunashukuru kwa kazi nzuri, Mheshimiwa Mnzava lakini pia, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma, tunawashukuru sana kwa kuendelea kuisimamia vizuri Kamati hii ambayo pia inasimamia Wizara hii. Wajumbe wote wa Kamati hii pamoja na ninyi wote Waheshimiwa Wabunge, wengine mnatokea katika maeneo ambayo kuna changamoto huko na siyo Wajumbe wa hii Kamati, lakini wanafanya kazi nzuri ya kuhakikisha hoja zenu zinasikika upande wa Kamati, lakini pia hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri jambo moja kwenye hotuba yako ukurasa wa 26 umezungumza kuhusu wanyama wanahamishwa kutoka maeneo mbalimbali na umetaja hapo kuwa baadhi wanapelekwa huku, baadhi wanapelekwa huku aina mbalimbali za wanyama. Hawa wanyama kwa sababu nao wana familia zao, sasa sijui kama wakati ule wa kuwakamata na wale mnaoamua kuwahamisha kama huwa mnaangalia familia, kama mnahamisha nazo au mnamkamata tu myama halafu mnampeleka akifika huko anajikuta yupo katika mazingira magumu kidogo, kwa sababu, wanaishi kwa makundi na kwa zile familia. *(Makofi)*

Ninafikiri ni muhimu kuzingatia hizo, sijui kama zitaitwa haki za wanyama, lakini ninafikiri ni muhimu kuzingatia wale wanapohamishwa ni lazima wahamishwe kwa sura ambayo haendi huko akajikuta yeye ndiyo yuko peke yake, halafu wote wako na mazingira yao na yeye amewaacha wenzake wote huku. Sasa sijui huwa mnaangalia vigezo gani, ninadhani kulikuwa kuna changamoto kidogo upande wa Kitulo, kuna wanyama kama wawili, watatu hivi waliondolewa wakaacha familia zao mahali, halafu wakashindwa kujikuta kwamba zile familia zilizoko kule kwamba wanaweza kuendana nazo.

Kwa hiyo, hili tunafikiri kwa sababu teknolojia imeshakua sana na nyinyi kama mlivyoeleza kwenye kitabu cha hotuba, kwa kweli mnafanya kazi nzuri, mnawawekea hawa wanyama vile vifaa vya kutambua wanaelekea wapi kama kundi, wanafanya nini, basi hivyo vinaweza pia kuonyesha kwamba ili tukiwa tunatoa familia basi tusimtoe yeye pekee yake, angalau aambatane na wanafamilia wachache wakaanzishe huko familia iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, tunakutakia kila la kheri katika hayo, pamoja na kwamba tunaenda kwenye uchaguzi, lakini tunaamini kwa sababu Watendaji wataendelea kuwepo, wataendelea kuyafanyia kazi haya kwa sababu teknolojia imeshakua sana, kwa hiyo hamna haja ya kuwaletea maumivu wanyama kama tunaweza kuyapunguza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, basi ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.44 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 20 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)